**SERIKALI YA MAPINDUZI YA ZANZIBAR**

# MAPITIO YA HALI YA UCHUMI 2025 NA UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO 2025/2026

**KITABU CHA KWANZA**

**TUME YA MIPANGO ZANZIBAR**

**JUNI, 2026**

# YALIYOMO


**ORODHA YA VIFUPISHO**........................................................... vi
**UTANGULIZI** ......................................................................... viii
**SURA YA KWANZA**................................................................... 1
**1.0 HALI YA UCHUMI** ............................................................... 1
1.1 Uchumi wa Dunia ..................................................................... 1
1.2 Uchumi wa Nchi Zilizoendelea .................................................. 2
1.3 Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi ............ 2
1.4 Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika................................................ 4
1.4.1 Uchumi wa Afrika..................................................................... 4
1.4.2 Uchumi wa Nchi za Visiwa Vilivyo Barani Afrika.................... 7
1.4.3 Uchumi wa baadhi ya Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara. .......................................................................... 9
1.4.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki.................... 11
1.4.5 Nchi zenye Uhusiano wa Kibiashara na Zanzibar (*Zanzibar Trading Partners*).................................................... 14
1.5 HALI YA MFUMKO WA BEI ........................................................ 15
1.5.1 Mfumko wa Bei wa Dunia........................................................ 15
1.5.2 Mfumko wa Bei kwa Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara .. 16
1.5.3 Mfumko wa bei wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki........ 17
1.5.4 Mfumko wa bei kwa Nchi zenye Uhusiano wa Kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners) ....................................... 19
1.5.5 Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya bidhaa katika Soko la Dunia.. 21

**SURA YA PILI**........................................................................... 24
**2.0 HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR**............................................. 24
2.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi ............................................ 24
2.2 Pato la Mwananchi..................................................................... 25
2.3 Mwenendo wa Mfumko wa Bei Zanzibar ..................................... 26
2.4 Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani........................................................................... 28
2.5 Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar................................ 29
2.6 Ukuaji wa Sekta katika Pato la Taifa ........................................... 30
2.6.1 Sekta ya Huduma.................................................................... 30
2.6.2 Sekta ya Viwanda.................................................................... 32
2.6.3 Sekta ya Kilimo ...................................................................... 33

2.7 Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa ............................................ 34
2.7.1 Sekta ya huduma ........................................................................ 34
2.7.2 Sekta ya Viwanda........................................................................ 34
2.7.3 Sekta ya Kilimo .......................................................................... 35
2.8 Ukuzaji Rasilimali ............................................................................. 44
2.8.1 Mgawanyo wa Umiliki wa Miradi iliyosajiliwa na ZIPA.......... 46
2.8.2 Mgawanyo wa Miradi Iliyosajiliwa na ZIPA Kulingana na Mabara ........................................................................................ 47
2.8.3 Nafasi za Ajira Zilizosajiliwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) Kutoka Miradi ya Uwekezaji ....... 47
2.9 Hali ya Upatikanaji wa Ajira Zanzibar ............................................. 48

**SURA YA TATU** ...................................................................................... 50
**3.0 SEKTA YA NJE** .................................................................................. 50
3.1 Usafirishaji wa Bidhaa Kwenda Nje ya Nchi ..................................... 50
3.1.1 Usafirishaji wa Mazao Makuu ya Biashara ...................................... 50
3.2 Uagiziaji wa Bidhaa Kutoka Nje ya Nchi........................................... 52
3.3 Urari wa Biashara ............................................................................... 53
3.4 Uhaulishaji wa Bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara............. 54

**SURA YA NNE** ......................................................................................... 56
**4.0 SEKTA YA FEDHA** ............................................................................ 56
4.1 Sekta Ndogo Ya Benki ........................................................................ 56
4.1.1. Benki Kuu ya Tanzania (BOT) ...................................................... 56
4.1.2 Mafanikio........................................................................................ 57
4.1.3 Huduma za Kibenki ......................................................................... 59
4.1.4 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishwaji wa Fedha za Kigeni (Exchange Movement)................................................... 62
4.1.5 Benki Ya Watu Wa Zanzibar (PBZ) ............................................... 63
4.2 Mamlaka Ya Usimamizi Wa Bima Tanzania (TIRA)......................... 64
4.2.1 Hali Ya Soko La Huduma Za Bima Zanzibar. .............................. 67
4.2.2 Mafanikio Ya TIRA Na Bima.......................................................... 67
4.2.3 Matumizi Ya Bima Kwa Smz .......................................................... 67
4.3 Utekelezaji Wa Bima Ya Safari (*Inbound Travel Insurance*)............. 68
4.4 Changamoto ......................................................................................... 68
4.5 Shirika La Bima Zanzibar (ZIC).......................................................... 78

4.6 Mfuko Wa Hifadhi Ya Jamii Zanzibar (ZSSF) .................................. 86
4.7 Huduma Ndogo Za Fedha (Microfinance)......................................... 95
4.8 Idara Ya Maendeleo Ya Ushirika...................................................... 96

**SURA YA TANO** .................................................................................. 101
**5.0 SEKTA YA MIUNDOMBINU** ....................................................... 101
5.1 Wakala wa Barabara........................................................................ 101
5.3 Nishati ya Umeme............................................................................ 105
5.4Mamlaka ya Maji Zanzibar (Rand Water). ......................................... 107
5.4.1 Usimamizi na Uendelezaji Rasilimali Maji na Utatuzi wa Changamoto za Maji. ................................................................ 107
5.4.2 Juhudi, Huduma, na Mchanganuo wa Utekelezaji wa Huduma ya Maji Mkoa wa Mjini kwa Mwaka 2025. .............................. 118
5.4.3 Huduma ya Maji Vijijini ........................................................... 109

**SURA YA SITA** ................................................................................... 111
**6.0SEKTA YA ELIMU** ...................................................................... 111
6.1Elimu na Mafunzo ya Amali ............................................................. 111
6.1.1 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Serikali ............................................................. 112
6.1.2 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Binafsi ............................................................. 114
6.1.3 Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari kwa Jinsia kwa skuli za Serikali na Binafsi. ...................................................... 115
6.2 Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu.............................................. 118
6.2.1 Idadi ya Mikopo iliyotolewa...................................................... 118
6.2.2 Mwenendo wa utoaji wa mikopo na Utaratibu wa kurejesha mikopo ................................................................................... 119
6.2.3 Ukusanyaji wa marejesho ya mikopo ........................................ 119
6.2.4 Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu..................................... 120
6.2.5 Mapendekezo ya Kutatua Changamoto za Urejeshaji Mkopo wa Elimu ya Juu; ...................................................................... 121
6.2.6 Mikakati ya Bodi Juu ya Urejeshajiwa Mikopo kwa Wanufaika ............................................................................... 121

**SURA YA SABA** ........................................ 123
**7.0 SEKTA YA AFYA** ........................................ 123
7.1 Wataalamu wa afya ........................................ 123
7.1.2 Idadi ya Vituo vya Afya na Wagonjwa ........................................ 124
7.1.3 Idadi ya Wagonjwa waliopata huduma za Mfuko wa bima ya Taifa ya Zanzibar mwaka 2024 -2025........................................ 125
7.2 Idadi ya Kinamama Waliojifungua na Vizazi hai ........................................ 126
7.2.1 Wilaya na Idadi ya Vizazi hai ........................................ 126
7.2.2 Idadi ya Kinamama Wajawazito Waliojifungua Kwa Njia ya Upasuaji, Kawaida na Mimba Zilizoharibika........................................ 127
7.2.3 Lishe ya Mama na Mtoto ........................................ 128
7.3 Mpango wa Damu Salama ........................................ 129
7.4 Magonjwa Kumi Yaliyoripotiwa Mara kwa Mara 2024/2025 ........................................ 130
7.4.1 Hali ya maambukizi ya Ugonjwa wa Ukimwi nchini ........................................ 130
7.5 Huduma za Upasuaji Mkubwa ........................................ 131
7.6 Idadi ya Vifo kwa Wagonjwa ........................................ 131
7.7 Mpango wa Kumaliza Malaria Nchini........................................ 131
7.7.1 Dawa Zinazotumika Kutibu Malaria Nchini ........................................ 132
7.7.3 Mikakati ya Kupambana na Malaria Zanzibar 2021-2025 ........................................ 133
7.7.4 Idadi ya Nyumba Zilizopuliziwa Dawa ........................................ 134
7.8 Maradhi ya Kuambukiza ........................................ 135
7.9 USTAWI WA JAMII ........................................ 136
7.9.1 Hali ya Madawa ya kulevya Zanzibar ........................................ 136
7.9.2 Idadi ya Nyumba na Wakaazi Walioathirika na Uraibu wa Madawa ya Kulevya (Sober Houses)........................................ 137
7.9.3 Idadi ya Waraibu Kwenye Nyumba za Kurekebisha Tabia. ........................................ 137
7.10 Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto ........................................ 138
7.10.1 Idadi ya Wazee na Watoto Yatima Kwenye Nyumba za Hifadhi........................................ 139
7.10.2 Watu wenye Mahitaji Maalumu Zanzibar 2025/26 ........................................ 140
7.11 Hali ya Wanawake na Watoto. ........................................ 140
7.12 Visa vya Unyanyasaji wa Kijinsia mwaka 2025 ........................................ 141
7.13 Makosa ya Jinai........................................ 142
7.14 Ajali za Barabarani........................................ 143
7.15 Waathirika wa ajali za barabarani ........................................ 144

**SURA YA NANE** ........................................ 145

**8.0MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII ZANZIBAR MWAKA 2024.** ........................................................................ 145
**SURA YA TISA**........................................................................ 147
**9.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2024/2025** ........... 147
9.1 Mapato ya Serikali ........................................................................ 147
9.1.1 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani........................................... 147
9.1.2 Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi ........................................... 147
9.1.3 Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ......................... 148
9.2 Matumizi ya Serikali 2025/2026.................................................. 148
9.2.1 Matumizi ya Kazi za Kawaida............................................... 148
9.2.2 Mishahara ........................................................................ 148
9.2.3 Matumizi Mengineyo........................................................... 148
9.2.4 Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali ................................... 149
9.2.5 Matumizi ya Kazi za Maendeleo. ........................................... 149
9.3 Deni la Taifa........................................................................ 149

**SURA YA KUMI** ........................................................................ 150
**10.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026**.. ........................................................................ 150
**SURA YA KUMI NA MOJA** ........................................................ 179
**11.0 UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026**....... 179
**11.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 KWA KILA WIZARA** .......................................... 180

## ORODHA YA VIFUPISHO

| | |
|---|---|
| ARUTI | Mfumo wa kielektroniki wa Rasilimali watu |
| ATMs | Automated Teller Machines |
| BADEA | Arab Bank for Economic Development in Africa |
| BAMAS | Mfumo wa Bajeti na Matumizi ya Serikali |
| BMEJZ | Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar |
| BOA | Bank Of Africa |
| BPRA | Business and Property Registration Agency |
| BRELA | Business Registration and License Agency |
| CCECC | China Civil Engineering Construction Corporation |
| CRDB | Bank Cooperative Rural Development Bank |
| CRJE | China Railway Jianchang Engineering |
| DTB | Diamond Trust Bank |
| EFT | Electronic Fund Transfer |
| FAO | Food and Agricultural Organization |
| FSDMP | Financial Sector Development Master Plan |
| Fumis CAG | Fumis Controller and Auditor General |
| GIZ | German Society for International Cooperation |
| HIV | Human Immune Virus |
| IS | Information System |
| JICA | Japan International Cooperation Agency |
| JKU | Jeshi la Kujenga Uchumi |
| KfW | German Development Bank |
| KM | Kilometer |
| KMKM | Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo |
| KVZ | Kikosi cha Valantia |
| KWh | Kilowatt per hour |
| KZU | Kikosi cha Zimamoto na Uokozi |
| MUCOBA | Mufindi Community Bank |
| NBC | National Bank of Commerce |
| NBC | National Bank of Commerce |
| NIDA | National Identification Authority in Tanzania |
| NIP | National Insurance Policy |
| NMB | National Microfinance Bank |

| | |
|---|---|
| OC | Operating Cost |
| OPEC | Organization of the Petroleum Exporting Countries |
| PBZ | People Bank of Zanzibar |
| POs | Point of Sale |
| SADC | Southern Africa Development Community |
| SDGs | Sustainable Development Goals |
| SMT | Serikali ya Muungano ya Tanzania |
| SMZ | Serikali ya Mapinduzi ya Zanziabr |
| SNR | Sema na Rais |
| SUZA | State University of Zanzibar |
| TASAF | Tanzania Social Action Fund |
| TCB Bank | Tanzania Commercial Bank |
| TEHAMA | Teknolojia ya Habari na Mawasiliano |
| TIO | Telecommunication Industry Ombudsman |
| TIRA | Tanzania Insurance Regulatory Authority |
| TIRA MIS | Tanzania Insurance Regulatory Authority Management |
| TIRA RBS | Tanzania Insurance Regulatory Authority |
| TRA | Tanzania Revenue Authority |
| TUKUZA | Tumia Umeme kwa Uangalifu Zanzibar |
| TZS | Tanzania Shilling |
| UNICEF | United Nation Childrens Fund |
| UN-WOMEN | United Nation for Women |
| URTI | Upper Respiratory Track Infection |
| WHO | World Health Organization |
| ZADEP | Zanzibar Development Plan |
| ZAFICO | Zanzibar Fisheries Company |
| ZARSTA | Zanzibar Road Transport and Safety Authority |
| ZBC | Zanzibar Broadcasting Cooperation |
| ZIC | Zanzibar Insurance Corporation |
| ZIPA | Zanzibar Investment Promotion Authority |
| ZOLAS | Zanzibar Online Local Application System |
| ZRA | Zanzibar Revenue Authority |
| ZSSF | Zanzibar Social Security Fund |

# UTANGULIZI

Uchumi wa Zanzibar umeendelea kukua kwa kasi, licha ya kukabiliwa na mabadiliko ya sera za kichumi na kisiasa ambazo pia huathiri mwenendo wa viashrira vya ukuaji wa uchumi na maendeleo endelevu. Hali ya muunganiko wa sera shindanishi ambazo huathiri biashara za kimataifa sambamba na athari za mabadiliko ya tabia nchi, Zanzibar inahitaji sera madhubuti na mikakati ya kukabiliana na mabadiliko kwa lengo la kukuza uchumi na kuleta maendeleo endelevu ya wananchi wa Zanzibar, kwa kutanua wigo wa shughuli za huduma, biashara za kimataifa (uingizaji na usafirishaji wa mazao ya biashara), uhaulishaji wa huduma zitokanazo na utalii pamoja shughuli zinazotokana na huduma hizo. Aidha, Serikali imeweka mkazo zaidi katika kudhibiti mfumko wa bei hasa kwa bidhaa muhimu za chakula , kwa kufuatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa muhimu katika soko la dunia sambamba na kushajiisha uzalishaji wa ndani hasa kwa mazao ya chakula, ili kuondokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa hizo. Moja ya hatua hizo ni kutoka misamaha na nafuu ya ushuru wa forodha kwa bei za vyakula muhimu vinavyoagizwa na wafanyabiashara hapa nchini ikiwa kama sera ya kudhibiti athari za kupanda kwa bei za bidhaa hizo katika soko la dunia.

Kwa mwaka 2025/2026 Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imepiga hatua kubwa katika kuandaa sera madhubuti za mipango ya maendeleo yenye kuchochea ukuaji wa uchumi wenye lengo la kuimarisha ustawi wa wananchi kiuchumi na kijamii pamoja na kusimamia misingi ya utawala bora kama ilivyoainishwa katika Dira ya Maendeleo ya Zanzibar (ZDV 2050) na kutafsiriwa na Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar wa muda wa kati (ZADEP 2021-2026) pamoja na Mipango mengine ya Kitaifa ikiongozwa na Ilani ya Uchaguzi ya Chama cha Mapinduzi ya Mwaka 2025 - 2030 na Hotuba ya Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi aliyoitoa wakati akizindua Baraza la kumi na moja mwezi wa Januari 2026.

Aidha, Mpango huu pia umezingatia Sera, Mipango na Mikakati ya kufikia Malengo ya Dira za Kisekta, Kikanda na Kimataifa kama vile Dira ya Maendeleo ya Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) ya mwaka 2050; Dira ya Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) ya mwaka 2050; Ajenda ya Maendeleo ya Afrika ya mwaka 2063; na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) ya mwaka 2030.

Kwa mwaka 2025, kasi ya ukuaji wa uchumi wa Dunia imeongezeka kwa wastani wa asilimia 3.4, ikilinganishwa na asilimia 3.2 mwaka 2024. Uchumi wa nchi Zilizoendelea umefikia ukuaji wa wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 1.6 mwaka 2024. Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi umefikia ukuaji wa wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2025, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2024.

Aidha, mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika na kufikia wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa asilimia 7.1 mwaka 2024. Pato halisi la Taifa (GDP at constant price) limefikia thamani ya TZS 4,307.9 bilioni mwaka 2025 kutoka thamani ya TZS 4,026.4 bilioni mwaka 2024. Hata hivyo, Pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at current price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 7,029.9 bilioni mwaka 2025 kutoka thamani ya TZS 6,572.6 bilioni mwaka 2024.

Kuongezeka kwa Pato la Taifa ni kiashiria cha kuimarika kwa uchumi wa Zanzibar ikiwa ni matokeo ya juhudi za Serikali katika kubuni na kutekeleza miradi ya maendeleo, kuweka mazingira mazuri ya kuwavutia wawekezaji, kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kiuchumi na kijamii, kuongeza wigo wa ukusanyaji wa mapato ya ndani na kusimamia nidhamu ya matumizi bora ya rasilimali fedha.

Mwaka 2025, Kasi ya mfumuko wa bei imepungua kufikia wastani wa asilimia 4.1 kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024. Kupungua kwa kasi ya mfumko wa bei kumetokana na kushuka kwa bei za bidhaa za chakula na zisizo za chakula katika soko la dunia. Serikali inaendelea na juhudi za kufatilia na kusimamia mwenendo wa bei za bidhaa na huduma, ikiwemo kupunguza ushuru na msamaha wa kodi kwa bidhaa muhimu za chakula zinazoingizwa nchini, kutoa bei elekezi za bidhaa za chakula na vifaa vya ujenzi, Juhudi hizo zimepelekea wananchi kupata huduma muhimu na zimeweza kupunguza kasi ya mfumko wa bei nchini na kuendelea kuwa na kiwango cha tarakimu moja.

Katika juhudi za kufanikisha Mpango wa Maendeleo kwa mwaka wa fedha 2024/2025, Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar imetekeleza miradi mikubwa ya kimkakati sambamba na utekelezajiwa miradi ya kijamii ikiwemo ujenzi wa miundombinu ya mawasiliano, afya, elimu na programu ndogo zenye lengo la kuwajengea uwezo na mazingira bora wananchi wenye kipato cha chini na mahitaji maalum, juu ya utoaji huduma za kibiashara, kilimo, uvuvi, utalii na ujasiriamali kwa ajili ya kuinua vipato vyao.

## SURA YA KWANZA

# 1.0 HALI YA UCHUMI

## 1.1 Uchumi wa Dunia

Kwa mujibu wa Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Duniani "World Economic Outlook" (WEO) ya mwezi April 2026, iliotolewa na Shirika la Fedha Duniani (IMF). Uchumi wa Dunia umekuwa kwa kasi ya wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2025, ikilinganishwa na kasi ya ukuaji wa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2024. Ukuaji wa uchumi wa Dunia ni matokeo ya kuimarika kwa uchumi katika nchi Zilizoendelea, Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi pamoja na nchi zilizoko Kusini mwa Jangwa la Sahara, ambazo huchangia wastani mdogo ikilinganishwa na maeneo mengine.

Ukuaji wa uchumi wa Dunia umetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa za chakula na kilimo na kupungua kwa bei za bidhaa muhimu za chakula na nishati katika soko la dunia, hali iliyopelekea kuongezeka kwa mahitaji na matumizi.Vikwazo vya biashara za kimataifa pamoja na ongezeko la tozo za forodha nchini marekani, kumepelekea kuongezeka kwa upatikanaji wa bidhaa hizo katika soko Dunia. Aidha, kuimarika kwa masoko ya hisa kwa nchi zilizoendelea kumeongeza upatikanaji wa mitaji kwa kampuni za uwekezaji na kuongeza kasi ya ukuaji uchumi katika nchi zinazoendelea.

Ukuaji wa uchumi kwa **Nchi Zilizoendelea** umefikia wastani wa asilimia1.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na asilimia 1.7 mwaka 2024 kutokana na kuimarika kwa sera za usimamizi wa fedha na uwekezaji. Uchumi wa **Nchi Zinazoendelea** na **Zinazoibukia kiuchumi** umefikia wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2025, ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2024. Kwa upande wa **Nchi za Afrika,** kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa mazingira ya uwekezaji ikiwemo miundombinu ya mawasiliano na kupelekea kuvutia wawekezaji binafsi hasa katika sekta za nishati na madini pamoja na kuimarika kwa mifumo ya technologia ya huduma za fedha katika nchi za Nigeria, Senegal na Ghana.

**Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara**, kasi ya ukuaji uchumi mwaka 2025 imefikia wastani wa asilimia 4.5 kutoka wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2024, kuimarika kwa uchumi katika nchi za eneo hili, kumetokana na uwekezaji

wa miradi mikubwa ikiwemo miradi ya nishati ya umeme na teknolojia ya huduma za kifedha na benki, ambapo kumeshajihisha zaidi wawekezaji binafsi kuekeza katika miradi ya maendeleo. Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa **Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki** imefikia wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2025, kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa uwekezaji wa uma, viwanda na huduma kwa nchi ya Uganda, kuimarika kwa miradi ya miundombinu, utalii pamoja na kuimarika kwa sekta ya uchimbaji madini na gesi asilia kwa Tanzania vile vile kuimarika kwa sekta ya kilimo,ujenzi na huduma kwa nchi ya Kenya na kuimarika viwanda kwa nchi ya Rwanda.

### 1.2 Uchumi wa Nchi Zilizoendelea

Hizi ni nchi ambazo zina wastani mkubwa wa Pato la Taifa (*GDP*) ikilinganishwa na nchi nyengine duniani. Miongoni mwa nchi hizi ni badhi ya nchi za Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, pamoja na nchi za Japan, Marekani, Canada, Ujerumani Ufaransa, Norway na Uingereza. Katika kipindi cha mwaka 2025, uchumi wa nchi hizi umefkia wastani wa asilimia 1.9 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.8 mwaka 2024. Ukuaji huo umetokana na kuimarika kwa biashara za kimataifa sambamba na kuongezeka kwa mahitaji na uzalishaji wa bidhaa za kieletroniki, gari na mashine zenye kutumia teknologia ya kisasa ya kupunguza matumizi ya hewa ya mkaa (*Green energy*) kama vile nishati za umeme, gesi na nguvu za jua.

Kiujumla, ukuaji wa uchumi wa nchi zilizoendelea unategemeana na ukuaji wa uchumi wa nchi zenye nguvu na ushawishi zaidi katika biashara za kimataifa ikiwemo Marekani ambayo kasi ya ukuaji wake umefikia wastani wa asilimia 2.1 mwaka 2025, kutoka 2.8 mwaka 2024, **Uingereza**, kasi ya ukuaji uchumi ilifikia wastani wa asilimia 1.3 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 1.1 mwaka 2024. Nchi ya **Japani,** kasi ya ukuaji ilifikia wastani wa asilimia 1.2 mwaka 2025, ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.1 mwaka 2024. Jumuia ya Ulaya, kasi ya ukuaji uchumi ilifikia wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 0.9 mwaka 2024.

### 1.3 Uchumi wa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi


Mwenendo wa ukuaji wa uchumi wa Dunia huchangiwa zaidi na kasi ya ukuaji wa uchumi kwa Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi zikiwemo

India, China na Afrika ya Kusini, Brazil na Urusi. Nchi hizi ni maarufu sana katika biashara za kimataifa kutokana na uwezo mkubwa wa kusarifu, kuzalisha na kusafirisha malighafi na bidhaa katika soko la dunia. Nchi hizi pia ni kiunganishi cha biashara za kimataifa, mitaji na uwekezaji kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara na nchi Zilizoendelea duniani kwa kusaidia teknolojia na utaalamu wa kuzalisha na usarifu wa bidhaa viwandani kufikia viwango vya kimataifa. Kwa mwaka 2024, ukuaji wa uchumi kwa nchi hizi umefikia wastani wa asilimia 4.4 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2024.

Nchi ya **Brazil** kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 2.3 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 3.4 mwaka 2024. Ukuaji huo umeathiriwa na madiliko ya sera za fedha ikiwemo udhibiti wa mikopo na usimamizi wa deni la taifa na kuongezeka kwa vikwazo vya biashara za kimataifa hasa kutoka nchi ya Marekani. Kwa upande wa nchi ya **India**, kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 7.6 mwaka 2025, kutoka wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2024, kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji viwandani, na kuimarika kwa masoko ya fedha na kuvutia mitaji ya uwekezaji. Nchi ya **China** kwa mwaka 2025, kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 5.0 sawa na mwaka 2025. Kasi hii ya ukuaji wa uchumi imetokana na kuimarika kwa sekta ya utalii na uzalishaji wa vifaa vyenye kutumia nguvu ya nishati ya umeme na jua kama vile gari na mashine za viwandani. Hata hivyo, kasi ya ukuaji wa uchumi wa China imeathiriwa na vikwazo vya kibiashara za kimataifa (Ongezeko kubwa la ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazoingia Marekani).

Kwa upande wa nchi ya Urusi, kasi ya ukuaji wa uchumi imepungua hadi kufikia wastani wa asilimia 1.0 mwaka 2025, kutoka wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2024. Hali ya mgogoro wa kivita na Ukraine pamoja na vikwazo vya biashara za kimataifa hasa kutoka kwa nchi zinazounda Jumuiya ya Ulaya na washirika NATO zimeendelea kuathiri ukuaji wa uchumi kwa nchi ya Urusi ***(Mchoro Nambari 1).***

**Mchoro Nambari 1: Ukuaji wa Uchumi wa Dunia, nchi Zilizoendelea na Nchi Zinazoendelea na Zinazoibukia Kiuchumi 2022-2025.**




*Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia na OECD, 2026.*


## 1.4 Hali ya Uchumi wa Bara la Afrika

### 1.4.1 Uchumi wa Afrika

Uchumi wa Bara la Afrika umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2025, kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024 (Mchoro Nambari 2). Kwa Kanda ya Kaskazini mwa Bara la Afrika, uchumi umefikia wastani wa asilimia 4.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2024; Kanda ya Kusini imefikia wastani wa asilimia 2.0 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 1.8 mwaka 2024; Kanda ya Magharibi ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2024; Kanda ya Afrika Mashariki ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 6.4 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2024. Kwa nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ukuaji wa uchumi umefikia wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2025 kutoka ukuaji wa wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2024. Kanda ya Afrika ya Kati imefikia wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 4.3 mwaka 2024. Kasi ya ukuaji uchumi katika Kanda hii imeonekana kuzorota kutokana na kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi wazalishaji wa mafuta zikiwemo Equatorial Guinea

asilimia (-1.6) na Gabon asilimia 2.3 mwaka 2025. Hali hii imeathiriwa na uzalishaji mdogo wa mafuta na gesi. ***(Mchoro nambari 2).***

**Mchoro Nambari 2: Wastani wa Kasi ya Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Afrika mwaka (2020 - 2025).**




***Chanzo: Uchumi wa Afrika, (AfDB) 2026***

**Kwa mwaka 2025, nchi za Afrika ambazo uchumi wake ulikuwa kwa kasi kubwa ni pamoja na;**

**(a) Jamhuri ya Afrika ya Kati (Central Africa)**

Kwa mwaka 2025, uchumi wa nchi ya Jamhuri ya Afrika ya Kati umekua kwa wastani wa asilimia 4.8 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 1.9 mwaka 2024. Kasi ya ukuaji huo imetokana na kuimarika kwa sekta ya kilimo hasa katika usafirishaji wa mbao, pamba na bidhaa za chakula viwandani na kuongezeka kwa mitaji ya uwekezaji.

**(b) Chad**

Uchumi wa nchi ya Chad umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 5.6 kutoka wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2024. Ukuaji huo umetokana na kupungua kwa athari za kiuchumi na kibajeti zilizotokana na wimbi la wakimbizi kutoka Sudan na kuongezeka kwa uzalishaji wa nishati ya mafuta baada ya kuanza program ya ukarabati wa miundombinu iliochakaa na kuimarika kwa sekta ya kilimo baada ya mafuriko yalioikumba nchi hiyo mwaka 2024.

**(c) Zimbabwe**

Zimbabwe ni moja ya nchi inayotumia sarafu mbili (Dola ya Zimbabwe na Dola ya Marekani). Uchumi wa nchi hii hutegemea kilimo, madini na usafirishaji wa mazao ya biashara hasa tumbaku. Kwa mwaka 2025, Ukuaji wa uchumi wa nchi hii ulifikia wastani wa asilimia 7.5, kutoka wastani wa asilimia 1.7 mwaka 2024. Hii imetokana na kuimarika kwa sekta ya kilimo baada ya athari za ukame, sekta ya madini na usafirishaji wa mazao ya biashara hasa tumbaku.

**Kwa mwaka 2025, miongoni mwa nchi za Afrika zilizokuwa na Kasi Ndogo ya Ukuaji wa Uchumi ni;**

**(a) Cabo Verde**

Kasi ya ukuaji wa uchumi imepungua  na kufikia wastani wa asilimia 5.5 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 7.2 mwaka 2024. Upungufu huo umetokana na ukuaji mdogo wa sekta ya utalii, kupungua kwa uhaulishaji wa fedha za kigeni (*Remittance)* kutoka kwa Wazawa wanaofanyakazi nje ya nchi.Uchumi wa Carbo verde unategemea kwa kiwango kikubwa cha sekta ya uhuduma hususani utalii ambao unachangia kwa kiwango kikubwa mapato ya fedha za kigeni, ajira, na shughuli za biashara.

**(b) Equatorial Guinea**

Equatorial Guinea ni maarufu katika uchimbaji na usafirishaji wa nishati ghafi ya mafuta na gesi duniani. Kwa mwaka 2025, uchumi wa Equatorial Guinea umekua kwa kasi pungufu ya wastani wa asilimia hasi ya (6.4) kutoka wastani wa asilimia 0.9 mwaka 2024. Hali hii imetokana na kupungua kwa uzalishaji wa nishati ghafi ya mafuta na gesi. Mwaka 2025 uzalishaji wa mafuta na gesi umeshuka kwa takribani 16.8 kutokana na visima vya mafuta kuzeeka na kupungua kwa kiwango cha uzalishaji.

**(c) Niger**

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi hii imepungua na kufikia wastani wa asilimia 6.9 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 10.3 mwaka 2024, hali iliyochangiwa zaid  kutokana na vikazo vya kiuchumi vilivyowekwa na jumuiya ya kiuchumi kwa nchi za Afrika magharibi kutoka (ECOWAS), pamoja  na kuyumba kwa sekta ya fedha na uwekezaji. Hata hivyo, Athari hizo zinatarajiwa kupungua kufuatia hatua za hivi karibuni kutangaza nia ya

kujiondoa katika Uanachama wa ECOWAS jambo ambalo linaweza kuleta muelekeo mpya wa kiuchumi na biashara katika ukanda huo.

**Jadweli Nambari 1: Ukuaji Halisi wa Uchumi kwa Kanda za Afrika kwa Mwaka 2024 -2025**

| KANDA ZA AFRIKA | UKUAJI HALISI (%) | |
|---|---|---|
| | 2024 | 2025 |
| Afrika | 3.5 | 4.2 |
| Kanda ya Kusini | 1.8 | 2 |
| Kanda ya Kaskazini | 2.7 | 4.1 |
| Kanda ya Magharibi | 4.7 | 4.8 |
| Kanda ya Mashariki | 4.3 | 6.4 |
| Kanda ya Kati | 4.3 | 3.9 |

***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi Barani Afrika, (AfDB) 2026.***

### 1.4.2 Uchumi wa Nchi za Visiwa Vilivyo Barani Afrika

Zanzibar ni moja ya visiwa maarufu sana duniani ambavyo hutegemea sana mapato ya fedha za kigeni, yatokanayo na uhaulishaji wa huduma za utalii (Receipts from Service Transfer), shughuli za uchumi wa buluu, usarifu na usafirishaji wa bidhaa za viungo zikiwemo karafuu na mwani.

Licha ya mafanikio makubwa ya kiuchumi yaliojitokeza katika miaka ya hivi karibuni, Zanzibar inaendelea kukabiliwa na ushindani mkubwa kutoka nchi zenye uchumi wa visiwa barani Afrika na Duniani kote kama vile Mauritius, Seychelles, Comoro na Madagascar, ambazo pia ni maarufu sana katika sekta ya utalii na biashara za viungo *(spices)*. Hivyo, ni muhimu kufatilia mwenendo wa uchumi wa nchi hizo ili kubuni sera zenye kubaini fursa mpya za kiuchumi na kubadili changamoto za ukuaji wa uchumi kuwa fursa za maendeleo endelevu katika mzingira ya uchumi shindani. Kwa mwaka 2025, uchumi wa visiwa hivyo uliripotiwa kama ifuatavyo:

#### a. Comoro

Visiwa vya Comoro ni moja ya visiwa ambavyo vinapatikana ndani ya bahari ya Hindi ambavyo ni mshirika wa kibiashara na Zanzibar hasa katika biashara za viungo, bidhaa za kilimo na utamaduni. Kwa mwaka 2025, uchumi wake umekua na kufikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024. Kasi ya ukuaji wa uchumi wa visiwa vya Comoro ilitokana na kuimarika kwa sekta ya fedha, na huduma, kuongezeka kwa shughuli za biashara na mchango

wa sekta ya kilimo na uvuvi pamoja na fedha kutoka nje pamoja na fedha kutoka kwa wazawa wanofanya kazi nje ya nchi *(remittence)*. Sekta hizi zimesababisha kuongezeka kwa mahitaji ya ndani na mzunguko wa fedha, licha ya uchumi kuendelea kubaki kua mdogo na unaotegemea sekta chache.

**b. Madagascar**

Uchumi wa Madagascar hutegemea sana sekta ya utalii, kilimo na uzalishaji viwandani. Kwa mwaka 2025, kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi ya Madagascar imepungua na kufikia wastani wa asilimia 2.8 kutoka wastani wa asilimia 4.2 mwaka 2024. Upungufu huo umetokana na kuongezeka kwa ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazosafirishwa kwenda Marekani na kuathiri uzalishaji viwandani hasa kwa bidhaa za nguo na kilimo.

**c. Mauritius**

Kwa mwaka 2025, kasi ya ukuaji uchumi imepungua kufikia wastani wa asilimia 3.1 kutoka wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2024. Kasi ndogo ya ukuaji wa uchumi ilisabishwa na kuanguka kwa sekta ya utalii pamoja na kuyumba kwa sekta ya fedha na thamani ya sarafu ya nchi hiyo.


**d. Seychelles**

Nchi ya Seychelles ni moja ya visiwa maarufu kwa uvuvi na utalii duniani. Kasi ya ukuaji uchumi wa nchi hiyo imeongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 2.9 mwaka 2024. Sababu za ukuaji huo ni kuongezeka kwa uhaulishaji wa huduma za kitalii na uwekezaji katika miradi ya miundombinu ya Teknolojia ya Mawasiliano na Habari (TEHAMA).

Kwa mujibu wa tathmini ya pamoja ya mwenendo wa uchumi kwa nchi za visiwa barani Afrika, Zanzibar imeendelea kuwa na ukuaji wa uchumi endelevu wenye kasi zaidi ikilinganishwa na nchi nyengine za visiwa Barani Afrika. Zanzibar imendelea kuwa kitovu muhimu cha biashara za kimataifa pamoja na uhaulishaji wa huduma za utalii pamoja na shughuli za uchumi wa buluu na mazao ya baharini. Hii imetokana na juhudi za makusudi za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuandaa sera na kubuni mikakati madhubuti inayoendana na mabadiliko ya kiuchumi na teknolojia kwa lengo la kuinua vipato vya wananchi. Miongoni mwa juhudi hizo ni pamoja na kuvutia mitaji

ya uwekezaji hasa katika sekta za utalii na miundombinu ya barabara, afya, elimu na mawasiliano, pamoja na kuitangaza Zanzibar katika masoko mapya ya utalii kupitia ndege za kimataifa za moja kwa moja *(Direct International Flights)*. Hatua hiyo imeongeza idadi ya watalii wa kimataifa na siku za kutalii kwa mwaka 2025 ***(Mchoro Nambari 3).***

**Mchoro Nambari 3: Wastani wa Kasi ya Ukuaji wa Uchumi kwa Nchi za Visiwa Vilivyo Barani Afrika ikiwemo Zanzibar kwa mwaka (2024-2025).**




| | Zanzibar | Mauritius | Seychelles | Comoro | Madagascar |
|---|---|---|---|---|---|
| 2024 | 7.1 | 4.9 | 2.9 | 3.3 | 4.2 |
| 2025 | 7.0 | 3.1 | 5.1 | 3.8 | 2.8 |

***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi Barani Afrika, (AfDB) 2026.***

### 1.4.3 Uchumi wa baadhi ya Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara.

Kwa Nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara, kasi ya ukuaji uchumi kwa mwaka 2025, imefikia wastani wa asilimia 4.5 kutoka wastani wa asilimia 3.8 mwaka 2024, kuimarika kwa uchumi katika nchi za eneo hili kumetokana na uwekezaji wa miradi mikubwa ikiwemo miradi ya nishati ya umeme na kukua kwa teknolojia ya huduma za kifedha na benki ambazo zimeongeza matumizi jumuishi ya huduma za kifedha *(Financial inclusion)* na kushajihisha urasimishaji wa shuguli za kibiashara, ujasiriamali na uwekezaji binafsi. Mwenendo wa ukuaji uchumi kwa baadhi ya nchi za Kusini mwa Jangwa la Sahara ni kama ifutatvyo;

### (a) Burkina Faso

Kasi ya ukuaji wa uchumi kwa nchi ya Burkina Faso imefikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2024. Kasi hii ya ukuaji uchumi imetokana na kuimarika kwa sekta ya kilimo hasa kwa mazao ya chakula na usindikaji wa bidhaa hizo viwandani na kuongezeka kwa thamani ya mauzo ya dhahabu katika soko la dunia.

### (b) Ethiopia

Kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi ya Ethiopia imefikia wastani wa asilimia 9.2 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 8.1 mwaka 2024. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika nchi hii, kumetokana na uwekezaji mkubwa wa miundombinu ya kuzalishia umeme, kukua kwa biashara ya nishati ya umeme na kuongezeka kwa mitaji ya uwekezaji hasa katika teknolojia ya mawasiliano na usafirishaji.

### (c) South Afrika

Kwa mwaka 2025, ukuaji wa uchumi wa nchi ya *South Afrika* umefikia wastani wa asilimia 1.1 kutoka wastani wa asilimia 0.5 mwaka 2024. Hii ni kutokana na kumarika kwa sekta ya viwanda, kilimo na madini, kuongezeka kwa thamani ya usafirshaji kwa bidhaa zitokanazo na kilimo, mifugo na kupanda kwa thamani ya mauzo ya dhahabu ndani na nje ya nchi.

**Jadweli Nambari 2: Mwenendo wa Uchumi kwa Nchi za Uchumi wa Visiwa na Baadhi ya Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara mwaka (2024 - 2025) kwa Asilimia**

| Nchi za Uchumi wa Visiwa Afrika na Nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara | 2024 | 2025 |
|---|---|---|
| **Nchi za Uchumi wa Visiwa (Island Economies)** | **(%)** | **(%)** |
| Comoro | 3.3 | 3.8 |
| Mauritius | 4.9 | 3.1 |
| Madagasca | 4.2 | 2.8 |
| Seychelles | 2.9 | 5.1 |
| Zanzibar | 7.1 | 7.0 |
| | | |
| **Nchi zenye Kipato cha Kati (LMICs)** | | |
| Angola | 4.4 | 3.1 |
| Cameroon | 3.5 | 3.1 |
| Ghana | 5.7 | 6.0 |
| Namibia | 3.7 | 2.4 |
| Nigeria | 4.1 | 4.0 |
| | | |
| **Nchi zenye Kipato cha Chini (LICs)** | | |
| Ethiopia | 8.1 | 9.2 |
| Malawi | 1.8 | 2.1 |
| Mali | 4.7 | 4.9 |
| Niger | 10.3 | 6.9 |
| Zambia | 4.0 | 3.8 |

***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi Barani Afrika, (AfDB) 2026.***

### 1.4.4 Uchumi wa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2025, kutoka wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024. Hii imetokana na kuimarika kwa uwekezaji wa uma, viwanda na huduma kwa nchi ya Uganda, kuimarika kwa miradi ya miundombinu, utalii pamoja na kuimarika kwa sekta ya uchimbaji madini na gesi asilia kwa Tanzania vile vile kuimarika kwa sekta ya kilimo,ujenzi na huduma kwa nchi ya Kenya na kuimarika viwanda kwa nchi ya Rwanda.

### (a) Tanzania

Uchumi wa Tanzania umekua kwa kasi ya wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2025, kutoka wastani wa asilimia 5.4 mwaka 2024. Uchumi wa Tanzania umeonekana kuimarika baada ya kuongezeka kwa miradi na usajili wa mitaji mikubwa ya uwekezaji hasa katika sekta za utalii, madini, na uzalishaji viwandani kwa vifaa vya ujenzi, pembejeo za kilimo na mbolea.

Aidha kukamilika kwa miradi ya bandari kavu za Kwala zikisaidiwa na Bandari jumuishi za Dar es Salaam, Mtwara na Tanga kumeongeza thamani ya usafirishaji wa mizigo na biashara za kikanda na kimataifa.

**(b) Kenya**

Ukuaji wa uchumi wa nchi hii umefikia wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 4.7 mwaka 2024. Ukuaji mdogo huo umetokana na kuimarika kwa sekta ya usafirishaji baada ya kufanyika kwa uwekezaji wa miundombinu ya barabara na bandari za Mombasa na Lamu pamoja na kuongezeka uwekezaji katika masoko ya fedha na hatifungani.

**(c) Uganda**

Kasi ya ukuaji uchumi wa Uganda imekua na kufikia wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2024. Kuongeza huko kumetokana na ukuaji wa sekta ya kilimo na kuongeza uzalishaji wa mazao ya chakula hasa mazao ya matunda na mbogamboga na kuongezeka kwa usambazaji wa nishati ya mafuta, gesi na umeme.

**(d) Rwanda**

Kwa mwaka 2025, uchumi wa Rwanda umefikia wastani wa asilimia 7.0 kutoka wastani wa asilimia 8.9 mwaka 2024. Kasi hii ya ukuaji wa uchumi imetokana na kupungua kwa uzalishaji wa bidhaa za kilimo na chakula viwandani na kupungua kwa shughuli za kibiashara hasa eneo la mashariki baada ya kuzorota kwa uhusiano baina ya nchi hiyo na Jamhuri ya Demokrasia ya Congo (DRC).

**(e) Burundi**

Uchumi wa Burundi umefikia wastani wa asilimia 3.9 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 3.5 mwaka 2024. Kukua kwa uchumi wa Burundi, kumetokana na kuimarika kwa usambazaji wa miundombinu ya umeme na maji ambayo imeongeza shughuli za kiuchumi na uzalishaji viwandani.

**(f) Sudani ya Kusini**

Uchumi wa nchi hii umekua kwa wastani wa asilimia 46.1 mwaka 2025 kutoka upungufu wa asilimia (26.1) mwaka 2024. Hali hii imetokana na kurejea kwa uthibiti wa miundombinu ya kusafirishia mafuta, kuongezeka kwa shughuli

za biashara, ufugaji na ujasirimali baada ya kusitishwa kwa vita baina ya makundi ya kijeshi na Serikali.


### (g) Jamhuri ya Demokrasia ya Congo

Kwa mwaka 2025, uchumi wa nchi hii umefikia wastani wa asilimia 5.7 kutoka wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2024. Kasi ndogo ya Ukuaji uchumi imetokana na kuzorota kwa hali ya amani na utulivu baada ya kuzuka kwa mapigano ya mara kwa mara baina ya majeshi ya serikali na Waasi wa M23 hasa katika eneo la mashariki ambalo lina utajiri mkubwa wa madini ya kimkakati.

### (h) Somalia

Nchi hii hutegemea sana usafirishaji wa mifugo na samaki, kwa asilimia 76 ya jumla ya thamani kwa bidhaa zinazosafirishwa nje. Kwa mwaka 2025, uchumi wa Somalia umefikia wastani wa asilimia 3.8 kutoka wastani wa asilimia 3.7 mwaka 2024. Ukuaji wa uchumi nchini Somalia, umetokana na kuongezeka kwa shughuli za ufugaji na uvuvi pamoja na ujenzi na ukarabati wa nyumba za biashara na makaazi kupitia uhaulishaji wa fedha za kigeni kutoka kwa Wazawa (Remittances) nje ya nchi ***(Mchoro Nambari 4).***

**Mchoro Nambari 4: Kasi ya Ukuaji wa Uchumi kwa nchi za Afrika Mashariki mwaka 2024 na 2025.**




| | Tanzania | Rwanda | Uganda | Kenya | Burundi | Sudani ya Kusini | Somalia | Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 2024 | 5.4 | 8.9 | 6.3 | 4.7 | 3.5 | -26.1 | 3.7 | 6.5 |
| 2025 | 5.9 | 7.0 | 6.7 | 4.9 | 3.9 | 46.1 | 3.8 | 5.7 |

*Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi Duniani (WEO)na Barani Afrika, (AfDB) 2026.*

#### 1.4.5 Nchi zenye Uhusiano wa Kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners)

Zanzibar ni moja ya nchi yenye kutegemea Uchumi wa Huduma (Service Oriented Economy), ambao fursa za ukuaji wa uchumi zinatokana na wigo wa shughuli za huduma, biashara za kimataifa (uingizaji na usafirshaji wa mazao ya biashara), uhaulishaji wa huduma zitokanazo na utalii na uhaulishaji wa fedha za kigeni kutoka kwa Wazawa wanaoishi nje ya nchi (Remittance). Uchambuzi wa fursa za kiuchumi na tathmini ya vihatarishi vyake, ni muhimu sana katika kubuni sera na mikakati ya kuimarisha ukuaji wa uchumi endelevu wenye ushindani baina ya nchi zenye uhusiano na Zanzibar kiuchumi na kibiashara. Kuimarika kwa uchumi kwa nchi za China, India, Jumuiaya ya Umoja wa Ulaya, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), India, na Uturuki ni muhimu sana katika kuimarisha wigo wa biashara za kimataifa na kuinua hali za wanachi kiuchumi na kijamii. Aidha, kuanguka kwa uchumi wa nchi hizi kunaweza kuathiri mwenendo wa uchumi wa Zanzibar ikizingatiwa kuwa Zanzibar hutegemea mitaji ya uwekezaji, biashara za kimataifa (uingizaji na usafirshaji wa mazao ya biashara).

**a) China**

Kwa mwaka 2025, kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi ya China ilifikia wastani wa asilimia 5.0 sawa na ukuaji kama huo kwa mwaka 2024. Ukuaji wa uchumi wa China umendelea kuimarika, hasa katika uwekezaji wa kimataifa katika masoko ya hisa na mitaji. Kwa upande wa biashara za kimataifa China imeendelea kujikita zaid katika soko la Afrika baada ya Makarekani kupandisha ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka katika nchi hiyo.

**b) India,**

Kwa mwaka 2025, kasi ya ukuaji wa uchumi imefikia wastani wa asilimia 7.6, kutoka wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2024, ukuaji huo umetokana na kuongezeka kwa uzalishaji viwandani hasa katika teknolojia ya mawasilino na vipuri vya kuendeshea mitambo viwandani pamoja kupungua kwa sekta zisizo rasmi hasa kwa viwanda vidogo vya uzalishaji bidhaa za nguo na chakula.

**c) Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E)**

Kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024. Kasi hii ya ukuaji wa uchumi imetokana

na kuongezeka kwa uzalishaji wa mafuta pamoja na kukua kwa tecknolojia na mawasiliano ambazo pia zimechochea ukuaji wa sekta ya huduma na uchumi wa kidigitali.

**d) Ukanda wa Nchi za Ulaya**

Kasi ya ukuaji uchumi imefikia wastani wa asilimia 1.4 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 0.8 mwaka 2025. Kuongezeka kwa kasi ya ukuaji wa uchumi katika eneo hili kumetokana na kurejea kwa fursa za ajira na biashara baina ya nchi wanachama wa Jumuiya hiyo, kupungua kwa bajeti ya kufadhili wakimbizi na vita kutoka Ukraine na kuongezeka kwa thamani ya usafirishaji wa bidhaa kwenda Marekani na China baada ya nchi hizo mbili (Marekani na China) kuwekeana zuio la ongezeko la ushuru wa forodha kutoka kila upande. Kuimarika kwa uchumi katika eneo hilo huongeza wigo wa wageni kuongeza safari za kutalii, ikizingatiwa kuwa kwa mwaka 2025, Zanzibar ilipokea jumla ya idadi ya watalii 611,892 kati ya 917,167 kutoka Bara la Ulaya sawa na asilimia 66.6. Ongezeko hilo limekwenda sambamba na kuongezeka kwa mapato ya fedha za kigeni kutokana na uhaulishaji wa huduma za kitalii *(Receipts from Service Export)* na shughuli zinazohusiana nazo.

**e) Uturuki**

Kwa mwaka 2025, kasi ya ukuaji uchumi kwa nchi ya Uturuki ilifikia wastani wa asilimia 3.2 kutoka wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2024. Kasi hii ya ukuaji wa uchumi ilitokana na mabadiliko ya sera za biashara za kimataifa zikiongozwa na Marekani na baadhi ya nchi zinazounda Jumuiya ya Ulaya, kuongezeka kwa biashara za uuzaji na ukodishaji majengo, kuwepo kwa sera za uthibiti wa fedha na utulivu wa bei za masoko ya fedha na mitaji.

## 1.5 Hali ya Mfumko wa Bei

### 1.5.1 Mfumko wa Bei wa Dunia

Kwa mwaka 2025, Kasi ya mfumko wa bei duniani imefikia wastani wa asilimia 4.1 kutoka wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2024. Kupungua kwa mfumko wa bei duniani kumetokana na mabadiliko ya biashara za kimataifa ambayo yameongeza upatikanaji wa bidhaa muhimu kama vile mbolea, vyakula, nishati za mafuta na kemikali zinazotumika viwandani. Aidha, utulivu wa bei za masoko ya fedha duniani sambamba na sera ya kupunguza

matumizi ya Dola ya Marekani kwa biashara za kimataifa kwa baadhi ya nchi kumepunguza gharama za uagiziaji wa bidhaa na huduma.


Kasi ya mfumko wa bei kwa Nchi **Zilizoendelea** imepungua kwa wastani wa asilimia 2.5 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 2.6 mwaka 2024.

Hii ni kutokana na Benki kuu ya Marekani (U.S. Federal Reserve) na Benki Kuu ya Ulaya (European Central Bank) kudhibiti mfumuko wa bei kwa Kuongeza viwango vya riba kuwa juu na kudhibiti kiwango cha fedha kwenye uchumi na kupelekea kupunguza matumizi kupita kiasi kwa ajili ya kupunguza kasi ya kupanda kwa bei. Nchi **Zinazoendelea na Zinazoibukia kiuchumi** zimefikia wastani wa asilimia 5.2 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 8.0 mwaka 2024. Hali hiyo imetokana na kupungua kwa uzalishaji wa nishati mbadala itokanayo na nafaka na mabaki ya kilimo (Biomass), na kusababisha kushuka kwa bei za masoko ya minada ya bidhaa ghafi duniani *(Commodity Auction Markets)* kama vile nafaka, mabaki ya kilimo na bidhaa nyenginezo zinazotumika kuzalisha nishati hiyo. ***(Mchoro nambari 5).***

### 1.5.2 Mfumko wa Bei kwa Nchi Zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara

Kasi ya mfumko wa bei katika ukanda wa nchi zilizo Kusini mwa Jangwa la Sahara imepungua na kufikia wastani wa asilimia 12.5 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 20.7 mwaka 2024. Kupungua kwa mfumko wa bei katika eneo hilo kumetokana na kuongezeka kwa shughuli za kilimo hasa mazao ya chakula baada nchi zilizokumbwa na madiliko ya tabia nchi ikiwemo mafuriko na ukame katika nchi za Malawi, Jamhuri ya Afrika ya kati, Chad na Mali. Aidha, kuimarika kwa miundombinu ya usafiri wa reli, barabara na bandari, inayounganisha kusini, mashariki na kati ya eneo hilo (*Lobito and East – Southern Corridors*), kumepunguza ghrama za usafirishaji mizigo na bei za bidhaa kwa ujumla.

**Mchoro Nambari 5: Kasi ya Mfumko wa Bei Duniani Mwaka (2021 - 2025)**




***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia (IMF), 2026.***

### 1.5.3 Mfumko wa bei wa nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki

Mfumko wa bei wa Jumuiya ya Afrika Mashariki unajumuisha Nchi nane (8) zikiwemo Tanzania, Kenya, Uganda, Burundi, Rwanda, Jamhuri ya Demokrasia ya Congo, Sudan ya Kusini na Somalia. Kwa mwaka 2025, mfumko wa bei wa Jumuiya hii umepungua na kufikia wastani wa asilimia 10.4, kutoka wastani wa asilimia 10.5 mwaka 2024. Hii imesababishwa na kupungua kwa gharama za uagiziaji wa bidhaa kutokana na kuimarika kwa miundombinu ya usafiri na ufanisi wa bandari tegemezi za Dar es salaam - Tanzania na Mombasa - Kenya. (***Mchoro nambari 6).***

#### (a) Tanzania

Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi ya Tanzania, imefikia asilimia 3.2 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024. Kushuka kwa kasi ya mfumko wa bei kulichangiwa na utulivu wa bei za nishati ya mafuta, utulivu wa sarafu ya Tanzania, kuongezeka kwa mazao ya chakula na viwanda vidogo na vya kati vya kusarifu mazao ya chakula pamoja na kuimarika ufanisi wa miundombinu ya usafirishaji na bandari.

#### (b) Kenya

Mwaka 2025, mfumko wa bei kwa nchi ya Kenya umefikia wastani wa asilimia 4.1 kutoka wastani wa asilimia 4.5 mwaka 2024. Kushuka kwa mfumko wa bei

kumetokana na kurejea kwa hali ya utulivu wa kisiasa, kurejea kwa biashara baina ya nchi wanachama, kuimarika kwa miundombinu ya usafirishaji ambayo imepelekea kupunguza gharama za usafirishaji wa bidhaa.

**(c) Uganda**

Mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 3.6 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024. Moja ya sababu za kupanda kwa mfumko wa bei nchini Uganda ni kutokana na kuongezeka kwa bei za usafiri wa ndani, kupungua kwa uzalishaji bidhaa viwandani na kuongezeka kwa bei za huduma muhimu (Utilities).

**(d) Rwanda**

Mwaka 2025, kasi ya mfumko wa bei nchini Rwanda, imeongezeka hadi kufikia wastani wa asilimia 7.0 kutoka wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2024. Hii imetokana na kupungua kwa uzalishaji wa ndani hasa mazao ya kilimo na kuongezeka kwa mahitaji ya bidhaa za chakula hasa katika maeneo ya karibu na mashiriki ya DRC baada ya kurejea kwa matishio ya vita.

**(e) Burundi**

Kwa nchi ya Burundi kasi ya mfumko wa bei imeongezeka kwa wastani wa asilimia 34.2 mwaka 2025, kutoka wastani wa asilimia 20.2 mwaka 2024. Kupanda zaidi kwa mfumko wa bei nchini Burundi kumetokana na kuyumba kwa sarafu ya nchi hiyo na kuongezeka kwa bei za huduma za msingi kama vile maji na umeme na kuongezeka kwa gharama za uzalishaji viwandani na pembejeo za kilimo.

**(f) Sudani ya Kusini**

Mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 97.8 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 99.8 mwaka 2024. Hali hii imetokana na kurejea kwa uthibiti wa miundombinu ya kusafirishia mafuta, kuongezeka kwa shughuli za biashara, ufugaji na ujasiriamali.

**(g) Jamhuri ya Demokrasia ya Congo**


Mfumo wa bei wa nchi ya Congo, umepungua na kufikia wastani wa asilimia 7.4 kutoka wastani wa asilimia 17.7 mwaka 2024. Kushuka kwa mfumko

wa bei katika nchi hiyo kumetokana na kuimarika kwa sarafu ya nchi hiyo, kupungua kwa gharama za uagiziaji wa bidhaa baada ya ufanisi wa bandari tegemezi kupitia nchi jirani ya Tanzania.

### (h) Somalia

Mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 4.8 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2024. Kupungua kwa kasi ya mfumko wa bei kwa nchi ya Somalia kumetokana na kushuka kwa bei za chakula na zisizo za chakula baada ya kupungua kwa machafuko ya kivita na hali ya ukame katika miaka ya hivi karibuni na kupelekea kuimarika kwa shughuli za kilimo cha mazao ya chakula na ufugaji.

**Mchoro Nambari 6: Kasi ya Mfumko wa Bei kwa Nchi za Jumuiya ya Afrika Mashariki (2024-2025)**




*Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia (IMF) na Afrika, (AfDB), 2026*

### 1.5.4 Mfumko wa bei kwa Nchi zenye Uhusiano wa Kibiashara na Zanzibar (Zanzibar Trading Partners)

Zanzibar ni moja ya nchi yenye kutegemea zaidi Uchumi wa Huduma (Service Oriented Economy), ambao fursa za ukuaji wa uchumi zinatokana na shughuli za huduma. Uchambuzi wa fursa za kiuchumi na tathmini ya vihatarishi vyake baina ya nchi zenye uhusiano na Zanzibar ni muhimu sana katika kubuni sera na mikakati ya kuthibiti mfumko wa bei.

Kupanda au kushuka kwa mfumko wa bei kwa nchi za China, India, Jumuiya ya Umoja wa Ulaya, Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE), India, na Uturuki kunapunguza au kuongeza gharama za uagiziaji wa bidhaa zinazotoka katika nchi hizo hali inayoathiri mwenendo wa mfumko wa bei hasa kwa bidhaa muhimu za chakula, na zisizo za chakula, dawa, na pembejeo za kilimo, hapa nchini. Aidha, kwa upande wa huduma kupanda au kushuka kwa mfumko wa bei kunaweza kupandisha au kushusha gharama za huduma za kitalii *(Zanzibar Tourism Destination Cost)* ikilinganishwa na nchi nyegine zenye kutegemea uchumi wa huduma. Katika mwaka 2025, hali ya mfumko wa bei kwa nchi washirika wa kibiashara iliripotiwa kama ifuatavyo:

**(a) China**

Mfumko wa bei kwa nchi ya china imefikia wastani wa asilimia 0.2 mwaka 2025 sawa na mwaka uliopita wa 2024. Hii ni kutokana na kuimarika kwa sera ya udhibiti wa sarafu ya China wenye lengo la kuongeza wigo wa biashara za kimataifa. Zanzibar huagiza bidhaa za nguo, dawa, vifaa vya kieletroniki, mashine za uzalishaji viwandani, na vifaa vya ujenzi.

**(b) Jumuiya ya Nchi za Falme za Kiarabu (U.A.E)**

Kasi ya mfumko wa bei kwa nchi za UAE imepanda na kufikia wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024. Hii imetokana na kuongezeka kwa bei za bidhaa zisizo za chakula, vifaa vya kieletroniki, kodi za majengo, pamba na nguo.

**(c) India**

Kwa mwaka 2025, kasi ya mfumko wa bei imepungua na kufikia wastani wa asilimia 2.1 kutoka wastani wa asilimia 4.6 mwaka 2024. Kupungua kwa mfumko wa bei kumetokana na kuimarika kwa sarafu yao kutokana na usafirishaji wa bidhaa za viwandani, kushuka kwa bei za vyakula hasa vyakula vya nafaka kama mchele, ngano, adesi na mbaazi pamoja na kupungua kwa mahitaji ya bidhaa za nafaka katika kuzalishia nishati ya umeme (Biomass), katika soko la dunia.

**(d) Ukanda wa nchi za Ulaya (Euro Zone)**

Kwa mwaka 2025, kasi ya mfumko wa bei imepungua na kufikia wastani wa asilimia 2.1 kutoka wastani wa asilimia 2.4 mwaka 2024. Kupungua kwa

mfumko wa bei kumetokana na kushuka kwa bei za chakula na zisizo na chakula na kushuka kwa bei ya nishati ya gesi.

**(e) Thailand**

Kwa mwaka 2025, kasi ya mfumko wa bei imepungua na kufikia wastani wa asilimia 0.1 kutoka wastani wa asilimia 0.4 mwaka 2024. Kupungua kwa mfumko wa bei kumetokana na kushuka kwa bei za bidhaa za chakula na bidhaa za kilimo. Zanzibar huagiza bidhaa muhimu za mchele, (*Thailand rice/ Mapembe)*, nguo na vyombo vya usafiri. Kufuatilia kwa karibu mwenendo wa mfumko wa bei wa Thailand kumesaidia serikali kudhibiti bei za bidhaa za chakula zinazoingizwa hapa nchini *(Food Price Ceiling)*.

**(f) Uturuki**

Kwa mwaka 2025, kasi ya mfumko wa bei imepungua na kufikia wastani wa asilimia 34.9 kutoka wastani wa asilimia 58.5 mwaka 2024. Kupungua kwa mfumko wa bei kwa nchi ya Uturuki kumetokana na kushuka kwa bei za bidhaa za chakula na huduma za msingi kama umeme na gesi pamoja na kuendeleza sera za udhibiti wa sarafu yao (Lira). Zanzibar huagiza bidhaa nyingi kutoka nchi hiyo zikiwemo nguo, mashine za uzalishaji viwandani, vifaa tiba, dawa za binadamu na huduma za kitabibu na matibabu.

**Jadweli Namba 3: Mfumko wa Bei kwa Nchi zenye Uhusiano wa Karibu wa Kibiashara na Zanzibar (Trading Partners) 2024 na 2025.**

| Nchi zenye Uhusiano Zaidi wa Kibiashara na Zanzibar | 2024 | 2025 |
|---|---|---|
| India | 4.6 | 2.1 |
| Umoja wa Falme za Kiarabu (UAE) | 4.0 | 5.8 |
| China | 0.2 | 0.2 |
| Ukanda wa Nchi za Ulaya (Euro zone) | 2.1 | 2.4 |
| Thailand | 0.4 | -0.1 |
| Uturuki | 58.5 | 38.9 |

***Chanzo: Ripoti ya Mtazamo wa Uchumi wa Dunia, 2026***

### 1.5.5 Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya bidhaa katika Soko la Dunia

Kuweka mikakati na sera ya kudhibiti mfumko wa bei ili kunusuru upandaji wa bei za bidhaa zinazoagizwa kuja katika soko la ndani ni moja ya juhudi za Serikali za kuleta maendeleo kwa wananchi wake sambamba na kuhakikisha wananchi wa vipato vya chini wanamudu gharama za maisha. Katika

kufanikisha hilo, Serikali inaendelea kufatilia kwa karibu mwenendo wa bei za bidhaa muhimu katika soko la dunia kwa lengo la kudhibiti mfumko wa bei hasa kwa bidhaa muhimu hapa nchini.

Moja ya hatua hizo ni kutokana na misamaha nafuu ya ushuru wa forodha kwa bei za vyakula vinavyoagizwa na wafanyabiashara hapa nchini ikiwa kama sera ya kudhibiti athari za kupanda kwa bei za bidhaa hizo katika soko la dunia. Kwa mwaka 2025, bei za bidhaa zenye matumizi makubwa zinazoagizwa hapa nchini kwa mujibu wa takwimu za bei katika soko la dunia ni kama ifuatavyo:

**i. Nishati ya Mafuta**

Bei ya nishati ya mafuta kwa mwaka 2025, ilifikia wastani wa Dola za Kimarekani 67.4 kwa pipa kutoka Dola za Kimarekani 78.7 kwa pipa mwaka 2024. Sawa na punguzo la asilimia 14.4. katika kipindi hicho bei za mafuta duniani zimeonekana kushuka kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hizo hasa kwa nchi zisizo mwanachama wa OPEC, kuongezeka kwa matumizi ya nishati mbadala hasa nishati za nguvu ya jua na gesi na mabadiliko ya sera za biashara za kimataifa.

**ii. Mchele**

Kwa mwaka 2025, bei ya mchele, imeshuka kufikia Dola za Kimarekani 407.8 kwa tani ikilinganishwa na Dola za Kimarekani 588.4 kwa tani mwaka 2024. Sawa na punguzo la asilimia 30.7. Hii ni kutokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa bidhaa hiyo katika nchi zinazozalisha mchele kwa wingi, zikiwemo Thailand, Vietnam na India na kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa hiyo kwenda soko la Marekani na baadhi ya nchi za ulaya kutokana na zuio la ongezeko la ushuru wa forodha kwa bidhaa zinazoingizwa kutoka nchi hizo.

**iii. Unga wa Ngano**

Kwa mwaka 2025, bei ya unga wa ngano katika soko la dunia ilishuka na kufikia wastani wa Dola za Kimarekani 219.6 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 230.8 kwa tani mwaka 2024. Sawa na upungufu wa asilimia 4.9. Hii ni kutokana kupungua kwa gharama za uzalishaji na usambazaji, baada ya baadhi ya nchi wanachama wa BRICS, kama Urusi, Brazil na China kufanya biashara za kimataifa kwa makubaliano ya sarafu zao.

### iv. Sukari

Kwa mwaka 2025, bei ya sukari katika soko la dunia imepungua na kufikia wastani wa Dola za kimarekani 370.0 kwa tani ikilinganishwa na wastani wa Dola za Kimarekani 450.0 kwa tani mwaka 2024, sawa na punguzo la asilimia 17.1. Kupungua kwa bei ya sukari katika soko la dunia kumetokana na kuongezeka kwa uzalishaji wa sukari katika nchi za Brazil na India ambao ni wazalishaji wakuu duniani pamoja na kupungua kwa usafirishaji wa bidhaa hiyo kwenda soko la Marekani kutokana ongezeko la ushuru wa forodha ***(Jadweli nambari 4):***

**Jadweli nambari 4: Mwenendo wa Bei kwa baadhi ya Bidhaa katika Soko la Dunia**

| BIDHAA | KIPIMO | 2024 Bei kwa (USD) | 2025 Bei kwa (USD) | TOFAUTI Aslimia (%) |
|---|---|---|---|---|
| Mchele | Tani | 588.4 | 407.8 | -30.69 |
| Unga wa Ngano | Tani | 230.8 | 219.6 | -4.85 |
| Sukari | Tani | 450.0 | 370.0 | -17.78 |
| Nishati ya Mafuta | Pipa | 78.7 | 67.4 | -14.36 |

***Chanzo: Takwimu za Bidhaa za Dunia, 2026.***

***Tanbihi; Takwimu hizi zinaonyesha hali halisi ya bei za bidhaa muhimu kwa mwaka 2025 katika soko la dunia.***


## SURA YA PILI

## 2.0 HALI YA UCHUMI WA ZANZIBAR

### 2.1 Pato la Taifa na Ukuaji wa Uchumi

Kwa mwaka 2025 uchumi wa Zanzibar umeendelea kuimarika ambapo kwa mujibu wa viashiria vya kiuchumi, Pato Halisi la Taifa (GDP at Constant Price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 4,307.9 bilioni kutoka thamani ya TZS 4,026.4 bilioni mwaka 2024 sawa na kasi ya ukuaji wa asilimia 7.0 kwa mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 7.1 kwa mwaka 2024. Aidha, pato la Taifa kwa bei ya soko (GDP at Current Price) limeongezeka na kufikia thamani ya TZS 7,029.9 bilioni kutoka thamani ya TZS 6,572.6 bilioni mwaka 2024. ***(Mchoro nambari 7)***

**Mchoro Nambari 7: Kasi ya Ukuaji wa Uchumi mwaka (2021-2025)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2026***

Kuongezeka kwa Pato la Taifa na kuimarika kwa hali ya ukuaji wa uchumi kumetokana na sababu zifuatazo:-

i. Kuimarika kwa sekta ya Kodi za bidhaa, ambapo kwa mwaka 2025 imekuwa kwa wastani wa asilimia 12.8 kutoka wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2024,

ii. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii nchini wapatao 917,167 mwaka 2025 kutoka watalii 736,755 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 24.5 na

iii. Kuongezeka kwa miradi mipya ya uwekezaji kwa asilimia 3.8 kufikia miradi 136 yenye thamani ya TZS 1,894,078 milioni iliyosajiliwa mwaka 2025 kutoka miradi 131 yenye thamani ya TZS 1,877,760 milioni iliyosajiliwa mwaka 2024.

iv. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia TZS 1,615.8 bilioni Julai-Machi mwaka 2025/26 ikilinganishwa na jumla ya TZS 1,299.0 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 24.3

Miongoni mwa sababu zilizopelekea kupungua kwa kasi ya ukuaji wa uchumi mwaka 2025 ikilinganishwa na mwaka 2024 ni kutokana na:

i. Kupungua kwa mchango wa sekta ya kilimo ambayo inajumuisha sekta ndogo ya Mazao, Ufugaji, Misitu na Uvuvi kufikia asilimia 23.5 mwaka 2025 kutoka asilimia 24.3 mwaka 2024


ii. Kupungua kwa ukuaji wa sekta ya viwanda ambayo inajumuisha sekta ndogo ya uchimbaji mawe na mchanga, Ujenzi, Umeme na Gesi, Utengenezaji wa Bidhaa za Viwandani na shughuli za Usambazaji Maji na Maji taka kufikia asilimia 19.3 mwaka 2025 kutoka asilimia 20.2 mwaka 2024.

## 2.2 Pato la Mwananchi

Kuongezeka kwa Pato la Taifa kumepelekea kuongezeka kwa kipato cha Mwananchi. Kwa mwaka 2025 Pato la Mwananchi Zanzibar limeongezeka

na kufikia TZS 3.3 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,320 kutoka TZS 3.2 milioni sawa na Dola za Kimarekani 1,243 mwaka 2024. Zanzibar inakadiriwa kufikia idadi ya watu 2,099.0 milioni ambapo kasi ya ongezeko la idadi ya watu limefikia wastani wa asilimia 3.7 ***(Mchoro nambari 8)***.

**Mchoro Nambari 8: Idadi ya Watu Pamoja na Pato la Mwananchi kwa Thamani ya (TZS) na (USD) (2021 - 2025)**





***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2026***

## 2.3 Mwenendo wa Mfumko wa Bei Zanzibar

Kasi ya mfumko wa bei kwa mwaka 2025 imepungua na kufikia wastani wa asilimia 4.1 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.1 mwaka 2024. Upungufu huo umesababishwa na kupungua kwa bei za bidhaa za chakula ambapo mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 5.0 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 8.4 mwaka 2024. Aidha, kwa upande wa bidhaa zisizo za chakula kwa mwaka 2025 mfumko wa bei umefikia wastani wa asilimia 3.4 ukilinganisha na wastani wa asilimia 2.7 mwaka 2024, (Mchoro nambari 9).

**Mchoro Nambari 9: Kasi ya Mfumko wa Bei wa Zanzibar (2021-2025)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2026***

Serikali inaendelea kuchukua hatua za kupunguza na kudhibiti kasi ya mfumko wa bei na kuhakikisha upatikanaji wa huduma na bidhaa muhimu kwa wananchi. Hatua zilizochukuliwa ni kama ifuatavyo:-

i. Kupunguza ushuru na misamaha ya kodi kwa bidhaa muhimu za chakula na zisizo za chakula zinazoingizwa nchini;

ii. Kuendelea kutoa bei elekezi na kusimamia baadhi ya bidhaa za chakula zinazoingia nchini zikiwemo mchele, sukari na vifaa vya ujenzi;

iii. Kupitia Benki Kuu ya Tanzania (BoT) inaendelea kufuatilia na kuchukua hatua za kudhibiti, kushuka kwa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine duniani;

iv. Kuimarisha ufanisi wa Bandari ya Malindi kwa ununuzi wa vifaa vya kisasa kwa ajili ya kupunguza muda wa kutoa mizigo bandarini;

v. Serikali kuimarisha maghala na mifumo ya uhifadhi wa chakula ili kuwa na uhakika wa chakula nchini *(Food Security)* sambamba na kuendelea kutoa na kusimamia utoaji wa ruzuku kwa pembejeo za kilimo ili kuengeza uzalishaji wa mazao ya chakula;


## 2.4 Mwenendo wa Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola ya Kimarekani.

Mwenendo wa thamani ya sarafu ya Tanzania dhidi ya sarafu nyengine Duniani ni muhimu kutokana na mauzo na ununuzi wa bidhaa nje ya nchi. Kwa mwaka 2025 Fedha ya Tanzania ilibadilishwa kwa wastani wa TZS 2,538 kwa Dola moja ya kimarekani ikilinganishwa na wastani wa TZS 2,597.0 kwa mwaka 2024. Sawa na ongezeko la thamani kwa wastani wa asilimia 2.2 Benki Kuu ya Tanzania inaendelea kuchukua hatua madhubuti za kudhibiti Sarafu ya Tanzania katika hali ya utulivu kwa kuongeza mzunguko wa fedha (Money circulation), kupitia usafirishaji wa madini ya dhahabu na bidhaa za chakula.

### Akiba ya Fedha za Kigeni

Fedha za kigeni zinaendelea kuhifadhiwa (Foreign reserve) ili kukidhi mahitaji ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi. Katika kipindi cha mwaka 2024/25, kiwango cha akiba ya fedha za kigeni ilifikia dola za Marekani 6.2 bilioni ikilinganishwa na dola za Marekani 5.3 bilioni kipindi kama hicho mwaka 2023/2024. Kiasi hicho kinatosheleza malipo ya uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi cha miezi minne. Kiasi hicho ni zaidi ya lengo la nchi la kuwa na akiba ya fedha za kigeni inayokidhi uagizaji wa bidhaa na huduma kutoka nje kwa miezi isiyopungua minne.

**Mchoro Nambari 10: Thamani ya Shilingi ya Tanzania dhidi ya Dola moja ya Kimarekani (2021-2025)**




***Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania, 2026***

## 2.5 Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar

Serikali inaendelea kuimarisha sekta ya utalii ikiwa ni kiongozi kwa uchumi wa Zanzibar inayochangia zaidi ya asilimia 30 ya Pato la Taifa. Kwa mwaka 2025 idadi ya watalii imeongezeka kwa asilimia 24.5 kufikia watalii 917,167 ikilinganishwa na watalii 736,755 waliorikodiwa mwaka 2024. Ongezeko hili limepelekea kuongezeka kwa thamani ya mauzo yatokanayo na uhaulishaji wa huduma (Receipts from Service Account) yenye jumla ya Dola za kimarekani 1,409.4 milioni kwa mwaka ulioishia Disemba 2025, kutoka dola za kimarekani 1,126.4 milioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 25.1 na kuongezeka kwa wastani wa siku za kutalii (Average days of stay) kufikia siku 7 kutoka siku 6 mwaka 2024. Jitihada zilizochukuliwa na Serikali pamoja na Sekta Binafsi ni:

i. Kuitangaza Zanzibar kimataifa kupitia ziara za Viongozi Wakuu na wanadiplomasia;

ii. Kuongezeka kwa mawakala wa usafirishaji wa watalii mfano (kampuni ya Tui, Fisherman Tour and Travel Agency);

iii. Kuimarika kwa uwekezaji Nchini, kuimarika kwa masoko ya utalii Duniani;


iv. Kuimarika kwa miundombinu ya usafirshaji, kuimarika kwa huduma za Kitalii nchini zikiwemo hoteli za Nyota tano sambamba na huduma zinazotolewa;

v. Kuendelea kushiriki katika makongamano ya kibiashara na uwekezaji katika mataifa mbali mbali duniani; na

vi. Kuhamasisha masoko mapya ya utalii na kuleta ndege za moja kwa moja (*Direct Flights)* kuja Zanzibar; na

vii. Kuendelea kuimarika kwa hali ya amani na utulivu nchini.

**Mchoro Nambari 11: Mwenendo wa Uingiaji wa Watalii Zanzibar (2021-2025)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2026.***

Nchi ambazo zimeongoza kwa kuleta watalii wengi mwaka 2025 ni Itali watalii 104,265 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 11.4, Ufaransa watalii 71,268 sawa na ongezeko la asilimia 7.8, Ujerumani watalii 70,619 sawa na ongezeko la asilimia 7.7, Poland watalii 55,678 sawa na ongezeko la wastani wa asilimia 6.1. Uingereza watalii 53,309 sawa na ongezeko la asilimia 5.8 na nchi nyengine za Afrika watalii 73,328 sawa na ongezeko la asilimia 8.0


## 2.6 Ukuaji wa Sekta katika Pato la Taifa

### 2.6.1 Sekta ya Huduma

Sekta ya Huduma inajumuisha sekta ndogo za Elimu, Chakula na Vinywaji, Afya, Mawasiliano, Malazi, Sanaa, Burudani na Ubunifu, na nyenginezo. Sekta hii ni miongoni mwa sekta muhimu katika kuimarisha Uchumi wa Zanzibar. Sekta ya Huduma imekua na kufikia wastani wa asilimia 7.9 mwaka 2025 ikilinganishwa na ukuaji wa wastani wa asilimia 9.0 mwaka 2024. Ukuaji huo mdogo umesababishwa na kushuka kwa ukuaji wa sekta ndogo ya Huduma ya Chakula na Vinywaji, ambapo kwa mwaka 2025 ukuaji wa sekta hiyo umefikia wastani wa asilimia 13.4 kutoka wastani wa asilimia 16.3

mwaka 2024. Sekta ndogo ya Malazi na Chakula imekua na kufikia wastani wa asilimia 11.8 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia13.7 mwaka 2024, sekta ndogo ya Malazi imekua na kufikia wastani wa asilimia 11.5 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 13.2 mwaka 2024. Sekta ndogo ya Huduma na Fedha kwa mwaka 2025 imekua na kufikia wastani wa asilimia 13.2 kutoka wastani wa asilimia 13.7 mwaka 2024, sekta ndogo ya biashara na ukarabati imekuwa na kufikia wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 11.6 mwaka 2024, sekta ndogo ya Ustawi wa Afya ya Jamii kwa mwaka 2025 imekua na kufika wastani wa asilimia 4.9 kutoka wastani wa asilimia 8.2 mwaka 2024, sekta ndogo ya Elimu imekua kwa ukuaji mdogo na kufikia wastani wa asilimia 6.7 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 7.0, sekta ndogo ya Mali zisizohamishika *(Real Estate Activities)* kwa mwaka 2025 imekua na kufikia wastani wa asilimia 1.4 kutoka wastani wa asilimia 7.3 mwaka 2024. Aidha, sekta ndogo ya Taaluma ya Sayansi na Ufundi kwa mwaka 2025 imekua kwa wastani wa asilimia 3.9 kutoka wastani wa asilimia 6.6 mwaka 2024. ***(Mchoro Namba 12.).***

**Mchoro Namba 12 : Ukuaji wa Sekta ya Huduma katika Pato la Taifa (2021-2025)**




***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, 2026.***

Kwa upande wa sekta zilizoonesha ukuaji mzuri kwa mwaka 2025, sekta ndogo ya usafirishaji na Uhifadhi kwa mwaka 2025 imekua na kufikia wastani wa asilimia 5.0 kutoka wastani wa asilimia 0.0 mwaka 2024, sekta ndogo ya Huduma ya Utawala imekua na kufikia wastani wa asilimia 8.1 mwaka 2025 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 5.9 mwaka 2024.

Sekta ndogo ya Habari na Mawasiliano kwa mwaka 2025 imekua na kufikia wastani wa asilimia 8.8 kutoka wastani wa asilimia 4.9 mwaka 2024, hii imetokana na upanuzi wa miundo mbinu ya mawasiliano visiwani,ukuaji wa huduma za kifedha kidijitali ,kuimarika kwa huduma za Serikali Mtandao (e-Government) na ukuaji wa utalii unaotegemea teknolojia. sekta ndogo ya Utawala wa Umma kwa mwaka 2025 imekua na kufikia wastani wa asilimia 4.4 kutoka wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2024,

Sekta ndogo ya Sanaa, Burudani na Ubunifu imekua na kufikia wastani wa asilimia 9.7 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 8.5 mwaka 2024 ukuaji huo umetokana na kuwepo kwa mafunzo na mikutano ya kuhamasisha nafasi ya sanaa katika maendeleo ya Taifa, kuwepo kwa matumizi ya Tehama katika shughuli za Baraza la Sanaa kulikopelekea udhibiti mzuri wa kazi za sanaa, matumizi mazuri ya mitandao ya jamii, kuimarisha mashirikiano ya kitaasisi katika kazi za kila siku za Baraza la Sanaa, kuwepo kwa ziara za ukaguzi katka maeneo ya Taasisi mbali mbali za sanaa na uwelewa mzuri wa elimu na nafasi ya sanaa katika jamii.

### 2.6.2 Sekta ya Viwanda


Sekta ya Viwanda imejumuisha sekta ndogo ya Uzalishaji Viwandani, Ujenzi, Uchimbaji Mawe na Mchanga, Umeme na Gesi, na nyenginezo. Mwaka 2025, sekta ya Viwanda imekua kwa kasi ndogo na kufikia wastani wa asilimia 3.2 kutoka wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2024. Upungufu huu mdogo umetokana na kupungua kwa sekta ndogo ya Umeme na Gesi, ambapo kwa mwaka 2025 , sekta hiyo imekua na kufikia wastani wa asilimia 8.5 kutoka wastani wa asilimia 11.2 mwaka 2024.

Sekta ndogo ya Uchimbaji Mawe na Mchanga, imekua na kufikia wastani wa asilimia 4.0 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 17.0 mwaka 2024, sekta ndogo ya Usambazaji Maji Safi na Maji Taka kwa mwaka 2025 imekua kwa wastani wa asilimia 2.9 kutoka wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2024, sekta ndogo ya Ujenzi, kwa mwaka 2025 imekua na kufikia wastani wa asilimia 0.4 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 6.3 mwaka 2024.

Sekta iliyoonesha ukuaji mzuri kwa mwaka 2025 ni sekta ndogo ya Uzalishaji Viwandani, kwa mwaka 2025, sekta hii imekua kwa wastani wa asilimia 5.4

kutoka wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024. Hali hii imetokana na kuanza kwa uzalishaji kwa baadhi ya viwanda vipya vikiwemo vya nguo *(MAMA AFRICA TEXTILE*), kiwanda cha Maji cha (Ikram Water), kuongezeka kwa uzalishaji wa kiwanda cha (Drop na Zainab bottler) na kuongezeka kwa uzalishaji kwa kiwanda Unga cha Bakhresa. ***(Mchoro namba. 13):***

**Mchoro Nam 13 : Ukuaji wa Sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa (2021-2025)**




| | Umeme na gesi | Ujenzi | mchanga | Uzalisi viwanc |
|---|---|---|---|---|
| 2021 | 8 | 8.9 | 9.9 | 1.1 |
| 2022 | 22.3 | 10.2 | 9.1 | 8.1 |
| 2023 | 12.4 | 5.5 | 10.4 | 6.9 |
| 2024 | 11.2 | 6.3 | 17 | 3.3 |
| 2025 | 8.5 | 0.4 | 4 | 5.4 |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali, 2026.***

### 2.6.3 Sekta ya Kilimo

Sekta ya Kilimo inajumuisha sekta ndogo za Misitu, Ufugaji, Uvuvi na Mazao. Sekta hii ni muhimu kwa Uchumi wa Zanzibar na ndio tegemeo kubwa la upatikanaji wa chakula nchini. Kwa mwaka 2025, sekta ya Kilimo imekua kwa kasi na kufikia wastani wa asilimia 5.4 kutoka wastani wa asilimia 3.3 mwaka 2024. Ukuaji huo umetokana na kukua kwa sekta ndogo ya Ufugaji, kwa mwaka 2025 sekta hii imekua na kufikia wastani wa asilimia 4.9 kutoka wastani wa asilimia hasi 10.8 mwaka 2024.

Sekta ndogo ya Uvuvi kwa mwaka 2025 imekua kwa kasi ndogo na kufikia wastani wa asilimia 5.7 kutoka wastani wa asilimia 14.2 mwaka 2024 jambo linaloonesha kuwa sekta inaendelea kukua lakini si kwa kasi kama ilivyokua

awali, hali hii inaonesha umuhimu wa kuimarisha uwezeshaji, miundo mbinu na sera ili kuongeza tija na kasi ya ukuaji wa sekta.

Sekta ndogo ya Mazao kwa mwaka 2025 ukuaji wake umekua kwa wastani wa asilimia 6.4 kama ilivyokua kwa mwaka 2024 na sekta ndogo ya Misitu kwa mwaka 2025 imekuwa kwa wastani wa asilimia 0.1 kama ilivyokua kwa mwaka 2024.

## 2.7 Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa

### 2.7.1 Sekta ya huduma

Sekta ya huduma ina mchango mkubwa zaidi katika kukuza Uchumi wa Zanzibar. Mchango wa sekta ya huduma katika Pato la Taifa umeongezeka na kufikia wastani wa asilimia 48.1 mwaka 2025 kutoka asilimia 46.8 mwaka 2024. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa sekta ndogo ya Huduma ya chakula na Malazi ambayo imechangia kwa wastani wa asilimia 17.5 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 16.9 mwaka 2024. Sekta ndogo ya malazi imechangia wastani wa asilimia 14.3 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 13.9 mwaka 2024, sekta ndogo ya biashara na ukarabati kwa mwaka 2025 imechangia wastani wa asilimia 6.5 kutoka wastani wa asilimia 6.1 mwaka 2024, sekta ndogo ya huduma ya Chakula na Vinywaji imechangia kwa wastani wa asilimia 3.2 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 3.0 mwaka 2024, sekta ndogo ya bima na Fedha kwa mwaka 2025 imechangia wastani wa asilimia 6.0 kutoka wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2024.

Hata hivyo, sekta ambayo mchango wake umepungua ni sekta ndogo ya Utawala kwa mwaka 2025 sekta hii imechangia kwa wastani wa asilimia 4.3 kutoka wastani wa asilimia 4.4 mwaka 2024.


### 2.7.2 Sekta ya Viwanda

Kwa mwaka 2025 mchango wa sekta ya Viwanda katika Pato la Taifa umefikia wastani wa asilimia 19.3 kutoka wastani wa asilimia 20.2 mwaka 2024. Sekta ndogo ambazo mchango umepungua ni sekta ndogo ya Ujenzi , kwa mwaka 2025 sekta hii imechangia kwa wastani wa asilimia 9.5 kutoka wastani asilimia 10.0 mwaka 2024, hii imetokana na miradi mingi kusimama kwa utekelezaji wake na miradi mengine kutokuanza kabisa. Sekta ndogo ya Uzalishaji viwandani imechangia wastani wa asilimia 7.4 mwaka 2025

kutoka wastani wa asilimia 7.8 mwaka 2024, hii ni kutokana na kiwanda cha Basra kusitisha uzalishaji katika mwaka mzima uliopita na kupungua kwa kiwango cha uzalishaji katiaka kiwanda cha sukari.

Hata hivyo sekta ndogo ya Uchimbaji Mawe na Mchanga kwa mwaka 2025 imechangia kwa wastani wa asilimia 0.8 kama ilivyochangia mwaka 2024, sekta ndogo ya Usambazaji Maji Safi na Maji Taka kwa mwaka 2025 imechangia kwa wastani wa asilimia 0.5 kama ilivyochangia mwaka 2024 na sekta ndogo ya umeme na gesi imechangia kwa wastani wa asilimia 1.0 kama ilivyochangia mwaka 2024. ***(Mchoro nambari 14.)***

**Mchoro Namba 14: Mchango wa Sekta katika Pato la Taifa (2021-2025)**




***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2026.***

### 2.7.3 Sekta ya Kilimo

Kwa mwaka 2025 mchango wa sekta ya kilimo umepungua na kufikia wastani wa asilimia 23.5 ikilinganishwa na wastani wa asilimia 24.3 mwaka 2024. Mchango huu umetokana na kupungua kwa sekta ndogo ya Ufugaji ambayo imechangia kwa wastani wa asilimia 10.0 mwaka 2025 kutoka wastani wa

asilimia 10.5 mwaka 2024, sekta ndogo ya Mazao imechangia wastani wa asilimia 6.5 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 6.8 mwaka 2024.

Sekta ndogo ya Uvuvi imechangia wastani wa asilimia 5.8 mwaka 2025 kutoka wastani wa asilimia 5.7 mwaka 2024.Hii inaonesha kuwa sekta inaendelea kuwa thabiti na yenye nafasi muhimu katika Uchumi wa Zanzibar. Na sekta ndogo ya Misitu kwa mwaka 2025 imechangia kwa wastani wa asilimia 1.2 kama ilivyochangia mwaka 2024.

#### 2.7.3.1 Sekta ndogo ya Mazao

Sekta hii imejumuisha Uzalishaji wa mazao ya Chakula na mazao ya Biashara. Kwa upande wa uzalishaji wa mazao ya Chakula kwa mwaka 2025 ni kama ifuatavyo:-

**(a) Zao la Mpunga.**

Kwa upande wa Zanzibar kuna njia mbili za uzalishaji wa zao la Mpunga. Mpunga unaotegemea umwagiliaji maji na njia ya kutegemea mvua. Kwa mwaka 2025, kilimo cha mpunga kwa njia ya kutegemea mvua uzalishaji wake umeongezeka na kufikia tani 33,327.90 zenye thamani ya TZS 39,108.90 milioni kutoka tani 29,767.50 zenye thamani ya TZS 32,463.70 milioni mwaka 2024. Hali hii imetokana na kuongezeka kwa eneo la uzalishaji na kuongezeka kwa tija ya uzalishaji kwa eneo.

Pia eneo la uzalishaji wa mpunga wa kutegemea mvua limeongezeka na kufikia ekari 25,170.40 mwaka 2025 kutoka ekari 24,565.40 mwaka 2024.

Kwa upande wa zao la mpunga kwa njia ya umwagiliaji maji, uzalishaji umeongezeka na kufikia tani 12,682.40 zenye thamani ya TZS 18,360.60 milioni mwaka 2025 kutoka tani 11,634.50 zenye thamani ya TZS 15,653.80 milioni mwaka 2024. Hii imetokana na kuongezeka kwa tija ya uzalishaji kwa eneo.

Eneo la uzalishaji wa mpunga wa njia ya umwagiliaji maji limepungua na kufikia ekari 4,976 mwaka 2025 kutoka ekari 5,750 mwaka 2024. Upungufu huo umesababishwa na kubadilisha matumizi ya mashamba ya uzalishaji wa zao la mpunga na kuzalisha mazao ya mboga mboga.

### (b) Zao la Muhogo

Kwa mwaka 2025 uzalishaji wa zao la muhogo umeongezeka na kufikia tani 179,125.60 zenye thamani ya TZS 156,969.50 milioni ikilinganishwa na tani 117,871.70 zenye thamani ya TZS 95,996.40 milioni mwaka 2024. Aidha, eneo la uzalishaji limeongezeka na kufikia ekari 30,515.43 mwaka 2025 kutoka ekari 20,080.40 mwaka 2024.

### (c) Zao la Ndizi

Kwa mwaka 2025 uzalishaji wa ndizi umeongezeka na kufikia tani 74,204.90 zenye thamani ya TZS 114,869.50 milioni kutoka tani 62,808.30 zenye thamani ya TZS 90,360.10 milioni mwaka 2024. Eneo la uzalishaji limeongezeka na kufikia ekari 8,628.48 mwaka 2025 kutoka ekari 7,303.30 mwaka 2024.

### (d) Zao la Viazi Vikuu

Kwa mwaka 2025 uzalishaji wa zao la viazi vikuu limeongezeka na kufikia tani 15,985.30 zenye thamani yz TZS 20,480.80 milioni kutoka tani 14,293.40 zenye thamani ya TZS 17,019.60 milioni mwaka 2024. Eneo la uzalishaji limeongezeka na kufikia ekari 3,197.06 mwaka 2025 kutoka ekari 2,876.70 mwaka 2024.

### (e) Zao la Njugu Nyasa

Kwa mwaka 2025 uzalishaji wa zao la njugu nyasa umeongezeka na kufikia tani 610.1 zenye thamani ya TZS 1,508.20 milioni kutoka tani 519.4 zenye thamani ya TZS 1,193.40 milioni mwaka 2024. Kwa upande wa eneo la uzalishaji limeongezeka na kufikia ekari 1,270.95 mwaka 2025 kutoka ekari 1,082.10 mwaka 2024.

### (f) Mboga mboga za Majani

Mboga za Majani hujumuisha kilimo cha mazao ya mboga mboga na matunda kama vile matikiti, tungule, matango, mabilingani, bamia, pili pili na nyenginezo za aina hiyo. Mwaka 2025, uzalishaji wa mazao hayo umeongezeka na kufikia tani 96,843.20 kutoka tani 80,044.20 mwaka 2024.
Jumla ya ekari 25,352.30 zimetumika katika ulimaji wa mazao mwaka 2025, ikilinganishwa na ekari 23,264.90 mwaka 2024. Uzalishaji wa Mazao hayo umeongezeka kutokana na muamko wa wakulima katika kilimo cha mboga mboga, hali ya hewa yakuridhisha, Kudhibiti miripuko ya wadudu

na magonjwa kwenye kilimo, pamoja na upatikanaji wa mbolea kwa ajili ya mazao hayo. ***(Jadweli Namba 5)***

**Jadweli Namba 5: Eneo la Uzalishaji kwa ekari kwa mazao ya chakula (2021-2025)**

| Zao | Ekari | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
| **Mpunga** | 25,383.60 | 26,243.00 | 25,591.30 | 24,565.40 | 25,170.40 |
| **Muhogo** | 30,948.60 | 34,500.80 | 37,548.90 | 20,080.40 | 30,515.43 |
| **Ndizi** | 7,104.00 | 6,085.70 | 8,664.40 | 7,303.30 | 8,628.48 |
| **Njugu nyasa** | 775 | 1,300.50 | 1,454.30 | 1,082.10 | 1,270.95 |
| **Viazi vikuu** | 1,549.30 | 1,338.40 | 1,848.30 | 2,876.70 | 3,197.06 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na kijamii Zanzibar, 2026.***

**Jadweli Namba 6: Kiwango na Thamani ya Bidhaa za Chakula Zilizozalishwa (2021-2025) (TZS milioni)**

| **Zao** | **2021** | | **2022** | | **2023** | | **2024** | | **2025** | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamain |
| Mpunga | 25,511.00 | 25,369.10 | 23,683.00 | 24,069.40 | 36,362.40 | 39,480.80 | 29,767.50 | 32,463.70 | 33,327.90 | 39,108.90 |
| Muhogo | 181,668.00 | 126,210.50 | 202,519.50 | 143,792.00 | 220,411.80 | 167,920.00 | 117,871.70 | 95,996.40 | 179,125.60 | 156,969.50 |
| Ndizi | 61,094.40 | 80,147.40 | 52,337.30 | 70,16980. | 74,514.10 | 107,195.50 | 62,808.30. | 90,360.10 | 74,204.90 | 114,869.50 |
| Viazi vikuu | 7,746.30 | 8,410.80 | 6,692.00 | 7,425.90 | 9,241.30 | 11,003.30 | 14,293.40 | 17,019.60 | 15,985.30 | 20,480.80 |
| Njugu nyasa | 372 | 729 | 624.2 | 1,250.20 | 698 | 1,500.20 | 519.4 | 1,193.40 | 610.1 | 1,508.20 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2026*.**

Serikali imechukua hatua za kuendeleza na kukuza kilimo ili kuongeza uzalishaji na kuhakikisha upatikanaji wa chakula, hatua zilizochukuliwa ni pamoja na:-

i. Kufanya ukarabati mabonde 8 ya Umwagiliaji Maji; Mtwango, Mwera, Bumbwisudi, Kibokwa, Kianga, Saninga, Kinyakuzi, Weni, Makombeni na Tibirinzi.

ii. Kuendelea na kuboresha miundo mbinu katika mabonde 6 ya umwagiliaji maji: Cheju, Kilombero, Kinyasini, Kibokwa, Chaani na Mlemele.

iii. Kufanya ukarabati na utunzaji wa miundombinu ya umwagiliaji (Visima na Pampu) katika Mabonde yote ya Umwagiliaji Maji na kutoa mafunzo kwa wakulima na wataalamu juu ya usimamizi na uendeshaji wa skimu pamoja na kushajiisha wakulima kuchangia gharama.

iv. Kufanya mapitio ya 'Mpango Mkuu wa Umwagiliaji Maji wa Mwaka 2002' (Irrigation Master Plan).

v. Mafunzo ya udereva wa zana za kilimo kwa madereva wa Wakala wa Matrekta na zana za kilimo na wakulima.

vi. Uzalishaji wa mbegu ya mpunga katika eneo la ekari 2.5 Kibonde Mzungu na ekari 1 Mwera kupitia Mradi wa Uhimilivu wa Chakula.

vii. Ukarabati wa visima katika maeneo 6 ya vitalu.

viii. Kudhibiti miripuko ya wadudu na magonjwa kwenye kilimo.

ix. Kugawa mitego na dawa kwa wakulima.

x. Ukarabati wa maghala 8 (Unguja 3 na Pemba 5) na ujenzi wa vihenge.

xi. Ujenzi wa kituo cha uhifadhi wa chakula – Unguja.

xii. Ununuzi wa chakula cha akiba.

**MAZAO YA BIASHARA:**

Mazao makuu ya biashara kwa uchumi wa Zanzibar ni karafuu na mwani. Kwa mwaka 2025, mavuno ya zao la karafuu yameongezeka na kufikia tani 5,230.4 zenye thamani ya TZS 78,152.5 milioni ikilinganishwa na tani 1,167.4 zenye thamani ya TZS 17,250.7 milioni mwaka 2024.

Ongezeko hili limesababishwa na kuwepo kwa msimu mkubwa wa uzalishashi wa zao hilo.

Kwa upande wa zao la mwani mwaka 2025 kwa ujumla uzalishaji umeongezeka na kufikia tani 20,074.6 zenye thamani ya TZS 14,253.4 milioni kutoka tani 19,716.0 zenye thamani ya TZS 16,144.6 milioni mwaka 2024. Hii imetokana na kushuka bei kwa zao la mwani katika soko la Dunia.

**Jadweli Namba 7: Uzalishaji wa mazao ya Karafuu na Mwani (2021-2025) (TZS milioni)**

| Zao | 2021 | | 2022 | | 2023 | | 2024 | | 2025 | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | Tani | Thamani | Tani | Thamnia | Tani | Thamani | Tani | Thamani | Tani | Thamani |
| Karafuu | 7,840.0 | 102,030.8 | 4,734.1 | 63,145.9 | 2,654.70 | 37,980.6 | 1,167.4 | 17,250.7 | 5,230.4 | 78,152.5 |
| Mwani | 10,530.8 | 6,402.8 | 12,593.7 | 10,054.4 | 16,652.9 | 16,514.8 | 19,716.0 | 16,144.6 | 20,074.6 | 14,253.4 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa Takwimu za Kiuchumi na Kijamii Zanzibar, 2026.***

#### 2.7.3.2 Sekta Ndogo ya Mifugo

Kwa mwaka 2025 jumla ya idadi ya ng'ombe waliochinjwa imepungua na kufikia 31,747 ikilinganishwa na ng'ombe 31,953 mwaka 2024 sawa na upungufu la asilimia - 0.64. Kwa mwaka 2025, idadi ya kuku waliochinjwa imefikia jumla ya kuku 1,472,903 ikilinganishwa na idadi ya kuku 1,085,856 waliochinjwa mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 35.64. Kwa mwaka 2025 idadi ya mbuzi waliochinjwa imeongezeka na kufikia mbuzi 11,814 ikilinganishwa na mbuzi 11,282 waliochinjwa mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 4.71. Idadi ya kondoo waliochinjwa mwaka 2025 imeongezeka na kufikia kondoo 1,781 ikilinganishwa na kondoo 795 waliochinjwa mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 124.0. Kwa ujumla, ongezeko hilo ni kutokana na kuongezeka kwa mahitaji ya mazao ya mifugo.

#### 2.7.3.3 Sekta Ndogo ya Uvuvi.

Zanzibar ni visiwa vilivyozungukwa na bahari, shughuli za uvuvi ni maarufu sana ambazo huinua hali ya kipato kwa wananchi wake.

Kwa mwaka 2025 upatikanaji wa samaki umeongezeka na kufikia tani 79,431 zenye thamani ya TZS 624,954 milioni kutoka tani 78,943 zenye thamani ya TZS 618,183 milioni mwaka 2024. Sawa na ongezeko la asilimia 0.61 ya tani za upatikanaji wa samaki, ongezeko hili limetokana na kuimarika kwa shughuli za uvuvi mdogo, usimamizi bora wa rasilimali za Bahari, pamoja na kuongezeka kwa mahitaji ya soko.

#### 2.7.3.4 Sekta ndogo ya Misitu

Misitu ni rasilimali muhimu kwa Uchumi wa Zanzibar. Serikali inaendelea na mikakati ya kutunza na kuhifadhi misitu ya asili ili kupunguza athari za tabianchi. Bidhaa za misitu zilizouzwa kwa mwaka 2025 ni kama ifuatavyo: Jumla ya Boriti 1,691.3 zenye thamani ya TZS 228.0 milioni ikilinganishwa na boriti 3,200.0 zenye thamani ya TZS 395.5 milioni zimeuzwa mwaka 2024, nguzo 2,256.3 zenye thamani ya TZS 413.7 milioni zimeuzwa mwaka 2025 ikilinganishwa na nguzo 2,333.0 zenye thamani ya TZS 389.0 milioni zimeuzwa mwaka 2024, mapau 2,843.1 zenye thamani ya TZS 1,279.4 mwaka 2025

ikilinganishwa na mapau 2,455.0 yenye thamani ya TZS 982.0 milioni yameuzwa mwaka 2024, jumla ya mizigo ya kuni 28,541.0 zenye thamani

ya TZS 1,427.0 yameuzwa mwaka 2025 ikilinganishwa na mizigo 21,002.0 yenye thamani ya TZS 1,050.0 milioni yameuzwa mwaka 2024, fito 1,345.8 zenye thamani ya TZS 246.7 milioni mwaka 2025 ikilinganishwa na fito 1,201.0, zenye thamani ya TZS 200.0 milioni zimeuzwa kwa mwaka 2024 na kwa upande wa makaa jumla ya tani 1,427.0 zenye thamani ya TZS 2,411.1 milioni mwaka 2025 ikilinganishwa na tani 2,207.0 zenye thamani ya TZS 2,759.0 milioni zimeuzwa mwaka 2024 .

### 2.8 Ukuzaji Rasilimali

Ukuzaji rasilimali nchini umeendelea kuchangia Ukuaji wa Uchumi kupitia ongezeko la upatikanaji wa ajira, ukusanyaji wa mapato, uingiaji wa fedha za kigeni, uimarishaji wa miundombinu, pamoja na ujenzi wa nyumba za biashara.

Kwa mwaka 2025, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) imesajili jumla ya miradi 136 yenye thamani ya TZS 1.89 trilioni kutoka miradi 131 yenye thamani ya TZS 1.87 trilioni mwaka 2024 sawa na asilimia 0.86 ya thamani ya miradi hiyo. Miradi yenye thamani kubwa zaidi iliyowekezwa nchini ni miradi ya nyumba za biashara/mali zisizohamishika *(Real Estate)* yenye thamani ya TZS 803.2 bilioni ikifuatiwa na miradi ya hoteli na migahawa *(Accommodation and Food Services)* yenye thamani ya TZS 726.6 bilioni. ***(Jadweli Nambari 8):***

**Jadweli Namba 8: Idadi ya Miradi na Thamani iliyoidhinishwa na ZIPA**

| ORODHA YA MIRADI | *2023* | | *2024* | | *2025* | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Miradi** | **TZS Mil** | **Miradi** | **TZS Mil** | **Miradi** | **TZS Mil** |
| Kilimo , Misitu na Uvuvi | 3 | 139,512 | 7 | 44,945 | 4 | 4,208 |
| Uchimbaji Madini, Mawe na Mchanga | 0 | 0 | 0 | 0 | 1 | 2,882 |
| Uzalishaji Viwandani | 7 | 1,030,080 | 8 | 194,144 | 16 | 305,843 |
| Umeme na Gesi | 5 | 1,495,920 | 1 | 747 | 0 | 0 |
| Shughuli za Usimamizi wa Taka Taka | 0 | 0 | 0 | - | 1 | 1,275 |
| Shughuli za Ujenzi | 1 | 24,480 | 0 | - | 1 | 1,275 |
| Biashara za (jumla na reja reja), pamoja na Vyombo vya Moto | 4 | 13,968 | 5 | 103,887 | 1 | 255 |
| Usafiri na Uhifadhi | 1 | 9,600 | 3 | 44,322 | 3 | 37,485 |
| Huduma za Malazi na Migahawa | 44 | 1,248,666 | 56 | 553,165 | 55 | 726,674 |
| Huduma za Fedha na Bima | 1 | 4,800 | 0 | - | 0 | 0 |
| Habari na Mawasiliano | 0 | 0 | 0 | - | 1 | 1,275 |
| Huduma za Ukodishaji | 33 | 286,909 | 37 | 902,686 | 47 | 803,216 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| wa Nyumba za Biashara | | | | | | |
| Shughuli za Kiutawala | 0 | 0 | 0 | - | 0 | 0 |
| Elimu | 0 | 0 | 1 | 249 | 1 | 2,550 |
| Huduma za Afya na Kazi za Kijamii | 2 | 6,840 | 5 | 11,579 | 1 | 1,785 |
| Sanaa na Michezo | 11 | 380,475 | 6 | 7,844 | 3 | 4,080 |
| Huduma Nyenginezo | 2 | 4,800 | 2 | 14,193 | 1 | 1,275 |
| **Jumla** | **114** | **4,646,050** | **131** | **1,877,760** | **136** | **1,894,078** |

*Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026*

### 2.8.1 Mgawanyo wa Umiliki wa Miradi iliyosajiliwa na ZIPA

Kwa mwaka 2025, Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar, ilisajili jumla ya miradi mipya 31 yenye thamani ya TZS 447.2 bilioni ni miradi iliyowekezwa na Wazawa ikilinganishwa na miradi 26 iliyosajiliwa kuwekezwa mwaka 2024, ambapo miradi 105 yenye thamani ya TZS 1.4 trilioni ni miradi iliyowekezwa na wageni mwaka 2025 ikiwa ni sawa na miradi 105 iliyosajiliwa kuwekezwa mwaka 2024. Hivyo, miradi 31 ya wazawa na miradi 105 ya wageni imefikisha jumla ya miradi mipya 136 iliyosajiliwa na ZIPA mwaka 2025.

**Jadweli Namba 9: Mchanganuo wa Umiliki wa Miradi na Thamani iliyoidhinishwa na ZIPA**

| **Umiliki** | **Idadi ya Miradi** | **Thamani TZS (000,000)** | **Idadi ya Miradi** | **Thamani TZS (000,000)** | **Idadi ya Miradi** | **Thamani TZS (000,000)** | **Idadi ya Miradi** | **Thaman i TZS (000,000)** |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | **(2022)** | | **(2023)** | | **(2024)** | | **(2025)** | |
| Wazawa | 35 | 216,512 | 28 | 226,075 | 26 | 520,201 | 31 | 447,219 |
| Wageni | 58 | 4,333,557 | 86 | 4,419,975 | 105 | 1,357,559 | 105 | 1,446,859 |
| **Jumla** | **93** | **4,550,069** | **114** | **4,646,050** | **131** | **1,877,760** | **136** | **1,894,078** |

*Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026*

### 2.8.2 Mgawanyo wa Miradi Iliyosajiliwa na ZIPA Kulingana na Mabara

Kwa mwaka 2025, Jumla ya miradi 49 iliyosajiliwa ni kutoka Bara la Afrika, miradi 51 kutoka Bara la Australia, miradi 29 kutoka Bara la Asia miradi 4 kutoka Bara la Ulaya na miradi 3 kutoka Bara la Amerika. Miradi hio imewekezwa katika sekta mbali mbali nchini zikiwemo sekta za kilimo, misitu na uvuvi; sekta za mahoteli na migahawa; sekta za nyumba zisizohamishika, na nyenginezo.

**Jadweli Namba 10: Mgawanyo wa Miradi iliyosajiliwa kwa Mabara (2021-2025)**

| Mabara | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Afrika | 38 | 37 | 38 | 36 | 49 |
| Ulaya | 36 | 33 | 44 | 0 | 4 |
| Asia | 13 | 17 | 25 | 6 | 29 |
| Amerika | 9 | 4 | 7 | 47 | 3 |
| Australia | 1 | 2 | 0 | 42 | 51 |
| Jumla | 97 | 93 | 114 | 131 | 136 |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026***

### 2.8.3 Nafasi za Ajira Zilizosajiliwa na Mamlaka ya Kukuza Uwekezaji Zanzibar (ZIPA) Kutoka Miradi ya Uwekezaji

Kwa mwaka 2025, miradi 136 iliyosajiliwa na ZIPA imechangia upatikanaji wa ajira mpya 6,494 kutoka ajira 4,109 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 58.0. Kati ya ajira hizo, jumla ya ajira mpya 3,888 kati ya ajira mpya 6,494 sawa na asilimia 60 zilizosajiliwa mwaka 2025 zimetokana na miradi ya sekta ya huduma za hoteli na migahawa, ikifuatiwa na miradi ya sekta ya mali zisizohamishika kufikia ajira 1,527 sawa na asilimia 24. Kuendelea kuimarika kwa sekta ndogo ya utalii visiwani Zanzibar kumesaidia kuongeza nafasi za ajira kupitia miradi mipya iliyosajiliwa mwaka 2025.

**Jadweli Namba 11: Idadi ya Ajira Zilizosajiliwa katika Miradi ya Uwekezaji ZIPA**

| AJIRA ZA SEKTA | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kilimo , Misitu na Uvuvi | 496 | 446 | 65 | 454 | 55 |
| Uchimbaji Madini, Mawe na Mchanga | 0 | 0 | 0 | 0 | 50 |
| Uzalishaji Viwandani | 2,779 | 206 | 100 | 176 | 589 |
| Umeme na Gesi | 0 | 100 | 120 | 0 | 0 |
| Shughuli za Usimamizi wa Taka Taka | 30 | 0 | 0 | 0 | 140 |
| Shughuli za Ujenzi | 520 | 383 | 70 | 0 | 25 |
| Biashara za (jumla na reja reja), pamoja na Vyombo vya Moto | 40 | 127 | 39 | 201 | 8 |
| Usafiri na Uhifadhi | 266 | 400 | 15 | 318 | 60 |
| Huduma za Malazi na Migahawa | 2,043 | 1,240 | 4,442 | 1,834 | 3,888 |
| Huduma za Fedha na Bima | 19 | 0 | 20 | 0 | 10 |
| Habari na Mawasiliano | 0 | 30 | 0 | 0 | 0 |
| Huduma za Ukodishaji wa Nyumba za Biashara | 234 | 903 | 1,019 | 933 | 1,527 |
| Shughuli za Kiutawala | 20 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Elimu | 215 | 20 | 0 | 10 | 15 |
| Huduma za Afya na Kazi za Kijamii | 900 | 20 | 25 | 130 | 15 |
| Sanaa na Michezo | 190 | 95 | 204 | 38 | 97 |
| Huduma Nyenginezo | 39 | 0 | 27 | 15 | 15 |
| **Jumla** | **7,791** | **3,970** | **6,146** | **4,109** | **6,494** |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026***

## 2.9 Hali ya Upatikanaji wa Ajira Zanzibar

Kwa mwaka 2024/2025, jumla ya ajira mpya 85,182 zilisajiliwa zikilinganishwa na ajira 83,430 za mwaka 2023/24, ambapo ajira za wanaume zilikuwa 42,760 sawa na asilimia 50.1 na wanawake ajira 42,422 sawa na asilimia 49.8. Katika ajira mpya hizo, nafasi za ajira za Serikali zimefikia 41,377 (wanaume 16,110 na wanawake 25,267); ajira za Mashirika ya Serikali zimefikia 9,299 (wanaume 5,611 na wanawake 3,688), na ajira za Sekta Binafsi zimefikia 34,506 (wanaume 21,039 na wanawake 13,467). Wastani wa mchanganuo

wa ajira za Serikali umefika asilimia 49, ikifuatiwa na asilimia 41 ya ajira za Sekta Binafsi, na asilimia 11 ya ajira za Mashirika ya Serikali Zanzibar.

**Jadweli Namba 12: Mchanganuo wa Ajira Mpya kwa Sekta na Jinsia (2019/20 – 2024/25)**

| Sekta | Jinsia | 2019/20 | 2020/21 | 2021/22 | 2022/23 | 2023/24 | 2024/25 |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Serikali | Wanaume | 15,545 | 16,190 | 15,541 | 15,603 | 15,786 | 16,110 |
| | Wanawake | 19,888 | 22,556 | 21,648 | 22,264 | 22,498 | 25,267 |
| | Jumla ndogo | 35,433 | 38,746 | 37,189 | 37,867 | 38,284 | 41,377 |
| Mashirika ya Serikali | Wanaume | 4,306 | 4,526 | 4,522 | 4,442 | 5,224 | 5,611 |
| | Wanawake | 2,153 | 2,476 | 2,365 | 2,411 | 3,206 | 3,688 |
| | Jumla ndogo | 6,459 | 7,002 | 6,887 | 6,853 | 8,430 | 9,299 |
| Binafsi | Wanaume | 17,102 | 14,141 | 15,947 | 23,598 | 22,619 | 21,039 |
| | Wanawake | 8,101 | 6,767 | 8,609 | 13,907 | 14,097 | 13,467 |
| | Jumla ndogo | 25,203 | 20,908 | 24,556 | 37,505 | 36,716 | 34,506 |
| Jumla | Wanaume | 36,953 | 34,857 | 36,010 | 43,643 | 43,629 | 42,760 |
| | Wanawake | 30,142 | 31,799 | 32,622 | 38,582 | 39,801 | 42,422 |
| | Jumla Kuu | 67,095 | 66,656 | 68,632 | 82,225 | 83,430 | 85,182 |

*Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026*

# SURA YA TATU

## 3.0 SEKTA YA NJE

Sekta ya biashara ina mchango mkubwa katika uchumi wa Zanzibar kupitia fursa za ajira, mabadilishano ya fedha za kigeni, maendeleo ya viwanda pamoja na kuongeza mapato ya Serikali. Zanzibar imeendelea kupiga hatua ya ushindani wa biashara hali iliyopelekea kukuza uchumi wake pamoja na kuimarisha uhusiano bora baina ya mataifa mengi ikiwemo nchi za Falme za Kiarabu, China, India, Singapore, Uganda, Oman na nyenginezo.

### 3.1 Usafirishaji wa Bidhaa Kwenda Nje ya Nchi

Kwa mwaka 2025, usafirishaji wa bidhaa kwenda nje ya nchi umefikia thamani ya TZS 92.4 bilioni kutoka thamani ya TZS 105.2 bilioni ya mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 12.0. Upungufu huu umetokana na usafirishaji wa bidhaa za baharini kufikia thamani ya TZS 35.5 bilioni mwaka 2025 kutoka thamani ya TZS 36.1 bilioni mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 2.0. Upungufu huo umechangiwa na upatikanaji mdogo wa samaki aina ya dagaa mwaka 2025 kufikia tani 18,318 kutoka tani 18,678 mwaka 2024 sawa na upungufu wa tani 360.


#### 3.1.1 Usafirishaji wa Mazao Makuu ya Biashara

Mazao makuu ya biashara nchini ni zao la karafuu na mwani, hata hivyo kuimarika kwa sekta ya uchumi wa buluu kumesaidia kuimarika kwa usafirishaji wa bidhaa nyengine za baharini ikiwemo majongoo bahari, dagaa kavu, kaa, kamba, samaki, ngisi, pweza, makome, na nyenginezo, aidha usafirishaji wa bidhaa za viungo ikiwemo mdalasini na hiliki zimeendelea kusafirishwa na kuongeza thamani ya usafirishaji. Usafirishaji wa mazao hayo huimarisha mchango wa ukuaji wa uchumi wa Zanzibar kupitia ajira, kuongeza thamani ya usafirishaji na kuongeza fedha za kigeni. Mbali na hayo, mazao ya karafuu na mwani hutumiwa na wazawa kama kiungo katika vyakula na tiba za asili.

Kwa mwaka 2025, usafirishaji wa zao la karafuu umefikia jumla ya tani 3,186.1 zenye thamani ya TZS 52.8 bilioni kutoka tani 1,974.4 zenye thamani ya TZS 30.7 bilioni zilizosafirishwa mwaka 2024. Ukuaji huo umechangiwa

kwa kuimarika uzalishaji wa zao la karafuu kufikia tani 5,230.4 mwaka 2025 kutoka tani 1,167.4 mwaka 2024 zilizonunuliwa na ZSTC kutoka kwa wakulima nchini.

**Mchoro Namba 15: Tani na Thamani ya Usafirishaji wa Zao la Karafuu 2025.**




| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Thamani TZS Mil | 115,358.70 | 118,287.30 | 47,081.10 | 30,737.30 | 52,806.30 |
| Tani | 6,775.50 | 6,452.80 | 3,197.30 | 1,974.40 | 3,186.10 |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026***

Kwa mwaka 2025, bidhaa za baharini zimeendelea kusafirishwa nchini ambapo usafirishaji wa dagaa kavu umefikia jumla ya tani 6,035 zenye thamani ya TZS 27.9 bilioni mwaka 2025 kutoka tani 5,466.62 zenye thamani ya TZS 24.5 bilioni mwaka 2024. Zao la mwani limefikia jumla ya tani 3,901.8 zenye thamani ya TZS 5.2 bilioni mwaka 2025 kutoka tani 7,089.5 zenye thamani ya TZS 10.7 bilioni mwaka 2024. Usafirishaji wa Majongoo bahari umefika tani 29 zenye thamani ya TZS 726.3 milioni mwaka 2025 kutoka tani 22.5 zenye thamani ya TZS 679.6 milioni mwaka 2024. Usafirishaji wa Kaa umefikia tani 299 zenye thamani ya TZS 1.1 bilioni mwaka 2025 kutoka tani 304.9 zenye thamani ya TZS 1.5 bilioni mwaka 2024. Aidha, Serikali inaendelea kutekeleza mikakati mbalimbali ya kuimarisha sekta ya Uchumi wa Buluu ikiwemo kutumia rasilimali za bahari kwa njia endelevu ili kuongeza uzalishaji, ajira, kipato cha wananchi, pamoja na kuchochea ukuaji wa uchumi.

**Jadweli Namba 13: Tani na Thamani ya Usafirishaji wa (Baadhi ya) Bidhaa za Baharini 2025.**

| | 2024 | | 2025 | |
|---|---|---|---|---|
| | **TANI** | **THAMANI TZS,Mil** | **TANI** | **THAMANI TZS,Mil** |
| **Dagaa kavu** | 5,466.6 | 24,598.1 | 6,034.9 | 27,903.2 |
| **Mwani** | 7,089.5 | 10,738.7 | 3,901.8 | 5,225.5 |
| **Kaa** | 304.9 | 1,516.5 | 298.8 | 1,128.9 |
| **Majongoo bahari** | 22.6 | 679.7 | **29.5** | 726.4 |
| **Unga wa Dagaa** | 368.5 | 524.7 | 28.2 | 102.6 |
| **Samaki** | 1.5 | 16.3 | 4.6 | 69.3 |
| **Kamba** | 4.8 | 130.0 | 1.5 | 46.5 |
| **Ngisi** | 0.0 | 0.1 | 30.0 | 18.1 |

***Chanzo: MoBEF na OCGS, 2026***

## 3.2 Uagiziaji wa Bidhaa Kutoka Nje ya Nchi

Kwa mwaka 2025, thamani ya Uagiziaji wa bidhaa kutoka nje ya nchi imefikia TZS 2.4 trilioni kutoka thamani ya TZS 1.6 trilioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 50.0. Bidhaa zinazoingia nchini ni bidhaa za vyakula, nishati ya mafuta, bidhaa za mashine, vifaa vya viwandani, zana za kilimo, mali ghafi za viwandani, nguo na mapambo, bidhaa za Samani na thamani, vifaaa vya ujenzi na ofisini, na nyenginezo.

Miongoni mwa bidhaa kuu zinazoingia nchini ni pamoja na bidhaa za nishati ya mafuta ikiwemo petroli, dizeli, mafuta ya taa na mafuta ya ndege. Kwa mwaka 2025, uagiziaji wa bidhaa za nishati ya mafuta umeongezeka ikilinganishwa na mwaka 2024 ambapo mafuta ya petroli yamefikia jumla ya lita 131.1 milioni mwaka 2025, kutoka lita 113.5 milioni mwaka 2024. Mafuta ya dizeli yamefikia jumla ya lita 88.9 milioni mwaka 2025 kutoka lita

76.6 milioni mwaka 2024 na mafuta ya ndege yamefikia jumla ya lita 63.9 milioni mwaka 2025 kutoka lita 55.5 milioni mwaka 2024.

Kwa upande wa uagiziaji wa mafuta ya taa yameendelea kupungua hadi kufikia lita 900,000 mwaka 2025 kutoka lita 1.0 milioni mwaka 2024. Kuendelea kwa harakati za uhamisishaji wa utumiaji nishati ya umeme na gesi salama za kupikia nchini kumesaidia kupunguza uhitaji mkubwa wa matumizi ya nishati ya mafuta ya taa kwa wakaazi wa Zanzibar.

**Jadweli Namba 14: Uagiziaji wa Bidhaa za Nishati ya Mafuta, Mwaka 2025**


| Lita (Mil) | | | | |
|---|---|---|---|---|
| **Mwaka** | Petroli | **Diseli** | **Mafuta ya Taa** | **JET A-1** |
| **2023** | 110.9 | 71.8 | 2.9 | 47.9 |
| **2024** | 113.5 | 76.6 | 1.0 | 55.5 |
| **2025** | 131.1 | 88.9 | 0.9 | 63.9 |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026***

## 3.3 Urari wa Biashara

Kwa mwaka 2025, nakisi ya biashara imeongezeka kufikia thamani ya TZS 2.4 trilioni kutoka thamani ya TZS 1.4 trilioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 63.3, hali iliyosababishwa na ongezeko kubwa la thamani ya uagiziaji kuliko usafirishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kutokana na kuongezeka kwa uhitaji wa bidhaa za chakula na zisizo za chakula ambazo hazizalishwi hapa nchini. Hata hivyo, kuna haja ya kuongeza uzalishaji wa ndani na kupunguza utegemezi wa bidhaa zinazozalishwa nje ya nchi kutasaidia kupunguza nakisi ya biashara nchini.

**Mchoro Namba 16: Unaonesha Thamani ya Usafirishaji, Thamani ya Uagiziaji na Urari wa Biashara mwaka 2025.**





***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026***

## 3.4 Uhaulishaji wa Bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara

Kwa mwaka 2025, uhaulishaji wa bidhaa kutoka Zanzibar kwenda Tanzania Bara umefikia thamani ya TZS 155.3 bilioni kutoka thamani ya TZS 280.8 bilioni mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 45.0. Kupungua huko kumechangiwa na udhibiti wa uhaulishaji wa bidhaa ya mafuta ya kula kwa kipindi hicho. Kwa upande wa uhaulishaji wa bidhaa kutoka Tanzania Bara kuja Zanzibar umefikia thamani ya TZS 668.6 bilioni mwaka 2025 kutoka thamani ya TZS 549.6 bilioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 22.0. Miongoni mwa bidhaa zinazohaulishwa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara ni pamoja na mchele wa mbeya, mchele wa basmati, mafuta ya kupikia, vitunguu, tungule, mkaa, mayai, bidhaa za matunda, na nyenginezo.Hii ni kwasababu ya kuzibiti hali.

**Mchoro Namba 17: Uhaulishaji wa bidhaa baina ya Zanzibar na Tanzania Bara mwaka 2025.**




*Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026*

# SURA YA NNE

## 4.0 SEKTA YA FEDHA

Sekta ya Fedha ina mchango mkubwa katika kukuza maendeleo ya uchumi wa nchi kupitia kuwezesha upatikanaji wa huduma za kifedha, kuimarisha uwekezaji, kuongeza mzunguko wa fedha katika uchumi, na kusaidia utekelezaji wa shughuli mbalimbali za maendeleo ya kijamii na kiuchumi pia inanafasi muhimu katika kuchochea maendeleo ya uchumi wa nchi. Sekta hii inajumuisha huduma za Mabenki, Bima, Mfuko wa hifadhi ya jamii, Soko la mitaji na dhamana, Mifumo ya malipo na huduma ndondogo za Fedha (Microfinance).Kwa kipindi cha Julai hadi Machi, 2025/2026.Utekelezaji wa Sekta ya Fedha ulikuwa kama ifuatavyo:-

### 4.1 Sekta Ndogo Ya Benki

Sekta hii ni muhimu katika ukuaji wa Uchumi, inayojumuisha Benki Kuu ya Tanzania ikiwa ndiyo msimamizi mkuu wa shughuli za fedha nchini; pia benki za biashara; mawakala wa huduma za kibenki, huduma ndogo ndogo za fedha na mitandao ya simu. Katika robo ya nne ya mwaka 2025(Oktoba hadi Disemba 2025) Sekta ndogo ya fedha na huduma ya bima ilichangia asimilia 4.5 katika pato la taifa.

#### 4.1.1. Benki Kuu ya Tanzania (BOT)

Jukumu la msingi la Benki Kuu ya Tanzania ni kuandaa na kutekeleza sera ya fedha inayolenga kudhibiti mfumuko wa bei na kujenga mfumo wa fedha ulio imara na unaofaa kwa ukuaji endelevu wa Uchumi wa taifa.

Majukumu mengine ya Benki Kuu ya Tanzania

- Kutoa sarafu ya nchi ambayo ni Shilingi ya Tanzania
- Kusimamia na kudhibiti mabenki na taasisi za fedha
- Kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo nchini.
- Kuhifadhi akiba ya nchi ikiwemo fedha za kigeni
- Benki ya Serikali
- Benki ya Mabenki; na

- Kutoa ushauri juu ya masuala ya uchumi na fedha kwa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar.

### 4.1.2 Mafanikio

Benki Kuu, katika kutekeleza majukumu yake ya msingi kwa mujibu wa malengo na miongozo iliyowekwa, imeendelea kupata mafanikio makubwa na ya kuridhisha katika nyanja mbalimbali za kiuchumi na kifedha. Mafanikio haya yametokana na usimamizi thabiti wa sera, ufuatiliaji wa karibu wa mwenendo wa uchumi, pamoja na utekelezaji madhubuti wa majukumu yake ya kisheria na kiudhibiti, kama ifuatavyo:

**1) Kuandaa na Kutekeleza Sera ya Fedha**

Utekelezaji wa sera ya fedha kwa mwaka 2025/26 umekuwa wa mafanikio makubwa, katika robo ya tatu Benki Kuu iliendelea kuitekeleza Sera ya Fedha kwa kutumia Mfumo wa Riba (interest rate based monetary policy). Aidha, kwa kuzingatia mafanikio yaliyojitokeza katika robo ya tatu ya mwaka 2025/26, inayojumuisha kipindi cha Januari hadi Machi 2026, Benki kuu kwa kupitia Kamati ya Sera ya Fedha (MPC) ilifanya kikao cha kawaida, tarehe 1 Aprili 2026, kufanya tathmini ya mwenendo wa uchumi na Riba ya Benki Kuu (Central Bank Rate-CBR).

Kutokana na tathmini hiyo, Kamati iliamua kiwango cha Riba ya Benki Kuu kubaki asilimia 5.75 kwa robo ya pili ya mwaka 2026. Kiwango hicho kilionekana ni sahihi kwa sasa katika kudhibiti mfumuko wa bei kubakia ndani ya lengo la asilimia 3 hadi 5. Aidha, kiwango hicho kitawezesha kupunguza athari za mgogoro wa kisiasa unaoendelea Mashariki ya Kati kwenye uchumi wa nchi yetu. Mgogoro huo umeathiri biashara, uwekezaji, na ustahimilivu wa uchumi wa dunia.

**2) Usimamizi na Udhibiti wa Mifumo ya Malipo Nchini**

Mifumo ya Malipo ya Taifa inajumuisha shughuli zote zinazohusiana na malipo, michakato, mifumo, miundombinu, taasisi na watumiaji katika nchi. Benki Kuu imeendelea kusimamia na kudhibiti mifumo ya malipo nchini kwa kuzingatia sheria mbalimbali. Mifumo ya malipo nchini ipo katika makundi mawili;

a. Mifumo inayoendeshwa na Benki Kuu, ikijumuisha hasa mifumo ya malipo makubwa (zaidi ya shilingi milioni 10) kama vile Tanzania Interbank Settlement System (TISS); mfumo wa utumaji pesa kwa njia ya elektroniki (Electronic Funds Transfer, EFT) ambao hutumika kupitisha malipo mengi yenye thamani ndogo na mfumo wa malipo ya hundi (TACH).

b. Mifumo inayosimamiwa na Benki Kuu ikiwemo;

   i Mitandao ya malipo ya kadi *(Card Payment Schemes/Switches)* mfano Umoja Switch, VISA Switch, MasterCard Switch na UnionPay Switch.

   ii Mitandao ya malipo ya kieletroniki inayotumiwa na mabenki kama vile mifumo ya huduma za kibenki kwa njia ya simu za mkononi *(mobile banking)*; huduma za kibenki kupitia mtandao *(internet banking);* mashine za fedha (ATMs) na mashine za malipo ya kadi (POS).

   iii Mifumo ya huduma za kifedha kwa njia ya simu za mikononi *(mobile/electronic money)*.

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/26, mifumo ya malipo nchini imeendelea kuwa salama na kufanya kazi kwa ufanisi na matumizi ya malipo kwa njia ya mtandao (Digital payment platforms) pia imeendelea kuimarika. Vilevile, malipo ya EFT yameendelea vizuri, huku idadi ya matumizi ikiongezeka, kutokana na serikali kutumia mfumo huu.

**3) Kusambaza Noti na Sarafu**

Benki Kuu – Zanzibar imeendelea kutimiza jukumu lake la kusambaza fedha (noti na sarafu) ili kutosheleza mahitaji ya uchumi bila kusababisha mabadiliko ya kasi ya upandaji wa bei ya bidhaa na huduma (yaani mfumko wa bei). Katika kipindi cha Julai, 2025 hadi Machi, 2026, Benki Kuu ilisambaza Zanzibar jumla ya TZS Bilioni 663.18, kati ya hizo 576.64 TZS Billioni zilisambazwa kupitia Ofisi ya Unguja na 86.54 TZS Bilioni kupitia Kituo cha Pemba.

**4) Kuhifadhi Akiba ya Nchi**

Benki Kuu ni mtunzaji wa hazina ya fedha za kigeni kwa kuzingatia malengo ya usalama, ukwasi, faida na usimamizi wa madeni ya nje. Hadi kufikia Machi

2026, akiba ya fedha za kigeni iliongezeka hadi kufikia Dola billioni 6.2. Akiba itatosheleza kuagiza bidhaa na huduma kutoka nje ya nchi kwa kipindi kisichopungua miezi 4.8 .

**5) Utoaji wa Huduma za Kibenki kwa Serikali na Mabenki**

Miongoni mwa huduma za kibenki zinazotolewa ni kutunza fedha za Serikali na taasisi zake pamoja na kufanya malipo kwa Serikali. Kutoa mikopo ya muda mfupi kwa Serikali kwa kutumia huduma yake ya overdraft. Kutunza amana za benki za biashara hapa nchini zikiwemo amana za kisheria *(statutory minimum reserve requirement)* zinazotakiwa kuwekwa Benki Kuu pamoja na kiasi cha amana kinachohitajika kwa ajili ya malipo au matumizi ya kila siku *(Clearing balances)*. Benki Kuu inaendelea kuwa mhifadhi na mlipaji mkuu wa Serikali ya Mapinduzi – Zanzibar na Taasisi za Jamhuri ya Muungano zilizopo Zanzibar pamoja na kutoa huduma za kibenki kwa Benki za Biashara zilizopo Zanzibar.

**6) Kusimamia Sekta ya Fedha (Mabenki na Taasisi Nyingine za Fedha)**

Benki Kuu ina mamlaka na jukumu la kusimamia sekta ya kibenki na Taasisi zote zinazotoa huduma ya fedha zikiwemo maduka ya kubadilisha fedha za kigeni, makampuni yanayotoa karadha *(finance lease companies)*,

Taasisi zinazotoa huduma ndogo ndogo za fedha, Taasisi zinazohusika na utoaji wa taarifa za wakopaji *(Credit Reference Bureaus)* na mikopo ya nyumba *(Mortgage financing)*. Benki Kuu hutoa leseni kwa ajili ya uanzishwaji wa benki na asasi nyingine za fedha, ikiwa ni pamoja na kutoa kanuni mbali mbali za uendeshaji na pia iliendelea kuchambua taarifa zinazowasilishwa na benki na taasisi nyenginezo za fedha na kufanya ukaguzi wa mara kwa mara ili kuhakikisha uthabiti na uadilifu wa sekta ya fedha.

### 4.1.3 Huduma za Kibenki

Huduma za kibenki zinaendelea kuimarika kila siku zikichagizwa zaidi na kukua kwa teknolojia, utumiaji wa njia mbadala wa kufikisha huduma kwa wateja ikiwa ni pamoja na mawakala wa benki *(Agent Banking)*. Hadi kufikia Disemba 2025, idadi ya benki zilizokuwa zikitoa huduma ziliongezeka na kufikia 15, huku idadi ya matawi ya benki yakiwa 58, ambapo Pemba ilikuwa na matawi 20 na Unguja ikiwa na matawi 38. Idadi ya ATM zikiwa 389.

Vilevile , Maduka ya kubadili fedha za kigeni (Bureau de Change) yalikuwa 13 yenye matawi 34, hata hivyo benki zote za biashara pia zilitoa huduma ya kubadili fedha. Vile vile, Benki imerahisisha ubadilishaji wa fedha za kigeni na ilifanya maboresho ya kanuni za fedha za kigeni kwa kuruhusu hoteli kufungua madirisha ya kubadili fedha za kigeni ili kuwa na kiasi cha mtaji.


**a. Amana**

Kwa kipindi cha Julai -Machi 2025, Amana katika benki za biashara zilizopo Zanzibar ziliongezeka kwa asilimia 22.8 na kufikia shilingi 3,711 bilioni kutoka shilingi 3,021.25 bilioni ukilinganisha na kipindi kama hichi mwaka 2024. PBZ ilikuwa na asilimia 51.0 ya Amana zote; ikifuatiwa na benki za CRDB kwa asilimia 12.7, NMB kwa asilimia 10.8, NBC asilimia 8.4 na bakaa ilikuwa kwa benki nyingine za biashara.

**b. Mikopo**

Hadi kufikia mwezi Disemba, 2025, thamani ya mikopo iliyotolewa na benki za biashara, Zanzibar iliongezeka na kufikia TZS 2,510.2 bilioni ukilinganisha na shilingi TZS 2,171.3 billioni katika mwaka 2024. Mikopo binafsi (ambayo zaidi inalenga wafanyakazi wa muda mrefu au wenye mikataba) ilichukua asilimia 26.1 ya mikopo yote iliyotolewa katika kipindi kinachoishia Disemba mwaka 2025. Hii ilifuatiwa mikopo iliyoelekezwa katika sekta ya biashara na utalii ambazo kwa pamoja zilipata asilimi 25.8 ya mikopo yote iliyotolewa. Aidha, kwa upande mikopo iliyoelekezwa katika Sekta ya utalii, iliongezeka kwa asilimia 14.8 hadi kufikia TZS 136.7 billioni ilikinganishwa na kipindi kama hicho mwaka 2024.

**Mchoro Namba 18: Sekta zilizonufaika na mikopo**
***TZS (Billioni)***




***Chanzo: Benki za Biashara***

## c. Wakala wa Huduma za Kibenki

Hadi kufikia mwezi Disemba 2025, idadi ya mawakala wa benki (agent banking) waliongezeka na kufikia mawakala 8,597 ambao ni asilimia 4.6 ya mawakala wote nchini Tanzania ikilinganishwa na mawakala 6,379 waliokuwepo kipindi kama hicho mwaka 2024. Pemba kulikwa na mawakala 4,462 na Unguja mawakala 4,135. Thamani ya miamala pia ilipungua na

kufikia Bilioni 532.57 kutoka Billion 921.04 katika kipindi kama hicho mwaka 2024. Na kwa upande wa kutoa thamani ya miamala ilipungua hadi kufikia TZS 305.61 bilioni kutoka TZS 370.78 bilioni mwaka 2024.

**Jadweli 15: Wakala wa benki, Zanzibar**

| KUWEKA | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | Disemba, 2024 | | Disemba, 2025 | | |
| | Idadi ya Mawakala | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala | Idadi ya Mawakala | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala |
| PEMBA | 3380 | 666,573 | 515,866,076,855.25 | 4,462 | 75,371 | 92,708,932,481.80 |
| UNGUJA | 2999 | 549,449 | 405,173,605,376.51 | 4,135 | 468,767 | 439,859,198, |
| Zanzi bar | 6,379 | 1,216,022 | 921,039,682,231.8 | 8,597 | 544,138 | 532,568,131,176.3 |
| **KUTOA** | | | | | | |
| | | Disemba, 2024 | | Disemba, 2025 | | |
| | Idadi ya Mawa kala | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala 170,368,580, 649.00 200,415,162, 362.70 | Idadi ya Mawakala | Idadi ya Miamala | Thamani ya Miamala 48,312,814, 362.00 257,294,471, 670.00 |
| PEMBA | 3380 | 432,232 | | 4,462 | 166,505 | |
| UNGUJA | 2999 | 452,878 | | 4,135 | 578,646 | |
| Zanzi bar | 6,379 | 885,110 | 370,783,743,011.7 | 8,597 | 745,151 | 305,607,286s,032.0 |

***Chanzo: Benki Kuu ya Tanzania***

### 4.1.4 Mwenendo wa Viwango vya Ubadilishaji wa Fedha za Kigeni (*Exchange Rate Movement*).

Hadi kufikia Machi 2026, shilingi ya Tanzania iliendelea kuwa tulivu dhidi ya dola ya Marekani. Kwa wastani, shilingi ilibadilika hadi kufikia 2,559.80

kwa Dola, ikilinganishwa na 2,550.81 kwa Dola mwezi uliopita, na 2,613.68 katika kipindi kama hicho mwaka 2025. Aidha, shilingi iliendelea kuimarika, kutokana na kuwepo kwa akiba ya kutosha ya fedha za kigeni, mfumuko mdogo wa bei ikilinganishwa na nchi washirika wa kibiashara, pamoja na nakisi ndogo ya urari wa biashara ya bidhaa, huduma na uhamisho wa mali kutoka nchi za nje. Hali hii pia iliimarishwa na hatua zilizochukuliwa ili kuongeza utulivu katika soko la fedha za kigeni nchini.

#### 4.1.5 Benki Ya Watu Wa Zanzibar (PBZ)

Benki ya Watu wa Zanzibar PBZ katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, benki ilitarajia kupata Mapato kutoka vyanzo vyake vya riba na visivyo na riba kwa TZS. 223 bilioni na ikafanikiwa kupata mapato halisi kwa TZS. 201 billioni ambayo ni sawa na asilimia 90 ya lengo. Vilevile ikilinganishwa na kipindi kama hicho cha mwaka 2024, benki ilipata mapato ya TZS.162 bilioni. Hivyo mapato ya mwaka 2025 yameongezeka kwa asilimia 24. Hii imetokana na Uboreshaji wa mikakati ya uuzaji wa huduma za kifedha, Upanuzi wa mtandao wa matawi na huduma bora.

##### 4.1.5.1 Miradi Ya Maendeleo Ya Benki Ya Watu Wa Zanzibar PBZ – Iliyokamilika Kutoka Julai 2025 Hadi Machi 2026

Kwa upande wa miradi, iliyofanikiwa ndani ya kipindi cha Julai 2025 mpaka Disemba 2025.

i. Kuanza kwa utoaji wa huduma za kibenki kituo cha Ubungo, pamoja na kuboresha tawi la Mpirani kuwa katika muonekano wa kisasa.

ii. Kuanza kwa utoaji wa huduma za kibenki tawi la Arusha, pamoja na vituo vya kutolea huduma vya Konde na Madungu kwa upande wa pemba.

iii. Kufikia Machi 2026 benki imefanikiwa kua na mawakala 2,311 ukilinganisha na kipindi kama hicho cha mwaka 2025 ilikua na mwakala 1,626 ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 42

iv. Benki imefanikiwa kuongeza ATM 3 kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 na kufanya PBZ kufikia idadi ya ATM 55.

v. Benki imefanikiwa kuanzisha huduma ya LIPA HAPA, ambayo inawezesha ufanyikaj wa malipo wa huduma na bidhaa kupitia mabenki mengine na mitandao tofaut ya simu kwa uharaka na ufanisi.

vi. Kuendelea kuboresha PBZ App ili kusaidia wateja kupata huduma iliyokuwa nzuri zaidi na sehem yoyote na wakati wowote.

## 4.2 Mamlaka Ya Usimamizi Wa Bima Tanzania (TIRA)

Kwa mujibu wa Sheria ya Bima Sura 394, shughuli za Mamlaka hufanyika Tanzania Bara na Visiwani. TIRA inaongozwa na Kamishna wa Bima ambaye ndie Mtendaji Mkuu wa Mamlaka chini ya uongozi wa Bodi ya Bima ya Taifa *(National Insurance Board)*. Kamishna wa Bima anasaidiwa na Naibu Kamishna wa Bima ambaye anaongoza shughuli za Mamlaka kwa upande wa Zanzibar.

Majukumu mahsusi ya Mamlaka ni; kusajili na kutoa leseni kwa watoa huduma za Bima; kusimamia mwenendo,ustahimilivu, uendelevu na ukwasi kwa watoa huduma za Bima; Kulinda maslahi ya wateja, walaji na wanufaika wa huduma na bidhaa za Bima; Kuendeleza soko la Bima; Kutoa elimu kwa umma na kuishauri Serikali kuhusu masuala ya Bima.

### 1) Usajili wa watoa huduma za Bima

Mamlaka imesajili aina kumi na saba (17) ya watoa huduma za Bima hapa Tanzania ambao wanaleta jumla ya watoa huduma 2,425. Kati ya aina hizo 17, ni aina sita (6) tu ndiyo zinapatikana na kutoa huduma hapa Zanzibar ambazo zinapelekea kuwa na jumla ya watoa huduma 113 sawa na aslimia 4.66% ya wasajiliwa wote Tanzania na asilimia 6.32% ukilinganisha na uwiano wa zile aina sita za Bima zinazotoa huduma hapa Zanzibar.

**Jadweli Namba 16: Ulingano wa watoa huduma za Bima Zanzibar ukilinganisha na Tanzania.**

| Na. | Watoa huduma za Bima | Idadi | | % ya Jumla |
|---|---|---|---|---|
| | | Tanzania | Zanzibar | |
| 1 | Kampuni za Bima | 35 | 18 | 51.43% |
| 2 | Washauri wa Bima/Madalali | 146 | 2 | 1.37% |
| 3 | Mawakala wa Bima | 1,419 | 81 | 5.70% |
| 4 | Benki wakala | 35 | 6 | 17.14% |
| 5 | Watoa huduma za afya (HSPs) | 154 | 6 | 3.31% |
| **Jumla** | | **1,789** | **113** | **6.32%** |

## 2) Mfumo wa Kusimamia na Kudhibiti Soko la Bima

Katika kuhakikisha soko la Bima linakua imara, thabiti na kutoa huduma kwa mujibu wa Sheria, Mamlaka ina mfumo unaojulikana kama TIRA RBS unatumika kuwasilisha hesabu, kuchambua na kutoa taarifa mbalimbali zinazohusu utendaji wa soko la Bima nchini. Pia ipo mifumo mengine ya TEHAMA inayotumika na Mamlaka kama; TIRA-ORS unaotumika kusajili wa watoa huduma za Bima na TIRA-MIS unatumika kuhakiki Bima zilizotolew. Mifumo hii inasomana na baadhi ya mifumo mengine ya Serikali kama; NIDA, TRA, BRELA, ZRA, BPRA, Polisi n.k kwa lengo la kubadilishana taarifa sahihi na kamili kulingana na mahitajii. Mifumo hii pia imeunganishwa na mifumo ya kampuni zote za Bima nchini.

## 3) Msuluhishi wa migogoro ya Bima (Ombudsman)

Ofisi ya Msuluhishi wa Migogoro ya Bima Tanzania (TIO) ni Taasisi inayojitegemea iliyoanzishwa chini ya sheria ya Bima ya Mwaka 2009 Sura ya 394. Lengo la kuanzisha ofisi hii ni kutatua migogoro baina ya wateja wa Bima na kampuni za Bima kupitia njia za usuluhishi nje ya utaratibu wa kawaida wa kimahakama. TIO imefungua madawati kwenye ofisi za Kanda kwa lengo la kupokea na kusajili migogogoro ambayo hapo awali walalamikaji walikuwa wanapeleka moja kwa moja ofisini kwao (TIO). Lengo la kufungua madawati haya ni kuisogeza ofisi karibu na wananchi na kuwapunguzia gharama za usafiri. Maafisa kutoka TIO huwa wanatembelea ofisi za Kanda ikiwemo Zanzibar pale uhitaji wa kufanya hivyo unapotokea na hushirikiana kwa karibu na maafisa wengine wa Kanda hizo.

### 4) Mipango Mikakati na Matarajio ya baadaye ya Mamlaka.

Mpango Mkakati wa Mamlaka ni kuendeleza Mpango Mkuu wa Taifa wa Sekta ya Fedha nchini (Financial Sector Development Master Plan-2020-2030). Mpango huu unalenga kuongeza uelewa wa Bima hadi kufikia asilimia 80, matumizi ya Bima asilimia 50, na pia kuhamasisha Kampuni za Bima kuandaa bidhaa za Bima zinazohitajika na wananchi ili kuakisi uchumi wa kijani na uchumi wa bluu.

Matarajio ya baadae ya Mamlaka yanaendana na shabaha mahususi zilizoainishwa katika Mpango Mkuu wa Maendeleo wa Sekta ya Fedha (FSDMP 2020/21 – 2029/30) na kwenye Sera ya Uchumi wa Bluu kama ifuatavyo: -

i. Kukamilishwa kwa Sera ya Bima ya Taifa (National Insurance Policy - NIP);

ii. Kuendelea na uunganishwaji wa mifumo ya TEHAMA ya usimamizi wa Bima kati ya TIRA na Taasisi zingine za Serikali kama Mamlaka ya Usafiri na Usalama Barabarani Zanzibar (ZARTSA)

iii. Kushiriki kwenye mchakato wa marekebisho ya Sheria ya Bima kwa Vyombo vya Moto Zanzibar unaoratibiwa na ZARTSA ili iendane na uhalisia wa sasa

iv. Kukamilisha kwa Kanuni za Bima za Lazima. TIRA kama msimamizi wa Bima inaendelea kukamilisha kanuni za Bima za lazima katika maeneo ya; Majengo ya Biashara, Masoko ya Umma, Bidhaa zinazotoka nje, Vyombo vya Usafiri wa Majini kama vile Meli, Boti na Feri au Vivuko.

Aidha, Mamlaka kwa kushirikiana na wadau mbalimbali itaendelea na utekelezaji wa matakwa ya Mpango Mkuu wa Serikali wa Kuendeleza Sekta ya Fedha (FSDMP) ikiwemo, kutekeleza mkakati wa kitaifa wa elimu ya Bima; kutekeleza mkakati wa kitaifa wa Bima jumuishi na kuweka na kutekeleza mfumo madhubuti wa kushughulikia madai, malipo na malalamiko ya wateja.

### 4.2.1 Hali Ya Soko La Huduma Za Bima Zanzibar.

Hali ya soko la Bima kwa upande wa Zanzibar kwa kipindi cha Oktoba hadi Disemba 2025 imeimarika kwenye bidhaa nyingi kasoro Vyombo vya Moto na Anga. Biashara ya Bima imekuwa kwa asilimia 222% ambapo kukua huko kumesababishwa na kuongezeka kwa kiwango kikubwa bidhaa zinazounda kundi la Bima nyinginezo ikiwemo Bima za Miamala ya Fedha (Money Insurance), Bima ya Wasafiri Wanaoingia nchini (Inbound Travelling Insurance), Bima za Wizi, Fidia kwa Wafanyakazi (Worksman Compensation), Hati Funganii, nk. Makampuni ya Bima yanayotoa huduma yameendeelea kubaki kumi na nane (18) huku Mawakala wa wa Bima wakiongezeka na kufikia 81.

Biashara zenye thamani ya Bilioni 94.77 kwa bidhaa zote za Bima ziliandikishwa ambapo madai yaliyolipwa yalikuwa na thamani ya Bilioni 14,33 ambayo yalilipwa kwa wahanga 3,594 .

### 4.2.2 Mafanikio Ya TIRA Na Bima

I. Utekelezaji wa bima ya wageni wanaoingia nchini kama hatua ya kimkakati ya kuimarisha sekta ya utalii zanzibar

II. Kuimarika kwa huduma za takaful

III. Kuimarishwa kwa ushirikiano wa taasisi (inter-agency coordination) kwenye utekelezaji wa bima za lazima. Kuwa na mashirikiano ya kimfumo na ZRA, Jeshi la Polisi Zanzibar na sasa wapo kwenye majadiliano na ZARTSA.

IV. Uhamasishaji na elimu ya bima kwa umma ambapo tumekuwa tukishiriki matukio mbalimbali ikiwemo maonyesho ya biashara na nanenane.

V. Kufungua Ofisi za Kanda za Unguja na Pemba

### 4.2.3 Matumizi ya Bima Kwa SMZ

Katika kutambua matumizi ya Bima kwenye mali za serikali, TIRA imekuwa ikifanya kaguzi mbalimbali kwa vyombo vya moto vinavyopita kwenye barabara za umma kwa lengo la kuhakikisha mtu wa tatu analindwa pindi janga linapotokea. Vilevile TIRA imekuwa ikifanya uhakiki wa Bima kwa majengo

ya watu binafsi hasa mahoteli kwa lengo la kuwahamasisha kukata Bima ili kuweza kufidiwa pale majanga ambayo hayakutarajiwa pindipo yanapotokea.

Muitikio wa matumizi ya Bima za lazima na zile za hiyari bado ni mdogo, hali ambayo inayotaka kuongezewa nguvu kwenye suala zima la utoaji elimu kwa Umma.

#### 4.2.3.1 Kuendelea Kutoa Elimu Endelevu ya Bima kwa Umma

Katika jitihada za kuimarisha utoaji wa elimu ya Bima kwa Umma, mbinu mbalimbali zimeendelea kutumika ikiwemo kutoa elimu kupitia warsha na matamasha mbalimbali yalifanyika Zanzibar.

### 4.3 Utekelezaji Wa Bima Ya Safari *(Inbound Travel Insurance)*

i. Shirika la Bima la Zanzibar (ZIC) kupitia bidhaa mpya ya Bima ya Safari (Inbound Travel) ambayo ilianza kutekelezwa tarehe 24 Julai 2024, limeendelea kufanya maboresho katika upatikanaji wa huduma hiyo kwa watalii na wageni wanaoingia Zanzibar hivyo kupunguza changamoto zilizojitokeza awali wakati wa utekelezaji. Bidhaa hiyo inalenga kutoa kinga ya Bima kwa wageni na watalii wote wanaoingia Zanzibar kutoka nje ya nchi. Huduma hiyo inaendelea kuwapa watalii na wageni uhakika wa kinga dhidi ya majanga mbalimbali wakati wakiwa Zanzibar. Utekelezaji wa Bima ya safari kwa watalii na wageni wanaoingia Zanzibar imechangia kuongeza mapato ya Sekta ndogo ya Bima na kuchochea ukuaji wa Sekta ya Utalii Zanzibar.

### 4.4 Changamoto

i. Ushiriki mdogo wa wananchi katika pogramu za elimu kwa umma kama vile maonesho .
ii. Kiasi kidogo cha adhabu kwa vyombo vya moto kutokana na makosa ya bima. Hali hiyo inapelekea baadhi ya watu kuamua kutokuwa na Bima.
iii. Baadhi ya vyombo vya moto vya Serikali kutokuwa na Bima wakati ni takwa la kisheria na inapaswa kuwa mfano.

**Jadweli Namba 17: Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar kwa bidhaa za Bima Julai 2025- Machi 2026**

| Nam. | Bidhaa | Jumla ya ada za Bima | | Ziada/ Pungufu |
|---|---|---|---|---|
| | | Julai-Disemba 2025 | Julai25- Machi2026 | |
| 1 | Moto | 6,519,894,433 | 13,307,901,462 | 104% |
| 2 | Ufundi | 1,141,532,379 | 5,966,885,287 | 423% |
| 3 | Majini | 1,422,757,363 | 3,250,021,156 | 128% |
| 4 | Vyombo vya Moto | 5,635,852,469 | 8,063,893,974 | 43% |
| 5 | Mchang anyiko | 27,699,303,816 | 38,021,576,493 | 37% |
| 6 | Anga | 714,749,378 | 22,505,619,093 | 3049% |
| 7 | Afya | - | 764,278,069 | 0% |
| 8 | Nyenginezo | 1,221,103,533 | 2,414,133,525 | 98% |
| 9 | Maisha | 315,589,407 | 471,365,127 | 49% |
| | **Jumla** | **44,670,782,777** | **94,765,674,187** | **112%** |

***Chanzo: Kampuni za Bima zilizopo Zanzibar***

**Jadweli Namba 18: Hali ya soko la huduma za Bima Zanzibar kwa kampuni Julai 2025-Machi 2026.**

| Nam | Makampuni ya Bima | Thamani ya Bima za kawaida | Idadi ya mika taba ya Bima za kawaida | Tha mani ya Bima za maisha | Idadi ya Mikat aba ya Bima za maisha | Jumla ya thamani ya Bima | Juml a ya Mikataba ya Bima |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BUMACO | 1,121,90 9,001 | 7004 | - | 0 | 1,121,909,001 | 7,004 |
| 2 | HERITAGE | 2,100,200,513 | 5600 | - | 0 | 2,100,200,513 | 5,600 |
| 3 | MAYFAI R | 572,076,234 | 3879 | - | 0 | 572,076,234 | 3,879 |
| 4 | NIC | 857,776,274 | 355 | 36,116,676 | 631 | 893,892,950 | 986 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 5 | MUA | 1,855,637,488 | 590 | - | 0 | 1,855,637,488 | 590 |
| 6 | RELIANCE | 296,082,039 | 1909 | - | 0 | 296,082,039 | 1,909 |
| 7 | SANLAMGEN | 11,023,126,330 | 1835 | - | 0 | 11,023,126,330 | 1,835 |
| 8 | SANLAM LIFE | - | 0 | 435,248,451 | 6647 | 435,248,451 | 6,647 |
| 9 | STRATE GIES | 1,576,287,321 | 3265 | - | 0 | 1,576,287,321 | 3,265 |
| 10 | NEWTAN | 155,999,023 | 468 | - | 0 | 155,999,023 | 468 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 11 | ZIC | 68,753,320,293 | 393513 | - | 0 | 68,753,320,293 | 393,513 |
| 12 | ICEA LION | 992,317,769 | 13711 | - | 0 | 992,317,769 | 13,711 |
| 13 | MILEMB E | 20,036,400 | 85 | - | 0 | 20,036,400 | 85 |
| 14 | FIRST ASSURA NCE | 444,626,704 | 2509 | - | 0 | 444,626,704 | 2,509 |
| 15 | GA INSURAN CE | 64,512,410 | 473 | - | 0 | 64,512,410 | 473 |
| 16 | MO ASSURA NCE | 329,531,445 | 2596 | - | 0 | 329,531,445 | 2,596 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 17 | TANZINDIA | - | 0 | - | 0 | - | - |
| 18 | ZIC TAKAFUL | 4,130,869,817 | 55675 | - | 0 | 4,130,869,817 | 55,675 |
| | JUMLA | 94,294,309,061 | 493467 | 471,365,127 | 7278 | 94,765,674,187 | 500,745 |

***Chanzo: Kampuni za Bima zilizopo Zanzibar***

**Jadweli Namba 19: Hali ya malipo ya fidia ya Majanga ya Bima Zanzibar Kuanzia Julai 2025- Machi 2026**

| Nam | Makampuni ya Bima | Thamani ya fidia za majanga ya Bima za kawaida | Idadi ya fidia za Bim a za kawai da | Thamani ya fidia za majang a ya Bima za maisha | Idadi ya fidia za Bim a za maisha | Jumla ya thamani ya fidia za majanga ya Bima | Ju mla ya Idadi Ya fidia za Bima |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | BUMACO | 21,864,148 | 6 | - | - | 21,864,148 | 6 |
| 2 | HERITAGE | 5,089,467,827 | 65 | - | - | 5,089,467,827 | 65 |
| 3 | MAYFAIR | 1,450,903 | 34 | - | - | 1,450,903 | 34 |
| 4 | NIC | 136,675,152 | 2 | 20,158,296 | 31 | 156,833,448 | 33 |
| 5 | MUA | - | - | - | - | - | - |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 6 | RELIANCE | 1 | 2 | - | - | 1 | 2 |
| 7 | SANLAM GEN | 845,818,004 | 73 | - | - | 845,818,004 | 73 |
| 8 | SANLAM LIFE | - | - | 270,020,662 | 1,488 | 270,020,662 | 1,488 |
| 9 | STRATEGIES | 4,570,509,368 | 1,271 | - | - | 4,570,509,368 | 1,271 |
| 10 | NEWTAN | 21,226,262 | 2 | - | - | 21,226,262 | 2 |
| 11 | ZIC | 2,584,178,532 | 509 | - | - | 2,584,178,532 | 509 |
| 12 | ICEA LION | 200,314,320 | 26 | - | - | 200,314,320 | 26 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 13 | MILEMBE | - | - | - | - | - | - |
| 14 | FIRST ASSURANCE | - | 5 | - | - | - | 5 |
| 15 | GA INSURANCE | - | | - | - | - | - |
| 16 | MO ASSURANCE | - | 1 | - | - | - | 1 |
| 17 | TANZINDI A | - | - | - | - | - | - |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 18 | ZIC TAKAFUL | 565,853,819 | 79 | - | - | 565,853,819 | 79 |
| | JUMLA | 14,037,358,336 | 2,075 | 290,178,959 | 1,519 | 14,327,537,295 | 3,594 |

## 4.5 Shirika La Bima Zanzibar (ZIC)

Shirika la Bima la Zanzibar ni Taasisi ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar iliyoanzishwa mwaka 1969 kwa legal notes Namba 11 ya mwaka 1969. Shirika kwa sasa linafanya kazi zake chini ya Sheria ya Msajili wa Hazina namba 6 ya mwaka 2021 na Sheria ya bima namba 10 ya mwaka 2009 ya Jamuhuri ya Muungano wa Tanzania.

Shirika lilianzishwa likiwa na Ofisi moja tu iliyopo Zanzibar. Baada ya kuanzishwa kwa soko huria mwaka 1990, Shirika lilifungua Ofisi Pemba na Tanzania Bara. Shirika la Bima la Zanzibar hadi sasa lina jumla ya Ofisi kumi na moja (11). Ofisi hizo ni kama zifuatazo: - Ofisi ya Makao Makuu Mpirani, Ofisi ya Tawi Amani Unguja, Ofisi ya Tawi Pemba, Kanda ya Pwani Dar es salaam, Kanda ya Ziwa Mwanza, Kanda ya kati Dodoma, Kanda ya Nyanda za Juu Kusini Mbeya, Kanda ya Kaskazini Arusha, Kanda ya Kusini Mtwara, Ofisi ya mauzo Tanga, na Ofisi ya mauzo Kahama. Vile vile Shirika linatoa huduma zake katika maeneo mbali mbali kupitia ofisi za Mawakala na Madalali ambapo hadi sasa Shirika lina jumla ya Mawakala mia moja na thelathini (130) na Madalali kumi (10). Vilevile Shirika lina jumla ya Wafanyakazi mia moja themanini na mbili (182) kati ya hao wanaume ni mia na nne (104) na wanawake ni sabini na nane (78).

### 4.5.1 Majukumu Makuu ya Shirika la Bima Zanzibar

Shirika la Bima la Zanzibar limepangiwa kutekeleza miongoni mwa majukumu yake kama ifuatavyo: -

i. Kusimamia mapato ya Shirika kutokana na vyanzo mbali mbali vya mapato. Mapato hayo yanajumuisha bima za Magari, bima za Moto, Meli, na mchanganyiko pamoja na mapato yatokanayo na Uwekezaji;

ii. Kusimamia Mali za Shirika kupitia usimamizi wa ununuzi, utunzaji na uondoaji wa mali za Shirika kwa mujibu wa Sheria za Ununuzi;

iii. Kusimamia fedha za Shirika. Katika jukumu hili Shirika linasimamia utekelezaji wa Bajeti yake kwa kila mwaka wa fedha, huduma za Uhasibu na ukaguzi wa ndani na ukaguzi wa nje;

iv. Shirika linasimamia maendeleo ya Sekta ya Bima Tanzania kwa kushirikiana na wadau wote na;

v. Kusimamia Teknolojia ya Habari, na Mawasiliano (TEHAMA) kupitia mifumo inayohusisha kudhibiti mapato na matumizi ya Shirika.

### 4.5.2 Utekelezaji wa Bajeti ya Shirika kwa Mwaka wa Fedha 2025/2026

Shirika la Bima la Zanzibar utekelezaji wa bajeti yake umegawika katika maeneo makuu manne (4), maeneo hayo ni.

i Mapato yatokanayo na mauzo ya bima;

ii Utekelezaji wa matumizi ya uwendeshaji (Management Expenses)

iii Utekelezaji wa matumizi ya Madai kwa wateja na

iv Utekelezaji wa matumizi ya ujira kwa Mawakala na Madalali.

### a. Mapato

Katika kipindi cha Julai – Machi 2026, Shirika limefanikiwa kukusanya jumla ya TZS 122.9 bilioni ya mauzo ya bima ambayo ni sawa na asilimia 112 ya makadirio ya kukusanya TZS 109.7 bilioni katika kipindi cha tathmini.

Shirika limeweza kufikia malengo ya ukusanyaji wa mapato hayo katika kipindi hicho kwa kutekeleza mikakati ifuatayo: -

i. Shirika limeendelea kutoa taaluma na kujitangaza kwa Wananchi na kwa Taasisi mbalimbali za Serikali na binafsi juu ya suala la kujiwekea kinga mali zao kwa lengo la kuongeza mapato ya Shirika;

ii. Shirika limeendelea kuzidisha mashirikiano ya utekelezaji wa majukumu yake kwa mawakala na madalali wake wanaofanya baishara ya kuuza bima kwa niaba ya Shirika;

iii. Shirika limeendelea kushirikiana kikamilifu na mabenki mbalimbali katika mfumo wa "Bancassurance" kwa lengo la kuongeza mapato yake; na

iv. Shirika limeendelea kushirikiana na Serikali ya Mapinduzi Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano Tanzania kwa kuhakikisha Miradi mikubwa ya Maendeleo na Mkakati kwa Wananchi inakatiwa kinga za bima na Shirika.

**b. Matumizi**

Utekelezaji wa matumizi ya Shirika kwa mwaka fedha kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, yamegawika katika mchanganuo kama ufuatavyo: -

i TZS 12.7 bilioni zilitumika kwa ajili ya gharama za uwendeshaji wa ofisi (*Management Expenses*) sawa na asilimia 88 ya makadirio ya matumizi katika kipindi cha tathmini ambayo ni TZS 14.4 bilioni;

ii TZS 8.1 bilioni zimetumika kulipa madai 884 mbalimbali ya wateja waliopata ajali na kutimiza matakwa ya Sheria za bima ambayo ni sawa na asilimia 48 ya makadirio TZS 16.8 bilioni katika kipindi cha tathmini;

iii TZS 6.26 milioni zimetumika katika kulipa ujira kwa mawakala na madalali wanaofanya biashara ya bima kwa niaba ya Shirika ambayo sawa na asilimia 64 ya makadirio katika kipindi cha tathmini ya TZS 9.8 bilioni.

**c. Mafanikio**

Chini ya usimamizi wa Serikali ya Mapinduzi Zanzibar, Shirika limeendelea kufanya kazi zake kwa kutoa huduma bora kwa Wananchi Tanzania nzima na limepata mafanikio mbalimbali kama ifuatavyo: -

**a) Uwanzishwaji wa Bima ya lazima ya Wasafiri wanaoingia Nchini (*Mandatory Inbound Travel Insurance*)**

Shirika limefanikiwa kuendelea kutoa kinga ya bima ya lazima ya Wasafiri wanaoingia Nchini ni bima inayowakinga wageni wote wanaoingia Zanzibar dhidi ya majanga mabalimbali yanayowapata wanapokua Nchini. Serikali ya Mapinduzi Zanzibar imeifanya kuwa sharti kwa wageni wote wanaoingia Nchini ili kuhakikisha wageni wanakuwa na kinga dhidi ya afya zao, na majanga mengine.

**i Faida zinazopatikana kwa Wageni**

- Kugharamiwa matibabu, pamoja na huduma nyengine pale inapotokea dharura kama vile ajali, kupoteza mizigo yao pamoja na huduma nyengine za dharura.
- Kupata usalama na utulivu wanapokua Nchini.

**ii Faida Kwa Serikali**

- Kupunguza mzigo wa kugharamia matibabu ya wageni.
- Kuongeza mapato kupitia ada za bima.
- Kuimarisha taswira ya Zanzibar nje ya mipaka yake kama eneo salama la utalii.

**iii Faida Kwa Shirika**

- Kuongezeka kwa mapato Shirika la Bima la Zanzibar
- Kuimarika kwa teknolojia na mifumo ya usajili wa wageni pamoja na kupanua wigo wa kutoa huduma za Shirika kimataifa.
- Kuongezeka kwa utambulisho na ushindani wa Shirika kimataifa.

**iv Faida kwa Sekta ya Utalii Nchini**

- Kuongeza uaminifu wa kimataifa kwa Zanzibar.
- Kuwavutia waandaaji wa safari na kuongeza ushindani wa Zanzibar dhidi ya visiwa vingine vya utalii.

**b) Kukuwa kwa Sehemu ya Soko la Bima na Nafasi ya Shirika.**

Kwa mwaka fedha 2025/2026 Shirika limeendelea na limeimarisha nafasi yake katika soko la bima Tanzania kwa kiwango kikubwa ambapo sehemu ya soko (*Market share*) ni asilimia 11.02, na vilevile, Shirika limefanikiwa kushika nafasi ya 3 kati ya makampuni 30 yanayofanya biashara ya bima Tanzania.

**Mafanikio haya yamepatikana kutokana na:**

- Ufanisi wa mikakati ya uuzaji na usambazaji wa huduma ya bima.
- Ushindani ulioboreshwa dhidi ya makampuni mengine ya bima.
- Kuongezeka kwa uaminifu kwa wateja wa Shirika.
- Kuwepo kwa mashirikiano mazuri ya kimkakati kati ya Shirika, Mawakala na Madalali.
- Shirika limeweza kulipa madai ya aina mbalimbali ya halali na yaliyohakikiwa kwa wateja wake kwa wakati.
- Wafanyakazi wameendelea kupatiwa mafunzo mbalimbali ya kuwajengea uwezo na kuboresha utendaji kazi wao.
- Shirika limefanikiwa kuongeza wigo wa Biashara ya Bima kwa mashirikiano ya kimkakati na Makampuni na Mabenki mbalimbali katika mfumo wa (Bancassurance) kama vile (VodaBima, Zanztel Yas Bima, Shirika la Posta Tanzania, NMB Bank, CRDB Bank, EXIM Bank, TCB Bank, DCB Bank, NBC Bank, BOA Bank, Mwalimu Commercial Bank, Equity Bank, MUKOBA Bank na PBZ Bank).

**c) Mageuzi ya Kidijitali (*ZIC Digital Transformation*)**

Shirika limefanikiwa kufanya mageuzi makubwa katika sekta ya bima Nchini kupitia "Digital Transformation" kama ifuatavyo: -

**i Kuanzishwa kwa Programu ya Bima kiganjani (*ZIC Bima App*)**

- Kuwawezesha wateja kununua bima moja kwa moja kwa kutumia simu zao;
- Kufanya Malipo ya bima kwa njia za kidijitali;
- Kuwapunguzia wateja uhitaji wa kufika ofisini kwa kupata huduma za bima;
- Kuongeza upatikanaji wa huduma kwa mikoa yote Tanzania.

**ii Kuanzishwa kwa Mfumo wa Kidijitali wa Usimamizi wa Madai (*Digital Claims Management System*)**

- Kumuwezesha mteja kuleta madai pasi na kufika ofisini kwa kutumia njia ya kidijitali;
- Kuliwezesha Shirika kupokea madai na kuyafanyia kazi kwa wakati kwa mujibu wa miongozo ya Mamlaka ya Usimamizi wa Bima Tanzania (TIRA) na;
- Kuongeza uwazi na uwajibikaji kwa Shirika pamoja na kupunguza malalamiko ya wateja.

**iii Shirika limefanikiwa kuanzisha Kituo cha Huduma kwa Wateja cha Saa 24/7 (*24/7 Customer Service Centre*)**

- Kutoa huduma kwa wateja kupitia kituo cha huduma kwa wateja (*Call Center*), *(WhatsApp)*, na Mitandao ya kijamii (*Social Media*).
- Kuwahudumia wateja na kupata majibu ya shida zao ndani ya muda mfupi.
- Kutunza kumbukumbu ya malalamiko ya wateja pamoja na mtiririko wa shida zao na kuzitumia kumbukumbu hizo kwa ajili ya kuboresha huduma za Shirika.

**d) Mafanikio katika kutoa kinga ya bima kwa Ulinzi kwa Miradi ya Kimkakati ya Serikali**

Shirika limefanikiwa kutoa kinga dhidi ya majanga yatokanayo na miradi mbalimbali ya Serikali kama vile, Barabara kuu na zandani, Miradi ya kimaendeleo kama Hospitali na Majengo mbalimbali ya Serikali.

Vile vile, Shirika limefanikiwa kuhakikisha kuwa sekta ya uvuvi kupitia Sera ya Uchumi wa buluu inalindwa kwa kuhakikisha boti zilizotolewa kwa shughuli za uvuvi zinapatiwa kinga dhidi ya majanga mbalimbali kama vile kuzama, kupotea n.k ili kuhakikisha Uchumi wa Wananchi unaendelea kubaki salama.

**e) Uzinduzi na umiliki wa ZIC Takaful (Bima ya Kiislamu)**

Shirika limefanikiwa kuwa taasisi ya kwanza Tanzania kuanzisha kampuni

tanzu ya Bima ya Kiislamu Takaful, hatua iliyoleta mabadiliko makubwa katika wigo wa kifedha nchini.

**Huduma Zinazotolewa Kupitia Kampuni Tanzu Ya Takaful**

- Bima inayozingatia misingi na maadili ya Shariah.
- Mfumo wa uwakala unaofuata kanuni na taratibu za Kiislamu.
- Ujumuishwaji wa Wananchi ambao hapo awali hawakunufaika na bima za kawaida.

**Faida kwa Taifa**

- Upanuzi wa soko la bima na utoaji huduma jumuishi kwa Wananchi unaofuata misingi ya Kisharia.
- Kuimarika Kwa ujumuishwaji wa kifedha miongoni mwa jamii zenye imani tofauti.
- Kuongezeka Kwa mapato ya Taifa kupitia huduma mpya za kifedha ya Bima ya Kiislamu.
- Kuchochea maendeleo ya sekta ya fedha yenye uadilifu na miiko ya kidini kwa Wananchi.

**f) Uwanzishwaji wa kutoa huduma za Bima ya Maisha**

Shirika lipo katika hatua za kuanza kutoa huduma za Bima ya Maisha kwa Wananchi.

**Faida za Bima**

- Kuongeza mapato ya Shirika.
- Kuongeza wigo wa kuweza kuwafikia Wananchi.
- Kutoa huduma zote za bima chini ya Shirika moja kwa Wananchi.
- Kuwapa kinga za maisha pale panapotokea majanga ya maisha yao.
- Kuwapatia huduma za akiba ya muda mrefu Kwa mujibu wa matakwa ya Wananchi kwa bidhaa (Product) watakayohitaji.

- Kupunguza athari za utegemezi kwa wanufaika pindi panapotokezea majanga ya kifo au ulemavu wa kudumu.

### 4.5.3 Changamoto na Utatuzi

Pamoja na mafanikio yaliyopatikana katika utekelezaji wa majukumu yake, Shirika linakabiliwa na changamoto mbali mbali licha ya jitihada zinazochukuliwa na Shirika katika kuzipatia ufumbuzi, changamoto hizo ni kama zifuatazo: -

- Baadhi ya Taasisi za Serikali Zanzibar bado zinashindwa kulipia malipo ya bima kwa wakati licha ya kuwahi kuchukuwa ankara za malipo hayo na Taasisi nyengine za Serikali kutokata kabisa kinga za Bima za magari na mali za Serikali ya Mapinduzi Zanzibar.

#### 4.5.3.1 Utatuzi wa Changamoto:

- Shirika linaendelea kushirikiana na Wizara ya Fedha na Mipango pamoja na Ofisi ya Msajili wa Hazina Zanzibar katika kuzifuatilia Taasisi hizo na kuhakikisha zinakata bima za mali na magari ya Serikali.
- Shirika linakabiliana na changamoto ya kutokupewa kipaumbele na usaidizi kutoka kwa Taasisi na Idara Kuu za Serikali zenye dhamana ya kusimamia Miradi Mikubwa ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kuipa kinga za bima Miradi hiyo inayotekelezwa hapa Nchini.
- Shirika linandelea kuomba usaidizi kupitia Wizara ya Fedha na Mipango kutoa miongozo kwa Taasisi na Idara zote zenye dhamana ya kusimamia Miradi Mikubwa ya Serikali kwa kuweka vipengele katika mikataba kwa kuhakikisha Kinga za bima zinatolewa na Shirika la Bima la Zanzibar badala ya kupewa Makampuni binafsi ya bima Nchini.
- Kuwepo kwa ushindani mkubwa katika soko la bima Tanzania unaosababishwa na kuongezeka kwa Makampuni yanayotoa huduma hizo za bima kwa Wananchi, vilevile kuruhusiwa kwa Mabenki katika mfumo wa Benki Bima “Bancassurance” kutoa huduma za bima Nchini.

- Shirika linaendelea kuleta ushindani utakaowezesha kufikia malengo yake ya ukusanyaji wa mapato yanayotokana na mauzo ya bima.

### 4.6 Mfuko Wa Hifadhi Ya Jamii Zanzibar (ZSSF)

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar (ZSSF), umeanzishwa chini ya sheria nambari 2 ya mwaka 1998 ambayo ilifanyiwa mapitio makubwa na kuundwa upya na sheria nambari 2 ya mwaka 2005. Lengo kuu ni kutoa hifadhi ya jamii kwa njia ya kulipa mafao kwa wanachama wachangiaji katika sekta za Serikali na sekta Binafsi.

Malengo mengine madogo ya Mfuko wa Hifadhi ya Jamii ni haya yafuatayo:

i. Kusajili wanachama waajiri, waajiriwa na wanaojiajiri.

ii. Kukusanya michango ya wanachama.

iii. Kuweka taarifa za wanachama kwa usahihi na

iv. Kuwekeza fedha zinazokusanywa ili kuwezesha kuwalipa wanachama mafao yao.

Ripoti hii inaeleza utekelezaji wa shughuli za Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar na Maendeleo yake kwa kipindi cha kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026 kwa mwaka wa fedha 2025/2026 ikijumuisha mafanikio, changamoto, mikakati pamoja matarajio ya baadae kama ifuatavyo: -

#### 4.6.1 Utekelezaji Kwa Kipindi Cha Julai 2025 Hadi Machi 2026

Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko umeendelea na utekelezaji wa majukumu yake kwa mujibu wa Mpango Kazi wa Mwaka wa fedha 2025/2026 kama ifuatavyo: -

**1) Usajili wa Wanachama**

**i. Usajili wa waajiri**

Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko umesajili waajiri 263 sawa na asilimia 90 ya makisio ya kuwasajili waajiri 293 na hadi sasa. Mfuko una Waajiri waliosajiliwa wamekifikia 3,668 ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2024 hadi Machi 2025. Mfuko

ulitarajia kusajili waajiri 289, Waajiri 245 wamesajiliwa, ikiwa ni sawa na asilimia 85. Idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hadi kufikia mwezi Machi 2025 ni 3,327 kwa Mfuko wa lazima.

**ii. Idadi ya wanachama kwa Mfuko wa lazima**

Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko umesajili waajiriwa 12,418 sawa na asilimia 62 ya makisio ya kuwasajili waajiriwa 20,160 na hadi sasa Mfuko una wajiriwa waliosajiliwa ni 166,464 ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2024 hadi Machi 2025. Mfuko ulitarajia kusajili waajiriwa 21,792 na kufanikiwa kusajili waajiriwa 11,655, sawa na asilimia 53. Idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hadi kufikia mwezi Machi 2025 ni 153,351 kwa Mfuko wa lazima.

**iii. Idadi ya wanachama kwa Mfuko wa Hiari**

Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko wa Hiari umesajili wanachama 1,963 sawa na asilimia 24 ya makisio ya kuwasajili wanachama 470. Hadi sasa idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii wamefikia 13,968 kwa Mfuko wa kujichangia kwa Hiari ukilinganisha na kipindi kama hiki cha Julai 2024 hadi Machi 2025. Mfuko wa Hiari ulitarajia kusajili wanachama 1,797, Wanachama 769 wamesajiliwa, sawa na asilimia 43. Idadi ya wanachama wa Mfuko wa Hifadhi ya Jamii hadi kufikia mwezi Machi 2025, ni 13,364 kwa Mfuko wa kujichangia kwa Hiari.

Kwa kulinganisha utekelezaji wa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026 na Julai 2024 hadi Machi 2025, malengo ya usajili yameonekana kutokufikiwa. Hii imetokana na kupungua kwa ajira za Serikali, kutokukamilika vielelezo vya kufanyiwa usajili kwa baadhi ya waajiriwa ambapo kumechangia kupungua kwa usajili wa wanachama. Kwa upande wa Mfuko wa Hiari bado mwamko ni mdogo wajamii katika kujiwekea akiba ya baadae ndio sababu ya kutofikia malengo ya usajili.

### 4.6.2 Michango Ya Wanachama

Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kukusanya TZS 155.08 bilioni kutoka kwa michango ya wanachama na zilikusanywa TZS 135.90 bilioni sawa na asilimia 88 ya ufanisi ukilinganisha

kipindi kama hiki cha Julai 2024 hadi Machi 2025. Mfuko ulikusanya TZS 117.18 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 16. Mchanganuo wa michango ya wanachama kama ufuatavyo: -

i. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kukusanya TZS 146.27 bilioni kutokana na Mfuko wa lazima. Hadi kufikia March 2026 mfuko ulikusanya TZS 129.10 bilioni sawa na asilimia 88 ya lengo. Ukilinganisha na TZS 111.24 bilioni zilizokusanywa kwa kipindi kama hicho mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 16.

ii. Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kukusanya TZS 54.51 milioni kutokana na adhabu ya michango. Hadi machi 2026 Mfuko ulikusanya jumla ya TZS 56.44 milioni sawa na asilimia 104 ukilinganisha kipindi kama hiki mwaka 2024 Mfuko ulikusanya TZS 31.10 milioni sawa na ongezeko la asilimia 81.

iii. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kukusanya TZS 524.85 milioni kutokana na Mfuko wa hiari. Hadi kufikia Machi 2026 Mfuko ulikusanya jumla ya TZS 409.55 milioni sawa na asilimia 78 ukilinganisha na kipindi kama hichi mwaka 2024,Mfuko ulikusanya TZS 422.52 milioni sawa na upungufu wa asilimia 3.

iv. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kukusanya TZS 7.31 bilioni kutokana na Skimu ya Fidia na zilikusanywa TZS 6.33 bilioni sawa na asilimia 87 ukilinganisha mwaka Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko ulikusanya jumla ya TZS 5.48 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 16

v. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kukusanya TZS 922.04 milioni kutokana na Hifadhi ya Jamii kwa Misingi ya Shariahadi kufikia Machi 2026, Mfuko haujaanza kukusanya michango kutokana na Hifadhi ya Jamii kwa Misingi ya Sharia.

### 4.6.3 Malipo ya Mafao na Marejesho kwa Wanachama

Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kutumia jumla ya TZS 83.38 bilioni kulipia mafao. Hadi kufikia Machi 2026 Mfuko umelipa jumla ya TZS 69.18 bilioni sawa na asilimia 83 ya makadirio ukilinganisha na kipindi kama hichi 2024 Mfuko ulitumia jumla ya TZS 66.86 bilioni, kwa ajili ya kulipa mafao sawa na ongezeko la asilimia 3. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa idadi ya wastaafu waliostaafu katika kipindi hicho.

**Mchanganuo wa michango ya wanachama kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kama ufuatavyo: -**

i. Mfuko ulipanga kulipa mafao ya uzeeni (kiinua mgongo) kwa TZS 26.58 bilioni kwa wanachama 1,021. Jumla ya wanachama 864 wamelipwa mafao yao na jumla ya TZS 22.67 bilioni zimetumika sawa na asilimia 85 ya makadirio ukilinganisha kipindi kama hicho mwaka 2024. Mfuko uliwalipa jumla ya wanachama 855 kwa jumla ya TZS 23.59 bilioni zimetumika sawa na upungufu wa asilimia 4.

ii. Mfuko ulipanga kulipa mafao ya urithi kwa TZS 3.59 bilioni kwa wanachama 114. Jumla ya wanachama 117 wamelipwa mafao na jumla ya TZS 3.82 bilioni zimetumika sawa na asilimia 107 ya makadirio. Ukilinganisha Julai 2024 hadi Machi 2025. Mfuko umelipa jumla ya TZS 3.37 bilioni kwa wanachama 61 sawa na ongezeko la asilimia 13.

iii. Mfuko ulipanga kulipa wastaafu 13,993 kwa TZS 40.90 bilioni. Jumla ya wastaafu 14,335 wamelipwa pencheni na jumla ya TZS 32.27 bilioni zimetumika sawa na asilimia 79 ya makadirio ukilinganisha Julai 2024 hadi Machi 2025. Mfuko uliwalipa jumla ya wastaafu 13,419 kwa jumla ya TZS 32.46 bilioni zimetumika sawa na upungufu wa asilimia 0.6.

iv. Mfuko ulipanga kulipa mafao ya ulemavu kwa TZS 1.22 bilioni kwa wanachama 58. Jumla ya wanachama 12 wamelipwa mafao na jumla ya TZS 487.97 milioni zimetumika sawa na asilimia 40 ya makadirio. Ukilinganisha na mwaka uliopita kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko uliwalipa jumla ya wanachama 14 kwa jumla ya TZS 541.10 milioni zimetumika sawa na upungufu wa asilimia 10.

v. Mfuko ulipanga kulipa mafao ya uzazi kwa TZS 236.69 milioni kwa wanachama 1,443. Jumla ya wanachama 1,376 wamelipwa mafao na jumla ya TZS 215.71 milioni zimetumika sawa na asilimia 91 ya makadirio. Ukilinganisha na mwaka uliopita kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko uliwalipa jumla ya wanachama 1,213 kwa jumla ya TZS 253.63 milioni zimetumika sawa na upungufu wa asilimia 15.

vi. Mfuko ulipanga kulipa marejesho ya TZS 7.75 bilioni kwa wanachama 442. Jumla ya wanachama 440 wamelipwa mafao na jumla ya TZS 7.12 bilioni zimetumika sawa na asilimia 92 ya makadirio.Ukilinganisha na mwaka uliopita kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko uliwalipa jumla ya wanachama 183 kwajumla ya TZS 4.91 bilioni zimetumika sawa na ongezeko la asilimia 45.

vii. Mfuko ulipanga kulipa marejesho kwa wanachama wa mfuko wa kujichangia kwa Hiari kwa TZS 337.50 milioni kwa wanachama 1,968. Jumla ya wanachama 496 wamelipwa mafao na jumla ya TZS 222.99 milioni zimetumika sawa na asilimia 66 ya makadirio. Ukilinganisha na mwaka uliopita kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko uliwalipa jumla ya wanachama 394 kwa jumla ya TZS 192.39 milioni zimetumika sawa na na ongezeko la asilimia 16.

viii. Mfuko ulipanga kulipa mafao ya upotevu wa ajira kwa TZS 2.42 bilioni kwa wanachama 300. Jumla ya wanachama 768 wamelipwa mafao na jumla ya TZS 2.13 bilioni zimetumika sawa na asilimia 88 ya makadirio. Ukilinganisha na mwaka uliopita kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko uliwalipa jumla ya wanachama 355 kwajumla ya TZS 1.36 bilioni zimetumika sawa na ongezeko la asilimia 57.

ix. Mfuko ulipanga kulipa mafao ya kuumia kazini (Fidia) kwa TZS 360.19 milioni kwa wanachama 125. Jumla ya wanachama 65 wamelipwa mafao na jumla ya TZS 250.85 milioni zimetumika sawa na asilimia 70 ya makadirio. Ukilinganisha na mwaka uliopita kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025, Mfuko uliwalipa jumla ya wanachama 73 kwa jumla ya TZS 180.09 milioni zimetumika sawa na ongezeko la asilimia 39.

### 4.6.4 Uwekezaji

**a) Mapato ya Uwekezaji**

**i. Mapato yatokanayo na Uwekezaji wa kawaida**

Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kukusanya TZS 118.44 bilioni kutoka mapato ya uwekezaji na mapato mengineyo. Mfuko ulikusanya jumla ya TZS 204.92 bilioni sawa na asilimia 173 ya ufanisi na ukilinganisha na mwaka uliopita kuanzia Julai 2024 hadi Machi 2025 Mfuko umeweza kukusanya TZS 85.50 bilioni katika uwekezaji sawa na ongezeko la asilimia 140.

**ii. Mapato yatokanayo na Uwekezaji wa Sharia**

Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Mfuko ulipanga kukusanya TZS 7.81 bilioni kutoka mapato ya uwekezaji kwa Skimu ya Sheria. Mfuko ulikusanya jumla ya TZS 5.53 bilioni sawa na asilimia 71 ya ufanisi.

**b) Thamani ya Uwekezaji hadi kufikia Machi 2026**

Uwekezaji wa Mfuko unajumuisha uwekezaji wa mabenki, hati fungani, ununuzi wa hisa, uwekezaji wa majengo na mikopo hadi kufikia Machi 2026, thamani ya uwekezaji wa Mfuko imeongezeka kwa asilimia 27 sawa na TZS 1.481 trilioni ukilinganisha na uwekezaji hadi kufikia Machi 2025 kwa kiasi TZS 1.165 trilioni. Ongezeko hilo limechangiwa na uwekezaji wa ziada uliofanywa katika kipindi hicho kutokana na ongezeko la mapato ya uwekezaji na mapato mengineyo.

### 4.6.5 Utekelezaji wa Miradi

Pamoja na kuwekeza kwenye masoko ya fedha, na maeneo mengine yenye fursa nzuri za uwekezaji, Mfuko unaendelea kutekeleza miradi mbali mbali ya kijamii yenye tija na maslahi kwa taifa kama inavyoonekana hapo chini:

i. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa nyumba za gharama nafuu uliyopo Mombasa Zanzibar, majengo 14 yamekamilika kujengwa na utekelezaji umefikia asilimia 100. Mradi huo umefunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi, Mheshimiwa Dkt. Hussein Ali Mwinyi.

ii. Kwa upande wa mradi wa ujenzi wa Soko la Mombasa uliyopo Mombasa Zanzibar, kwa sasa mradi huo umekamilika na utekelezaji umefikia asilimia 100. Mradi huo tayari umefunguliwa rasmi na Rais wa Zanzibar.

iii. Ujenzi wa Kituo cha kisasa cha Mabasi Malindi, kwa sasa mradi huo wa ujenzi umekamilika na utekelezaji umefikia asilimia 100. Mradi huo tayari umeshawekewa jiwe la msingi na Waziri wa Nchi — Ofisi ya Rais, Tawala za Mikoa Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ.

iv. Kwa upande wa ujenzi wa kituo cha mabasi Jumbi na Koani, taratibu za kupata eneo la awamu ya kwanza Jumbi limeshakamilika na eneo hilo limeshasafishwa. Kwa upande wa awamu ya pili Jumbi na Koani tayari tathmini imeshakamilika kwa wamiliki wa maeneo hayo na fidia zao zinaendelea kutolewa hadi kukamilika kwake.

### 4.6.6 Mafanikio

**i. Utekelezaji wa ahadi ya Mh. Rais ya Ongezeko la kima cha chini cha Pencheni**

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umefanya malipo kwa ongezeko la pensheni kutoka TZS 90,000 hadi kufikia TZS 180,000 kuanzia mwezi Julai 2023. Hii ikiwa ni kutekeleza ahadi ya Mheshimiwa Rais aliyoitoa katika Sherehe za Mei Mosi mwaka 2023.

**ii. Uimarishaji Utendaji kazi**

Mfuko umeweza kuboresha, kuimarisha usimamizi na utendaji kazi kwa kuongeza ufanisi wa watendaji kwa kuweka utaratibu maalum wa kuwapima jambo ambalo limeweza kuongeza uwazi na uwajibikaji katika kutekeleza majukumu ya Mfuko na kufanikisha kufikiwa kwa malengo. Mfuko umeanzisha mfumo wa kielektroniki wa Rasilimali watu (ARUTI) kwa ajili ya kuwapima watendaji wake.

**iii. Uwekezaji**

Kutokana na Uwekezaji mzuri unaoendelea kufanyika pia kuongezeka kwa Mapato ya uwekezaji na Ukusanyaji wa Michango, Mfuko umeendelea kuimarika uhimilivu wake na kuongezeka uwezo wa kulipa Mafao kwa miaka 25 ijayo bila ya kutetereka.

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar unaendelea kuongeza juhudi katika utafutaji wa fursa za uwekezaji zenye faida, tija na salama kwa ajili ya michango ya wanachama ndani na nje ya nchi kwa mustakabali mpana wa uhimilivu wa Mfuko. Thamani ya Mfuko imekuwa kutoka TZS 1.165 trilioni katika kipindi cha Machi 2025 hadi kufikia TZS. 1.481 trilioni katika kipindi cha Machi 2026, sawa na ongezeko la TZS 316 bilioni sawa na wastani wa asilimia 27.

**iv. Mifumo ya Tehama**

Muendelezo wa kusimamia mifumo mipya ya mawasiliano na TEHAMA kwa lengo la kuboresha utendaji kazi na kurahisisha huduma kwa wanachama na wateja kwa ujumla, mifumo ambayo imesaidia wafanyakazi wetu kujipima utendaji kazi na ufanisi wa huduma wanazozitoa. Mifumo hiyo imesaidia wanachama kupata taarifa fupi kupitia simu zao za mkononi ikiwemo kujua mienendo ya michango yao na taarifa mbalimbali zinazohusiana na Mfuko. Mifumo yenyewe ni kama ifuatayo: -

a) Mfumo wa ukusanyaji michango -Employers' Portal.

b) Mfumo wa Uhakiki kwa wastaafu-Mobile App.

c) Mfumo wa Utunzaji na utafuataji wa nyaraka kwa kutumia makabati ya kielektroniki (Electronic document management system).

d) Mfumo maalum wa kielektroniki wa mchakato wa upitiaji wa Mafaili ya wastaafu- Fumis CAG.

e) Mfumo wa Fao la Upotevu wa Ajira - Fumis Labor Commission.

f) Mfumo wa kuangalia michango na salio - Whatsapp Chatbot.

**v. Kuogezeka Ukwasi wa Mfuko.**

Kutokana na utofauti baina ya dhima, mapato ya uwekezaji na rasilimali unazomiliki, Mfuko umeendelea kuongeza ukwasi wake na unaweza kumudu kulipa mafao kwa wanachama wake bila ya wasiwasi wowote. Aidha Mfuko unalipa pencheni kwa wastaafu kila ifikapo tarehe 15 ya kila mwezi ili kuwapunguzia wazee msongamano katika Mabenki.

### 4.6.7 Changamoto

Pamoja na mafanikio makubwa yaliopatikana, changamoto zilizojitokeza kama zifuatazo:-

i. Kukosa utayari wa kufuata Sheria za Hifadhi ya Jamii kwa baadhi ya waajiri na waajiriwa wa sekta binafsi hali inayopelekea kutokuwajibika katika uchangiaji na usajili.

ii. Kushuka kwa viwango vya faida katika uwekezaji wa soko la fedha duniani.

iii. Kukosekana kwa sera za kodi za uwekezaji wa nyumba za gharama nafuu kwa taasisi za Serikali kunapelekea Mfuko kushindwa kutimiza malengo yake.

### 4.6.8 Hatua za Kuondoa Changamoto Zilizojitokeza

Mfuko wa Hifadhi ya Jamii Zanzibar umepanga kufanya yafuatayo ili kuondoa changamoto zilizojitokeza: -

i. pamoja na wachangiaji kwa hiari umuhimu wa kujisajili na kuchangia Mfuko unaendelea kutoa elimu kwa ajili ya kuelewesha waajiri, waajiriwa pamoja na kuwachukulia hatua kwa waajiri wanaokiuka Sheria;

ii. Mfuko utaendelea kutafuta fursa za uwekezaji zenye tija pamoja na kuongeza juhudi katika utafutaji wa masoko yenye faida ndani na nje kwa mustakabali mpana wa uhimilivu wa Mfuko na;

iii. Kuendelea kufanya mazungumzo na Serikali na mamlaka husika juuya uanzishwaji wa  sera ya uwekezaji wa nyumba za gharama nafuu ili kuwezesha taasisi za Serikali kushiriki katika uwekezaji huo kwa lengo la kuwasaidia wananchi na taifa kwa ujumla.

### 4.6.9 Mikakati ya Mfuko

Pamoja na utekelezaji wa majukumu ya kawaida, Mfuko pia umepanga kutekeleza mikakati yake ya baadae kama ifuatayo: -

i. Kuendeleza na kuimarisha mashirikiano na taasisi za Serikali kwa lengo la kuimarisha usajili wa wanachama na kuwasilisha michango na kusaidia ukusanyaji wa mapato ya Serikali;

ii. Kufanya miradi yenye tija kubwa na maslahi ya moja kwa moja kwa wananchi na Mfuko kwa ujumla;

iii. Kuendelea kufanya uwekezaji wa fedha kwa kipindi cha muda mfupi na muda mrefu katika hatifungani, uwekezaji katika mabenki

na kuendelea kutoa mikopo kwa Serikali, Mashirika, Taasisi na Kampuni binafsi yenye tija katika Mfuko;

iv. Kusimamia uwekezaji wa majengo kwa kuhakikisha kuwa malipo yanalipwa kwa wakati, mikataba inasainiwa na hali ya majengo inaendelea kuwa vizuri; na

v. Kukamilisha utoaji wa huduma za hifadhi ya jamii kwa kuzingatia misingi ya Sharia.

### 4.6.10 Matarajio ya Baadae

i. Kuendeleza kufanya tathmini katika soko la fedha na soko la majengo ili kuengeza fursa za uwekezaji na faida kupitia uwekezaji wa Mfuko;

ii. Kuendeleza kufanya uhakiki kwa wanachama wake na kuendelea kuweka sawa taarifa za wanachama wa Mfuko kwa lengo la kuboresha taarifa zao na kurahisisha ulipaji wa mafao kwa wakati;

iii. Kuendelea kusimamia uwekezaji wa majengo kwa ajili ya kukusanya mapato kwa wakati na kuhakikisha majengo yanakuwa katika hali nzuri;

iv. Kufuatilia maendeleo ya ujenzi wa miradi ya Mfuko kwa ukaribu na kuhakikisha miradi inamalizika kwa wakati uliopangwa; na

v. Kutafuta washirika wa kuwekeza katika sekta ya uchumi wa bluu kwa njia ya hisa na kuendelea kufuatilia uwekezaji uliofanyika katika Shirika la ZAFICO na Mwani.

## 4.7 Huduma Ndogo Za Fedha (Microfinance)

Utekelezaji wa shughuli za usimamizi na udhibiti wa huduma ndogo za fedha umewezeshwa kupitia Sheria ya Huduma Ndogo za Fedha ya mwaka 2023 pamoja na Kanuni za Huduma Ndogo za Fedha za mwaka 2025, ambapo kwa upande wa Zanzibar, jukumu la usimamizi wa shughuli hizo limekabidhiwa Benki Kuu ya Tanzania. Mfumo huu wa usimamizi umeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha taasisi zote zinazotoa huduma ndogo za fedha zinafanya kazi kwa kuzingatia sheria, kanuni na viwango vinavyolinda maslahi ya wananchi pamoja na kuimarisha uthabiti wa sekta ya fedha.

Kwa mujibu wa sheria hiyo, watoa huduma ndogo za fedha wamegawanywa katika daraja kuu nne (Four Tiers) kulingana na aina na ukubwa wa huduma wanazotoa.

**Daraja 1** inahusisha mabenki na taasisi za fedha zinazopokea amana kutoka kwa wateja.
**Daraja 2** linajumuisha taasisi za huduma ndogo za fedha ambazo hazipokei amana kutoka kwa wateja.

**Daraja 3** inahusisha Vyama vya Ushirika wa Akiba na Mikopo (SACCOS), ambavyo huanzishwa kwa lengo la kuwawezesha wanachama kuweka akiba na kupata mikopo kwa masharti nafuu.

**Daraja 4** inajumuisha vikundi vya kijamii vinavyotoa huduma ndogo za kifedha katika ngazi ya jamii vinavyojulikana kama Community Groups.

Aidha, mfumo huu wa daraja 4 (Tiers 4) umeanzishwa kwa lengo la kuweka mazingira bora ya usimamizi wa huduma ndogo za fedha, kuongeza uwajibikaji wa taasisi zinazotoa huduma hizo, kulinda maslahi ya watumiaji wa huduma za kifedha pamoja na kukuza ujumuishaji wa huduma za fedha kwa wananchi wengi Zaidi.

### 4.8 Idara Ya Maendeleo Ya Ushirika

Idara ya Maendeleo ya Ushirika Zanzibar ipo chini ya Wizara ya Vijana, Ajira na Uwezeshaji Zanzibar. Idara hii ina dhamana ya kusimamia maendeleo na ustawi wa Vyama vya Ushirika Zanzibar. Idara imeanzishwa rasmi mwaka 1980, kwa mujibu wa Sheria ya Vyama vya Ushirika Zanzibar Nambari 3 ya mwaka 1979. Hivi sasa Idara ya Maendeleo ya Ushirika inaendeshwa kwa mujibu wa Sera ya Maendeleo ya Ushirika 2014, Sheria ya Vyama vya Ushirika Nambari 15 ya mwaka 2018 na Kanuni ya mwaka 2019.

#### 4.8.1 Maendeleo ya Ushirika Zanzibar

Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, Idara ya Maendeleo ya Ushirika, imetekeleza majukumu yafuatayo: -

i. Idara imesimamia Mikutano Mikuu ya Vyama vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) 13, (Unguja 8; Pemba 5), vikiwemo *BoT SACCO*S, *Dhowshed SACCOS*, *Mshikamano SACCOS*, Bandarini

*Taxi SACCOS*, Teacher's *Development SACCOS* (TDS), *Beach Porters* SACCOS. *Melinne SACCOS* na *Watanga SACCOS* na kwa upande wa Pemba ni Nanga ya *Shaba SACCOS*, *Sawazisho SACCOS*, Pemba *Teacher's SACCOS*, *Beach Porters SACCOS* na *Mshikamano SACCOS*. Mikutano Mikuu hiyo imeonesha uimarikaji wa Utawala Bora, Uwajibikaji wa Viongozi, Usimamizi na Udhibiti mzuri wa Fedha pamoja na Faida iliyotengenezwa kwa kipindi cha mwaka. Aidha, *Melinne SACCOS*, *Watanga SACCOS* na Bandarini *Taxi SACCOS* walifanya Uchaguzi wa Viongozi ambao wataongoza *SACCOS* hizo kwa kipindi cha miaka mitatu ili kudumisha Demokrasia ndani ya *SACCOS* ya kuwapa haki Wanachama ya kuchagua Viongozi wanaowataka. Lengo la mikutano hiyo ni kutoa Haki kwa Wanachama ya kujadili shughuli za Vyama vyao ikiwemo mafanikio na changamoto. Pia kuidhinisha Mipango kazi na Bajeti, kujadili utekelezaji wa shughuli za Ushirika, kuthibitisha Wanachama wapya na kuwatoa Wanachama waliokosa sifa za kuwa Wanachama wa Chama cha Ushirika.

ii. Imekagua Hesabu za Vyama vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS)* 14, (Unguja 8; Pemba 6). Matokeo yameonesha baadhi ya Vyama vinafanya shughuli zake bila ya kuwa na makisio ya mapato na matumizi, elimu ndogo juu ya uendeshaji na usimamizi, elimu ndogo juu ya usimamizi wa fedha, utunzaji wa kumbukumbu na mbinu za kubuni miradi ya uzalishaji.

iii. Imefanya ukaguzi wa kawaida na ufuatiliaji kwa Vyama vya *SACCOS* 26, (Pemba 20; Unguja 6). Lengo ni kujiridhisha juu ya uendeshaji wa shughuli za Vyama kwa ujumla, ikiwemo utunzaji wa vitabu vya hesabu, kumbukumbu, uendeshaji vikao zinaendeshwa kwa mujibu wa sheria Nam. 15 ya mwaka 2018, Kanuni na Sheria zao ndogo ndogo, pamoja na kutoa ushauri wa kitaalamu kwa changamoto zinazoonekana. Aidha jumla ya *SACCOS* 3 za Unguja zimekata leseni kwa upande wa Unguja, *SACCOS* zenyewe ni *Beach Porters SACCOS* (Daraja B), *Airport SACCOS* (Daraja A) na *Melinne SACCOS* (Daraja A).

iv. Idara imeshiriki katika Uzinduzi wa Taarifa ya Utendaji wa Vyama Vya Ushirika vya Akiba na Mikopo (*SACCOS*) vya Tanzania Bara pamoja na Maadhimisho ya Siku ya Vyama vya Akiba na Mikopo (*ICUD)* shughuli hizi zilifanyika jijini Arusha tarehe 29 Septemba hadi tarehe 2 Oktoba. Ambapo shughulli hizi zilisimamiwa na kuendeshwa na Tume ya Maendeleo ya Ushirika Tanzania Bara (*TCDC*) kwa kushirikiana na chama Kikuu cha Akiba na Mikopo (*SCCULT*), lengo hasa ni kujifunza na kupata uelewa wa Maadhimisho haya yanavyofanyika ili na Zanzibar nayo iweze kuadhimisha siku hiyo, vile vile kuelewa namna ya kuandaa Taarifa hiyo ya Utendaji ya Vyama vya *SACCOS* na Zanzibar iweze kuandaa.

v. Idara imeshiriki kutatua migogoro 6 kutoka vyama 6 vya ushirika, vyenye mivutano baina ya Viongozi wakuu wa *SACCOS* na Viongozi wa Kamati mbali mbali za Ushirika kutokana na kukiukwa Taratibu za fedha, vyama vyenyewe ni *Watanga SACCOS* cha Unguja na kwa upande wa Pemba ni *Dhowshed SACCOS*, *Shikamana SACCOS*, Nanga ya *Shaba SACCOS*, *Sawazisho SACCOS*, Beach *Porters SACCOS*, vyama hivi vyote vina chanzo kinachofanana cha Migogoro ambayo ni kugombaniana kazi (kutaka kazi ya aina moja katika maeneo ya bandari). Hadi sasa migogoro hiyo imefikia hatua nzuri ya Usuluhishi na hatua za kuweka saini hati za maridhiano zinaendelea.

vi. Imeshiriki Kikao na Viongozi wa Vyama vya *SACCOS* na Uzalishaji kuhusiana na ujio wa *Coop Bank* kwa upande wa Zanzibar ili kuja kujitambulisha na kuhamasisha vyama kununua Hisa katika Benki hiyo, washiriki wa kikao hicho ni 69 (w'ke 16: w'me 53). Matokeo ya uhamasishaji huo Chama cha Ushirika cha Wachukuzi Bandarini Unguja (*Beach Porters*) kimenunua Hisa zenye thamani ya Shilingi 2,000,000/= na kupatiwa Hati ya umiliki wa Hisa. Aidha, baada ya mwaka mmoja wataweza kupatiwa faida ya uwekezaji wa Hisa.

vii. Ilishiriki kikao cha Viongozi wa *SACCOS*, *ZASCCU* na *CUZA* (Jumla ya washiriki wa kikao hicho cha Viongozi ni vyama 6 vya *SACCOS*), kuhusiana na maazimio yaliyotokana na kikao cha siku ya Uhamasishaji wa ununuzi wa Hisa katika *Coop Bank*, moja

wapo ni kumteua M/kiti wa *CUZA* kuungana na uongozi wa *Coop Bank* kwenda kuonana na Mhe. Rais kwa ajili ya kumuelezea lengo la kufungua Branch katika Visiwa vya Zanzibar, kufuatia agizo lake alilolitoa katika uzinduzi wa Baraza la 11 la Wawakilishi lililofanyika tarehe 10/11/2025.

viii. Idara kwa kushirikiana na BoT Ofisi ndogo ya Zanzibar pamoja na Wizara ya Fedha Zanzibar ilitoa Mafunzo kwa Viongozi, Wanachama na Watendaji wa *SACCOS* mbali mbali ziliopo Unguja kuhusiana na Elimu ya Fedha.

### 4.8.2 Mafanikio

Mafanikio yaliyopatikana kwa SACCOS ni pamoja na: -

- Kukua kwa Demokrasia katika *SACCOS*; Kwa sasa *SACCOS* zinaendesha Mikutano yao na Wanachama wanapata fursa ya kuhoji na kupata maelezo ya kutosha juu ya shughuli zinazoandaliwa na *SACCOS* zao kupitia Mikutano Mikuu. Hii ni kutokana na kufuatwa kwa Sheria na Kanuni za Ushirika na pia taaluma za Ushirika kwa Wanachama na Viongozi wa *SACCOS.*

- Wanachama wameanza kupata uelewa wa Kanuni mpya ya *SACCOS* ya mwaka 2024.

- *SACCOS* zipatazo 29 zimewekeza kwa thamani ya Tzsh. 1,622,878,800/- katika vitega uchumi mbali mbali, lengo ni kutanua fursa za maendeleo na kujiongezea kipato, baadhi ya maeneo ambayo *SACCOS* zimewekeza ni Majengo/Nyumba, Maduka, Mashamba, Gari (Mizigo, Utalii, Taxi), Maholi, Boti za Utalii, Viwanda, Vinu vya Kukobolea na Kusaga Nafaka, Uwakala wa Fedha, Hati Fungani, Uwakala wa Bima, Maegesho, Biashara n.k.

- *SACCOS* 24 zimezalisha ajira rasmi 546 (Ke 80; Me 466) za nafasi mbali mbali zikiwemo za Mameneja, Wahasibu, Makarani Fedha, Madereva, Maafisa Mikopo, Maafisa Manunuzi, Afisa Mipango, Afisa Elimu, Karani, Wachukuzi, Wahudumu na Walinzi.

### 4.8.3 Changamoto

Changamoto zinazo zikabili *SACCOS* za Zanzibar ni kama zifuatazo: -

- Uwekaji wa Taarifa za *SACCOS;* Baadhi ya *SACCOS* wanatumia njia za Kawaida katika uwekaji wa Taarifa zao hali ambayo inapelekea kupotea na kutokupatikana kwa wakati zinapohitajika. Idara imewashauri kutumia angalau (*Excel Sheet*) katika kuweka taarifa zao ili iwe wepesi kupatikana wakati zitakapohitajika.

- Ucheleweshaji wa taarifa za *SACCOS*; Baadhi ya *SACCOS* zinachelewesha taarifa za mwenendo wa Ushirika wao hii hupelekea kutokupatikana kwa taarifa za *Portfolio* ndani ya wakati. Idara imechukuwa hatua ya kuhamasisha *SACCOS* kutumia mifumo kurahisisha upatikanaji wa *portfolio* kwa wakati.

- Ufuatwaji wa Sheria; Baadhi ya *SACCOS* hazifuati sheria hivyo kupelekea migogoro kwenye vyama vyao na ukiukwaji wa utekelezaji wa majukumu yao. Katika kulitatua hili Idara inaendelea kutoa taaluma ya Sheria na kanuni za ushirika ili kupunguza migogoro kwenye vyama vyetu. Jumla ya *SACCOS* 3 zilifundishwa.

- Kuibua mbinu za uwekezaji (Taaluma ya Uwekezaji); baadhi ya vyama vya ushirika havina taaluma ya uwekezaji, hali hii inapelekea kukosa kuwa na vyanzo ambavyo vitawasaidia wanachama na ushirika kwa ujumla. Katika kulitatua hili Idara tayari imeanzisha programu za mafunzo ambazo zimejumuisha somo la Uwekezaji katika vyama vya ushirika. Jumla ya *SACCOS*

# SURA YA TANO

## 5.0 SEKTA YA MIUNDOMBINU

Sekta ya miundombinu ni miongoni mwa kichocheo kikubwa cha ukuaji wa uchumi wa nchi, maendeleo ya jamii na kukuza uwekezaji katika sekta mbalimbali kama vile biashara na utalii. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, inaendelea kuchukua juhudi za kuimarisha miundombinu nchini ili kurahisisha upatikanaji wa huduma kwa wananchi wake.

### 5.1 Wakala wa Barabara

Wakala wa ujenzi wa barabara wa Serikali ni taasisi yenye kujitegemea ambayo imeundwa kwa Sheria Namba 11 kifungu Namba 3 (1) ya mwaka 2019.

Serikali iliiwezesha wakala wa barabara kwa kuwapatia vifaa vipya na rasilimali watu ilikuingia katika soko la ushindani na mapato yanayopatikana katika biashara na shughuli zinazofanywa na wakala, yanatumika kuendeshea kazi zao za kila siku.

Taasisi hii imetokana na mageuzi yaliyofanywa ya muundo wa Idara ya Ujenzi na Utunzaji wa Barabara (UUB) kwa lengo la kuimarisha huduma zinazotolewa na taasisi hiyo. Hata hivyo, Zanzibar ina barabara zenye urefu wa kilomita 1,803.60 kati ya hizo zenye lami ni kilomita 1,218.17 na zisizo na lami ni kilomita 585.43 Barabara kuu ni kilomita 358.31 barabara za vijijini kilomita 576.25 barabara za mijini ni kilomita 133.1 na barabara za ndani ni kilomita 735.94 ***(Jadweli namba 20):***

**Jadweli Nambari 20: Mchanganuo wa Barabara za Zanzibar kwa mwaka 2025**

| Aina za Barabar a | Urefu (km) | Zenye Hali Nzuri | | Zilizo Afadhali | | Zenye Hali Mbaya | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | km | Asilimia (%) | km | Asilimia (%) | km | Asilimia (%) |
| Barabar a Kuu za Lami | 358.31 | 236.72 | 66.07 | 30.08 | 8.4 | 91.51 | 25.53 |
| Barabar a Kuu zisizoku a na lami | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Barabar a za Vijijini zenye lami | 407.34 | 298.47 | 73.37 | 18.54 | 4.55 | 90.33 | 22.17 |
| Barabar a za Vijijini zisizoku a na lami | 168.91 | 51.93 | 30.74 | 69.67 | 41.25 | 47.31 | 28.01 |
| Barabar a za Mjini zenye lami | 111.91 | 95.76 | 85.57 | 16.15 | 14.43 | 0 | 0 |
| Barabara za Mjini zisizoku a na lami | 21.19 | 0 | 0 | 13.86 | 65.41 | 7.33 | 34.59 |
| Barabar a za ndani zenye lami | 340.61 | 237.52 | 69.73 | 79.6 | 23.37 | 23.49 | 6.9 |

| | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| Barabar a za Ndani zisizokua na lami | 395.33 | 126.25 | 31.94 | 105.18 | 26.61 | 163.9 | 41.45 |
| **Jumla (km)** | **1,803.60** | **1,046.65** | **58.03** | **333.08** | **18.47** | **423.87** | **23.5** |

***Chanzo: Wakala wa Barabara, 2026***

### 5.1.1 Mchanganuo Wa Matumizi Ya Fedha Kwa Ujenzi na Matengenezo ya Barabara Kwa Mwaka Wa Fedha (Julai 2025 - Machi 2026) iliofanywa na Wakala wa Barabara.

Kwa kipindi cha julai 2025-Machi 2026, Wakala wa barabara umeweza kutumia jumla ya TZS 7.5 Bilioni kwa ajili ya kufanya ukarabati katika maeneo mbali mbali kwa Matengenezo ya Muda Maalum kama vile Ujenzi wa Barabara mbalimbali za ndani, Ujenzi wa Barabara Mchangani Msikitini kwa kiwango cha lami, na Ujenzi wa Barabara ya Uchukuni Pemba kwa Kiwango cha Lami na matengenezo mengineyo. (***Jadweli nambari 21*** ).

**Jadweli Nambari 21: Mchanganuo Wa Matumizi Ya Fedha Kwa Ujenzi Wa Barabara Kwa Mwaka Wa Fedha Unguja na Pemba, (2025-Machi 2026)**

| MCHANGANUO WA MATUMIZI YA FEDHA KWA MWAKA 2025 - 2026 HADI MACHI | | | |
|---|---|---|---|
| **S/N** | JINA LA MRADI | KIPIMO | GHARAMA (FEDHA) |
| 1 | Ujenzi wa njia za watembea kwa miguu pamoja na taa za barabarani Kizimkazi | 2.6 Km | 2,730,000,000 |
| 2 | Ujenzi wa Barabara Mchangani `Msikitini | 1.4 Km | 345,000,000 |
| 3 | Ujenzi wa Barabara ya Uchukuni | 4.5 Km | 300,000,000 |
| | | | |
| 4 | Ujenzi wa Barabara ya Pandani Mlindo | 3.2 Km | 290,957,670 |
| 5 | Ujenzi wa Barabara ya Mgelema Wambaa, Msiwakwe Wete Spitali. | 6.65 Km | 2,751,754,935.51 |
| 6 | Kazi za uzibaji wa mashimo na utiaji wa viraka Barabarani kwa Unguja na Pemba | 4,874 mita za mraba | 239,841,577 |
| 7 | Matengenezo ya dharura | LS | 393,250,000 |
| 8 | Uwekaji wa Alama na michoro Barabarani kwa Unguja na Pemba | 18 Km | 329,941,255.20 |
| 9 | Utunzaji wa Barabara kwa kuimarisha mfumo wa matengenezo (RMMS) | 303.81 km | 50,000,000 |
| 10 | Kazi za Ukataji wa majani , Usafi wa madaraja na kalvati | 118.6 Km | 54,261,896 |

***Chanzo: Wakala wa Barabara, 2026***

### 5.3 Nishati ya Umeme.

Nishati ya umeme ni kiungo muhimu katika kuhakikisha maeneo yote ya maendeleo ya kiuchumi na kijamii yanafanya kazi zake kwa ufanisi. Nishati hii hutumika kwa shughuli mbalimbali zikiwemo miradi ya uwekezaji, viwandani na majumbani.

Idadi ya wateja waliounganishwa na huduma ya umeme katika Gridi ya Taifa imeongezeka na kufikia wateja 41,225 mwaka 2025 ikilinganishwa na wateja 32,547 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 26.6.

Ongezeko hilo linatokana na jitihada za serikali za kuwekeza katika huduma hii na kupunguza gharama za uunganishwaji wa umeme kwa wananchi ***(Jadweli nambari 22)***.

**Jadweli Nambari 22: Idadi ya Wateja Wapya Waliounganishwa na Gridi ya Taifa Zanzibar (2021 – 2025).**

| Eneo | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 | Asilimia (%) ya ukuaji kwa mwaka 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| **Unguja** | 25,346 | 23,046 | 31,053 | 27,796 | 34,702 | 24.84 |
| **Pemba** | 7,703 | 4,974 | 4,785 | 4,751 | 6,523 | 37.29 |
| **Zanzibar** | **3,349** | **2,820** | **35,838** | **32,547** | **41,225** | **26.66** |

***Chanzo: Shirika la Umeme Zanzibar, 2026***

Kiwango cha umeme kilichosambazwa kimeongezeka na kufikia 949,957 kWh mwaka 2025 kutoka 671,732 kWh mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 41.4 Thamani ya mauzo ya umeme katika kipindi hicho imeongezeka na kufikia TZS 224,486 bilioni mwaka 2025 kutoka TZS 195,517 bilioni mwaka 2024. Ongezeko hilo limetokana na kuongezeka kwa huduma za upatikanaji wa umeme katika mahoteli, viwandani na majumbani. (***Jadweli nambari 23.).***

**Jadweli namba 23: Kiwango cha Umeme kilichosambazwa (2021-2025) (KWH "000")**

| MAELEZO | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Majumbani (Z0) | 13 | 25 | 27 | 37 | - |
| Majumbani na Biashara (Z1) | 2,494 | 1,710 | 1,853 | 1513 | 227,193 |
| Viwanda Vidogo vidogo (Z 2) | 8,914 | 13,070 | 21,516 | 21,307 | 32,273 |
| Viwanda vya Kati na Vikubwa (Z3) | 142,154 | 162,707 | 182,799 | 206,380 | 194,833 |
| TUKUZA | 286,136 | 323,763 | 354,507 | 442,495 | 495,658 |
| **Jumla** | **439,711** | **501,275** | **560,702** | **671,732** | **949,957** |

***Chanzo: Shirika la Umeme Zanzibar, 2026***

**Jadweli Nambari 24 : Thamaniya Umeme Uliosambazwa (2021 – 2025) (TZS Milioni)**

| MAELEZO | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Majumbani (Z0) | 2.9 | 7.7 | 7.9 | 10 | - |
| Majumbani na Biashara (Z1) | 698 | 479 | 520 | 903 | 4380 |
| ViwandaVidogovid ogo (Z2) | 2,038 | 2,773 | 4,306 | 4230 | 6,031 |
| Viwanda vya Kati na Vikubwa (Z3) | 24,263 | 28,284 | 31571 | 38,291 | 37,800 |
| TUKUZA | 97,997 | 110,291 | 122,043 | 152,083 | 176,274 |
| **Jumla** | **124,9999** | **141,835** | **158,448** | **195,571** | **224,486** |

***Chanzo: Shirika la Umeme Zanzibar, 2026***

## 5.4 Mamlaka ya Maji Zanzibar (*Rand Water*).

Maji ni rasilimali muhimu kwa maisha na maendeleo ya mwanadamu. Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuweka mkazo katika kuhakikisha upatikanaji wa maji safi na salama kwa wananchi wake, na kuendelea kuvitunza, na kuhifadhi vyanzo vya asili vya maji. Hili ni moja ya lengo la Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar ya kuwaondolea wananchi changamoto za upatikanaji wa huduma muhimu ya maji safi na salama na maendeleo katika jamii.

Kwa mwaka 2025, visima vinavyozalisha maji vimeongezeka na kufikia jumla ya visima 408 kutoka visima 389 mwaka 2024. Hii imetokana na kuongezeka kwa idadi ya watu na makaazi na kupelekea kuongezeka uchimbaji wa visima katika maeneo hayo ilikupata huduma ya maji safi na salama. ***(Jadweli nambari 25 )***

**Jadweli Nambari 25: Visima Vinavyozalisha Maji na Kutoa Huduma (2021 – 2025)**

| Mkoa | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini Unguja | 46 | 46 | 47 | 51 | 51 |
| KusiniUnguja | 48 | 44 | 44 | 59 | 75 |
| MjiniMaghribi | 81 | 81 | 82 | 132 | 126 |
| Kaskazini Pemba | 48 | 49 | 53 | 53 | 76 |
| Kusini Pemba | 70 | 81 | 83 | 94 | 80 |
| **Jumla** | **293** | **301** | **309** | **389** | **408** |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2026***

### 5.4.1 Usimamizi na Uendelezaji Rasilimali Maji na Utatuzi wa Changamoto za Maji.

Mamlaka ya Maji Zanzibar (Rand Water) inaendelea kutatua tatizo la kuondosha wavamizi na waharibifu katika maeneo ya vianzio vya maji na

kufanya shughuli ambazo hazistahiki katika sehemu hizo kama vile kilimo, ujenzi wa nyumba na makaazi. Wanachi wanazidi kupata uelewa juu ya umuhimu wa kutunza vyanzo vya maji na kushirikiana na Serikali na kuunga mkono hatua za Mamlaka ya Maji ya kuvitunza vyanzo hivyo. Kwa mwaka 2025, imeibuka migogoro 1,596 inayohusiana na maeneo ya uzalishaji wa maji, kati ya migogoro hiyo 1,268 imetatuliwa 328 bado inaendelea. Aidha Mamlaka ya Maji Zanzibar inaendelea kuchukua juhudi za kutatua migogoro iliyobakia, (***Jadweli nambari 26***).

**Jadweli Nambari 26: Migogoro ya Watumiaji Maji Iliyopatiwa Ufumbuzi (2020-2025)**

| Hali ya migogoro | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Migogoro iliyomalizika | 3 | 5 | 120 | 298 | 1,268 |
| Migogoro inayoendelea | 6 | 2 | 2 | 100 | 328 |
| **Jumla** | **9** | **7** | **122** | **398** | **1,596** |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2026***

Vile vile kwa mwaka 2025, Mamlaka ya Maji Zanzibar imeweza kuzalisha na kusambaza maji jumla ya Cubic Meter 218.0 milioni ukilinganisha na Cubic Meter 223.7 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia hasi 2.5 na kukusanya TZS 4,328 bilioni kwa mikoa yote ya Unguja na Pemba.

Upungufu huo umetokana na kupungua kwa idadi ya visima vya maji vilivyo chimbwa kwa mwa 2025. ***(Jadweli nambari 27)***

**Jadweli Namba 27: Ukusanyaji Mapato, Uzalishaji na Usambazaji Maji (2025)**

| Mwaka | Jumla ya uzalishaji wa maji (Milion Cubic meter) | Makadirio ya mahitaji ya maji (Milion Cubic meter) | Upungufu katika mahitaji ya maji (asilimia) | Ukusanyaji wa mapato |
|---|---|---|---|---|
| **2021** | 131.8 | 240.7 | 45.20 | 2,613 |
| **2022** | 108.5 | 188.6 | 42.4 | 2,271 |
| **2023** | 192 | 276 | 30 | 2,127 |
| **2024** | 223.7 | 276 | 18.9 | 3,317 |
| **2025** | 218.0 | 252.0 | 34.0 | 4,328 |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2026***

### 5.4.2 Juhudi, Huduma, na Mchanganuo wa Utekelezaji wa Huduma ya Maji Mkoa wa Mjini kwa Mwaka 2025.

**1. Juhudi zinazochukuliwa kuwafikia wasiopata huduma ya maji.**

a) Wizara kupitia Rand Water Zanzibar inaendelea na utekelezaji wa miradi midogo ikiwa ni utatuzi wa dharura kwa maeneo yenye changamoto ya maji kwa muda mrefu kwa kutumia fedha zake za ndani. Aidha; matarajio yetu ni kuongeza mtandao wa maji katika

maeneo yaliyokuwa hayajafikiwa na huduma ya maji pamoja na maeneo mengine yaliyoharibiwa miundombinu kutokana na ujenzi wa barabara.

b) Utekelezaji wa Miradi mbali mbali ya maji kutoka kwa Wafadhili na washirika wa maendeleo

**2. Huduma za maji Mkoa wa Mjini 2025.**

Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka 2025, kwa upande wa Mkoa wa Mjini imelaza mtandao wa maji wenye urefu wa kilomita 467 kupitia Mradi wa Uhaulishaji na Uimarishaji wa Mfumo wa Usambazaji Maji Zanzibar pamoja na juhudi za kazi za kawaida za Mamlaka ya Maji Zanzibar ambapo jumla ya kilomita 4.8. Hivyo; kufanya jumla ya kilomita 471.8 kwa mwaka 2025.

**3. Mchanganuo/mfumo wa usambazaji maji Mjini**

Mamlaka ya Maji Zanzibar inaendelea kutoa huduma kupitia mifumo miwili mikuu.

i. Usukumaji wa maji moja kwa moja (*Direct Pumping*); na

ii. Mifumo ya kuhifadhi maji kwenye matangi ya chini (Storage Tanks) kisha kupandishwa kwa matangi ya juu (Elevated tank) na baadae kuruhusiwa maji kwenda yenyewe kwa wananchi yamekarabatiwa na kujengwa kwa lengo la kusambaza huduma ya maji kwa ufanisi zaidi badala ya kutumia mfumo wa usukumaji wa moja kwa moja (Direct Pumping) kunakopelekea kuharibika kwa pampu mara kwa mara.

### 5.4.3 Huduma ya Maji Vijijini

Mamlaka ya Maji Zanzibar kwa mwaka 2025, imeweza kusimamia na kuendeleza kusambaza huduma ya maji safi na salama ili kurahisisha shughuli za maendeleo Unguja na Pemba. Hata hivyo miradi mitatu (3) ya usambazaji maji imetekelezwa katika kipindi cha mwaka 2025 na miradi minane (8) iliyotekelezwa mwaka 2024, miradi hiyo mitatu (3) imetekelezwa chini ya ufadhili wa Washirika wa Maendeleo kwa mwaka 2025. ***(Jadweli nambari 28 ).***

**Jadweli Nambari 28 : Idadi ya miradi ya maji na wafadhili (2021-2025)**

| Aina ya Ufadhili | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar | 1 | 1 | 2 | 1 | 0 |
| Washirika wa Maendeleo | 1 | 1 | 3 | 7 | 3 |
| **Jumla** | **2** | **2** | **5** | **8** | **3** |

***Chanzo: Mamlaka ya Maji Zanzibar, 2026***

# SURA YA SITA

## 6.0 SEKTA YA ELIMU

### 6.1 Elimu na Mafunzo ya Amali

Uwekezaji katika rasilimali watu ni jambo muhimu linaloendelea kutiliwa mkazo kitaifa na kimataifa. Elimu inaanza tokea elimu ya msingi na kuendelea na elimu ni haki ya msingi ya binaadamu katika kukuza na kuendeleza maendeleo ya uchumi wa nchi.

Serikali inaendelea kuwekeza katika sekta ya elimu kwa ujenzi wa skuli mpya zenye vifaa vya kisasa vya maabara na kushajihisha wanafunzi kwa kuendelea kuwapa hamasa pale wanapofaulu kwa madaraja ya juu na kuondoa michango ya wanafunzi. Kuwekeza katika sekta ya elimu kunalihakikishia taifa kuwa na wataalamu na kuweza kutatua changamoto za maendeleo za sasa na baadae.

Kwa mwaka 2025, Zanzibar imeripotiwa kuwa na jumla ya skuli za Maandalizi 300 kutoka skuli 349 mwaka 2024, (kati ya Skuli hizo, Serikali ina jumla ya skuli 84 mwaka 2025 kutoka skuli 67 mwaka 2024 na skuli Binafsi ni 216 mwaka 2025 kutoka skuli 282 mwaka 2024) sawa na upungufu wa asilimia 14.0. Hii inatokana na baadhii ya skuli kupandisha daraja kutoka maandalizi kwenda msingi.

Skuli za Msingi mwaka 2025 zimefikia 642 kutoka skuli 627 mwaka 2024, ambapo (mwaka 2025 skuli za Serikali zimefikia 336 kutoka skuli 328 mwaka 2024) na skuli Binafsi mwaka 2025 zimefikia 306 kutoka skuli 299 mwaka 2024.

Aidha, skuli za Sekondari mwaka 2025 zimeongezeka na kufikia skuli 244 kutoka skuli 236 mwaka 2024 (jumla ya skuli za Serikali ni 221 mwaka 2025 kutoka skuli 217 mwaka 2024 na skuli Binafsi ni 23 mwaka 2025 kutoka skuli 19 mwaka 2024). Vyuo vya Amali 69 (Serikali 13 na Binafsi 56), Taasisi 23 (Serikali 12 na Binafsi 11) na Vyuo vikuu 3.

Idadi ya wanafunzi waliopata fursa ya kujiunga na elimu ya Maandalizi; Serikali na Binafsi mwaka 2025 imeongezeka kufikia wanafunzi 105,101 kutoka wanafunzi 103,581 mwaka 2024. Hii imetokana na muamko wa wazazi unaotokana na uhamasishaji unaofanywa na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali juu ya umuhimu wa elimu kwa jamii na Taifa kwa ujumla. Hata hivyo, idadi ya wanafunzi wanaoendelea na masomo katika skuli za Msingi za Serikali na Binafsi kwa mwaka 2025 imeongezeka kufikia wanafunzi 403,886

kutoka wanafunzi 391,388 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 3.2. Hii imetokana na jitihada zinazochukuliwa na Serikali kuweka miundombinu mizuri ya kujisomea kwa wanafunzi hao.

### 6.1.1 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Serikali

Kwa mwaka 2025 jumla ya wanafunzi 107,273 wameandikishwa katika skuli za Maandalizi na Msingi za Serikali kutoka wanafunzi 111,273 walioandikishwa kwa mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 3.6 Kwa upande wa skuli za Maandalizi za Serikali kwa mwaka 2025 idadi imeongezeka na kufikia wanafunzi 63,099 kutoka wanafunzi 62,974 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 0.2. Kati ya hao, wanafunzi wa kiume kwa mwaka 2025 ni 31,759 kutoka wanafunzi 31,573 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 0.6 na wanafunzi wa kike kwa mwaka 2025 ni 31,340 kutoka wanafunzi 31,401 kutoka mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 0.1.

Kwa upande wa skuli za Msingi za Serikali kwa mwaka 2025 idadi imefikia wanafunzi 331,108 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 327,500 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 1.1 ambapo wanafunzi wa kiume ni 168,553 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 165,592 mwaka 2024 na wanafunzi wa kike ni 162,465 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 161,908 mwaka 2024.

Idadi ya wanafunzi wapya walioandikishwa darasa la kwanza katika skuli za Msingi za Serikali na Binafsi kwa mwaka 2025 imeongezeka na kufikia wanafunzi 61,501 kutoka wanafunzi 48,299 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 27.3. Kati ya hao wanafunzi wa kiume ni 31,541 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 24,795 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 27.2 na wanafunzi wa kike ni 29,960 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 23,504 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 27.4 Hii ni kutokana na kuongezeka kwa uhamasishaji unaofanya na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali pamoja na ukaribu wa skuli hizo kwa jamii.

Idadi ya wanafunzi waliofaulu Kidato cha Pili kwa mwaka 2025 wameongezeka na kufikia wanafunzi 21,489 kutoka wanafunzi 18,934 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 13.5, ambapo wanafunzi wa kiume ni 8,579 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 8,905 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 3.7 na wanafunzi wa kike ni 12,910 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 10,029 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 29.1. Hii imetokana na kuwepo kwa

mazingira mazuri na maabara za kisasa kwa skuli mbalimbali za Unguja na Pemba kulikopelekea kuongezeka kwa shauku ya wanafunzi katika kujifunza.

Kwa upande wa Kidato cha nne kwa mwaka 2025 idadi ya wanafunzi waliofaulu imepungua na kufikia 19,075 kutoka wanafunzi 21,333 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 10.6 kati ya hao wanafunzi wa kiume ni 7,399 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 8,724 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 15.2 na wanafunzi wakike ni 11,676 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 12,609 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 7.3. ***(Jadweli namba 29)***.

**Jadweli Namba 29: Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari za Serikali kuanzia kidato cha I-IV (2021-2025)**

| Mwaka | | Kidato | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | **Jinsia** | **I** | **II** | **III** | **IV** | |
| 2021 | Wanaume | 15,445 | 14,964 | 10,688 | 8,897 | 49,994 |
| | Wanawake | 16,710 | 16,260 | 15,051 | 12,693 | 60,714 |
| | **Jumla** | **32,155** | **31,224** | **25,739** | **21,590** | **110,708** |
| 2022 | Wanaume | 7,610 | 13,670 | 8,922 | 9,206 | 39,408 |
| | Wanawake | 11,075 | 14,960 | 12,261 | 12,902 | 51,198 |
| | **Jumla** | **18,685** | **28,630** | **21,183** | **22,108** | **90,606** |
| 2023 | Wanaume | 12,841 | 9,138 | 10,658 | 8,937 | 41,574 |
| | Wanawake | 11,547 | 12,068 | 14,292 | 13,029 | 50,936 |
| | **Jumla** | **24,388** | **21,206** | **24,950** | **21,966** | **92,510** |
| 2024 | Wanaume | 18,739 | 11,571 | 7,747 | 9,806 | 47,863 |
| | Wanawake | 20,962 | 11,134 | 11,506 | 13,522 | 57,124 |
| | **Jumla** | **39,701** | **22,705** | **19,253** | **23,328** | **104,987** |
| 2025 | Wanaume | 19,745 | 17,990 | 8,661 | 7,101 | 53,497 |
| | Wanawake | 22,484 | 20,686 | 9,781 | 11,057 | 64,008 |
| | **Jumla** | **42,229** | **38,676** | **18,442** | **18,158** | **117,505** |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026***

### 6.1.2 Idadi ya Wanafunzi: Maandalizi, Msingi, Kati na Sekondari kwa Skuli za Binafsi

Kwa mwaka 2025 idadi ya wanafunzi walioandikishwa katika skuli za Maandalizi kwa skuli binafsi imeongezeka na kufikia 42,002 kutoka wanafunzi 40,607 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 3.4 ambapo wanafunzi wa kiume wamefikia 20,944 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 20,422 mwaka 2024, wanafunzi wa kike wamefikia 21,058 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 20,185 mwaka 2024.

Kwa mwaka 2025 Idadi ya wanafunzi kwa skuli za Msingi imeongezeka na kufikia 72,868 kutoka wanafunzi 63,888 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 14. Kati ya hao wanafunzi wa kiume wamefikia 36,269 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 31,702 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 14.4 na wanafunzi wa kike wamefikia 36,599 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 32,186 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 13.7.

Idadi ya wanafunzi katika skuli za Sekondari (Kidato cha Kwanza hadi cha Nne) kwa mwaka 2025, imeongezeka na kufikia wanafunzi 12,078 kutoka wanafunzi 11,647 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 3.7 Ambapo idadi ya wanafunzi wa kike imeongezeka na kufikia 6,566 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 6,174 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 6.3 na idadi ya wanafunzi wa kiume pia imeongezeka na kufikia 5,512 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 5,473 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia1. ***(Jadweli namba 30).***

**Jadweli Namba 30: Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari za Binafsi Kidato I-IV (2021-2025)**

| Mwaka | Kidato | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Jinsia | I | II | III | IV | |
| **2021** | Wanaume | 1,608 | 1,501 | 1,403 | 1,282 | 5,794 |
| | Wanawake | 1,665 | 1,527 | 1,837 | 1,602 | 6,631 |
| | **Jumla** | **3,273** | **3,028** | **3,240** | **2,884** | **12,425** |
| **2022** | Wanaume | 1,590 | 1,522 | 1,586 | 1,227 | 5,925 |
| | Wanawake | 1,742 | 1,613 | 1,769 | 1,634 | 6,758 |
| | **Jumla** | **3,332** | **3,135** | **3,355** | **2,861** | **12,683** |
| **2023** | Wanaume | 605 | 1,517 | 1,672 | 1,418 | 5,212 |
| | Wanawake | 475 | 1,766 | 1,898 | 1,672 | 5,811 |
| | **Jumla** | **1,080** | **3,283** | **3,570** | **3,090** | **11,023** |
| **2024** | Wanaume | 1,696 | 557 | 1,620 | 1,600 | 5,473 |
| | Wanawake | 1,919 | 517 | 1,891 | 1,847 | 6,174 |
| | **Jumla** | **3,615** | **1,074** | **3,511** | **3,447** | **11,647** |
| **2025** | Wanaume | 1,851 | 1,589 | 646 | 1,426 | 5,512 |
| | Wanawake | 2,137 | 1,940 | 676 | 1,813 | 6,566 |
| | **Jumla** | **3,988** | **3,529** | **1,322** | **3,239** | **12,078** |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026.***

### 6.1.3 Idadi ya Wanafunzi wa Skuli za Sekondari kwa Jinsia kwa skuli za Serikali na Binafsi.

Idadi ya wanafunzi wa Kidato cha Kwanza kwa mwaka 2025 imeongezeka na kufikia wanafunzi 46,217 kutoka wanafunzi 43,316 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 6.7, ambapo skuli za Serikali ni wanafunzi 42,229 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 39,701 mwaka 2024 na skuli Binafsi ni wanafunzi 3,988 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 3,615 mwaka 2024.

Wanafunzi wa kidato cha Pili kwa mwaka 2024 wameongezeka kufikia wanafunzi 42,205 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 23,779 mwaka 2024 kati ya hao wakiume ni 19,579 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 12,128 mwaka

2024 na wanafunzi wa kike ni 20,686 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 11,651 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 77.5.

Kwa upande wa kidato cha Tatu, kwa mwaka 2025 idadi imepungua na kufikia wanafunzi 19,764 kutoka wanafunzi 22,764 sawa na upungufu wa asilimia 13.1, ambapo wanafunzi wa kiume ni 9,307 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 9,367 mwaka 2024 na wakike ni 10,457 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 13,397 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 22.

Aidha, wanafunzi wa Kidato cha Nne kwa mwaka 2025 wamepungua na kufikia 21,397 kutoka wanafunzi 26,775 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 20.0, ambapo kwa mwaka 2025 wanafunzi wakiume wamefikia 8,527 kutoka wanafunzi 11,406 mwaka 2024 na wakike ni 12,870 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 15,369 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 16.3.

Kwa upande wa Kidato cha Tano kwa mwaka 2025, idadi imeongezeka na kufikia wanafunzi 5,699 kutoka wanafunzi 5,530 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 3 kati ya hao wanafunzi wakiume kwa mwaka 2025 ni 2,632 kutoka wanafunzi 2,483 mwaka 2024 na wakike kwa mwaka 2025 ni 3,067 kutoka wanafunzi 3,047 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 1. Hii imesababishwa na uwepo wa walimu wazuri wenye viwango vya kufundisha pamoja kujielewa kwa wanafunzi wenyewe juu ya matumizi bora ya mitandao ya kijamii kwa ajili ya kujisomea.

Kwa upande wa Kitado cha Sita kwa mwaka 2025 idadi ya wanafunzi imeongezeka na kufikia 4,965 kutoka wanafunzi 3,476 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 42.8 Kati ya hao wanaume ni 2,196 waka 2025 kutoka wanafunzi 1,710 mwaka 2024 na wanawake ni 2,769 mwaka 2025 kutoka wanafunzi 1,766 mwaka 2024. Hii inatokana na uwepo wa mazingira mazuri ya kujisomea ikiwemo vifaa vya kisasa, walimu wenye sifa na matumizi mazuri ya mitandao ya kijamii. ***(Jadweli namba 31).***

**Jadweli Namba 31: Idadi ya Wanafunzi wa Shule za Sekondari kwa Jinsia na Kiwango: Kidato I-VI (2021-2025)**

| Mwak a | Jinsia | Kidato | | | | | | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| | | I | II | III | IV | V | VI | |
| **2021** | Wanaume | 17,053 | 16,465 | 12,091 | 10,179 | 1,953 | 1,250 | 58,991 |
| | Wanawake | 18,375 | 17,787 | 16,888 | 14,295 | 2,090 | 1,403 | 70,838 |
| | **Jumla** | **35,428** | **34,252** | **28,979** | **24,474** | **4,043** | **2,653** | **129,809** |
| **2022** | Wanaume | 9,200 | 15,192 | 10,508 | 10,433 | 1,511 | 1,715 | 38,051 |
| | Wanawake | 12,817 | 16,573 | 14,030 | 14,536 | 1,467 | 1,891 | 61,314 |
| | **Jumla** | **22,017** | **31,765** | **24,538** | **24,969** | **2,978** | **3,606** | **109,873** |
| **2023** | Wanaume | 13,446 | 10,655 | 12,330 | 10,355 | 1,898 | 1,317 | 38,480 |
| | Wanawake | 12,022 | 13,834 | 16,190 | 14,701 | 1,933 | 1,364 | 60,613 |
| | **Jumla** | **25,468** | **24,489** | **28,520** | **25,056** | **3,831** | **2,681** | **110,045** |
| **2024** | Wanaume | 20,435 | 12,128 | 9,367 | 11,406 | 2,483 | 1,710 | 57,529 |
| | Wanawake | 22,881 | 11,651 | 13,397 | 15,369 | 3,047 | 1,766 | 68,111 |
| | **Jumla** | **43,316** | **23,779** | **22,764** | **26,775** | **5,530** | **3,476** | **125,640** |
| **2025** | Wanaume | 21,596 | 19,841 | 9,307 | 8,527 | 2,632 | 2,196 | 64,099 |
| | Wanawake | 24,621 | 22,626 | 10,457 | 12,870 | 3,067 | 2,769 | 76,410 |
| | **Jumla** | **46,217** | **42,467** | **19,764** | **21,397** | **5,699** | **4,965** | **140,509** |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026.***

## 6.2 Idadi ya Wanafunzi wa Elimu ya Juu

Zanzibar ina jumla ya Vyuo Vikuu vitatu, kati ya hivyo kimoja ni cha Serikali na Vyuo Vikuu Viwili ni vya Binafsi. Idadi ya wanafunzi waliodahiliwa katika Vyuo Vikuu vya Serikali na Binafsi imeongezeka na kufikia wanafunzi 14,053 kwa mwaka wa masomo 2025/26 kutoka wanafunzi 13,038 kwa mwaka wa masomo 2024/25 sawa na ongezeko la asilimia 7.8 ambapo wanaume ni 5,381 kutoka wanafunzi 5,061 mwaka 2024/25 na wanawake ni 8,672 kutoka wanafunzi 7,977. Hii inatokana na muamko wa wanafunzi pamoja na miundombinu ya kujifunzia ikiwemo majengo ya kisasa yenye vifaa vya kisasa vya kujifundishia pamoja na juhudi za Serikali kutoa mikopo kwa wahitaji kuanzia ngazi ya stashahada *(Diploma*).

### 6.2.1 Idadi ya Mikopo iliyotolewa

Kwa mwaka wa masomo 2025/2026 jumla ya wanafunzi waliomba mkopo kupitia Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar ni 11,780 kutoka wanafunzi 7,183 kwa mwaka wa masomo 2024/25, kati ya hao wanaume ni 4,919 kutoka wanafunzi 3,216 na wanawake ni 6,861 kutoka wanafunzi 3,967. Aidha, Bodi ya Mikopo Zanzibar kwa mwaka wa masomo 2025/26 ilifanikiwa kutoa mikopo kwa wanufaika 8,957 kutoka wanufaika 4,629 kwa mwaka wa masomo 2024/2025 kati ya hao wanaume ni 3,595 kutoka 1,839 na wanawake ni 5,362 kutoka 2,790. Hali hii imesababishwa na ufaulu mzuri kwa wanafunzi na Bodi kuanza kuwapa mikopo wanafunzi wanaomaliza elimu ya diploma. ***(Jadweli namba 32)***.

**Jadweli Namba 32: Idadi ya Wanafunzi wa Vyuo Vikuu Walioomba na Waliopata Mkopo Kutoka Bodi ya Mikopo Mwaka 2024/25 na 2025/2026**

| **Walioomba Mkopo** | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| **2024/25** | | | **2025/26** | | |
| Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| 3,216 | 3,967 | 7,183 | 4,919 | 6,861 | 11,780 |
| **Waliopata Mkopo** | | | | | |
| **2024/25** | | | **2025/26** | | |
| Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| 1,839 | 2,790 | 4,629 | 3,595 | 5,362 | 8,957 |
| **Wanaoendelea na kunufaika na Mkopo** | | | | | |
| **2024/25** | | | **2025/26** | | |
| Wanaume | Wanawake | Jumla | Wanaume | Wanawake | Jumla |
| 3,627 | 5,299 | 8,926 | 4,376 | 5,242 | 9,618 |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar, 2026***

### 6.2.2 Mwenendo wa utoaji wa mikopo na Utaratibu wa kurejesha mikopo

Utoaji wa mikopo ya elimu ya juu Zanzibar ulianza mwaka wa fedha 2006/2007 na hadi kufikia March mwaka wa fedha 2025/2026 jumla ya TZS 138,932,484,435/- zilishatumika kwa utoaji wa Mikopo hiyo kwa wanafunzi 27,411. Bajeti ya utoaji mikopo mwaka wa fedha 2025/2026 ni TZS 35,000,000,000/- kwa wanafunzi 14,495 (4,877 wapya na 9,618 wanaondelea.

Aidha, katika utaratibu wa urejeshaji wa mikopo mnufaika hutakiwa kuanza kulipa mkopo wake miaka miwili tangu kumaliza masomo yake na kupata ajira. Mkopo huo hulipwa kwa kiwango maalum cha malipo kwa mwezi na mnufaika hulipa deni hilo bila ya nyongeza yoyote (Riba).

### 6.2.3 Ukusanyaji wa marejesho ya mikopo

Urejeshaji wa mikopo ya elimu ya Juu Zanzibar ulianza mwaka wa fedha 2011/12 (mwezi Februari 2012) takribani miaka sita (6) tangu kuanza utoaji wa mikopo; na hadi mwezi Aprili 2026 wadaiwa 8,329 wameanza kurejesha mikopo yao na jumla ya deni lao ni TZS 69,882,915,134.14/-. Aidha, hadi Machi 2026 jumla

ya TZS 35,178,944,200.83/-zimekusanywa kutoka kwa wanufaika 8,329 kati ya hao wanufaika 4,195 wamemaliza kulipa mikopo yao.

Kwa kipindi cha miezi tisa ya mwazo ya mwaka wa fedha 2025/2026 (Julai 2025 – Machi 2026) jumla ya TZS 4,307,823,460 za marejesho ya mikopo zimekusanywa ikiwa ni wastani wa TZS 475,000,000.00 kwa mwezi.

### 6.2.4 Urejeshaji wa Mikopo ya Elimu ya Juu

Kuna changamoto nyingi katika urejeshaji wa mikopo ya elimu ya juu, miongoni mwa hizo ni;

i. Wanufaika wengi wa mikopo kutokuwa tayari kurejesha mikopo yao kwa hiyari pale muda wa kurejesha mkopo unapofika.

ii. Kuwepo kwa wanufaika wenye madeni makubwa ambao imekuwa vigumu kulipa madeni yao kupitia mishahara yao na kumaliza kwa wakati.

iii. Kuwepo wadaiwa wanaostaafu kazi kabla ya kumaliza kulipa madeni yao ya mkopo wa elimu ya juu Zanzibar. Kwa sasa utaratibu hauruhusu kukata kiinua mgongo cha mstaafu anayepokea mafao yake kutoka ZSSF kulipa deni la mkopo wa elimu ya juu Zanzibar.

iv. Kuwepo wanufaika wanaochukuwa likizo bila malipo kabla ya kumaliza kulipa madeni yao na kupelekea marejesho ya mikopo yao ya kila mwezi kusita.

v. Baadhi ya wanufaika wa mkopo wa elimu ya juu Zanzibar wamekopa mikopo mingine na hivyo kutowezekana kulipa kiwango kinachotakiwa cha mkopo wa elimu ya juu kutokana na kuwepo kwa muongozo unaokataza kukata zaidi thuluthi mbili ya mshahara wa mfanyakazi.

vi. Ugumu wa kuwatambua na kupata marejesho ya mkopo kutoka kwa wanufaika wanaofanya kazi katika baadhi ya Taasisi za SMT.

vii. Ugumu wa kupata orodha za waajiriwa wapya wa Taasisi za SMT kwa ajili ya kuhakiki walionufaika na mikopo ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar

viii. Ugumu wa kupata marejesho ya mikopo kutoka kwa wafanyakazi wa Sekta Binafsi. Mara nyingi waajiri wa Taasisi huwa hawako tayari kutoa mashirikiano na kuwakata wafanyakazi wao.

### 6.2.5 Mapendekezo ya Kutatua Changamoto za Urejeshaji Mkopo wa Elimu ya Juu;

a) Elimu iendelee kutolewa kwa jamii juu ya umuhimu na wajibu wa kurejesha mikopo ya Elimu ya Juu;

b) Kuwepo na ufuatiliaji wa kutosha wa makubaliano kati ya BMEJZ ya HESLB ya kubadilishana taarifa za waajiriwa katika Taasisi za Muungano na Taasisi za SMZ ili kuwatambua wanufaika wa mkopo wa BMEJZ wanaofanya kazi katika Taasisi za Muungano;

c) Waajiri wote (Serikalini na Taasisi Binafsi) waendelee kupewa elimu juu ya wajibu wa kutekeleza Sheria ya Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu Zanzibar (BMEJZ) na Sheria ya Utumishi wa Umma inayowataka kuwasilisha BMEJZ orodha za wafanyakazi wapya wanaowaajiri;

d) Makubaliano ya hiari ya kupokea mikato ya mikopo ya wafanyakazi wa Taasisi za SMT kupitia Hazina-SMT yafikiwe ili kuondoa changamoto ya kuchelewa kupokea mikato ya taasisi kwa wakati;

e) Ziwepo njia mbadala za kubadilishana taarifa na Taasisi nyengine ili kuwapata wanufaika wa mkopo kama vile uhakiki wa wanufaika wa mikopo wakati wa kutoa leseni za aina mbalimbali, kuomba mikopo katika Taasisi za Fedha na wakati wa kuomba hati ya kusafiria; na

f) Mkopo wa elimu ya juu uwe ni mkato wa lazima (compulsory deduction) kama ilivyo mikato ya kodi ya mapato na mifuko ya hifadhi ya jamii ili kusiwe na kikwazo cha thuluthi moja.

### 6.2.6 Mikakati ya Bodi, Juu ya Urejeshajiwa Mikopo kwa Wanufaika wa mikopo ya Elimu ya juu

i. Kuendelea kuunganisha mfumo wa Usimamizi wa Mikopo wa Bodi (ZOLAS) na mifumo ya TEHAMA ya ndani ya Nchi yenye taarifa za Watumishi wa Serikali na Sekta binafsi, taarifa za walipa kodi ili kuwabaini wadaiwa wa BMWEJZ;

ii. Kuwakumbusha Waajiri jukumu lao la kuwasilisha taarifa za waajiriwa wapya BMWEJZ kila unapofanyika uajiri;

iii. Kuendelea kutoa taaluma kwa jamii na wahitimu wote waliokopeshwa na BMWEJZ juu ya jukumu la kurejesha mikopo;

iv. Kuendelea kufanya ziara za ukaguzi katika Taasisi za Serikali na Binafsi kuwatafuta Waajiriwa ambao ni wanufaika wa mikopo.

v. Kuwatumia wadhamini wa wadaiwa katika kuwatafuta waliowadhamini na kuwataka waanze kurejesha mikopo yao;

vi. Kuwashajiisha wahitimu kuwa Wazalendo kwa kurejesha mikopo yao kwa hiyari kupitia vyombo vya habari na makongamano;

vii. Kufanya kazi kwa mashirikiano na Bodi ya Mikopo ya Wanafunzi wa Tanzania (HESLB) kwa kubadilishana taarifa za wajiriwa katika Taasisi za Serikali na Binafsi na kufanya ziara za pamoja kwenye Taasisi.

## SURA YA SABA

## 7.0 SEKTA YA AFYA

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kufanya mapinduzi makubwa ya utoaji wa huduma bora za Afya kwa wote nchini, utoaji wa huduma unaenda sambamba na maendeleo ya kiteklonojia ili kuboresha huduma hizo, ujenzi wa miundombinu ya Afya kwa kujenga na kukarabati vituo vya hospitali ili huduma zipatikane karibu na wananchi. Vilevile Serikali imetoa fursa mbalimbali za uwekezaji ndani ya sekta ya Afya kwa lengo la kuongeza rasilimali watu na fedha kwa maendeleo endelevu ya sekta ya Afya nchini. Aidha, Serikali inaendeleza upanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja, kuajiri na kuwajengea uwezo wataalamu wa afya ili kupunguza uhaba wa watumishi. Serikali pia inaendesha kampeni za afya ya umma na kuimarisha matumizi ya teknolojia (e-Health) ili kurahisisha huduma na kupunguza magonjwa nchini.

### 7.1 Wataalamu wa afya

Kwa mwaka 2025, idadi ya madaktari bingwa wazawa wamefikia 61 kutoka 83 mwaka 2024, sawa na asilimia hasi 26.5 iliyosababishwa na madaktari wengi kuendelea na masomo yao nje ya nchi ili kuongeza ufanisi wa utendaji wao wa kazi na kutoa matibabu bora kwa wananchi ilikujenga jamii yenye afya bora kwa maendeleo ya Taifa watakapomaliza masomo yao.

Kwa upande wa madaktari bingwa kutoka nje ya nchi wamefikia Madaktari 29 mwaka 2025 kutoka 36 mwaka 2024, sawa na asilimia hasi 19.4 Hii imetokana na mazingira ya uchumi wa nchi zao.

Mwaka 2025, Madaktari wasaidizi (*Medical doctors)* wameongezeka na kufikia 522 kutoka 498 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 4.8. Kwa upande wauguzi wanao hudumu kwenye hospitali nchini wamefikia 2146 mwaka 2025 kutoka wauguzi 1,486, mwaka 2024 sawa na asilimia 44.4. Ongezeko hilo limetokana na kurudi masomoni. Mabwana na Mabibi afya wamefikia 646 mwaka 2025 ikilinganishwa na 224 mwaka 2024 sawa na asilimia 188.3 Hii imetokana na baadhi ya mabibi na mabwana afya kurudi masomoni na waajiriwa wapya. ***(Jadweli nambari 33.)***

**Jadweli Nambari 33: Idadi ya Watumishi wa Afya ya Umma 2021 – 2025**

| Watumishi wa Afya na Kada zao | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Madaktari Bingwa wazawa | 64 | 71 | 81 | 83 | 61 |
| Madaktari wasaidizi (Medical Doctors) | 310 | 343 | 478 | 498 | 522 |
| Madaktari wa meno (Dentist) | 76 | 82 | 86 | 91 | 115 |
| Klinik Afisa | 371 | 375 | 359 | 401 | 472 |
| Wauguzi | 1,521 1 | 1,384 | 1,424 | 1,486 | 2,146 |
| Wataalamu wa Maabara | 437 | 398 | 366 | 390 | 524 |
| Fundi madawa | 337 | 327 | 269 | 274 | 543 |
| Mabwana na mabibi Afya | 444 | 171 | 227 | 224 | 646 |
| Radiographic/Medical Image | 28 | 31 | 24 | 27 | 31 |
| Matibabu ya mifupa | 4 | 5 | 6 | 6 | 65 |
| Matibabu ya macho | 6 | 13 | 5 | 7 | 3 |
| Anesthesiologist | 25 | 15 | 19 | 20 | 50 |
| Tiba ya kimwili | 32 | 32 | 48 | 55 | 58 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2024/25.***

### 7.1.2 Idadi ya Vituo vya Afya na Wagonjwa

Zanzibar kupitia Wizara ya Afya hupokea miongozo kutoka Shirika la Afya Duniani (*WHO*) juu ya mwenendo wa Afya na kuhakikisha Afya za Wananchi zipo salama ili kujenga jamii yenye Afya bora kwa maendeleo endelevu. Huduma hizo hutolewa kupitia ngazi za vituo mbali mbali vya Afya msingi na sekondari (*PHCUs* na *PHCU+*), hospitali za Wilaya, Mikoa na rufaa.

Vituo vya afya vimefikia 391 mwaka 2025 kutoka 384 mwaka 2024 (bila kujumuisha kliniki zinazotoa huduma moja), sawa na ongezeko la asilimia 1.8. Ongezeko hili limesababishwa na mikakati thabiti ya Serikali katika kuimarisha sekta ya Afya ili kutoa huduma bora kwa wananchi wake, mgawanyo wa vituo hivyo ni 94 vya *PHCU* mwaka 2025 kutoka 86 mwaka 2024 na vituo vya *PHCU+* vimeongezeka na kufikia 49 mwaka 2025 kutoka 48 mwaka 2024. Hospitali za mkoa zimefika 2 mwaka 2025 ni sawasawa na mwaka 2024, kwa upande wa Hospitali za Wilaya zimefika 10 mwaka 2025 ni sawasawa na mwaka 2024, hospitali maalumu (*Tertiary level*) zimefikia 3 mwaka 2025 kutoka 2 mwaka 2024 na Hospitali za Rufaa 1 mwaka 2025 ni sawa na mwaka 2024.

Idadi ya wagonjwa waliotibiwa na kurudi majumbani mwaka 2025 imefikia 3,323,669 kutoka wagonjwa 3,329,878 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia hasi 0.19 Kati ya wagonjwa hao, wagonjwa 2,553,689 mwaka 2025 walisajiliwa vituo vya umma kutoka 2,604,210 mwaka 2024 na wagonjwa waliosajiliwa katika vituo binafsi mwaka 2025 wamefikia 621,943 kutoka 535,860 mwaka 2024.

Kwa upande wa vituo vya mashirika vimesajili wagonjwa 131,735 mwaka 2025 kutoka wagonjwa 167,801 mwaka 2024. Idadi ya wagonjwa waliolazwa imefikia 43,053 mwaka 2025 kutoka 49,788 mwaka 2024 sawa na asilimia hasi 13.5 kwa hospitali za umma.

### 7.1.3 Idadi ya Wagonjwa waliopata huduma za Mfuko wa bima ya Taifa ya Zanzibar mwaka 2024 -2025.

Wananchi waliopata huduma ya mfuko wa bima ya Zanzibar wamefikia 488,389 mwaka 2025 kutoka wapata huduma 307,215 mwaka 2024 ongezeko la asilimia 59.0. Hii imetokana na muamko mkubwa wa wananchi kutumia huduma za mfuko wa bima ya Afya kutokana na umuhimu wake na utoaji wa elimu juu ya huduma zinazopatikana kwenye mfuko huo.

**Jadweli Nambari 34: Idadi ya Wananchi waliopata huduma ya bima ya Afya Zanzibar 2024 - 2025**

| | 2025 | | 2024 | |
|---|---|---|---|---|
| Vituo vya Afya | Wanaume | Wanawake | Wanaume | Wanawake |
| Dispensari | 47,743 | 54,957 | 30,498 | 34,324 |
| Hospitali za Wilaya | 50,145 | 63,238 | 32,580 | 38,755 |
| Vituo vya Afya | 10,526 | 12,294 | 6,856 | 7,567 |
| Hospitali za Refaa | 14,370 | 22,482 | 9,616 | 13,410 |
| Clinic maalum | 91,323 | 120,909 | 58,578 | 74,785 |
| Clinic | 145 | 257 | 99 | 151 |
| Jumla ndogo | **214,252** | **274,137** | **138,227** | **168,988** |
| Jumla Kuu | **488,389** | | **307,215** | |

***Chanzo: Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Zanzibar 2025/26.***

## 7.2 Idadi ya Kinamama Waliojifungua na Vizazi hai

Idadi ya watoto waliozaliwa hai katika vituo vya afya Zanzibar imeongezeka na kufikia 61,944 mwaka 2025, kutoka 53,540 mwaka 2024 ikiwa sawa na ongezeko la asilimia 15.7. Ongezeko hilo ni matokeo ya elimu ya uzazi bora kutolewa na mabwana na mabibi Afya kwenye ngazi ya shehiya na kupelekea wazazi wengi kupata muamko wa kwenda kliniki (clinic) mapema kipindi cha ujauzito na kujifungulia vituoni kwa wakati.

### 7.2.1 Wilaya na Idadi ya Vizazi hai

Wilaya ya Mjini, imekuwa na vizazi hai kufikia 12,355 mwaka 2025 kutoka 14,812 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 16.6. Kwa upande wa Wilaya ya Mjini wazazi wengi hujifungulia kwenye vituo vya Afya vya Wilaya na Mikoa na PHCU+ Wilaya ya Wete imefikia idadi ya vizazi hai 4,642 mwaka 2025 kutoka vizazi hai 3,782 mwaka 2024 sawa ongezeko la asilimia 22.7. Wilaya ya Chake Chake idadi ya vizazi hai imefikia 6,316 mwaka 2025 kutoka vizazi hai 5,338 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 18.3. Wilaya ya Magharibi 'B' imefikia idadi ya vizazi hai 9,276 mwaka 2025, kutoka idadi ya vizazi hai 7,149 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 29.7 na Wilaya ya Magharibi 'A' idadi ya vizazi hai imefikia 6,691 mwaka 2025 kutoka idadi 4,309 mwaka 2024 zilirekodi sawa na ongezeko la asilimia 55.3 ***(Jadweli Nambari 35)***

**Jadweli Nambari 35: Idadi ya Vizazi Hai kwa Wilaya za Zanzibar, 2021-2025**

| Wilaya | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini "A" | 4,590 | 5,112 | 5,600 | 5,171 | 5,716 |
| Kaskazini "B" | 532 | 512 | 648 | 761 | 1,543 |
| Kati | 1,010 | 1,154 | 1,830 | 3,118 | 4,825 |
| Kusini | 1,578 | 1,619 | 1,849 | 1,864 | 2,396 |
| Magharibi "A" | 1,580 | 1,819 | 2,805 | 4,309 | 6,691 |
| Magharibi "B" | 2,490 | 2,484 | 3,939 | 7,149 | 9,276 |
| Mjini | 23,013 | 23,669 | 22,777 | 14,812 | 12,355 |
| Chake chake | 5,673 | 5,381 | 5,513 | 5,338 | 6,316 |
| Micheweni | 4,140 | 3,900 | 4,359 | 4,102 | 4,937 |
| Mkoani | 3,298 | 3,027 | 3,371 | 3,134 | 3,247 |
| Wete | 4,188 | 3,961 | 4,227 | 3,782 | 4,642 |
| **Jumla** | **52,092** | **52,638** | **56,918** | **53,540** | **61,944** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2025/26.***

### 7.2.2 Idadi ya Kinamama Wajawazito Waliojifungua Kwa Njia ya Upasuaji, Kawaida na Mimba Zilizoharibika.

Mwaka 2025, jumla ya wazazi waliojifungua hospitalini na vituo vya Afya wamefikia 61,215, kutoka 60,248 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 1.6, waliojifungua kwa njia ya upasuaji mwaka 2025 wamefikia 8,558 kutoka 7,329 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 16.7 na Waliojifungua kwa njia ya kawaida 52,657 mwaka 2025.

Mimba zilizoharibika kwa mwaka 2025 zimefikia 6,490 kutoka mimba 3,516, mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 84.6. Ongezeko hilo limesababishwa na utumiaji holela wa madawa kwa kina mama wajawazito, mimba kutunga nje ya mji wa uzazi, kinamama wajawazito kushiriki kazi za nguvu na mtindo wa maisha katika ulaji na matumizi ya vileo.

Wizara ya Afya inaendelea na tafiti mbali mbali ili kuangalia sababu za kuongezeka kwa idadi ya kina mama wanaojifungua kwa njia ya upasuaji, sababu za kiujumla ni: kubeba mimba katika umri mdogo au umri mkubwa,

watoto kuwa wakubwa tumboni, kuchelewa au kutokwenda kliniki mapema kwa kinamama wajawazito, wazazi kushindwa kujifungua kwa njia ya kawaida na watoto kufia matumboni mwa mama zao kabla ya kuzaliwa.

**Jadweli Nambari 36: Kinamama Wajawazito Waliojifungua kwa njia ya Upasuaji na Walioharibu Mimba (2021– 2025)**

| | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Idadi ya kina mama waliojifungua kwa njia ya upasuaji | 6,028 | 6,684 | 7,285 | 7,329 | 8,558 |
| Idadi ya mimba zilizoharibika | 2,913 | 5,611 | 3,942 | 3,516 | 6,490 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2025/26.***

### 7.2.3 Lishe ya Mama na Mtoto

Hali ya lishe ya mama na mtoto Zanzibar katika mwaka 2024/2025 imeendelea kuimarika, hii imetokana na jitihada za Serikali kupitia Wizara kuhamasisha wanajamii kula mlo bora kwa wakati. Juhudi za Serikali na mashirika yasiyo ya Serikali (*UNICEF, WFP,* na *WHO*) kuendelea kuhakikisha kinamama wajawazito na watoto wanapatiwa muongozo bora wa lishe. Mipango ya ( *Zero Stunting Campaign*) inaendelezwa kwa kila kijiji na miji hapa nchini ili kupunguza athari za ukosefu wa lishe kwa watoto. Upatikanaji wa vyakula vya kutosha na virutubisho muhimu kama vile protini, vitamini, na madini, ni kipaumbele cha wizara na kuendelea kutoa madini ya folic acid na chumvi za iodini ni muhimu kwa maendeleo ya makuzi ya watoto na kinamama.

Mwaka 2025, jumla ya watoto 383,610 wamepatiwa matone ya Vitamini A na madini chuma kwenye vituo vya Afya kutoka 379,491 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 1.08. Vidonge vya Fefol/MMs 237,939 na Vidonge vya Minyoo kwa mama wajawazito 30,275 vimetolewa kwa watoto. Katika kuimarisha huduma za lishe kwa mama na watoto nchini, Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea na kampeni maalumu ya ulishaji wa matone ya Vitamin "A" kwa watoto chini ya miezi 5 hadi 6 ili kuimarisha afya za watoto nchini. Hii ikiwa ni kawaida kwa nchi nzima kwa kila mwaka, Mafanikio haya yamechangiwa na mashirikiano makubwa kutoka sekta za Serikali na jamii hususani Masheha na wahudumu wa afya wa kujitolea (CHVs).

Serikali inaendelea na jitihada kubwa ya kuhakikisha lishe bora ya mama na mtoto inapatikana ili kujenga Taifa imara kwa maendeleo endelevu. Wizara ya Afya kwa kushirikiana na Shirika la Afya Duniani, inaendelea kusimamia miongozo yake juu ya lishe bora ya mama na mtoto na kutoa maelekezo ya utekelezaji kwa kupitia na kukamilisha mkakati shirikishi wa lishe ambao unahusisha utekelezaji wa majukumu ya sekta zote. Mkakati huo una shajihisha Wizara na Jamii kwa ujumla.

### 7.3 Mpango wa Damu Salama

Damu ni uhai kwenye maisha ya kila binaadamu. Bila ya damu salama hakuna uhai. Hivyo, upatikanaji wa damu salama kwa wahitaji ni sehemu ya jitihada za kuokoa maisha ya binaadamu. Benki ya damu inaendelea kukusanya, kuchunguza, kuhifadhi na kusambaza damu salama katika hospitali nchini. Wananchi wengi wamehamasika kuchangia damu kwa hiari kwa ajili ya kuokoa maisha yao na wananchi wenzao.

Mwaka 2025, kupitia Mpango wa Damu Salama, Benki ya Damu imekusanya jumla ya chupa za damu 20,241 kutoka chupa 16,224 zilizokusanywa mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 24.7. Hii imetokana na jitihada ya Benki kuimarisha utoaji wa elimu na uhamasishaji kwa wananchi juu ya kuchangia damu kwa hiyari ili kuokoa maisha ya watu kupitia mabonanza, mikutano ya kidini na mikusanyiko mikubwa ya watu kwa lengo kuu la kuhakikisha uwepo wa damu ndani ya nchi. Licha ya mafanikio hayo, benki ya damu salama imekuwa na changamoto ambazo zinarudisha nyuma shughuli za ukusanyaji damu kwa wakati kulingana na mahitaji halisi kwa muda sahihi ili kuendana na mahitaji ya damu salama.

**Jadweli Nambari 37: Ukusanyaji wa Damu Kupitia Benki ya Damu 2021-2025**

| Mwaka | Idadi ya Chupa za damu |
|---|---|
| 2021 | 15,206 |
| 2022 | 14,552 |
| 2023 | 15,313 |
| 2024 | 16,224 |
| 2025 | 20,241 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2025/26***

### 7.4 Magonjwa Kumi Yaliyoripotiwa Mara kwa Mara 2024/2025

Mwaka 2025, Ugonjwa wa Upumuwaji wa Juu (*Upper Respiratory Tract Infections*) umeongezeka na kufikia kesi 3,362,063 kutoka 2,321889 mwaka 2024 sawa na asilimia 44.7 ikifuatiwa na homa ya baridi na kikohozi umefikia 343,015 kutoka 247,604 sawa na asilimia 38.5 na Magonjwa Mengine ya Ngozi kwa asilimia 6.9, ikilinganishwa na 9.1 kesi kama hizo mwaka 2024. Hali hii imetokana na jitihada kubwa zinazochukuliwa na Serikali kupambana na maradhi kwa kutoa huduma bora na kuhamasisha mifumo bora ya ulaji kwa wananchi walio wengi na kufata taratibu za kiafya katika ulaji wa vyakula.

#### 7.4.1 Hali ya maambukizi ya Ugonjwa wa Ukimwi nchini

Maambukizi ya Ugonjwa wa Ukimwi ni tatizo la kitaifa, ambalo husababisha kupoteza nguvu kazi kubwa ya uzalishaji nchini na familia kwa ujumla. Kwa mwaka 2025, waliofanya vipimo wamefikia 142,076 kutoka 159,982 mwaka 2024, kati ya waliofanya vipimo na waliogundulika na maambukizi mwaka 2025 wamefikia 962 kutoka 1,150 mwaka 2024. Hii ni sawa na upungufu wa asilimia 16.3 ***(Jadweli Nambari 38)***

**Jadweli Nambari 38: Maambukizi ya Ugonjwa wa Ukimwi na waliopima mwaka 2025/24.**

| Umri na makun di yao | 2025 | | | 2024 | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | Waliopim a | Walioathiri ka | Asilim ia | Waliopima | walioathir ika | Asilim ia |
| 0-1 | 139 | 1 | 0.7 | 358 | 2 | 0.6 |
| 1-4 | 2,254 | 9 | 0.4 | 3,022 | 9 | 0.3 |
| 5-9 | 1,888 | 5 | 0.3 | 2,486 | 6 | 0.2 |
| 10-14 | 2,084 | 6 | 0.3 | 2,639 | 8 | 0.3 |
| 15 -19 | 11,426 | 25 | 0.2 | 13,705 | 34 | 0.2 |
| 20-24 | 30,365 | 142 | 0.5 | 35,558 | 159 | 0.4 |
| 25-49 | 84,135 | 696 | 0.8 | 91,475 | 838 | 0.9 |
| Jumla | 142,076 | 962 | 0.7 | 159,982 | 1,150 | 0.7 |

***Chazo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii 2025/26.***

## 7.5 Huduma za Upasuaji Mkubwa

Serikali inaendelea na mikakati ya kupambana na magonjwa makubwa ambayo yanaigharimu Serikali pesa nyingi sana kuwapatia wananchi wake matibabu nje ya nchi. Jitihada za makusudi kuhakikisha huduma ya upasuaji mkubwa inapatikana nchini kwa lengo la kuboresha Afya za wananchi na kupunguza gharama kubwa ya upatikanaji wa huduma hizi. Upasuaji wa uti wa mgongo na ubongo (*Neurosurgery*) na tiba ya Kansa kupitia kambi maalumu ya wataalamu wazawa na wakigeni kutoka nchini na Nchi Washirika ikiwemo Hispania, India, China wanaendelea na kutoa matibabu ya upasuaji. Mwaka 2025, kitengo kimefanikiwa kuwapatia matibabu wagonjwa 189 kutoka wagonjwa Kutoka wagonjwa 73 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 158.9. Hii imetokan na kuimarika kwa huduma, kuongezeka kwa wataalamu, kuongezeka kwa ajali za barabarani , Serikali kupitia Wizara ya Afya inaendelea na mikakati ya kuongeza juhudi za kitaalamu na kuongeza idadi ya wataalamu wa fani mbalimbali kwa lengo la kudhibiti kupambana na magonjwa hayo nchini.

## 7.6 Idadi ya Vifo kwa Wagonjwa

Mwaka 2025, idadi ya vifo kwa wagonjwa imepungua na kufikia vifo 2,043 kutoka 2,262 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 9.7. Ajali ya mishipa ya damu ya ubongo (*Cerebrovascular; CVA*), inaendelea kuwa sababu kuu ya vifo nchini, Ugonjwa wa upungufu wa oksijini (*Asphyxia*) ya kuzaliwa ilipanda hadi nafasi ya pili, kufikia 336 mwaka 2025 kutoka 159 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 111.32 Aidha, idadi ya vifo vitokanavyo na ugonjwa wa homa ya Nimonia vilipungua na kufikia vifo 50 mwaka 2025 kutoka 86 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 41.86.

## 7.7 Mpango wa Kumaliza Malaria Nchini.

Hali ya Malaria nchini inaendelea kuzibitiwa na kufikia malengo ya Serikali, kampeni ya kupambana na kudhibiti ugonjwa huu nchini imekua ya mafanikio makubwa kampeni hizo zinaendelea kufanyika kwa kushirikiana na Mashirika ya Kimataifa, ili kuendelea na utoaji wa elimu na muamko kwa wananchi juu ya njia za kuzuia na kujikinga ugonjwa huo. Wakati Serikali ikiendelea na utoaji wa huduma za matibabu stahiki, hali ya ugonjwa imepungua, licha ya changamoto ambazo hupelekea kuzorotesha jitihada za kuondosha maradhi hayo, programu (Zero Malaria Inaanza na Mimi na Wewe), inaendelea na

mikakati mbalimbali ili kufikia azimio la kumaliza malaria nchini. Mwaka 2025, Wagonjwa wa malaria wamepungua na kufikia 17,118 ukilinganisha na wagonjwa 22,375 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 23.5. Zanzibar maambukizi ya malaria yapo zaidi kwa vijana kuanzia miaka 15 hadi 45. Zaidi ya miaka mitatu hakuna vifo vya mama wajawazito na watoto chini ya umri wa miaka mitano. Aidha, Vifo tisa (9) vimeripotiwa mwaka 2025 kutoka vifo 18 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 50. Upungufu huo umetokana na jitihada za Serikali kupitia Wizara Afya kuelimisha Wananchi juu ya kujikinga na ugonjwa huo. ***(Jadweli nambari 39)***.

**Jadweli Nambari 39: Hali ya Malaria nchini na idadi ya vifo 2021-2025**

| | **Hali ya Malaria nchini** | **2021** | **2022** | **2023** | **2024** | **2025** |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1 | Idadi ya wagonjwa wa malaria | 6,616 | 4,557 | 18,283 | 22,375 | 17,118 |
| 2 | Vifo vya malaria | 20 | 9 | 4 | 18 | 9 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2025/26***

### 7.7.1 Dawa Zinazotumika Kutibu Malaria Nchini

Dawa zinazoendelea kutumika ni zile zilizothibitishwa na kupewa nafasi ya kwanza kwa ajili ya kutibu ugonjwa wa malaria. Dawa zinaendelea kutumika nchini ni mchanganyiko wa *"Artemisinin Based Combination Therapy* (ACTs)"kiwango cha 0.25mg/kg na *"Primaquinephosphate, Artemether Lumefantrine"* na *"primaquine"* inatumika kama njia ya pili ya tiba ya kutibu ugonjwa wa malaria sugu, dawa hizi ziko katika mfumo wa vidonge.

Kwa upande wa watoto kuanzia miezi 0-5 wanapatiwa dawa yenye viwango vya kitoto "Pediatric formular" hii ni kwa mujibu wa ushauri wa Shirika la Afya Duniani (WHO) kupitia Madaktari Bingwa wa watoto waliopendekeza utumiaji wa dawa hiyo. Aidha, Serikali imepiga hatua kubwa katika kupambana na malaria hadi kufikia lengo la kiwango cha chini ya asilimia zero. Wizara inaendeleza mikakati mbali mbali ya kudhibiti malaria, Zanzibar bila malaria inawezekana kupitia programu ya Zero Malaria na utoaji wa vyandarua kwa kaya mbali mbali nchini.

### 7.7.2 Madaraja ya Dawa za Kutibia Malaria Nchini

Wizara ya Afya imeweka muongozo wa kutibu Malaria nchini ili kutoa tathmini halisi ya kitabibu juu ya matumizi sahihi ya utumiaji wa dawa kwa Hospitali za Serikali na Binafsi ili kuepuka kutumia madawa yasiyofaa kwa kutibia ugonjwa huo kama ifuatavyo:-

i) Daraja la kwanza ni *Artesunate +Amodiaqune (ASAQ)*

ii) Daraja la pili ni *Dihydroartemisin+Piperaquine (DHAP), Artemether+ Lumefantrine (ALU)*

iii) Daraja la tatu ni Sindano ya Artesunate au Sindano ya *Artemether.*

### 7.7.3 Mikakati ya Kupambana na Malaria Zanzibar 2021-2025

Wizara inaendelea na mikakati ya kupambana na Malaria nchini kwa kutumia njia mbalimbali zikiwemo za Utumiaji wa dawa za *(Artesunate+Amodiaqune (ASAQ) Dihydroartemisin+Piperaquine (DHAP), Artemether+ Lumefantrine (ALU)* na kwa homa kali ni Sindano ya *Artesunate* au Sindano ya *Artemether.* Pia zikiwemo:

a. Upulizaji wa dawa (viatilifu) ya kuuwa mbu wa malaria majumbani;

b. Utumiaji wa vyandarua vyenye dawa ya Muda mrefu kwa ajili ya kuua na kufukuza mbu waenezao ugonjwa wa malaria;

c. Ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani waliogundulika kuwa na ugonjwa wa malaria kwa lengo la kukata maambukizi ya malaria;

d. Utiaji wa (viatilifu ) dawa katika mazalio ya mbu; na

e. Utoaji wa elimu ya afya kwa jamii juu ya kujingika na ugonjwa wa malaria.

Kazi Kuu Zilizofanywa na Programu katika Kupambana na

i. Kuhakikisha wananchi wanapata elimu ya kutosha ya umuhimu wa utumiaji wa vyandarua vyenye dawa ya Muda mrefu kwa ajili ya kuua na kufukuza mbu waenezao ugonjwa wa malaria;

ii. Uchunguzi wa vinasaba vya mbu waenezao Malaria;

iii. Upulizaji wa dawa (viatilifu) ya kuuwa mbu wa malaria majumbani;

iv. Ufuatiliaji wa wagonjwa majumbani waliogundulika kuwa na ugonjwa wa malaria kwa lengo la kuondosha maambukizi ya malaria;

v. Utiaji wa Viatilifu (Dawa) katika mazalio ya mbu; na

vi. Kuwepo kwa kikosi kazi cha kukamata na kuchunguza mbu wanaosambaza malaria.

### 7.7.4 Idadi ya Nyumba Zilizopuliziwa Dawa

Wizara inaendelea na mikakati maalumu ya kupambana na kumaliza Malaria Zanzibar. Wananchi wanapewa elimu na kupata muamko mkubwa ili wakubali kupigiwa dawa kwa hiari baada ya kuelewa athari za ugonjwa huo.

Kwa mwaka 2025, jumla ya nyumba zilizopuliziwa dawa zimepungua na kufikia 16,718 ikinganishwa na nyumba 54,004 mwaka 2024 sawa na upungufu wa asilimia 69. Hii ni kutokana na kupungua kwa mazalia ya mbu kutoka shehia mbalimbali.....***(Jadweli Nambari 40)***

**Jadweli Nambari 40: Idadi ya Nyumba Zilizopuliziwa Dawa 2021/25**

| Mwaka | Mgawanyo | Kaskazi ni Unguja | Kusini Unguj a | Mjini Magharibi | Kaskazi ni Pemba | Kusini Pemba | Juml a |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **2025** | lengo | 1,495 | 544 | 1,202 | 2,865 | 579 | 6,685 |
| | Nyumba | 1,461 | 523 | 1,141 | 2,707 | 558 | 6,390 |
| | Asilimia | 97.7 | 96.1 | 94.9 | 94.5 | 96.4 | 95.6 |
| **2024** | lengo | 3,803 | 454 | 10,581 | 1,987 | 972 | 17,797 |
| | Nyumba | 3,658 | 450 | 9,762 | 1,928 | 920 | 16,718 |
| | Asilimia | 96.2 | 99.1 | 92.3 | 97.3 | 94.6 | 93.7 |
| **2023** | lengo | 948 | 18,560 | 34,212 | 2,372 | 995 | 57,087 |
| | Nyumba | 923 | 17,494 | 32,262 | 2,344 | 981 | 54,004 |
| | Asilimia | 97.4 | 94.3 | 94.0 | 98.8 | 98.5 | 95.0 |
| **2022** | lengo | 14 | 2,172 | 10,799 | 4,470 | 4,797 | 22,252 |
| | Nyumba | 14 | 2,117 | 10,291 | 4,356 | 4,692 | 21,470 |
| | Asilimia | 100.0 | 97.5 | 95.3 | 97.4 | 98.0 | 96.5 |
| **2021** | lengo | 6,126 | 13,969 | 17,300 | 7,528 | 1,042 | 45,965 |
| | Nyumba | 6,561 | 13,958 | 17,008 | 7,695 | 1,094 | 46,316 |
| | Asilimia | 107.1 | 99.9 | 98.3 | 102.2 | 105.0 | 100.8 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii 2025-2026***

## 7.8 Maradhi ya Kuambukiza

Wizara ya Afya inaendelea kuelimisha na kuhamasisha jamii juu ya kutunza afya zao dhidi ya maradhi ya kuambukiza, ikiwemo kufanya uchunguzi wa

afya mara kwa mara na kujenga tabia inayozingatia kanuni za afya. Wananchi wanaendelea kupata muamko mkubwa wa kujua afya zao na kujikinga na maradhi yanayoambukiza, ikiwemo Ukimwi, Gonoria, Kaswende na Ukoma. Wananchi wengi hufika hospitalini na kujua afya zao kwa kufanya vipimo, kupatiwa dawa na ushauri pale wanapogundulika wamepata maambukizi ya magojwa hayo.

Mwaka 2025, wagonjwa 1191 wamegundulika na ugonjwa wa Kifua kikuu kutoka 1279 mwaka 2024. Sawa na ongezeko la asilimia hasi 6.9. Hii imetokana na jitihada za Serikali kupitia wizara za kusisitiza utumiaji wa dawa za kifua kikuu kwa wakati na upimaji wa makohozi ili kuzuwia maambukizo mapya. Juhudi za kutoa elimu kwa wananchi zinaendelea kutolewa kupitia Maafisa wa Afya nchi nzima kwa kuwapa wanajamii muamko juu ya kupunguza zaidi maambukizi ya magonjwa hayo nchini. ***(Jadweli nambari 41***).

**Jadweli nambari 41: Magonjwa ya kuambukiza 2023/25**

| Mwaka | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|
| Chlamydia | 104 | 54 | 101 |
| Gonorria | 217 | 162 | 245 |
| Kaswende | 280 | 134 | 183 |
| Ukimwi | 1298 | 1,150 | 962 |
| Kifua kikuu | 1,135 | 1279 | 1191 |

***Chanzo: Wizara ya Afya Zanzibar 2025/2026.***

## 7.9 USTAWI WA JAMII

### 7.9.1 Hali ya Madawa ya kulevya Zanzibar

Madawa ya kulevya ni janga linaloathiri dunia kwa ujumla, likidhoofisha afya ya jamii na maendeleo endelevu ya Taifa. Zanzibar pia imekumbwa na tatizo hili, hasa kwa kuathiri nguvu kazi ya taifa hususani vijana. Kutokana na hali hiyo, Serikali imeendelea kuchukua hatua mbalimbali kupambana na janga hili ili kulinda jamii na kuhakikisha maendeleo endelevu yanafikiwa kwa manufaa ya kizazi cha sasa na kijacho.

### 7.9.2 Idadi ya Nyumba na Wakaazi Walioathirika na Uraibu wa Madawa ya Kulevya (Sober Houses)

Jumla ya nyumba tatu (3) za waathirika wa madawa ya kulevya (za wanaume pekee) ziliripotiwa ikilinganishwa na nyumba nne (4) za mwaka 2024. Hii imetokana na kutumiwa kwa nyumba tatu pekee za waraibu zenye kukidhi idadi ya waraibu hao.

**Jadweli Nambari 42: Nyumba za Kurekebisha Tabia (Sober Houses by Location), 2021 – 2025**

| Mwaka | Sehemu Zilizopo Nyumba | Nyumba za wanaume | Nyumba za wanawake | Jumla ya Nyumba |
|---|---|---|---|---|
| 2021 | Unguja | 4 | 0 | 4 |
| | Pemba | 1 | 0 | 1 |
| | Jumla | 5 | 0 | 5 |
| 2022 | Unguja | 4 | 0 | 4 |
| | Pemba | 1 | 0 | 1 |
| | Jumla | 5 | 0 | 5 |
| 2023 | Unguja | 3 | 0 | 3 |
| | Pemba | 1 | 0 | 1 |
| | Jumla | 4 | 0 | 4 |
| 2024 | Unguja | 3 | 0 | 3 |
| | Pemba | 1 | 0 | 1 |
| | Jumla | 4 | 0 | 4 |
| 2025 | Unguja | 3 | 0 | 3 |
| | Pemba | 0 | 0 | 0 |
| | Jumla | 3 | 0 | 3 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2025/26.***

### 7.9.3 Idadi ya Waraibu Kwenye Nyumba za Kurekebisha Tabia.

Jumla ya waraibu 279 waliripotiwa mwaka 2025 ikilinganishwa na waraibu 275 mwaka 2024. Waathirika wakubwa wa uraibu huo ni umri kati ya miaka 15-25 na 26-35. Ongezeko hilo limetokana na changamoto za kijamii na kiuchumi zikiwemo ukosefu wa ajira, kutengana kwa wazee, na kuporomoka kwa maadili ambapo vijana wengi zaidi kuathirika na janga hilo. ***(Jadweli Nambari 43)***

**Jadweli Nambari 43: Idadi ya Waraibu Katika Nyumba za Waathirika wa Madawa ya Kulevya Zanzibar (2025- 2021) kwa Umri**

| Miaka /Umri makundi husika | | 15–25 | 26–35 | 36–45 | 46 + | Jumla |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 2021 | M/me | 91 | 147 | 42 | 29 | 309 |
| | M/ke | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Jumla | 91 | 147 | 42 | 29 | 309 |
| 2022 | M/me<br>M/ke | 33<br>0 | 73<br>0 | 32<br>0 | 28<br>0 | 166<br>0 |
| | Jumla | 33 | 73 | 32 | 28 | 166 |
| 2023 | M/me | 58 | 99 | 75 | 43 | 275 |
| | M/ke | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Jumla | 58 | 99 | 75 | 43 | 275 |
| 2024 | M/me | 75 | 64 | 40 | 24 | 203 |
| | m/ke | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Jumla | 75 | 64 | 40 | 24 | 203 |
| 2025 | M/me | 133 | 79 | 29 | 38 | 279 |
| | M/ke | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| | Jumla | 133 | 79 | 29 | 38 | 279 |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2025/26***

## 7.10 Sekta ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto kupitia Idara ya Ustawi wa Jamii inaendelea kuhakikisha huduma za hifadhi ya jamii zinaendelea. Idara inaendelea kutoa huduma hizo kwa jamii kwa kuwatunza wazee waliopo kwenye makao ya Sebleni, Welezo, na Limbani. Sekta hii ina mchango mkubwa katika kuhakikisha ustawi na usawa katika jamii. Sekta hii inalenga kulinda haki na kupunguza udhalilishaji dhidi ya wanawake, watoto, na wazee.

Mikakati ya Wizara katika kupambana dhidi ya unyanyasaji na ukatili wakijinsia ni utoaji wa elimu kwa jamii ikiwemo:

i. Kupitia vyombo vya habari, mikutano kwa wanajamii, skuli na taasisi mbalimbali, lengo ni kubadilisha mitazamo hasi kuhusu ukatili wa kijinsia na kupinga mila potofu zinazochochea ukatili;

ii. Kuhamasisha jamii juu ya kutoa taarifa pindi inapotokea masuala ya unyanyasaji na ukatili kwa kuondoa muhali;

iii. Kuratibu huduma za msaada kwa waathirika ikiwemo Dawati za jinsia katika vituo vya Polisi na Hospitali;

iv. Kutoa Ushauri nasaha kwa waathirika ili kuweza kuzuwia kuendelea kwa vitendo hivyo na hata kwa wale ambao si waathirika ili kuweza kuwalinda na kujilinda wenyewe; na

v. Kutoa msaada wa kisheria kwa kushirikiana na vituo vya huduma za kisheria kwa kuwasaidia waathirika kurejea katika hali ya kawaida na kupata haki zao.

### 7.10.1 Idadi ya Wazee na Watoto Yatima Kwenye Nyumba za Hifadhi

Mwaka 2025, vituo vya Watoto Yatima vimepungua kwa asilimia 4.4. kufikia vituo 538, ikilinganishwa na vituo 563 mwaka 2024. Kati ya hao, Wavulana 309 na wasichana 229. Hali hii imesababishwa na kuimarika kwa mifumo ya malezi mbadala ikiwemo ulezi wa kifamilia na kijamii, pamoja na hatua za Serikali na taasisi za kidini katika kuelimisha jamii na wadau katika kuunganisha, kuboresha, usimamizi wa vituo hivyo.

Aidha, idadi ya wazee imefikia 65 kwa mwaka 2025 (ikiwa wanaume ni 39 na wanawake 26), kutoka wazee 60 mwaka 2024, ambao wanaendelea kupatiwa huduma za ustawi wa jamii kupitia Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar. ***(Jadweli nambari 44)***

**Jadweli Nambari 44: Idadi ya Vituo vya Wazee, na Watoto Yatima 2021- 2025.**

| Vituo | Jinsia | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|---|
| Vituo vya kutunzia mayatima | Watoto wa kiume | 205 | 264 | 196 | 302 | 309 |
| | Watoto wa kike | 132 | 173 | 188 | 261 | 229 |
| | **Jumla** | **337** | **437** | **384** | **563** | **538** |
| Vituo Vya kutunzia Wazee | Wazee wa kiume | 42 | 22 | 40 | 35 | 39 |
| | Wazee wa kike | 29 | 37 | 27 | 25 | 26 |
| | **Jumla** | **71** | **59** | **67** | **60** | **65** |

***Chanzo: Wizara ya Maendeleo, Jinsia, Wanawake na Watoto 2021-2025.***

### 7.10.2 Watu wenye Mahitaji Maalumu Zanzibar 2025/26

Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar inaendelea kuweka mikakati thabiti ya kuhakikisha watu wenye mahitaji maalum wanashirikishwa kikamilifu na kupewa vipaumbele vinavyostahili, ili kukuza ushiriki wao katika shughuli za uzalishaji pamoja na upatikanaji wa fursa za maendeleo ya kiuchumi na kijamii, kwa lengo la kujenga jamii yenye usawa, umoja na maendeleo endelevu.

Mikakati ya Wizara Kuwawezesha Watu Wenye Mahitaji Maalum ni;

i. Kukuza ujumuishwaji wa masuala ya Watu wenye Ulemavu katika ngazi za kitaifa na Kimataifa;

ii. Kuwawezesha watu wenye Ulemavu kupitia mfuko wa watu wenye Ulemavu;

iii. Kukuza upatikanaji wa Haki na Fursa kwa watu wenye Ulemavu Unguja na Pemba; na

iv. Kuimarisha ushiriki wa Kitaifa na Kimataifa katika upatikanaji wa fursa mbalimbali za ajira.

**Jadweli Nambari 45: Watu Wenye Ulemavu na Mahitaji Maalumu 2024/2025**

| Aina za ulemavu | Vijijini | Mjini | Jumla |
|---|---|---|---|
| Ulemavu wa macho | 33,921 | 38,469 | 72,390 |
| Ulemavu wa maskio | 18,939 | 14,195 | 33,134 |
| Ulemavu wa kutembea | 20,074 | 19,189 | 39,263 |
| Ulemavu wa Ngozi | 1,384 | 1,258 | 2,642 |
| Ulemavu wa kimwili | 5,559 | 5,294 | 10,853 |
| Ulemavu jumuishi | 6,692 | 5,707 | 12,399 |
| Ulemavu Mwengineo | 21,600 | 17,864 | 39,464 |
| **Jumla kuu** | **108,169** | **101,976** | **210,145** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2025/26.***

## 7.11 Hali ya Wanawake na Watoto.

Ukatili dhidi ya wanawake na watoto ni tatizo kubwa la kijamii na ukiukwaji wa haki za binadamu unaoathiri usalama, afya, na ustawi wa wahanga. Athari zake hujitokeza kwa njia mbalimbali, ikiwemo madhara ya kimwili,

kisaikolojia, na kijamii, na huweza kudumu kwa muda mrefu endapo hatua stahiki hazitachukuliwa. Kwa mwaka 2025, matukio ya ukatili wa kijinsia yalipungua hadi kufikia 1,591 kutoka 1,809 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 12.1. Hii imetokana na jitihada kubwa za Serikali kupambana na hali ya ukatili wa kijinsia kwa kuelimisha jamii kupitia vyombo vya habari, mikutano na wanajamii, shuleni, na taasisi mbalimbali. ***(Jadweli nambari 46)***

**Jadweli Nambari 46: Idadi ya Matukio ya Ukatili wa Kijinsia Yaliyoripotiwa kwa Aina ya Ukatili; 2021 - 2025**

| Aina za Ukatili wa kijinsia /Mwaka | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Ubakaji | 621 | 651 | 923 | 833 | 660 |
| Ulawiti | 177 | 200 | 246 | 157 | 95 |
| Udhihaki dhidi ya asili | 83 | 88 | 90 | 71 | 67 |
| Utekaji nyara | 95 | 84 | 109 | 139 | 146 |
| Shambulio la ukatili wa kimwili | 114 | 125 | 210 | 279 | 166 |
| Shambulio | 132 | 212 | 376 | 330 | 0 |
| **Makosa kwa ujumla** | **1,222** | **1,360** | **1,954** | **1,809** | **1,134** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2025/26.***

## 7.12 Visa vya Unyanyasaji wa Kijinsia mwaka 2025

Unyanyasaji wa Kijinsia umepungua kufikia visa 1,228 mwaka 2025 kutoka visa 1,809 mwaka 2024, sawa na asilimia 32.1. Hali hii imetokana na wananchi kupewa elimu mtambuka na kimaadili pamoja na kuripoti kesi vituoni bila ya kuchukua sheria mikononi mwao. ***(Jadweli Nambari 47)***

**Jadweli Nambari 47: Idadi ya Matukio ya Ukatili wa Kijinsia Yaliyoripotiwa kwa Wilaya, 2021-2025**

| Wilaya | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Kaskazini 'A' | 60 | 52 | 98 | 59 | 72 |
| Kaskazini 'B' | 80 | 59 | 113 | 75 | 79 |
| Kati | 101 | 110 | 94 | 97 | 133 |
| Kusini | 35 | 47 | 45 | 46 | 49 |
| Mjini | 169 | 279 | 457 | 384 | 167 |
| Magharibi 'A' | 290 | 253 | 433 | 429 | 247 |
| Magharibi 'B' | 182 | 288 | 417 | 431 | 191 |
| Wete | 111 | 115 | 93 | 77 | 91 |
| Micheweni | 53 | 39 | 42 | 46 | 54 |
| Chake Chake | 88 | 76 | 108 | 113 | 93 |
| Mkoani | 53 | 42 | 54 | 52 | 52 |
| **Jumla** | **1,222** | **1,360** | **1,954** | **1,809** | **1,228** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2026.***

## 7.13 Makosa ya Jinai

Makosa ya Jinai kwa mwaka 2025, yamepungua hadi kufikia 1,658 kutoka 1,736 mwaka 2024, sawa na upungufu wa asilimia 4.49. Hii imetokana na jitihada za Serikali kupambana na makosa ya uhalifu nchini. ***(Jadweli Nambari 48).***

**Jadweli Nambari 48: Makosa ya Jinai yaliyoripotiwa mwaka 2021-2025**

| Makosa ya jinai | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Mauwaji | 41 | 34 | 44 | 66 | 53 |
| Jaribio la kutaka kujiuwa | 4 | 22 | 40 | 0 | 0 |
| Ubakaji kwa umri wa miaka 18 na zaidi | 58 | 62 | 95 | 75 | 60 |
| Ubakaji kwa msichana (chini ya miaka 18) | 563 | 585 | 824 | 758 | 600 |
| Ubakaji kwa kikundi | 0 | 4 | 4 | 0 | 0 |
| Jaribio la Kubaka | 4 | 2 | 9 | 0 | 5 |
| Uliwati | 177 | 200 | 246 | 157 | 95 |
| Kuingilia kati dhidi ya Asili | 83 | 88 | 90 | 71 | 67 |
| Kuachwa kwa Mtoto | 1 | 3 | 2 | 0 | 7 |
| Kuiba mtoto | 0 | 0 | 0 | 0 | 2 |
| Utekaji nyara | 95 | 84 | 109 | 0 | 146 |
| Mashambulizi | 939 | 125 | 376 | 330 | 457 |
| Shambulio la Aibu | 114 | 212 | 210 | 279 | 166 |
| **Jumla** | **2,079** | **1,421** | **2,049** | **1,736** | **1,658** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2026***

## 7.14 Ajali za Barabarani

Mwaka 2025, idadi ya ajali za barabarani zimeongezeka na kufikia 260 kutoka ajali 222 mwaka 2024, sawa na ongezeko la asilimia 17.1, kati ya ajali hizo 209 kutokaUnguja na ajali 51 Pemba. Ajali 194 zimesababishwa na mwendo kasi na ajali 66 zimesababishwa na uzembe wa dereva. ***(Jadweli nambari 49.)***

**Jadweli Nambari 49: Ajali za Barabarani zilizorikodiwa 2021 – 2025**

| Mwaka | 2021 | 2022 | 2023 | 2024 | 2025 |
|---|---|---|---|---|---|
| Unguja | 165 | 137 | 143 | 178 | 209 |
| Pemba | 44 | 35 | 50 | 44 | 51 |
| **Jumla** | **209** | **172** | **193** | **222** | **260** |

***Chanzo: Ripoti ya Muhtasari wa takwimu za kiuchumi na kijamii Zanzibar 2026***

## 7.15 Waathirika wa ajali za barabarani

Mwaka 2025, jumla ya waathirika wa ajali za barabarani ilifikia 441 kutoka 413 mwaka 2024, sawa na asilimia 7.3. Kati ya ajali hizo watu 219 waliofariki (Wanaume 195 na Wanawake 24) ikilinganishwa na 189 (Wanaume 170 na Wanawake 19) mwaka 2024.

## SURA YA NANE

## 8.0 MAENDELEO YA KIUCHUMI NA KIJAMII ZANZIBAR

Uchumi wa Zanzibar umekuwa kwa wastani wa asilimia 7.1 mwaka 2025, ukuaji huo umekwenda sambamba na maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Juhudi na weledi wa Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar katika kubuni sera na mikakati ya kuimarisha uchumi, zimeendelea kuwa kichecho cha kubadili changamoto za ukuaji wa uchumi kuwa fursa za maendeleo. Mwaka 2025, miongoni mwa viashiria vya moja kwa moja vya maendeleo ya kiuchumi na kijamii ni kama ifuatavyo:

i. Kuimarika kwa sekta ya Kodi za bidhaa, ambapo kwa mwaka 2025 imekuwa kwa wastani wa asilimia 12.8 kutoka wastani wa asilimia 7.0 mwaka 2024,

ii. Kuongezeka kwa uingiaji wa watalii nchini wapatao 917,167 mwaka 2025 kutoka watalii 736,755 mwaka 2024 sawa na ongezeko la asilimia 24.5;

iii. Kuongezeka kwa miradi mipya ya uwekezaji kwa asilimia 3.8 kufikia miradi 136 yenye thamani ya TZS 1,894,078 milioni iliyosajiliwa mwaka 2025 kutoka miradi 131 yenye thamani ya TZS 1,877,760 milioni iliyosajiliwa mwaka 2024;

iv. Kuongezeka kwa mapato ya ndani kufikia TZS 1,615.8 bilioni julai-machi mwaka 2025/26 ikilinganishwa na jumla ya TZS 1,299.0 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025 sawa na ongezeko la asilimia 24.3;

v. Kuongezeka kwa ajira mpya zilizosajiliwa kutoka Serikalini, Mashirika ya Serikali na Sekta Binafsi kwa asilimia 2.0 kufikia jumla ya ajira 85,182 (Wanaume 42,760 na Wanawake 42,422), kutoka jumla ya ajira 83,430 (Wanaume 43,629 na Wanawake 39,801) mwaka 2023/2024;

vi. Kuongezeka kwa kiwango cha usambazaji umeme kwa asilimia 9.3 kutoka kWh 671,732 mwaka 2024 kufikia kWh 734,738 mwaka 2025;

vii. Kuongezeka kwa usafirishaji wa zao la Karafuu kufikia tani 3,186.1 zenye thamani TZS 52.8 bilioni mwaka 2025 kutoka tani 1,974.4 zenye thamani ya TZS 30.7 bilioni mwaka 2024 sawa na ongezeko la thamani la asilimia 71.9;

viii. Kuongezeka kwa idadi ya wanafunzi waliopata mikopo kwa asilimia 93 kutoka wanafunzi 4,629 mwaka 2024 kufikia wanafunzi 8,957 mwaka 2025. Kati ya hao, Wanafunzi wa kiume ni 3,595 kutoka Wanafunzi 1,839 mwaka 2024, na wanafunzi wa kike ni 5,362 kutoka Wanafunzi 2,790 mwaka 2024;

ix. Kuimarika kwa viwango vya miundombinu ya mawasiliano ya barabara (Standard Road Networks) kwa kiwango cha lami zenye jumla ya urefu wa kilomita 1,218.17 kati ya kilomita 585.43 zisizo na lami; na

x. Kuimarika kwa hali ya amani na utulivu hapa nchini.

## SURA YA TISA

## 9.0 UTEKELEZAJI WA BAJETI KWA MWAKA 2025/2026

### 9.1 Mapato ya Serikali

#### 9.1.1 Ukusanyaji wa Mapato ya Ndani

Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali ilikadiriwa kukusanya mapato kutokana na vyanzo vya ndani jumla ya TZS 2,397.84 bilioni sawa na asilimia 29.9 ya Pato la Taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 2,104.01 bilioni zilitarajiwa kukusanywa kutoka vyanzo vya kodi na TZS 293.83 bilioni kutokana na vyanzo visivyo vya kodi. Kati ya TZS 2,104.01 bilioni zitokanazo na kodi, Mamlaka ya Mapato Zanzibar ilitarajiwa kukusanya kiasi cha TZS 1,257.24 bilioni, Mamlaka ya Mapato Tanzania ilikadiriwa kukusanya TZS 825.8 bilioni na TZS 21 bilioni zilipangwa kukusanywa na Idara ya Mhasibu Mkuu wa Serikali kutokana na Kodi ya Mapato kwa wafanyakazi wa Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania waliopo Zanzibar.

Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 mapato ya ndani yalifikia TZS 1,615.8 bilioni sawa na asilimia 95.4 ya makadirio ya kipindi hicho ukilinganisha na jumla ya TZS 1,299.0 bilioni zilizokusanywa katika kipindi kama hicho mwaka 2024/2025, kumejitokeza ukuaji wa mapato wa TZS 316.8 bilioni sawa na asilimia 24.4. Kati ya makusanyo hayo, mapato kutokana na kodi yalifikia TZS 1,463.03 bilioni ambazo ni sawa na asilimia 97.4 ya makadirio. Mapato yasiyokuwa ya kodi yalifikia TZS 152.7 bilioni sawa na asilimia 79.8 ya makadirio.

#### 9.1.2 Ukusanyaji wa Mapato Kitaasisi

Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA) ilikusanya jumla ya TZS 620.7 bilioni sawa na asilimia 102.1 ya makadirio ya TZS 607.9 bilioni ikilinganishwa na ukusanyaji wa kipindi kama hicho kwa mwaka 2024/2025 ambapo jumla ya TZS 471.0 bilioni zilikusanywa, sawa na ongezeko la asilimia 29.1 . Aidha, Mamlaka ya Mapato Zanzibar (ZRA) ilikusanya jumla ya TZS 826.6 bilioni sawa na asilimia 94.1 ya makadirio ya TZS 878.6 bilioni. Mapato ya ZRA kwa mwaka 2025/2026 yameongezeka kwa asilimia 26.1 ikilinganishwa na makusanyo ya mwaka 2024/2025 ambapo jumla ya TZS 655.5 bilioni zilikusanywa. Mapato yasiyokuwa ya kodi yamefikia TZS 152.7 bilioni sawa na asilimia 79.8 ya makadirio ya TZS 191.3 bilioni.

### 9.1.3 Mapato kutoka kwa Washirika wa Maendeleo

Katika mwaka wa fedha 2025/2026, Julai 2025 hadi Machi 2026 Serikali ya Mapinduziya Zanzibar imepokea misaada ya kibajeti (GBS 4.5%) yenye thamani ya TZS 79.5 bilioni. Aidha, Ruzuku na Mikopo iliyopokelewa kwa ajili ya Miradi na Programu za Maendeleo imefikia TZS 491.7 bilioni sawa na asilimia 141.2 ya makadirio ya kipindi hicho ya TZS 348.2 bilioni.

## 9.2 Matumizi ya Serikali 2025/2026.

Katika mwaka wa fedha 2025/2026 Serikali ilikadiriwa kufanya matumizi ya jumla ya TZS 6,622.68 bilioni sawa na asilimia 94.2 ya Pato la Taifa. Kati ya fedha hizo, jumla ya TZS 2,083.04 bilioni ni matumizi ya kazi za kawaida na jumla ya TZS 4,539.64 bilioni ni matumizi ya kazi za Maendeleo. Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 mwaka wa fedha 2025/2026 Jumla ya TZS 2,752.6 bilioni zimekadiriwa kutumika. Kati ya matumizi hayo yaliyokadiriwa, TZS 1,453.5 bilioni ni kwa kazi za Kawaida na TZS 1,299.1 milioni ni kwa Kazi za Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, matumizi halisi yalifikia TZS 3,214.2 bilioni. Kati ya matumizi hayo TZS 1,444.9 bilioni sawa na asilimia 99.4 zilitumika kwa kazi za kawaida na TZS 1,769.3 bilioni sawa na asilimia 136 zilitumika kwa Kazi za Maendeleo.

### 9.2.1 Matumizi ya Kazi za Kawaida

Matumizi ya Kazi za Kawaida kwa kipindi cha (Julai, 2025 hadi Machi, 2026) mwaka wa Fedha 2025/2026 yalifikia jumla ya TZS 1,444.9 bilioni sawa na ongezeko la asilimia 33.6 ikilinganishwa na matumizi ya kawaida ya kipindi kama hicho mwaka 2024/2025, ambapo jumla ya TZS 1,081.9 bilioni zilitumika.

### 9.2.2 Mishahara

Kati ya matumizi ya kazi za kawaida, matumizi ya Mishahara yalifikia TZS 500.3 bilioni katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2025 mwaka wa fedha 2025/2026 sawa na asilimia 99.1 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi hayo ni sawa na ongezeko la asilimia 2.3 ikilinganishwa na kipindi cha mwaka wa fedha 2024/2025, ambapo jumla ya TZS 489.1 bilioni zililipwa.

### 9.2.3 Matumizi Mengineyo

Matumizi mengineyo ukitoa Mfuko Mkuu wa Serikali yamefikia TZS 217.6 bilioni sawa na asilimia 97.6 ya makadirio ya kipindi hicho, matumizi hayo ni

sawa na ongezeko la asilimia 2.0 ikilinganishwa na matumizi mengineyo ya mwaka wa fedha 2024/2025 ya jumla ya TZS 214. 1 bilioni.

### 9.2.4 Matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali

Katika kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 matumizi ya Mfuko Mkuu wa Serikali yalifikia TZS 561.6 bilioni sawa na asilimia 100.8 ya makadirio ya kipindi hicho. Matumizi hayo ni sawa na ongezezko la asilimia 97.3 ikilinganishwa na matumizi kama hayo katika mwaka wa fedha 2024/25, ambapo jumla ya TZS 284.6 bilioni zilitumika.

### 9.2.5 Matumizi ya Kazi za Maendeleo.

Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 mwaka wa fedha 2025/2026, jumla ya matumizi ya Maendeleo yalikuwa TZS 1,769.3 bilioni sawa na asilimia 136.2 ya lengo la TZS 1,299.1 bilioni. Kati ya fedha hizo, fedha za ndani zilikuwa TZS 1,414.5 bilioni, sawa na asilimia 151.5 ya makadirio, na fedha za nje zilikuwa ni TZS 354.7 bilioni sawa na asilimia 97.1 ya makadirio ya TZS. 365.2.

## 9.3 Deni la Taifa

Hadi Machi 2026, deni la Taifa la Zanzibar limefikia TZS 2,671.28 bilioni deni hilo limetokana na Mikopo iliyotumika kugharamia miradi mbali mbali ya maendeleo. Aidha, kati ya jumla ya deni la TZS 2,671.28 bilioni, TZS 2,656.68 ni deni la ndani na TZS 14.60 bilioni ni deni la nje.

## SURA YA KUMI

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA MIRADI YA KIMKAKATI KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

### 10.1 UTANGULIZI

Katika kuhakikisha Utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2025/26, Serikali ilipanga kutekeleza Programu na Miradi maalum ya kimkakati katika maeneo mahsusi ikiwemo kutumia fursa za Uchumi wa Buluu, Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu, Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi, Rasilimali Watu na Huduma za Kijamii, pamoja na Utawala Bora na Uhimilivu kama yalivyoanishwa katika Mpango wa Maendeleo (ZADEP) 2021-2026. Maeneo haya yametiliwa mkazo kwa matarajio ya kuleta matokeo chanya na kwa haraka ikiwemo kuongeza mapato ya Serikali, upatikanaji wa ajira kwa wananchi, kukuza uwekezaji pamoja na kuimarisha hali za wananchi.

Kwa mwaka 2025/2026, jumla ya Programu na Miradi 26 imepangwa kutekelezwa na kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya Programu na Miradi 25 ya kimkakati imetekelezwa. Kwa mwaka 2025/26, jumla ya TZS 3,275.72 bilioni zimepangwa kutumika katika kugharamia Programu na Miradi ya Kimkakati (TZS 2,411.00 bilioni sawa na asilimia 74 kutoka Serikalini na TZS 864.72 bilioni sawa na asilimia 26 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) jumla ya TZS 1,965.43 bilioni zilipangwa kutumika ili kutekeleza Programu na Miradi ya kimkakati (TZS 1,446.60 bilioni kutoka Serikalini na TZS 518.83 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1,455.54 bilioni sawa na asilimia 74 ya bajeti ya maendeleo iliyopangwa ya TZS 1,965.43 zimepatikana na kutumika katika utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo (TZS 1,210.20 bilioni sawa na asilimia 84 ya lengo la TZS 1,446.60 bilioni zilipatikana kutoka Serikalini na TZS 245.35 bilioni sawa na asilimia 47 ya lengo la TZS 518.83 bilioni zilipatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Kimkakati umefanyika katika maeneo matano (5) ambayo ni Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu; Mazingira Wezeshi na Uimrishaji wa Miundombinu; Kuimarisha mageuzi ya Kiuchumi; Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii na Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu, kama inavyoonekana hapo chini:-

### I) Kutumia Fursa za Uchumi wa Buluu

Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa kutekeleza Programu na Miradi ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 428.1 bilioni (TZS 298.1 bilioni kutoka Serikalini na TZS 130.0 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Programu na Miradi iliyopangwa kutekelezwa ni Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria; kuimarisha Miundombinu ya Utalii; Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi Shumba; Ujenzi wa Bandari Jumuishi – Mangapwani; Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi; na Ujenzi wa Viwanda vya Kuchakata na Kusarifu Samaki.
Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 256.86 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 178.86 bilioni kutoka Serikalini na TZS 78.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 193.38 bilioni sawa na asilimia 75 ya lengo zimepatikana kutoka Serikalini. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo: -

#### a) Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria.

Programu hii ina lengo la kuendeleza Sekta ya Utalii kwa kulinda, kuhifadhi na kutunza maeneo ya kihistoria yaliyopo nchini kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae. Vile vile, Programu inasimamia kukuza shughuli za utalii kwa kuongeza fursa za ajira, vivutio vya utalii na kuongeza Pato la Taifa. Programu hii ilianza mwaka 2017/18. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.6 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 406.01 milioni sawa na asilimia 11 ya lengo zimepatikana.

Shughuli zilizotekelezwa kwa kipindi cha miezi tisa (9) ni uandaaji wa michoro kwa ajili ya ujenzi wa uzio katika maeneo ya Mwera, Pete, Dunga, Kuumbi, Mwanampambe na Mvuleni. Aidha, ujenzi wa Duka, Mgahawa, Sehemu ya mapumziko, vyoo, upakaji wa rangi katika Ofisi, uwekaji wa ngazi, ujenzi wa ukuta wa kuzuia maji ya bahari, uwekaji wa njia za kupita na sehemu ya maegesho ya vyombo vya moto, uingizaji wa huduma ya maji na umeme, uchimbaji wa kisima, ujengaji wa hodhi na mnara wa maji, upandaji wa bustani pamoja na ukarabati wa majengo ya kihistoria yaliopo katika eneo la mradi lililopo Ras Mkumbuu – Pemba umekamilika. Kwa ujumla utekelezaji kwa upande wa Pemba umefikia asilimia 90. Aidha, katika kuimarisha eneo la kihistoria lililopo

Mangapwani – Unguja utekelezaji wake umefikia asilimia 95. Kazi zilizofanyika ni pamoja na uchimbaji wa visima vitatu (3), kuweka viluva (interlock) katika eneo la mradi, ujenzi wa duka, mgahawa, sehemu ya mapumziko, vyoo, ofisi, ujenzi wa ukuta wa uzio, na kuweka miundombinu ya huduma ya maji na umeme zimekamilika. Kazi zilizobaki ni kufanya usafi na kutengeneza bustani.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuyahifadhi na kuyalinda maeneo yote ya kihistoria ya Zanzibar, kuongeza mapato nchini kupitia viingilio katika maeneo hayo, pamoja na kukuza sekta ya Utalii kwa kuongezeka kwa vivutio vya utalii nchini.

**b) Mradi wa Ujenzi wa Bandari Jumuishi – Mangapwani**

Mradi huu una lengo la kujenga bandari jumuishi ya kisasa Mangapwani (Multipurpose Port) ambayo itajumuisha ujenzi wa gati ya mizigo, eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta na ujenzi wa chelezo cha kukarabati meli. Mradi umeanza mwaka 2020/21. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 205.10 bilioni kutoka Serikalini. Mradi huu unatekelezwa na Mkandarasi China Harbour Engineering Company chini ya mshauri elekezi Dar Al Handasah. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 123.06 bilioni.

Hadi kufikia Machi 2026 jumla ya TZS 186.04 bilioni sawa na asilimia 151 ya lengo la TZS 123.06 bilioni zimepatikana na kutekeleza kazi za uchimbaji wa msingi katika eneo la ujenzi, uzungushaji wa uzio katika eneo la ujenzi na ujenzi wa eneo la sehemu litakapotengezewa zege. Aidha, uwekaji wa ardhi sawa umefanyika katika eneo la bumbwini kwa ajili ya kutengeneza miguu (pile) ya kushikilia daraja la bandari. Kwa upande wa Ujenzi wa bandari ya mafuta na gesi pamoja na chelezo Mangapwani kwa ujumla ujenzi umefikia asilimia 15; kazi zilizofanyika ni uchunguzi wa udongo, upimaji wa kina cha maji, kufungwa kwa vifaa vya ujenzi vikiwemo *Flowmeter, manifold, buoys, pipe line na Platform.* Kazi za kuweka miundombinu ya bandari (CBM) inaendelea. Ujenzi wa nyumba 170 za fidia unaendelea kwa hatua za uwekaji wa miundombinu ya maji na umeme pamoja na hatua za mwisho za ujenzi (utiaji wa milango na madirisha) na nyumba 200 zimekamilika.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuinua uchumi wa Zanzibar, kutoa ajira kwa wananchi, kuimarisha harakati za kibiashara baina ya Zanzibar na bandari za Tanzania Bara pamoja na Nchi za jirani ikiwemo Kenya na Ukanda wa Bahari ya Afrika Mashariki. Aidha, mradi utarahisisha usafiri wa magari ya mizigo kutoka lango kuu la bandari kuelekea maeneo mengine ya kibiashara Zanzibar.

**c) Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Maruhubi**

Mradi huu una lengo la kujenga bandari ya kisasa ambayo itajumuisha ujenzi wa bandari ya abiria na mizigo. Mradi ni wa miaka mitatu (3) na umeanza mwaka 2024/25. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 130 bilioni kutoka katika sekta binafsi. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 78 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa ghala,maduka,ujenzi wa njia za watembea kwa miguu (causes way), mizani ya kupimia mizigo ujenzi na ufungaji wa tishali (Barge)zenye uwezo wa kuhudumia meli nne kwa pamoja ujenzi wa ukuta wa fensi na ufukiaji wa eneo la bahari. Utekelezaji wa mradi huu umefikia asilimia 87.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarisha usafirishaji wa abiria na mizigo ndani na nje ya nchi, kutaongeza ajira kwa wananchi na kuboresha maisha ya jamii, kutasaidia kuondoa msongamano katika bandari ya Malindi na itakuwa ni kivutio kwa wawekezaji na watalii wa Zanzibar pamoja na kuongezeka kwa Mapato ya wananchi na Serikali.

**d) Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya kuchakata na Kusarifu Samaki**

Mradi huu una lengo la kuimarisha mnyororo wa sekta ya uvuvi na uongezaji wa thamani wa bidhaa ya dagaa kupitia usindikaji wa kisasa pamoja na kujenga viwanda vitakavyoshughulikia ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa dagaa kwa masoko ya ndani na nje ya nchi. Mkandarasi Mkuu ni JKU na mshauri elekezi ni ZBA. Mradi ni wa miaka mitano (5) umeanza mwaka 2020/21. Kwa mwaka wa 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 51 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 30.60 bilioni.

Hadi kufikia Machi 2026, mradi umetumia bajeti ya mwaka 2024/25 kwa kujenga viwanda vya kusarifu dagaa na samaki katika maeneo ya Fungurefu, Ndagoni na Kama. Kwa upande wa Fungurefu ujenzi upo katika hatua ya misingi na

kazi imefikia asilimia 16. Kiwanda cha kusarifu dagaa Ndagoni ujenzi umefikia asilimia 45 ambapo ujenzi wa jengo la ofisi, jengo la kupakulia na kuoshea dagaa, vyoo, chumba cha baridi vimefikia katika hatua ya umaliziaji. Kwa upande wa majengo ya mkahawa, biashara, kubadilishia nguo yamefikia hatua ya kuezeka. Aidha, jengo la kiwanda cha kukaushia dagaa limefikia hatua ya msingi na barabara imejengwa kwa kiwango cha fusi.

Kwa upande wa kiwanda cha Kama, ujenzi umefikia asilimia 62. Ujenzi wa jengo la biashara, vyoo, jengo la kubadilishia nguo namba 1, majengo ya kupakulia, kuoshea na kuchemshia dagaa, na jengo la kuhifadhi kemikali yapo katika hatua ya ukamilishaji. Kwa upande wa jengo la kubadilishia nguo namba 2, nyumba za wajasiramali, nyumba za wateja ujenzi umefikia hatua ya kuezeka na Ofisi ipo hatua ya kupiga plasta. Eneo la kuanikia dagaa lipo katika hatua za mwisho. Aidha, ujenzi wa majengo ya viwanda vya kukaushia na kuchakata dagaa umefikia hatua ya msingi na barabara (mita 300) imejengwa kwa kiwango cha zege.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarika kwa mnyororo wa sekta ya uvuvi na kuongeza thamani ya mazao ya baharini hasa bidhaa ya dagaa kupitia usindikaji wa kisasa pamoja na kujenga viwanda vitakavyoshughulikia ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa dagaa kwa masoko ya ndani na nje ya nchi.

#### e) Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi –Shumba (PEMBA)

Mradi una lengo la kuimarisha mazingira ya wavuvi kwa kujenga miundombinu itakayochochea ukuaji wa Sekta ya uvuvi. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 29.99 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 17.99 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 6.94 bilioni sawa na asilimia 39 zimepatikana kutoka Serikalini. Fedha hizi zimehaulishwa kutoka katika fungu la mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi na kutumika kwa ajili ya unuzi wa mashine za Kiwanda cha Mwani.

Kukamilika kwa mradi kutapelekea kuimarika sekta ya uvuvi kwa kuboresha miundombinu ya kuhudumia shughuli za uvuvi, kuongeza thamani ya mazao ya uvuvi, kupunguza upotevu wa samaki baada kuvuliwa, na kuongeza kipato kwa wavuvi pamoja na fursa za ajira kwa wananchi wa eneo husika.

### II) Mazingira Wezeshi na Uimarishaji wa Miundombinu

Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa kutekeleza programu na miradi ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 1,078.92 bilioni (TZS 583.81 bilioni kutoka Serikalini na TZS 495.11 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa kujenga Barabara Kuu; Barabara za Ndani; na kutengeneza Barabara za Mjini; kuimarisha Viwanja vya Ndege; Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar; Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar; na kujenga Misingi ya Maji pamoja na kuondosha mabwawa ya maji yanayotuwama katika Maeneo ya Mji.

Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 720.85 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 423.79 bilioni kutoka Serikalini na TZS 297.06 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 678.70 bilioni sawa na asilimia 94. ya lengo la TZS 720.85 bilioni zimepatikana (TZS 554.09 bilioni kutoka Serikalini na TZS 124.61 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Utekelezaji halisi ni kama ifuatavyo: -

#### a) Programu ya Ujenzi wa Barabara Kuu

Programu hii ina lengo la kuunganisha miji mikubwa ya Zanzibar na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari ili kuhuisha uchumi na uwekezaji. Programu imeanza 2022/23. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 329.03 bilioni (TZS 133.4 bilioni kutoka Serikalini na TZS 195.63 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 197.42 bilioni (TZS 80.04 bilioni kutoka Serikalini na TZS 117.38 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 289.01 bilioni sawa na asilimia 146 ya lengo la TZS 197.42 bilioni (TZS 274.72 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 343 ya lengo la TZS 80.04 billioni na TZS 14.29 bilioni sawa na asilimia 12 ya lengo la TZS 117.38 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zimepatikana. Kazi zilizotekelezwa ni kama ifuatavyo:-

Kwa upande wa Unguja ni ujenzi wa barabara ya Kitogani - Paje (km 10.6) kwa kiwango cha lami, Mkwajuni- Kijini (0.6km) kwa tabaka la pili la kifusi na Barabara ya Unguja Ukuu –Uzi ng'ambwa (6.5km) unaendelea kwa kiwango cha lami kwa baadhi ya sehemu na kwa sasa ujenzi umesimama kutokana

changamoto ya wananchi 66 kukataa fidia kupisha utekelezaji wa mradi. Barabara ya Tunguu-makunduchi na kisauni-Fumba kazi ya *Topographical na Geotechnical survey* umefanyika na ujenzi wa kambi ya mkandarasi umefanyika katika maeneo ya Muyuni na Kibele pamoja na uthamini wa mali za wananchi na usanifu wa michoro unaendelea. Pia, Ujenzi wa barabara Tazari-Kilimani (3.0km) umekamilika kwa kiwango cha lami; Bumbwini-Pangatupu-Mahonda (11.3 km) imekamilika kwa kiwango cha lami na Daraja linaendelea sehemu za kuingilia (Inlet) na kutokea maji (Outlet) na limefikia asilimia 98%; Mangapwani-Zingwezingwe - Mahonda (8.4 km) imekamilika na uchimbaji wa mitaro (6.72 km) umekamilika, Mfenesini-Mangapwani (7.2km) inaendelea na usafishaji kwa baadhi ya maeneo (by section) yasiyokuwa na changamoto za fidia.

Kwa upande wa Pemba, barabara ya Chanjamjawiri -Tundaua yenye urefu wa (10.73 km). Kazi zilizofanyika ni usafishaji wa barabara (6.5km), uwekaji wa kifusi wa tabaka la 1 (3.5 km), uwekaji wa tabaka la pili (3 km) na tabaka la tatu (2.5 km). Barabara ya Wete - Chake-Chake ujenzi wa mitaro umefanyika kilomita 7 sawa na asilimia 31 ya barabara yote.

Kwa barabara ya Chake–Mkoani ( 43.5km), Mjenzi ni Kampuni ya Propav na Mshauri elekezi ni Dar al Handas. Kazi ya uchunguzi wa udongo imefanyika na uthamini wa mali za wananchi ambao wataathirika na mradi unaendelea chini ya Kampuni ya GRSK na mkandarasi anaendelea na kazi ya usanifu wa michoro. Kwa ujumla utekelezaji wa ujenzi wa programu hii imefikia asilimia 60.69.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuunganisha miji mikubwa ya Unguja na Pemba na kukuza shughuli za uchumi na uwekezaji kwani barabara hizi ni kiunganishi cha miji na maeneo ya usafirishaji ikiwemo viwanja vya ndege na bandari pamoja na maeneo mengine na hivyo kuchochea ukuwaji wa uchumi.

**b) Programu ya Ujenzi wa Barabara za Ndani**

Programu imeanza mwaka 2022/23. Lengo la Programu ni kujenga barabara za ndani na vijijini zenye urefu wa kilomita 275.9 za awali na kilomita 65 mpya katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Barabara hizi zitaunganisha mitaa na maeneo mengine ikiwemo barabara itakayosaidia kupunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba na kupendezesha miji na mitaa katika maeneo ya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 78.03 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai

2025 hadi Machi 2026) programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 46.82 bilioni, hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 143.49 bilioni sawa na asilimia 293 ya lengo la TZS 46.82 bilioni zimepatikana.

Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa barabara zenye jumla ya km 68 (km 33.58 zimejengwa kwa kiwango cha lami na km 34 zimejengwa kwa kiwango cha fusi) miongoni mwa barabara hizo ni Kajengwa-Koba-Kinandi-Mnarani 4.98km, Kajengwa-Uwandani-Kibwegele, 6.75km, Kigaeni-Blue Moon 4.2km, Mtandao-Chiyabonde 1.36km, Mtegani-Miwaleni 1.21km, Kuungoni-Kae Kuu-Madete 0.92km, Wawi Mesi-Mzambaraumboko 6.4km, Penjewani-Mjini Kiuyu 2.27km, Mgagadu-Kwautao 5.49km, Pembeni-Pandani 3.38km, Mzambarautakao-Mchangamdogo 6.3km, Kiungoni-Tovuni 2.96km, Gando-Chokaani 2.1km, Gando-Chaoni 1.0km, Bwagamoyo-Kele 5.25Km, Uondwe-Nyali 1.96km, Barawa-Mleteni 1.5km pamoja na Jambang'ome Jct – Jambangome 2.42km kwa upande wa Pemba.

Ujenzi wa barabara kilomita 163.22, ujenzi unaendelea na jumla ya 14.16km zimejengwa kwa kiwango cha lami (Unguja ni 8.85km na Pemba ni 5.31km). Barabara hizo ni pamoja na barabara ya Istiqama-Zanzibar University 0.395km, Nganani - Kumbini - Chuini - Bungi - Mtegani Spur 1.91km, Barabara ziendazo kwenye viwanja vya Michezo vya Wilaya 0.7km, Tasani - Mnarani – Pwani 1.63km, Mnarani – Kigaeni 2.19km, Madete skuli - Skuli ya Kusini 0.35km pamoja na Mwembesanda – Mavua 1.68km kwa upande wa Unguja na barabara ya Minazini-Mabaoni (Gando) 0.34km pamoja na Chanjaani-Mitamani-Pujini 4.97km kwa upande wa Pemba.

Aidha, ujenzi wa barabara kilomita 65.5, ujenzi huo unaendelea kwa hatua mbali mbali Unguja na Pemba, barabara ya Wete-Konde - Gando imejengwa kwa kiwango cha lami(km 18) na zilizobaki zinaendelea kujengwa kwa hatua mbali mbali za kifusi. Kwa ujumla utekelezaji wa programu hii ujenzi umefikia asilimia 73.15.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuunganisha mitaa na vijiji 62 vya Unguja na Pemba, kutapunguza msongamano katika barabara kuu pamoja na kuongeza haiba na kupendezesha mitaa na maeneo mengi ya miji na vijiji. Aidha, programu itasaidia kurahisisha usafirishaji wa mizigo na kuimarisha ukuaji wa uchumi, kuongeza kipato cha mwananchi mmoja mmoja pamoja na kuimairika kwa sekta nyengine za kiuchumi zikiwemo sekta ya kilimo na biashara.

### c) Programu ya Matengenezo ya Barabara za Mjini

Programu hii ina lengo la kuimarisha haiba ya mji wa Zanzibar kwa ujenzi wa barabara katika maeneo ya mjini. Mradi unahusisha ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za mjini na uimarishaji wa barabara katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Programu hii imeanza mwaka 2022/23. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 35 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 21.00 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 32.26 bilioni sawa na asilimia 154 ya lengo la TZS 21.00 bilioni zimepatikana.

Kazi zilizotekelezwa ni ujenzi wa barabara za juu (flyover) katika mzunguko (Roundabout) wa Mwanakwerekwe umekamilika kwa kuwekwa lami na uwekaji wa taa kwa asilimia 100. Ujenzi wa barabara za juu katika mzunguko wa Amani umefikia asilimia 70 ya utekelezaji. Aidha, ujenzi wa chelezo kwa pande zote mbili za ujenzi unaendelea na kwa baadhi ya barabara za mjini zinaendelea katika hatua mbali mbali zikiwemo barabara ya Mombasa Soko la Mboga – Azania (1.3km), Kwa kira-Kituo kipya cha Uwanja wa Ndege (1.03km) na na Mkapa road 5km zimekamilika kwa kiwango cha lami na Kinazini-Mtoni kilomita 0.86 (lumumba –JKU na Verde- Mkapa road zimewekwa lami upande mmoja) na ya Amani roundabout–Mikunguni-Biziredi (2.55km) na Kariakoo – Mwanakwerekwe (3.71km), hazijaanza kutoka na kusubiri malipo ya fidia kwa wananchi watakaoathirika na ujenzi.

Kukamilika kwa programu hii kutaongeza haiba na kupendezesha miji yetu na kusaidia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii na biashara na kuondoa misongamano pamoja na kupunguza ajali katika maeneo hayo.

### d) Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya Kimataifa vitakavyoweza kupokea ndege aina ya “Code 4C”. Programu itahusisha ujenzi wa Uwanja wa ndege wa Pemba, Nungwi na “Terminal II” AAKIA. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa jumla ya TZS 284.0 bilioni (TZS 124.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 159.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu

hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 170.40 bilioni (TZS 74.70 bilioni kutoka Serikalini na TZS 95.70 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 114.51 bilioni sawa na asilimia 67 ya lengo la TZS 170.40 bilioni (TZS 18.47 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 25 na TZS 96.04 bilioni sawa na asilimia 100.36 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepatikana. Kwa upande wa Terminal II AAKIA kazi ya kuezeka, skimming, kupaka rangi, ufungaji wa conveyer belt ,ujenzi wa immigration counter,uwekaji wa nguzo za kuunganisha terminal building II na Terminal building III pamoja na kazi za umaliziaji (skimming,floor tiles na ceiling) zinaendelea na utekelezaji wake umefikia asilimia 94. Kwa upande wa ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba, kazi za awali zimekamilika. Ujazaji wa kifusi umekamilika katika eneo la Terminal Building na eneo la ndani ya Uwanja (Airside) ,ujenzi wa njia ya kurukia ndege (Runway) unaendelea na kuchimbwa kwa ajili ya kujazwa kifusi ambapo utekelezaji umefikia asilimia 6.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuwa na miundombinu bora na ya kisasa kwa shughuli za usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga na kuwa katika viwango vya Kimataifa vitakavyoweza kupokea ndege aina ya “Code 4C” ambazo zitaweza kuleta wageni wengi ambao watakaotembelea visiwa vyetu na kukuza utalii wa Zanzibar. Pia programu hii itaongeza pato la taifa kutokana na kuongezeka kwa wageni watakaoingia nchini.

**e) Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar**

Programu hii ina lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi na salama katika maeneo ya mjini na vijijini kwa Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 154.56 bilioni (TZS 25.03 bilioni kutoka Serikalini na TZS 129.52 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 92.73 bilioni (TZS 15.02 bilioni kutoka Serikalini na TZS 77.71 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 38.72 bilioni sawa na asilimia 42 ya lengo la TZS 92.73 bilioni zimepatikana (TZS 24.45 bilioni kutoka Serikalini na TZS 14.27 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na kutekeleza miradi ifuatayo:-

### i) Mradi wa Uhuishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar

Mradi wa Uhuishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar (Miji 25 - INDIA) ni sehemu ya juhudi upatikanaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira Zanzibar. Kazi kuu za mradi ni uimarishaji wa huduma za Maji Endelevu Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 16.17 bilioni (TZS 2.52 bilioni kutoka Serikalini na TZS 13.65 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 9.70 bilioni (TZS 1.51 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo),

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 14.27 bilioni sawa na asilimia 147 ya lengo la TZS 9.70 bilioni zimepatikana kutoka kwa Washirika wa maendeleo kwa kufanya kazi ya Tathmini ya maeneo yatakayoathirika na mradi na ulipaji wa fidia na tathmini hiyo inaendelea na utekelezaji umefika asilimia 20.

Kukamilika kwa mradi huu kutahakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi na salama katika maeneo ya mjini kwa Unguja na Pemba pamoja na kuimarisha huduma ya maji safi na usafi wa mazingira Zanzibar.

### ii) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji Maji Mkoa wa Mjini Magharibi

Mradi huu una lengo la kuongeza uzalishaji na usambazaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya zake ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma hiyo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 41.49 bilioni (TZS 1.54 bilioni kutoka Serikalini na TZS 39.95 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 24.89 bilioni (TZS 924.60 milioni kutoka Serikalini na TZS 23.97 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 59.69 milioni sawa na asilimia 0.2 ya lengo la TZS 24.89 bilioni zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza kazi ya kuandaa taarifa ya kina ya kitaalamu (details design) ya mradi na Tathmini ya Kimazingira ambazo zimeshakamilika kwa asilimia 100. Vile vile, mpango wa manunuzi kwa ajili ya kumpata mkandarasi umefikia asilimia 70 na upo kwa washirika wa maendeleo JICA kwa ajili ya kuweka mapendekezo.

Kukamilika kwa mradi huu kutapelekea kuongeza uzalishaji na usambazaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya zake ili kupunguza changamoto za upatikanaji wa huduma hiyo.

**iii) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar**

Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu ya maji kwa kufanya usambazaji na uzalishaji wa maji safi na salama katika maeneo ya visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 15.78 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 9.47 bilioni.

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 16.95 bilioni sawa na asilimia 179 zimepatikana na kutekeleza kazi za uhakiki wa maeneo yatakayoathirika kwa ajili ya ujenzi wa Miundombinu ya Maji inaendelea, ununuzi wa pampu 40 maalumu, vifaa na bomba za kusafirishia maji utekelezaji wake umefikia asilimia 80, Ujenzi wa hifadhi za "hydrant" pamoja na ununuzi wa vifaa vya maji na bomba za kusafirishia maji utekelezaji wake umefikia asilimia 50. Aidha Matangi 12 ya kuhifadhia maji na ukarabati wa tangi la lita 250,000 la Kengeja umekamilika.

Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha miundombinu ya maji kwa kufanya usambazaji na uzalishaji wa maji safi na salama katika maeneo ya visiwa vya Zanzibar.

**iv) Mradi wa Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar**

Mradi huu una lengo la kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya kisiwa cha Pemba. Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW). Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 71.43 bilioni (TZS 2.60 bilioni kutoka Serikalini na TZS 68.83 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 42.86 bilioni (TZS 1.56 bilioni kutoka Serikalini na TZS 41.29 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 119.39 milioni sawa na asilimia 0.28 ya lengo la TZS 42.86 bilioni zimepatikana kutoka Serikalini na kutumika katika uendeshaji na usimamizi wa

mradi pamoja na utekelezaji wa hatua za awali za mradi ambazo ni kutafuta mkandarasi, kuandaa michoro na ununuzi wa vifaa.

Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya kisiwa cha Pemba.

**v) Mradi wa Uboreshaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Kaskazini Unguja**

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kufanya ukarabati wa visima na kuweka miundombinu ya umeme na pampu zinazotumia umeme wa jua kwa ajili ya kuendeshea visima hivyo. Mradi huu ni wa mwaka mmoja kwa hatua ya ujenzi pamoja na usimamiaji kwa kipindi cha miaka mitano. Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya National Energy Centre (NEC) ya Oman. Mradi huu utagharimu jumla ya USD 26.31 Milioni hadi kukamilika kwake. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.60 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.56 bilioni kutoka Serikalini.

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 7.32 bilioni sawa na asilimia 469 zimepatikana kutoka Serikalini.Kazi zilizo fanyika ni ujenzi wa matangi mawili ya kilindi, uchimbaji wa visima 3 mahonda visima viwili na kiashange- Matemwe 1, ujenzi na matengenezo ya vibanda 30 vya kuhifadhia mashine kati ya vibanda 51, ununuzi wa pampu 20 za nishati ya jua, ulazaji wa mabomba kwa urefu wa kilomita 7.798 Machui umekamilika, na ununuzi wa mita 10,000 za maji umeshafanyika.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarika kwa miundombinu ya usambazaji maji katika mkoa wa Kaskazini Unguja, kuongeza kiwango cha uzalishaji na upatikanaji wa huduma za maji safi, kuvutia shughuli za uwekezaji pamoja na kuimarisha usawa wa kijinsia.

### vi) Mradi wa Kuimarisha Usalama wa Maji na Uhimili wa Tabianchi katika Maeneo ya Mijini

Mradi huu una lengo la kuijengea uwezo sekta ya maji juu ya usimamizi wa usalama na upatikanaji wa maji nchini. Mradi umelenga kutekeleza maeneo makuu matatu (3) ambayo ni: Kusaidia Wizara katika usimamizi wa mikakati na miongozo ya mageuzi; Kuanzisha mfumo jumuishi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi na uchafuzi wa kimazingira na Kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji Zanzibar ili iweze kujiendesha kibiashara. Mradi huu unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) kupitia Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ). Mradi umeanza mwaka 2024/25. Kwa mwaka 2025/26, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.01 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.21 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Hadi kufikia Machi 2026, uandaaji wa miongozo ya sekta ya maji na usafi wa mazingira imekamilika kwa asilimia 100, watendaji 79 wamejengewa uwezo kutoka Wizara ya Maji na Nishati, ZURA, ZAWA na Serikali za Mitaa kwa fedha za bajeti ya mwaka 2024/25. Vile vile, kazi ya uandishi wa miongozo na vibali vya utiririshaji wa majitaka imefikia asilimia 90. Aidha Utafiti wa mbinu za ukusanyaji wa maji ya mvua umekamilika kwa asilimia 100, Vikundi 14 vya Wanawake wa Chama cha Watumiaji wa Maji (Women Water User Association) Unguja kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo vimepatiwa mafunzo kuhusu ufanisi wa maji na hatua za kulinda vyanzo vya maji katika mipango ya umwagiliaji ili kulinda vyanzo vya maji na kuweza kupanda miti 10,000.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarika upatikanaji wa maji salama kwa matumizi ya binaadamu mjini, uwezo wa kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi, uwezo wa kuvilinda vyanzo vya maji pamoja na kupunguza masafa ya upatikanaji wa huduma za maji.

### f) Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar

Programu hii imeanza mwaka 2023/24 ina lengo la kuwa na umeme wa kujitosheleza ikiwa ni nyenzo muhimu ya kuimarisha shughuli za kiuchumi, usafiri na huduma za jamii. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa

jumla ya TZS 50.79 bilioni ( TZS 40.35 bilioni kutoka Serikalini na TZS 10.44 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 30.48 bilioni (TZS 24.21 bilioni kutoka Serikalini na TZS 6.27 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 54.23 bilioni sawa na asilimia 178 ya lengo la TZS 30.48 bilioni zimepatikana kutoka Serikalini. Kwa mwaka 2025/26, programu imepanga kutekeleza miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

**i) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme**

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za umeme pamoja na miundombinu ya umeme katika vijiji 305 (180 Unguja na 125 Pemba) ili kupata huduma ya umeme yenye uhakika. Mradi huu ni wa miaka minne (4) na umeanza mwaka 2021/22. Kwa mwaka 2025/26, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 7.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.20 bilioni kutoka Serikalini.

Hadi kufikia Machi 2026, mradi huu umetumia fedha za bajeti ya 2024/2025. Kazi zilizofanyika ni pamoja usambazaji wa umeme katika vijiji 63 kati ya vijiji 65 (35 Unguja na 28 Pemba) sawa na asilimia 97 imefanyika, Nguzo 1,776 kati ya 2,500 sawa na asilimia 71 zimenunuliwa na nguzo 1,676 zimebadilishwa (1,155 Unguja na 521 Pemba), wateja wapya 38,800 (23,200 Unguja na 15,200 Pemba) kati ya wateja 43,000 wameunganishwa umeme, uvutaji wa njia mpya za umeme umefanyika na jumla ya wateja wapya 2,650 kati ya 2,500 sawa na asilimia 106 wameunganishwa (Pemba ni 825 na Unguja ni 1,825) na ununuzi wa nguzo na vifaa vya umeme umefanyika kwa kutumia fedha za bajeti ya mwaka 2024/25.

Kukamilika kwa mradi huu kutapunguza changamoto ya upungufu wa umeme katika maeneo tofauti ya Zanzibar na kuongezeka kwa shughuli za biashara zenye mahitaji ya umeme.

**ii) Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar**

Mradi huu una lengo la kuondoa tatizo la umeme mdogo pamoja na voltage ndogo kutoka Tanzania Bara na kusawazisha kuwa katika kiwango kinachohitajika. Mradi huu umeanza mwaka 2025/2026 Mradi umefunga capacitor bank na

voltage regulator katika maeneo mbali mbali ya mjini. Mradi huu umetekelezwa na Serikali kupitia Mkandarasi wa Novavis International kutoka Marekani. Mradi umekamilika kwa awamu ya kwanza na unaendelea kwa awamu ya pili.
Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 33.35 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 20.01 bilioni kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 54.23 bilioni sawa na asilimia 271 ya lengo la TZS 20.01 bilioni zimepatikana kutoka Serikalini kazi zilizofanyika ni Ufungaji wa Voltage regulators Capacitor Bank, katika maeneo 26 na zoezi la usanikishaji wa STATCOM limekamilika kwa asilimia 100. Aidha, malipo ya awali kwa Kampuni ya *ELECMECH SWITCHGEARS AND INSTRUMENTATION FZ-LLC* kwa ajili ya usanifu, ununuzi na ujenzi wa njia mpya ya umeme (33kV line upgrades) na kituo cha kuzalisha umeme wa jua yamefanyika.
Kukamilika kwa mradi huu kutaondoa tatizo la umeme mdogo pamoja na voltage ndogo kutoka Tanzania Bara na kusawazisha kuwa katika kiwango kinachohitajika.

### iii) Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati (ZESTA)

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo Taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati ili ziweze kuimarisha utoaji wa huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 6.47 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo.

Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 3.88 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, kazi zilizofanyika ni ulipaji wa fidia ambapo jumla ya waathirika 1,450 kati ya 1,510 wameshalipwa, shughuli za uhamasishaji wa wananchi katika maeneo ya miradi zinaendelea na ujenzi wa vituo vya kupokelea na kusambazia umeme (Sub-Station) unaendelea kwa maeneo ya Welezo, Makunduchi, Matemwe na Ubago. Njia za kusafirishia umeme pamoja na uwekaji wa nguzo za umeme kwa njia ya Welezo hadi Ubago, Ubago hadi Makunduchi na Ubago hadi Matemwe zinaendelea.

Aidha, ujenzi wa laini kubwa ya umeme yenye uwezo wa kilovoti 132 Mkandarasi anaendelea na uchimbaji wa misingi kwa ajili ya nguzo za umeme,

ujenzi wa kuta na majengo ya uendeshaji, usimikaji wa vyuma na uwekaji wa nyaya za umeme, na kazi ya Uwekaji wa mfumo wa kidigitali wa usimamizi na uendelezaji wa miundombinu ya umeme Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa vituo vya umeme kwa ajili ya ufungaji wa mitambo na kazi hii imefikia asilimia 93 ya utekelezaji wake. Aidha watendaji 28 kati ya 30 sawa na asilimia 93 katika sekta ya nishati wamepatiwa mafunzo juu ya utaalam wa umeme wa jua mafunzo hayo yalifanyika nchini india kwa muda wa wiki mbili.
Kukamilika kwa mradi huu kutaimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo Taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati ili ziweze kuimarisha utoaji wa huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba.

**III) Kuimarisha Mageuzi ya Kiuchumi**

Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa Kutekeleza Programu na Miradi ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 148.9 bilioni (TZS 136.4 bilioni kutoka Serikalini na TZS 12.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar; kufanya Mageuzi ya Kidigitali; Kuanzisha na Kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Industrial Parks); kufanya Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula; na Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), jumla ya TZS 89.35 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 81.85 bilioni kutoka Serikalini na TZS 7.5 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).
Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 23.15 bilioni sawa na asilimia 26 ya lengo la TZS 89.35 bilioni (TZS 7.35 bilioni kutoka Serikalini na TZS 15.79 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo: -

**a) Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar**

Programu hii ina lengo la kutoa huduma za kuimarisha sekta ya biashara na viwanda kwa kutoa msaada kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati katika maeneo ya Dimani na Chamanangwe. Programu imeanza 2017/18. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa jumla ya TZS 10.80 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.48 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 2.95 bilioni zimeingizwa sawa na asilimia 45 kwa ajili ya malipo

ya Kampuni ya JKU kwa ujenzi wa kituo cha maonyesho Dimani na matayarisho ikiwemo usimamishaji wa nguzo katika ghala la kuhifadhia vifaa, jengo la kuuzia chakula, eneo la kufurahishia watoto pamoja na ukumbi wa mikutano wa kisasa katika kituo cha Dimani.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuimarisha biashara na kuvutia uwekezaji. Programu hii itatoa fursa kwa wafanyabiashara wa ndani na wa kimataifa kuonesha bidhaa na huduma zao, hivyo kupanua masoko na kuongeza nafasi za ushirikiano wa kibiashara. Kituo hiki kitakuwa kiungo muhimu katika kuhamasisha maendeleo ya sekta ya biashara kwa kuwaweka pamoja wajasiriamali, wawekezaji na wadau wengine. Vile vile, programu hii itasaidia kukuza utalii wa kibiashara na kuinua uchumi wa Zanzibar kwa ujumla kupitia maonesho, mikutano na mawasiliano ya kibiashara kimataifa.

**b) Mradi wa Kuanzisha na Kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks)**

Mradi una lengo la kuimarisha maeneo tengefu ya viwanda ili kurahisisha viwanda vidogo vidogo na vya kati ili viwe katika maeneo maalum yatakayosaidia kukuza uchumi na kutoa ajira kwa wajasiriamali. Mradi huu ulianza mwaka wa fedha 2019/2020.Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 35.56 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 21.34 bilioni.

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.56 bilioni sawa na asilimia 7 zimepatikana kutoka Serikalini kwa ajili ya malipo ya Kampuni ya AE&Q CONSULTING kwa ajili ya kazi ya uandaaji wa Mpango Mkuu wa matumizi ya ardhi, kufanya uchunguzi wa udongo na tathmini ya athari za Mazingira na jamii katika eneo lililotengwa kwa viwanda la Pangatupu. Aidha, kazi zilizofanyika katika eneo la Chamanangwe ni ujenzi wa miundombinu ya maji kwa kuchimba visima 3, ujenzi wa mnara wa tangi la maji unaendelea na upo katika hatua ya kumwaga zege ya kitako cha tangi la maji na kufunga ring bin pamoja na kupiga plasta ukuta unaendelea na ujenzi umefikia asilimia 80 ya utekelezaji wake. Aidha ujenzi wa jengo la ofisi ya utawala na kibanda cha jenereta unaendelea kwa hatua ya kuezeka.

Kukamilika kwa Mradi huu kutasaidia kuimarisha uchumi wa Zanzibar kwa kuchochea uwekezaji wa ndani na nje. Maeneo haya yatatoa fursa ya kuanzisha

viwanda vipya, kutoa ajira kwa wananchi, na kuongeza thamani ya bidhaa zinazozalishwa nchini. Pia, yatasaidia kupunguza utegemezi wa uagizaji wa bidhaa kutoka nje, hivyo kuongeza kukuza biashara za ndani na ushirikiano wa kiuchumi. Aidha, ujenzi wa miundombinu ya kisasa katika maeneo hayo kutafungua milango kwa ukuaji wa sekta mbalimbali, na kuweza kuinua kiwango cha maendeleo hapa Zanzibar.

### c) Programu ya Mageuzi ya Kidigitali

Programu hii ina lengo la kuimarisha mifumo ya mawasiliano ambayo itarahisisha utoaji wa huduma za kimtandao nchini. Programu itahusisha mifumo mbali mbali Serikalini inayotumika katika utoaji wa huduma zenye ufanisi zaidi za mawasiliano na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Programu imeanza mwaka 2025/26. Kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa jumla ya TZS 76.05 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 42.03 bilioni.

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.09 bilioni sawa na asilimia 3 zimeingizwa na kutekeleza kazi za utoaji wa huduma ya mtandao katika maeneo ya umma (Public Wi-Fi ) katika eneo la Uwanja wa Amani Complex, uwanja mpya wa Fumba, masoko, forodhani na vituo vya mabasi na uhamishaji wa Mkonga kutokana na matengenezo ya barabara umefikia kilomita 72 katika maeneo (route) mbalimbali ikiwemo maeneo ya Mkwajuni, Mizingani, Bango la Mkoa, Kwa Mchina, Bumbwini, Bwejuu, K/Majongoo, Jang'ombe, Mbuyu mnene, Kidimni, Kiungoni, Mtuhaliwa, Pujini, Konde, Mchanga Mlima, Micheweni, Vikutani, Meli nne na Kiwani. Aidha, ZICTIA imeendelea na kazi ya uimarishaji wa vifaa kwa kuweka Rack pamoja na Rectifier kwa vituo (SITE) vyote Unguja na Pemba.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kuimarisha mifumo ya mawasiliano ambayo itarahisisha utoaji wa huduma za kimtandao nchini. Pia itarahisisha uwekaji mifumo Serikalini ambayo itatumika katika utoaji wa huduma zenye ufanisi zaidi za mawasiliano na kuongeza ukusanyaji wa mapato.

### d) Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kusaidia uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo

zinazohimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kujenga uwezo wa uhimilivu katika mifumo ya chakula. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 12.50 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 7.5 bilioni.

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 15.79 bilioni sawa na asilimia 211 ya lengo la TZS 7.5 bilioni zimepatikana na kutekeleza shughuli za mafunzo kwa maafisa ugani juu ya namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari, mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji na teknolojia ya kilimo shadidi na mafunzo kwa vijana juu ya kutoa huduma mashambani kwa kutumia trekta ndogo ndogo za kilimo yametolewa; jumla ya maofisa ugani 400 wamepatiwa mafunzo juu ya mbinu bora za uzalishaji na teknolojia ya kilimo shadidi na jumla ya vifaa 24 vimenunuliwa (mashine) nne (4) za kupandia mbegu, nne (4) za miche, nne (4) za kupalilia, na nane (8) za kuvunia na trekta nne (4) za kufungia mashine za kupandia).

Aidha, matayarisho ya ukarabati wa miundombinu ya maabara ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo na Mifugo Zanzibar iliyopo Kizimbani; matayarisho ya ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji maji kwa mabonde (nane) Unguja na Pemba; matayarisho ya ukarabati wa miundombinu ya mashamba ya mbegu; matayarisho ya ukarabati wa miundombinu ya vituo vya huduma za wakulima, matayarisho ya mfumo wa ufuatiliaji na tathmini wa mradi; utoaji wa mafunzo mbalimbali kwa mabwana na mabibi shamba pamoja na wakulima kuhusiana na kilimo himilivu; ufanyaji wa tafiti kwa ajili ya kupata teknolojia zinazohimili mabadiliko ya tabianchi yanaendelea. Mfumo wa ukusanyaji wa taarifa za kilimo na usajili wa wakulima umekamilika.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kujenga uwezo wa uhimilivu katika mifumo ya chakula.

### e) Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuwa na upatikanaji wa chakula katika ngazi ya Kaya na Taifa kwa ukarabati wa maghala ya chakula na ujenzi wa vihenge.

Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 20.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 12.0 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.76 billioni sawa na asilimia 15 zimeingizwa kwa ajili ya kuwalipa wakandarasi kwa kazi ya ukarabati wa maghala 8 ya Unguja na Pemba na kazi hii imefikia asilimia 70 kwa upande wa Pemba na asilimia 5 kwa upande wa Unguja. Vile vile kwa ujenzi wa Kituo cha Uhifadhi wa Chakula – Unguja hatua za manunuzi za kumpata Mshauri Elekezi zimeshaanza na kituo hicho kitakuwa na ukubwa wa G+2 na maabara.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarisha uhifadhi wa chakula na kuhakikisha upatikanaji wa chakula katika ngazi za Kaya na kukabiliana na tatizo la uhaba wa chakula nchini.

### IV) Kukuza Uwezo wa Watu na Maendeleo ya Jamii

Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa kutekeleza Programu na Miradi ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 1,243.64 bilioni (TZS 1,016.52 bilioni kutoka Serikalini na TZS 227.12 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa kuimarisha Miundombinu ya Elimu; Viwanja vya Michezo; Ujenzi wa Nyumba za Makaazi; Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja na Ujenzi wa Hospitali ya Binguni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 746.19 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 609.92 bilioni kutoka Serikalini na TZS 136.27 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 439.07 bilioni sawa na asilimia 59 ya lengo la TZS 746.19 bilioni zimepatikana (TZS 334.13 bilioni kutoka Serikalini na TZS 104.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo:-

#### a) Programu ya kuimarisha Miundombinu ya Elimu.

Programu hii imeanzishwa mwaka 2017/18 kwa lengo la kuimarisha Miundombinu ya Sekta ya Elimu ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu bora yenye viwango na ufanisi. Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 439.32 bilioni (TZS 247.65 bilioni kutoka Serikalini

na TZS 191.67 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa jumla ya TZS 263.59 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 148.59 bilioni kutoka Serikalini na TZS 115.01 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 199.15 bilioni sawa na asilimia 76 ya lengo la TZS 263.59 bilioni (TZS 95.08 bilioni sawa na asilimia 64 kutoka Serikalini ya lengo la TZS 148.59 bilioni na TZS 104.06 bilioni sawa na asilimia 90 ya lengo la TZS 115.01 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepatikana na kutekeleza uandaaji wa michoro ya awali kwa ajili ya kujenga madarasa 21 ya skuli za Msingi na madarasa 16 ya skuli za Sekondari. Tathmini ya awali kwa ajili ya kubaini skuli 108 zenye uhitaji wa haraka zaidi kwa kuzingatia hali ya miundombinu, mazingira ya kujifunzia na usalama wa wanafunzi pamoja na tathmini ya awali ya ukamilishaji madarasa 103 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi zimekamilika . Aidha, utaratibu wa kutafuta maeneo yatakayojengwa skuli tatu za Elimu Mjumuisho unaendelea na kwa sasa eneo moja limeshapatikana katika eneo la Langoni Mkoa wa Mjini Magharibi. Vile vile, uandaaji wa michoro na utafutaji wa maeneo yatakayojengwa karakana za ufundi zimeshakamilika na maeneo yaliyopatikana ni Bububu, Mtoni Kigomeni, Abeid Amani Karume, Kwarara, Mwanakwerekwe A, Chumbuni, Forodhani, Hurumzi, Mikunguni Technical Secondary School, Nyerere, Kwamtipura, Mahonda, Machui, Bambi, Hassan Khamis Hafidh (Munduli), Langoni na Fuoni kwa Unguja na kwa upande wa Pemba ni Vitongoji, Ole, Gando, Wete Sekondari, Kengeja Technical Secondary School, Uweleni, Micheweni na Konde.

Kwa upande wa ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi 500 ya wanawake na kuanza ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi 500 ya wanaume katika chuo cha SUZA, kazi zilizofanyika ni kusafisha eneo, kuchimba kisima na msingi kwa dakhalia ya wanawake na kuweka umeme eneo la ujenzi wa dakhalia. Aidha, ujenzi wa jengo la Skuli ya Kilimo, Maabara ya Sayansi ya Kisasa, na utoaji wa taaluma ya mahitaji maalum katika Kampasi ya Tunguu umefikia hatua ya utiaji wa tarazo, kuweka miundombinu ya umeme na maji, upigaji wa plasta na rangi, ufungaji madirisha ya grill pamoja na kuweka fremu za milango na madirisha ya alluminium.

Katika uendelezaji wa ujenzi wa Chuo cha IIT Madras, ujenzi huo umeshakamilika hatua inayoendelea ni ufungaji wa vifaa vya TEHAMA (simu na kamera za CCTV) sambamba na kuweka ardhi sawa (landscape) katika Dakhalia, pamoja na

ujenzi wa uwanja wa mpira. Aidha, michoro na BoQ ya jengo la Ofisi ya Baraza la Mitihani kwa ajili ya Kuanzisha Kituo cha kuchapisha mitihani imekamilika. Ujenzi wa karakana za Uhandisi Mitambo, Uhandisi ujenzi, Uhandisi magari katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume, hatua iliyofikia ni upakaji wa rangi na ufungaji wa milango na madirisha.

Vile vile, kazi ya kuunganisha Mkonga wa Taifa na skuli, vituo vya ubunifu wa kisayansi (HUBs) na vituo vya ualimu (TCs) imekamilika, vituo vyote 100 vilivyokusudiwa kuunganishwa na Mkonga wa Taifa vimefikiwa na vinapata huduma ya mtandao kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia.

Kwa upande wa ujenzi wa jengo la Wizara Chake Chake- Pemba hatua iliyofikia ni kufungwa kwa lift, kuezekwa na kazi ya skimming ya ndani inaendelea na Ujenzi wa jengo la wizara Unguja unaendelea kwa hatua ya uwekaji wa tufali ghorofa ya nne na upigaji wa plasta. Kwa upande wa Ukarabati na utanuzi wa Kituo cha Habari za Elimu Mkoroshoni – Pemba umekamilika na kwa upande wa Unguja, tathmini ya awali ya ukarabati na utanuzi wa Kituo cha Habari za Elimu Kwarara imefanyika na kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi.

Kukamilika kwa programu hii kutasaidia kupunguza idadi ya wanafunzi darasani, kuongezeka kwa kiwango cha ufaulu, kuwa na Mazingira bora ya kusomea na kufundishia pamoja na kuwa na mkondo mmoja tu wa masomo kwa siku.

**b) Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu katika ngazi zote kwa kuwapatia walimu na wanafunzi vifaa vya kujifunzia na kufundishia, mafunzo ya malimu na matumizi ya TEHAMA. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha kutoka Serikalini na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 48.15 bilioni (TZS 39.21 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), jumla ya TZS 28.89 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 23.52 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.37 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 14.37 bilioni sawa na asilimia 50 ya lengo la TZS 28.89 bilioni ( TZS 13.49 bilioni kutoka Serikalini na TZS 881.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepatikana na jumla ya skuli

36 zimepatiwa vifaa, zikiwemo skuli za sekondari 15, skuli za msingi 5 na skuli za maandalizi 16, magodoro 3,224 yamenunuliwa kwa ajili ya wanafunzi wa dakhalia 17 za Unguja na Pemba, Skuli 227 za sekondari zimepatiwa vitabu (1,108,270) vya kidato cha kwanza na cha pili kwa ajili ya mtaala mpya Unguja na Pemba, skuli 16 za maandalizi zimepatiwa samani, 5 za msingi na 15 za sekondari, Skuli 33 zimewekewa vifaa vya Maktaba mtandao, Maafisa 10 na Wakufunzi 50 tayari wamepatiwa mafunzo ya 'Zanzibar Learning Management System' ambayo yatawasaidia walimu kuboresha ufundishaji, uratibu wa masomo na ufuatiliaji wa wanafunzi kwa njia ya kidijitali Unguja na Pemba. Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia utoaji wa elimu katika ngazi zote, kupatikana kwa walimu wenye uwezo na mbinu madhubuti kufunzia na kufundishia.

**c) Programu ya Uimarishaji wa Viwanja vya Michezo**

Programu hii imeanza mwaka 2017/18 ina lengo la kuiwezesha sekta ya michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar itakayokidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kiasi cha TZS 414.08 bilioni (TZS 413.45 bilioni kutoka Serikalini na TZS 633.98 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), jumla ya TZS 248.45 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 248.07 bilioni kutoka Serikalini na TZS 380.39 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 221.68 bilioni sawa na asilimia 89 ya lengo la TZS 248.45 bilioni kutoka Serikalini zimepatikana na kuanza kazi ya ujenzi wa kiwanja kikubwa cha michezo kilichopo Fumba kwa kuweka nguzo na ujenzi wa majukwaa. Aidha, kwa upande wa viwanja viwili vya mazoezi kazi zinazoendelea ni usafishaji wa eneo la stadium, Ferry pier, viwanja vya kufanyia mazoezi, eneo la kuogelea (swimming pool) pamoja na uwekaji ardhi sawa. Vile vile, eneo la ujenzi wa Hoteli ya kisasa (4 star) kazi ya usafishaji imeshakamilika kwa ajili ya kuanza kwa hatua za ujenzi. Kwa upande wa ujenzi wa viwanja 17 vya michezo vya Wilaya na Mikoa viwanja nane vimeshakamilika kwa asilimia 100 navyo ni; (Gombani, Maisara, Prizi, Kitope, Kitogani, Mombasa, Mwehe na Mao ze Dong ) na viwanja tisa ujenzi wake unaendelea na umefikia hatua tofauti kama ifuatavyo; (Micheweni asilimia 98, Kangani asilimia 96, Unguja Ukuu asilimia 85, Pangatupu asilimia 85, Pandani asilimia 83, Ukutini asilimia 90, Kinyikani asilimia 52, Matemwe asilimia 20, na Maruhubi asilimia 5)

Aidha, kwa upande wa ujenzi wa viwanja sita vyenye miundombinu ya michezo

ya aina nne katika kiwanja kimoja (4 in 1) Unguja na Pemba viwanja hivi ujenzi wake umekamilika na maeneo yaliyobahatika kujengwa viwanja hivyo ni; Skuli ya Sekondari Tumbatu, Chuo cha Ufundi wa Amali Mkokotoni na Skuli ya Sekondari Regeza Mwendo kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba ni Skuli ya Sekondari Mchanga Mdongo, Skuli ya Sekondari Kangani na Chake Chake. Viwanja hivyo vitahusisha mchezo wa ‘Basketball, Netball, Tennis na Volleyball kwa kiwanja kimoja na utekelezaji wake umefikia asilimia 55.

Kukamilika kwa programu hii kutapelekea kupatikana kwa fursa za kuwa mwenyeji wa mashindano makubwa ya kikanda na kimataifa, kuimarisha uwezo wa vijana kushiriki katika michezo kwa kupata miundombinu bora pamoja na kuimarisha afya za wananchi kwa ujumla.

**d) Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Makaazi**

Programu hii ina lengo la kujenga nyumba za kisasa na bora ili kukidhi mahitaji ya makaazi, hasa katika maeneo yenye ongezeko la idadi ya watu na mahitaji ya nyumba. Programu pia ina lengo la kujenga nyumba za bei nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini na cha kati, ili kupunguza changamoto ya uhaba wa makazi. Programu imeanza mwaka 2024/25 inatekelezwa kwa fedha za Serikali. Kwa mwaka 2025/2026, Programu hii imepangiwa jumla ya TZS 300.12 bilioni. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026) programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 180.07 bilioni.

Hadi kufikia Machi 2026, kazi zilizofanyika ni ujenzi wa nyumba za makaazi Chumbuni ambapo jumla ya majengo mawili (2) yapo katika hatua za ukamilishaji, majengo mawili (2) yapo katika hatua ya ujenzi wa kuta kwa ghorofa zote nne (4) na majengo mawili (2) yapo katika hatua ya msingi. Kwa upande wa nyumba za Kisakasaka ujenzi upo katika hatua ya msingi. Aidha Ujenzi wa nyumba za makaazi na biashara zinazojengwa Mkungu Malofa - Chake Chake ujenzi unaendelea katika ghorofa ya kwanza na utiaji plasta sehemu ya chini, kwa Wete na Nyamanzi hatua iliyopo ni kuandaa Michoro na BoQ.

Kukamilika kwa Programu hii kutasaidia kupunguza changamoto ya nyumba za makaazi kwa wananchi wa Zanzibar, kupatikana kwa makaazi yaliyobora na salama, kuimarika na kukua kwa miji pamoja na kuongezeka kwa mapato ya Serikali.

#### e) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Hospitali ya Rufaa ya Mnazi Mmoja

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Kupitia mradi huu Serikali imepanga kufanya ukarabati mkubwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma zenye kukidhi mahitaji. Mradi umeanza mwaka 2021/2022, Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 24.40 bilioni (TZS 14.40 bilioni kutoka Serikalini na TZS 10.00 bilioni kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 14.64 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 8.64 bilioni kutoka Serikalini na TZS 6.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 2.31 bilioni sawa na asilimia 16 ya lengo la TZS 14.64 bilioni kutoka Serikalini zimepatikana na kazi ya kumpata Mkandarasi wa mradi ambae ni China Jiaxi International Economic and Technical Co-Operational Engineering Company Limited imefanyika. Kazi zinazoendelea ni ubomoaji wa majengo yaliyopo katika maeneo ya mradi na uhamishaji wa vifaa.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kutoa huduma bora za kimatibabu ya kibingwa kwa wagonjwa wote watakaopata rufaa kutoka hospitali nyengine zilizopo Zanzibar.

#### f) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Binguni.

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya rufaa na kuimarisha miundombinu ya kufundishia taaluma za Afya. Mradi huu umeanza mwaka 2023/2024, Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 17.56 bilioni (TZS 1.70 bilioni kutoka Serikalini na TZS 15.86 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya TZS 10.54 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 1.02 bilioni kutoka Serikalini na TZS 9.52 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo).

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.56 bilioni zimepatikana kutoka Serikalini sawa na asilimia 15 kwa ajili ya kulipa kampuni ya Norplan Tanzania Ltd kwa Usimamzi wa Mradi (PIU). Mchakato wa kumtafuta mshauri elekezi

unaendelea ambapo jumla ya kampuni nne zimefanyiwa tathmini na ripoti ya tathmini imeshatumwa kwa Mfadhili kwa kupata uthibitisho ili kuendelea na hatua zinazofuata.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarisha huduma za kibobezi za afya katika ngazi ya rufaa na kuimarisha miundombinu ya kufundishia taaluma za Afya.

### V) Kuimarisha Utawala Bora na Uhimilivu

Kwa mwaka 2025/2026 eneo hili limepangiwa kutekeleza miradi ya maendeleo ambayo itagharimu jumla ya TZS 43.3 bilioni kutoka Serikalini kwa kuimarisha Ulinzi na Usalama; kujenga Mahakama za Wilaya na Mikoa na kufanya shughuli za Uhifadhi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 152.19 bilioni zilipangwa kutumika kutoka Serikalini.

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 121.25 bilioni sawa na asilimia 80 ya lengo la TZS 152.19 bilioni kutoka Serikalini zimepatikana. Utekelezaji wa eneo hili ni kama ifuatavyo:-

#### a) Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama.

Mradi huu una lengo la kuimarisha usalama wa jamii kwa kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mikakati ya ulinzi na usalama na kuwa na miundombinu ya kisasa ya ulinzi na usalama ikiwemo uwekaji wa mifumo na vifaa vya kisasa vya ulinzi ili kulinda wananchi na mali zao dhidi ya uhalifu na viashiria hatarishi. Kwa mwaka 2025/2026 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 25.75 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 15.45 bilioni zilipangwa kutumika.

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 4.83 bilioni sawa na asilimia 31 zilipatikana kutoka Serikalini na kazi zilizofanyika ni kufanya vipimo vya udongo katika maeneo manne yanayotarajiwa kujengwa vituo vya CCTV Unguja na Pemba na vituo hivyo vimeshakabidhiwa kwa mkandarasi kwaajili ya kuanza ujenzi. Kazi ya matengenezo kwa kufanya urejeshaji wa mfumo wa kamera za CCTV inaendelea katika maeneo ya Mji Mkongwe, Michenzani, Kariakoo Mlandege na Biziredi na tayari kamera zimeanza kufanya kazi. Aidha, Mkataba

wa Ununuzi wa vifaa vya Idara Maalum umeshawasilishwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kupata idhini ya kusainiwa, taratibu za maombi ya Fedha zimeshakamilika kwa ajili ya kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ya ulinzi katika Idara Maalum za SMZ.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuimarisha utawala bora, Ulinzi na Usalama, kuongezeka kwa Amani na Utulivu iliopo nchini, pamoja na kuongezeka mapato ya Serikali,Watalii ,ajira na kipato kwa wananchi.

**b) Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa**

Mradi huu ni wa miaka mitano (5) na umeanza mwaka 2022/23. Lengo ni kuwa na Mahkama za kisasa zenye mazingira mazuri pamoja na kuongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria na kuhakikisha upatikanaji wa haki. Kwa mwaka 2025/26, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 13.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 7.8 bilioni zilipangwa kutumika.

Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 7.66 bilioni sawa na asilimia 98 ya lengo la TZS 7.8 bilioni kutoka Serikalini zimepatikana na kuendeleza ujenzi wa Mahkama za Pemba ambapo Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini, katika eneo la kinyasini kazi za ufungaji wa lift mbili, uwekaji wa suspended celling katika ghorofa ya pili ya jengo, ujenzi wa mitaro ya maji ya mvua kwa upande wa nje na skimming kwa kuta zimekamilika. Kazi zinazoendelea ni uungaji wa huduma (maji, umeme na tehama) na kufanya kazi za nje (land scape) na utiaji wa milango . Ujenzi huu umefikia asilimia 88. Kwa upande wa Mahakama ya Mkoa wa Kusini Pemba katika eneo la Changaweni kazi zinazoendelea ni ufungaji wa vifaa vya kuzuia mawimbi ya sauti (sound proof), ujenzi unaendelea kwa uwekaji wa balcon uwekaji wa vyuma katika ukuta wa fensi na mageti, pamoja na kazi za umeme (fitting). Ujenzi huu umefikia asilimia 88 ya utekelezaji wake. Mahakama ya Wilaya ya Micheweni katika eneo la Konde ujenzi upo katika hatua za uvutaji wa nyaya za umeme, uwekaji wa viyoyozi vya ukutani, uwekaji wa milango, utiaji wa vioo katika sehemu ya mapokezi, ujenzi wa vyumba visivyotoa sauti, na utiaji wa balcon. Kuweka sawa ardhi, ujenzi wa sehemu za bustani, upakaji rangi pamoja na uwekaji wa miundombinu ya maji taka katika eneo la jengo na miundombinu ya TEHAMA na maji umekamilika. Ujenzi umefikia asilimia 88 ya utekelezaji wake. Aidha, samani kwa majengo yote ya Mahakama Unguja na Pemba zimeshanunuliwa na zimeshaanza kutumika.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kuwepo kwa ufanisi zaidi katika utoaji wa huduma za kisheria pamoja na upatikanaji wa haki kwa wananchi.

### c) Mradi wa Uhifadhi wa Mazingira na Mabadiliko ya Tabianchi.

Mradi una lengo la kutathmini na kusaidia kupunguza athari za maeneo yaliyohatarini kutokana na mabadiliko ya tabianchi na kuchukua hatua mahsusi za kudhibiti na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa pwani. Mradi umeanza mwaka 2022/23, kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026,) jumla ya TZS 2.7 bilioni zilipangwa kutumika.

Hadi kufikia Machi 2026, hakuna fedha zilizopatikana. Tathmini ya hali halisi ya maeneo yaliyoathirika na mabadiliko ya tabianchi imefanyika katika maeneo 35 kwa kutumia pesa za matumizi ya kawaida (recurrent). Tathmini hiyo ilifanyika katika maeneo tofauti kwa shehia nne (4) za Pemba ( Kangani, Kukuu, Mjimbini, Kengeja na Kendwa) . Maeneo hayo ni kama, Fufuni, Maweni, Ngezi, Kukuu bandarini, Makunge, Kokoni kubwa na ndogo, Mkunguni,Takawani, Pangani na Chafyani.

Kukamilika kwa mradi huu kutasaidia kupunguza athari za maeneo yaliyo hatarini kutokana na mabadiliko ya tabianchi, kudhibiti na kuhimili mabadiliko ya tabianchi katika ukanda wa pwani.

## SURA YA KUMI NA MOJA

## UTEKELEZAJI WA MPANGO WA MAENDELEO KWA WIZARA KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026

### 11.1 Utangulizi

Mpango wa Maendeleo kwa mwaka 2025/26 ni mpango wa tano wa utekelezaji wa Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP 2021-2026) pamoja na Dira ya Maendeleo ya Zanzibar ya 2050. Mpango huo ulipanga kutekeleza programu na miradi ya maendeleo 97. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 4,539.64 bilioni kwa kutekeleza shughuli za maendeleo ambapo ni ongezeko la TZS 1,276.57 bilioni sawa na asilimia 39 ikilinganishwa na Bajeti yote ya Maendeleo ya mwaka 2024/25 ya TZS 3,263.07 bilioni. Kati ya fedha hizi (TZS 4,539.64 bilioni), TZS 3,231.40 bilioni kwa ajili ya Serikali Kuu ambapo Serikali ilielekeza kutumia TZS 2,411.00 bilioni kugharamia programu na miradi ya kimkakati na TZS 820.40 bilioni kwa miradi mengineyo. Aidha, kiasi cha TZS 1,308.24 bilioni zilipangwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (TZS 864.72 bilioni kwa kugharamia miradi ya kimkakati na TZS 443.52 bilioni kwa miradi mengineyo ) ikiwa TZS 962.74 bilioni ni mikopo na TZS 345.50 bilioni ni ruzuku sawa na asilimia 28.82 ya bajeti ya maendeleo.

Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025– Machi 2026), Serikali imepanga kutumia jumla ya TZS 2,723.78 bilioni ya fedha iliyopangwa kutumika kwa ajili ya Serikali kuu kwa kutekelezwa Programu na Miradi ya Maendeleo ambayo ni ongezeko la asilimia 52 ukilinganisha na mpango wa mwaka 2024/2025. Kati ya fedha hizo, Serikali ilipanga kutumia TZS 1,938.84 bilioni sawa na asilimia 71 ya bajeti ya Maendeleo kutoka fedha za ndani na TZS 784.94 bilioni sawa na asilimia 29 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kati ya fedha hizo (TZS 2,723.78 bilioni), TZS 1,965.43 bilioni zilipangwa kugharamia Programu na Miradi ya Kimkakati na yenye dhima na TZS 758.4 bilioni zilipangwa kutumika kwa Programu na Miradi mengineyo. Sura hii inaeleza Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kwa kila Wizara.

## 11.2 UTEKELEZAJI WA PROGRAMU NA MIRADI YA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2025 HADI MACHI 2026 KWA KILA WIZARA

Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, matumizi ya utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo yamefikia jumla ya TZS 1,943.31 bilioni sawa na asilimia 71 ya lengo la TZS 2,723.78 bilioni. Kati ya Fedha hizo TZS 1,451.56 bilioni sawa na asilimia 75 ya lengo la TZS 1,938.84 bilioni ni kutoka Serikalini na TZS 491.75 bilioni sawa na asilimia 63 ya lengo la TZS 784.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Sehemu hii inaeleza Utekelezaji wa Programu na Miradi ya Maendeleo kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kwa kila Wizara kama ifuatavyo;

### 11.2.1 Ofisi ya Rais Ikulu

Ofisi ya Rais Ikulu ina jukumu la kusimamia majukumu ya kikatiba na kisheria ya Baraza la Mapinduzi ili kuhakikisha jamii inapata uelewa juu ya utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo na sera zinazotekelezwa na Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi ya Rais Ikulu imepanga kutekeleza Miradi mitatu ya Maendeleo kwa gharama ya TZS 8.70 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Ofisi ya Rais Ikulu imepanga kutumia jumla ya TZS 5.22 bilioni kutoka Serikalini na imetekeleza Miradi kama ifuatavyo: -

**a. Mradi wa Kuimarisha Majengo ya Ikulu**

Mradi una lengo la kuimarisha majengo ya Ikulu ili kuwa na mazingira mazuri ya makaazi na mandhari za kupendeza kwa viongozi wa Serikali. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 3.6 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 500 milioni zimepatikana kutoka Serikalini sawa na asilimia 14 na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Ikulu ndogo liaborn Dar es salam | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Shughuli zilizotekelezwa ni Upakaji wa rangi majengo ya Ikulu, uwekaji wa Paving Stone, Curb Stone kwenye eneo lote lilopangwa na kutengeneza eneo la slabu |
| Ujenzi wa Ikulu Dodoma | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Shughuli zilizotekelezwa ni Upakaji wa rangi majengo ya Ikulu, ukarabati wa vyoo vya wafanya kazi na ujenzi wa choo kipya cha walinzi wanawake, kuongeza urefu wa ukuta wa fensi, |

**b. Mradi wa Uimarishaji wa Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais wa Zanzibar na Mwenyekiti wa Baraza la Mapinduzi**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mifumo ya ulinzi na usalama katika majengo ya Ikulu na makaazi ya Mheshimiwa Raisi wa Zanzibar kwa kuweka miundombinu ya mifumo iliyo imara katika makaazi hayo. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.2 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 727.33 milioni zimepatikana kutoka Serikalini sawa na asilimia 61 na kutekeleza shughuli ifuatayo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Uwekaji wa mfumo mpya wa kamera katika ikulu ndogo ya Dodoma | Asilimia ya uwekaji wa kamera iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi wa ukuta wa nyuma wa Ikulu umeongezwa, ufungaji wa kamera pamoja na utoaji wa mafunzo ya utumiaji wa kamera kwa watumiaji umefanyika. |

**11.2.1.1 Taasisi ya Rais ya Ufuatiliaji na Usimamizi wa Utekelezaji wa Majukumu ya Serikali.**

Taasisi hii imeanzishwa na Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar kwa lengo la kusaidia na kusimamia utekelezaji wa vipaumbele vya Rais ili kuhakikisha vinatekelezwa kwa viwango vilivyokusudiwa. Taasisi hii inafuatilia utendaji na

uwajibikaji, na inarahisisha mawasiliano kati ya viongozi wa Serikali pamoja na kuripoti kwa Mheshimiwa Rais. Kwa mwaka 2025/2026, Taasisi hii imepanga kutekeleza programu moja ya maendeleo iiliyopangiwa kugharimu jumla ya TZS 1.32 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), tasisi hii imepanga kutumia jumla ya TZS 793.80 milioni na imetekeleza Miradi kama ifuatavyo: -

**a. Programu shirikishi ya Maendeleo kwa Makuzi ya Awali ya Mtoto Zanzibar (Early Childhood Development (ECD) Program)**

Programu hii ina lengo la kuhakikisha kuwa watoto wapatao 276,739 wa Zanzibar wanapata huduma za malezi bora kupitia utekelezaji wa Programu Shirikishi ya Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto (ZM-ECDP) kwa kuzingatia afya, lishe, elimu ya awali na ulinzi. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 1.32 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 793.8 milioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 305.13 milioni kutoka washirika wa maendeleo sawa na asilimia 38 na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha Moduli ya "ECD" ambayo inakwenda kujumuishwa katika Mtaala wa wahudumu wa afya ngazi ya jamii (CHW) kwa upande wa malezi na makuzi ya awali ya Mtoto (ECD). | Asilimia ya moduli iliyokamilishwa | 100 | 95 | 95 | Tayari moduli ya ECD ilikamilishwa na imeanza kutumika katika kufundisha wahudumu wa afya ngazi ya jamii. |
| Kutoa mafunzo yanayohusiana na "ECD" kwa watoa huduma za afya 1200 wa ngazi ya jamii Unguja na Pemba; | Idadi ya watoa huduma waliopatiwa mafunzo | 1146 | 1031 | 90 | Jumla ya watoa huduma 1031 walipatiwa mafunzo (wanaume ni 115 na Wanawake ni 916). |
| Kuandaa Programu/Mpango wa Malezi na Makuzi ya Awali ya Mtoto – Zanzibar; | Asilimia ya uandaaji wa programu iliyofikia | 100 | 90 | 90 | Programu/Mpango wa malezi upo katika hatua za mwisho ambao unatarajiwa kuanza rasmi utekelezaji katika mwaka wa fedha 2026/2027 |
| Kutoa mafunzo kwa waandishi wa Habari vinara unguja na Pemba | Idadi ya wanahabari waliopatiwa mafunzo | 30 | 30 | 100 | Waandishi wa habari 30 wamepatiwa mafunzo na wanayatumia mafunzo hayo kueliisha jamii |
| Kuandaa mpango wa utetezi (advocacy plan) kwa upande wa "ECD" na kuifanyia kazi; | Asilimia ya maandalizi iliyofikia | 100 | 100 | 100 | Mpango wa utetezi umekamilika na umezinduliwa na mheshimiwa Mke wa Rais wa zanzibar, msarifu na mwenyekiti wa zanzibar maisha bora foundation |
| Kutoa mafunzo ya kujenga uelewa kuhusu programu jumuishi ya malezi na makuzi ya awali ya mtoto kwa umoja wa wajumbe wa baraza la wawakilishi wanawake Zanzibar (UWAWAZA) na kamati ya ustawi wa jamii | Idadi ya wajumbe waliopatiwa mafunzo | 30 | 30 | 100 | Mafunzo haya yanaweza kusaidia waheshimiwa katika kuitetea na kuipeleka mbele agenda ya ECD nchini. |
| Ujenzi wa kituo cha watoto katika soko la mwanakwerekwe, hospitali na jamii kwa ajili ya huduma rafiki za ECD. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Hatua za awali za ujenzi zinaendelea ambapo tathmini ya awali juu ya huduma rafiki za ACD zimefanyika na kwa mashirikiano na save the children kwa msaada wa stanbic bank. |

### 11.2.2 Ofisi ya Rais- Kazi, Uchumi na Uwekezaji

Ofisi hii ina jukumu la kuimarisha hali ya kijamii na kiuchumi ya wananchi wa Zanzibar kwa kutoa na kutumia fursa za kiuchumi zilizopo na zitakazokuja, kushajihisha utamaduni na uwezo wa ujasiriamali, kukuza uwekezaji wa ndani na nje, upatikanaji wa kazi za staha zenye kuzingatia Sheria na viwango vya kazi. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja ya maendeleo iiliyopangiwa jumla ya TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Ofisi imepanga kutumia jumla ya TZS 9.00 bilioni kutoka Serikalini na imetekeleza Programu kama ifuatavyo: -

#### a. Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji

Programu hii imeanzishwa mwaka 2021/2022 na inatarajiwa kukamilika mwaka 2025/2026. Programu ina lengo la kukuza maeneo huru ya uwekezaji kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, maji, umeme na mawasiliano katika maeneo yote yaliyoainishwa kwa uwekezaji ili kuwavutia wawekezaji wa ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 15.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 9 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 3.29 bilioni sawa na asilimia 37 zimeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa barabara za Zone B Micheweni | Asilimia ya ujenzi iliyofikia. | 100 | 18 | 18 | Tathmini ya gharama za ujenzi wa miundombinu ya maji na umeme pamoja na michoro na BoQ kwa ajili ya ujenzi wa maghala zimefanyika na hatua inayofuata ni kutafuta Mbia atakaeshrikiana na ZIPA katika kujenga maghala hayo. |
| Upelekaji wa miundombinu ya barabara, maji na umeme katika eneo la uwekezaji la Fumba | Asilimia ya ujenzi wa miundombinu iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Tathmini ya fidia katika maeneo ya ujenzi imefanyika ambapo wananchi 700 watakaoathirika na ujenzi wametambuliwa na taratibu za malipo zinaendelea katika maeneo ya (Sport City, IT Madrasa, Dimani Ndambani na eneo la ujenzi wa ukumbi wa Mikutano). Aidha, Ujenzi wa barabara kilomita 8 unaendelea katika eneo la fumba |

#### 11.2.2.1. Wakala wa Uwezeshaji Wananchi Kiuchumi Zanzibar

Taasisi hii imeanzishwa kwa lengo la kuweka mazingira wezeshi ya kuwawezesha wananchi kiuchumi ili kuongeza ajira kwa vijana na wajasiriamali, pamoja na kuongeza uzalishaji na upatikanaji wa masoko ya bidhaa kwa wafanyabiashara nchini. Kwa mwaka 2025/2026, Taasisi imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 10.60 bilioni (TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 6.10 billioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Wakala wa Uwezeshaji wananchi kiuchumi imepanga kutumia jumla ya TZS 6.36 bilioni kutoka Serikalini na imetekeleza Miradi kama ifuatavyo: -

**a) Mradi wa kuwasaidia Wajasiriamali Wadogowadogo, Wakati na Wakubwa.**

Mradi huu una lengo la kuwawezesha wajasiriamali Wadogo, Wakati na Wakubwa kwa kuwapatia mikopo itakayowasaidia kuongeza mitaji yao ili waweze kujitegemea. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Abudhabi kupitia Mfuko wa Khalifa (Khalifa Fund). Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 9.60 bilioni (TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.10 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 5.76 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 5.23 bilioni zimepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa mikopo kwa wajasiriamali, wazalishaji wadogo, wakati na wakubwa. | Idadi ya wajasiriamali waliopatiwa mikopo | 250 | 63 | 25 | Jumla ya wajasiriamali 63 (wanaume 38 na wanawake 25) wamepatiwa mikopo kutoka Mfuko wa Khalifa fund na jumla ya mikopo 12 imetolewa kwa wajasiriamali |
| | Idadi ya mikopo iliyotolewa | 25 | 12 | 48 | |

### 11.2.3 Ofisi ya Rais- Fedha na Mipango

Ofisi ya Rais - Fedha na Mipango ina jukumu la kutafuta, kudhibiti na kusimamia rasilimali fedha ili kuwezesha maendeleo ya kiuchumi na ustawi wa jamii. Ofisi pia ina jukumu la kusimamia ukusanyaji wa mapato kutokana na kodi, ushuru na vyanzo vingine pamoja na kudhibiti Taasisi za kifedha zikiwemo benki kuweka utulivu wa kifedha na usalama wa amana za wananchi. Ofisi hii inawajibu wa kuandaa na kutekeleza sera za kifedha zinazochochea ukuaji wa Uchumi, kuimarisha mzunguko wa fedha na kudhibiti kasi ya mfumko wa bei kwa kushirikiana na Benki Kuu ya Tanzania. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepangiwa kiasi cha TZS 686.27 bilioni (TZS 649.10 bilioni kutoka Serikalini na TZS 37.17 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa ajili ya kutekeleza programu tatu na mradi mmoja wa maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Wizara imepanga kutumia jumla ya TZS 411.76 bilioni na imetekeleza Programu na Miradi kama ifuatavyo: -

**i. Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar**

Programu hii ina lengo la kujenga na kukarabati majengo ya Ofisi za Serikali ili kuhakikisha kuwa utendaji kazi wa Taasisi na Idara za Serikali unakuwa bora, na pia kuweka mazingira mazuri ya kazi kwa wafanyakazi Serikalini yanayokwenda sambamba na utoaji huduma nzuri kwa wananchi. Programu inajumuisha ujenzi wa Ofisi mpya za Serikali katika maeneo yaliyotengwa ili kuhakikisha huduma za Serikali zinapatikana karibu na wananchi pamoja na kuimarisha majengo ya zamani ili yawe na usalama na kuendelea kutoa huduma. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 126.30 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 - Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 75.78 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 72.94 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 96.3 na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha ujenzi wa Taasisi za Serikali ikiwemo Mamlaka ya Kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi, Shirika la Magazeti, Ofisi ya Nyaraka, Mkurugenzi wa Mashtaka na Chuo cha Utawala wa Umma (IPA); | Asilimia ya ujenzi wa Taasisi ya Mamlaka ya kuzuia Rushwa na Uhujumu wa Uchumi iliyofikia | 100 | 40 | 40 | i)Jengo la Ofisi: Umwagaji wa jamvi la ghorofa ya kwanza umeshakamilika matayarisho ya kuendelea na ujenzi wa ghorofa ya pili yanaendelea<br>ii)Jengo la Mikutano:<br>Msingi wa jengo hili umeshakamilika matayarisho ya kusimamisha nguzo yanaendelea<br>iii) Mkahawa:<br>Ujenzi upo katika hatua ya kuezeka<br>Jengo la mahojiano: Ujenzi upo katika hatua ya kumalizia |
| | Asilimia ya ujenzi wa Ofisi ya Shirika la Magazeti iliyofikia | 100 | 86 | 86 | Utekelezaji wa Mradi huu umefikia 80% kwa jengo la Ofisi, Nyumba za wafanyakazi 95%, Jengo la Kiwanda 75 %, Jengo la Msikiti 95%, Kazi zilizobakia 14%. |
| | Asilimia ya ujenzi wa Ofisi ya Nyaraka iliyofikia. | 100 | 73 | 73 | Kazi za Kuweka milango, kuweka ngazi na kupiga plasta zinaendelea. |
| | Asilimia ya ujenzi wa Ofisi ya Mkurugenzi wa Mashtaka iliyofikia | 100 | 100 | 100 | |
| Kuanza ujenzi wa Taasisi za Serikali ikiwemo Baraza la Wawakilishi, Mamlaka ya Serikali Mtandao, Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya, Ofisi ya Usalama wa Serikali na Ofisi ya Kamisheni ya Utumishi Serikalini; | Asilimia ya ujenzi wa Ofisi ya Baraza la Wawakilishi iliyofikia | 100 | 10 | 10 | Michoro imeshaandaliwa na Mkandarasi ameshapatikana ambae ni CRJE kwa sasa taratibu za kuwalipa fidia waathirika zinaendelea |
| | Asilimia ya ujenzi wa Ofisi za Wakuu wa Mikoa na Wilaya iliyofikia | 100 | 5 | 5 | Michoro tayari imeshaandaliwa na kwa sasa hatua ya kumtafuta Mkandarasi inaendelea |
| | Asilimia ya Ujenzi wa Ofisi ya Usalama wa Serikali iliyofikia | 100 | 27 | 27 | Mkandarasi ameshapatikana ambae ni ***HITAJI COMPANY LIMITED*** na kwa sasa wanaendelea na utafutaji wa vibali, ukamilishaji wa michoro ya usanifu, na uthibitisho wa Nyaraka za mikataba. |
| | Asilimia ya Ujenzi wa Ofisi ya Tume ya Utumishi Serikalini iliyofikia | 100 | 27 | 27 | Hati ya Umiliki wa Ardhi imeshapatikana michoro ya ujenzi imeshaandaliwa na mkandarasi alieshinda mradi huo ni SCENIC CONSTRUCTION AND CONSULTANCY LTD. Hatua zinazo endelea ni kukamilika kwa taratibu za kiutendaji na kuanza kwa ujenzi. |
| | Asilimia ya Ujenzi wa Ofisi ya Chuo cha Utawala wa Umma iliyofikia | 100 | 25 | 25 | Ujenzi unaendelea ambapo hatua iliopo ni ya kurejesha kifusi (backfilling) ili kuimarisha msingi wa jengo na kuzuia mmong'onyoko na mipasuko kutokana na asili ya ardhi ya eneo la ujenzi. |
| Kuanza ujenzi wa Mji wa Serikali katika eneo la Kisakasaka | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 11 | 11 | Mshauri elekezi wa mradi ni Mhandisi Consultancy limited na Mkandarasi CRJE GROUP LTD . ameshakabidhiwa eneo la ujenzi Michoro ya ujenzi imesha andaliwa na waathirika wa mradi huo tayari wameshapatiwa stahiki zao na taratibu za kuanza ujenzi zinaendelea |

### ii. Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)

Programu hii inalenga kuimarisha miundombinu, huduma za msingi pamoja na kuimarisha haiba ya Miji ya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa jumla ya TZS 32.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 19.5 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 53.99 bilioni zimepatikana sawa na asilimia 277 kutoka kwa washirika wa maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga vituo viwili vya kusafirishia taka na vizimba 125 vya kukusanyia taka kwa Unguja na Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Jumla ya wazabuni 6 waliwasilisha maombi, tathmini ya kumpata Mkandarasi imekamilika. |
| | Idadi ya vizimba vya kukusanyia taka | 125 | 2 | 2 | Mradi umeshapata wakandarasi wawili ambao ni, OKRA (Z) Construction Company Limited kutoka Zanzibar, ambaye atajenga jumla ya vizimba 38 kwa upande wa Pemba na kampuni ya Faster (FST) Company Limited ya Zanzibar ambaye atajenga jumla ya vizimba 73 kwa upande wa Unguja. Kwa sasa wakandarasi hao tayari wameshakabidhiwa maeneo ya mradi (site possesions), aidha wakandarasi wamepatiwa maeneo ya kuweka kambi zao (site camps). Kwa upande wa Unguja kambi ya mkandarasi ipo eneo la Pwani Mchangani Kaskazini Unguja na Eneo la Kilimani Campsite(Botanic Garden), na upande wa Pemba eneo la kambi ya wakandarasi ipo katika kijiji cha Vitongoji eneo la Chuo Kikuu Huria Tanzania. |
| Kuendeleza maeneo ya utalii katika vijiji vya Nungwi, Chwaka na Makunduchi – Unguja | Asilimia ya kazi iliyofikiwa Nungwi | 100 | 5 | 5 | Mradi umetangaza zabuni mnamo tarehe 26 Febuari 2026 kwa ujenzi wa maeneo mawili(Chwaka na Makunduchi) Tatmini ya wakandarasi imekamilika kwa ujenzi wa maeneo mawili(Chwaka na Makunduchi) |
| | Asilimia ya kazi iliofikiwa Chwaka | 100 | 5 | 5 | |
| | Asilimia ya kazi iliyokiwa Makunduchi | 100 | 5 | 5 | |
| Kuzijengea uwezo Taasisi za Serikali zinazosimamia maendeleo ya Miji kwa kuwapatia watendaji mafunzo ya muda mfupi pamoja na ununuzi wa vitendea kazi; | Idadi ya maafisa waliojengewa uwezo. | 97 | 116 | 113 | Jumla ya Watumishi 116 wamepatiwa mafunzo katika fani mbali mbali zikiwemo: uchambuzi wa kodi na usimamizi wa fedha za miradi. |
| Kuandaa Mpango Mkuu wa Maendeleo ya Kijiografia kwa kisiwa cha Pemba | Asilimia ya uandaaji wa mpango iliyofikia | 100 | 65 | 65 | Ripoti ya hali halisi ya kisiwa cha pemba (Situational Analysis and Diagnostic report) na Dhana ya Mpango Mkuu wa Matumizi ya Ardhi ( Master Plan Concept) zimeshakamilika . Mshauri elekezi anaendelea uandaaji wa Mipango ya kimaeneo(special area and land use plan) katika maeneo mbali mbali ya kisiwa cha Pemba. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa Mfumo wa Utambuzi wa Taarifa za Kijiografia | Asilimia ya uandaaji wa mfumo uliyofikiwa | 100 | 80 | 80 | Ripoti ya usanifu wa mfumo (System design and deployment report) imeshaandaliwa<br>Mshauri elekezi amekamilisha kutoa mafunzo kwa watendaji wa serikali (MDAs na LGAs) kwa upande wa Unguja na Pemba. Mafunzo haya yanalenga kuwapa uelewa wa masuala ya ukusanyaji na uchakataji wa taarifa zinazohitajika katika kusimamia na kuendeleza matumizi endelevu ya Mfumo huo. Shughuli inayoendelea sasa ni kuunganisha mfumo wa SDI na mifumo mengine ya Serikali ikiwemo ZANMALIPO. |
| Kuandaa Kanuni za ujenzi Zanzibar | Asilimia ya uwandaaji wa kanuni iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Mshauri Elekezi tayari ameshawasilisha ripoti ya awali(inception report) na tayari imeshapitiwa na wadau na kupata maoni (comments). Kazi inayoendelea ni kufanya tathmini ya kina ya mradi (Situation Analysis) ambapo amepitia wadau kwa Unguja na anaendelea na zoezi hili kwa kisiwa cha Pemba. |
| Kununua gari za taka 26 (11 ya kushindilia taka na 15 ya kuchukulia taka) kwa ajili ya usafi wa mji; | Asilimia ya ununuzi wa gari za taka uliofikiwa | 100 | 30 | 30 | Utengezaji wa gari za taka unaendelea chini ya kampuni ya Gansu Construction Investment Heavy Industry Technology Co Ltd kutoka China na mwishoni mwa mwezi wa Aprili timu ya wataalamu wa mradi itakagua maendeleo ya utengenezaji wa gari hizo |
| Ujenzi wa mradi salama wa watembea kwa miguu katika eneo la Mji Mkongwe. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua za kumpata Mkandarasi zimeshakamilika. |

### iii. Programu ya Mageuzi katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP – VI)

Programu hii ina lengo la kuimarisha usimamizi wa fedha za umma katika utoaji wa huduma kwa wananchi. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 4.75 bilioni (TZS 350 milioni kutoka Serikalini na TZS 4.40 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 2.85 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 350 milioni sawa na asilimia 12 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya mapitio ya Sheria, Sera na Kanuni zinazohusiana na mapato, matumizi, udhibiti na ukaguzi | Idadi ya Sera zitlizofanyiwa mapitio | 1 | 1 | 100 | Sera ya Manunuzi ipo katika hatua za mwisho, ikisubiri kuwasilishwa katika Kamati ya Makatibu Wakuu kwa ajili ya kujadiliwa na kuidhinishwa |
| | Idadi ya kanuni zilizofanyiwa mapitio | 2 | 1 | 50 | Kanuni ya ZIAAT tayari imefanyiwa mapitio, na kwa sasa ipo katika hatua ya kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili kama sehemu ya maandalizi ya utekelezaji |
| | Idadi ya Miongozo zilizofanyiwa mapitio | 7 | 5 | 71 | Miongogozo mikano kati ya saba tayari imeandaliwa na baadhi inasubiri kuwasilishwa katika kamati ya uongozi na mengine |
| Kuandaa utafiti wa mtazamo wa utumiaji wa mfumo wa kutolea risiti za kielektroniki; | Asilimia ya kazi iliyofikia | 100 | 95 | 95 | Utafiti kuhusu mtazamo wa matumizi ya mfumo wa utoaji wa risiti za kielektroniki umekamilika, na ripoti yake ipo tayari ikisubiri kuwasilishwa katika Kamati ya Uongozi kwa ajili ya kujadiliwa na kutoa maamuzi |
| Kuwajengea uwezo watumishi kuhusiana na mageuzi ya fedha za umma. | Idadi ya watumishi waliojengewa uwezo | 889 | 674 | 74 | Wafanyakazi 674 wamejengewa uwezo katika masuala ya mageuzi ya fedha za umma kupitia mafunzo maalum katika fani mbalimbali, ikiwemo kodi, manunuzi na usimamizi wa miradi. Hatua hii imechangia kuimarika kwa ufanisi wa utendaji kazi, kuongezeka kwa uwajibikaji, pamoja na kuboreshwa kwa usimamizi wa rasilimali za umma kwa kuzingatia misingi ya nidhamu ya fedha. |

### a. Mradi wa Uimarishaji Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRMNRG)

Mradi una lengo la kuimarisha rasilimali za ndani na usimamizi wa maliasili kupitia Sera na Sheria stahiki. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa kutumia TZS 50.0 milioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 30 milioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 50 milioni kutoka Serikalini zimepatikana sawa na asilimia 167 na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa huduma za uratibu na usimamizi wa shughuli za mradi | Asilimia ya kazi iliyofikia | 100 | 20 | 20 | Kufanya warsha juu ya Rasimu ya Sheria ya kodi ya Faida ya Mafuta na Gesi asilia Unguja na Pemba na Kufanya warsha juu ya Sheria ya usimamizi wa mapato yatokanayo na utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia Unguja na Pemba |

### 1.2.3.1 Tume ya Mipango Zanzibar

Tume ya Mipango ya Zanzibar kwa mujibu wa Katiba ya Zanzibar ya mwaka 1984 ndiyo chombo cha juu chenye uwezo wa kupanga na kusimamia utekelezaji wa maendeleo ya kiuchumi na mipango ya huduma za jamii Zanzibar. Katika kutekeleza majukumu yake, Tume ya Mipango inaandaa Mipango ya maendeleo ya muda mrefu, muda wa kati na muda mfupi. Kwa mujibu wa Sheria Nambari 3 ya mwaka 2012 Tume ya Mipango pia ina jukumu la kuratibu masuala ya tafiti na idadi ya watu. Aidha, Tume ina jukumu la kutathmini hali ya Uchumi na kutoa ushauri kwa Serikali kuhusu mikakati ya kukuza uchumi na kupunguza changamoto za kiuchumi na kijamii ikiwemo ukosefu wa ajira, kuratibu na kupanga vipaumbele vya nchi na kutoa miongozo ya kimaendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, Tume ya Mipango imepangiwa jumla ya TZS 12.80 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza programu moja na miradi mitatu ya maendeleo Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Ofisi imepanga kutumia jumla ya TZS 7.68 bilioni na imetekeleza Programu na miradi kama ifuatavyo: -

### i) Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara

Programu hii inalenga kuinua hali za wananchi kupitia urasimishaji wa Ardhi na Biashara ili ziweze kutumika katika juhudi za kujiletea maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia kiasi cha TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 2.70 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Mach 2026, mradi huu umeingiziwa TZS 1.92 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 71 na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa masjala ya ardhi Chake Chake - Pemba; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 45 | 45 | Ujezi wa Msingi (Foundation) umekamilika na sasa unaendelea katika hatua ya ujenzi wa tabaka la chini (Ground Floor) |
| Ununuzi na uwekaji mfumo wa makabati ya kielektroniki kwa ajili yakuhifadhia kumbukumbu na nyaraka za biashara na ardhi. | Idadi ya Ofisi ziliwewekewa makabati | 2 | 2 | 100 | Makabati katika ofisi mbili moja Masjala ya Ardhi Makunduchi na Masjala ya Biashara katika Ofisi ya BPRA – Mazizi yamekamilika. |
| Upimaji na Usajili wa Ardhi | Idadi ya Maeneoyaliyo pimwa na kusajiliwa | 4000 | 3354 | 83 | Maeneo Mfikiwa 1521 kwa upande wa Pemba na 1833 Nganani makunduchi kwa upande wa Unguja yamepimwa. Aidha, hati 791 zimetolewa kwa wananchi (555 Unguja na 236 Pemba). |
| Kuimarisha mfumo wa usajili wa ardhi; | Asilimia ya utekelezaji iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Hadidu rejea ya kufanya maboresho ya Mfumo imekamilika kwa ajili kuendelea na matengenezo ya mfumo. |
| Kuwatambua na kuwasajili wafanyabiashara wadogo wadogo Unguja na Pemba | Idadi ya wafanyabiashara wadogowadogo waliotambuliwa Unguja | 1000 | 671 | 67 | Wafanyabiashara 671 wamepatiwa mafunzo ya uendeshaji wa biashara, usajili wabiashara na mbinu za upatikanaji wa mitaji. |

### a. Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2024/25 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026/27. Mradi una lengo la kuimarisha uratibu, usimamizi, ufuatiliaji na tathmini wa utekelezaji wa Mipango, Sera na Mikakati ya Kisekta, Kitaifa, Kikanda na Kimataifa ikiwemo Mpango wa Maendeleo wa Zanzibar (ZADEP) 2021-2026, Ajenda ya Afrika 2063 na Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs)

2030. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.80 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.08 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha TZS 1.01 bilioni sawa na asilimia 94 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwajengea uwezo Maafisa Ufuatiliaji na Tathmini katika Wizara, Idara, Wakala wa Serikali, Serikali za Mitaa na Asasi za Kiraia; | Idadi ya Maafisa waliojengewa uwezo | 400 | 310 | 78 | Jumla ya maafisa ufutatiliaji na tathmini na maafisa mipango 300 wamejengewa uwezo kutoka Tume ya Mipangio, MDAs na Serikali za mitaa Unguja na Pemba juu ya dhana ya ufuatiliaji na tathmini, mafunzo hayo yamefanyika mwezi wa Disemba 2025 na Januari 2026 na jumla ya maafisa 10 kutoka idara yaa ufuatiliaji na tathmini maandalizi ya kuwapeleka mafunzo ili kuongeza ufaanisi wa majukumu yao Tanzaniaa Bara yanaendelea. |
| Kuandaa Mfumo wa Ufuatiliaji na Tathmini (M&E Framework) wa Mpango wa Maendeleo wa mwaka 2026–2031; | Asilimia ya uandaaji wa mfumo iliyofikwa | 100 | 10 | 10 | ToR kwa ajili ya kufanya kazi hiyo imeshawalishwa kwa Afisa manunuzi kwa ajili ya kumtafuta Mshauri Elekezi kufanya kazi hii na hatua za manunuzi zinaendelea. |
| Kufanya tathmini ya Programu na Miradi ya Maendeleo | Asilimia ya programu na miradi iliyofanyiwa tathmini | 100 | 55 | 55 | Tathmini imefanyika kwa miradi 2 kati ya miraddi 5 iliyopaangwa ambayo ni Mradi wa kiwanda cha kusarifu dagaa na Ujenzi na ukarabati wa maghala, kazi inayoendelea ni uandishi wa ripoti, Tathmini ya huduma za afya aambazo zinafanywa na kampuni binafsi (Outsourcing) na Tathmini ya viwanda zinaendelea katika hatua ya uaandaaji wa zana za kukusanyia taarifaa na tathmini kwa miradi ya UVIKO 19 imefikia katika hatua ya utoaji wa mafunzo kwa wakusanyaji wa taarifa za tathmini. |
| Kushiriki mikutano ya Kikanda na Kimataifa ikiwemo ya Umoja wa Mataifa kuhusu SDGs na Ajenda ya Afrika 2063 | Idadi ya wafanyakazi waliohudhuria vikao vya kimataifa | 10 | 4 | 40 | Wafanyakazi wa Tume ya Mipango wamehudhuria katika kuwasilisha ripoti ya Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs),2024 katika Jukwaa la juu la siasa Jijini New York, Nchini Marekani, mwezi Julai 2025 na mwezi Septemba 2025 |
| Kuandaa na kuchapisha Ripoti ya Utekelezaji wa Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs) kwa Zanzibar kwa mwaka 2025–2026; na | Asilimia ya uandaaji wa ripoti iliyofikiwa | 100 | 60 | 60 | Rasimu ya ripoti ipo katika ukamilishaji amabyo itawasilishwa Tanzania Bara na kuunganishwa kua ripoti moja ya Tanzania na kuwasilishwa Umoja wa Mataifa mwaka 2026 |
| Kuandaa nyenzo shirikishi ya ufuatiliaji wa viashiria vya Malengo ya Maendeleo Endelevu | Asilimia ya nyezo ilioandaliwa | 100 | 10 | 10 | Maandalizi ya uandaaji wa nyezo zitakazotumika kukusanyia taarifa yameanza katika hatua za awali kwa kuandaa ToR kwa ajili ya kuimpata mshjauri Elekjezi ambae ataifanya kazi hiyo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| 2030, Mpango wa muda wa kati wa Maendeleo wa Zanzibar na Ajenda za Afrika 2063. | | | | | |

### b. Mradi wa Kuratibu, Kupanga na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo

Mradi huu una lengo la kuratibu shughuli za upangaji na usimamizi wa rasilimali fedha zinazotengwa na kutolewa katika utekelezaji wa shughuli za maendeleo. Mradi pia una lengo la kuimarisha uwezo wa Wizara na Taasisi za Serikali iliziweze kusimamia rasilimali fedha kwa ufanisi zaidi kwa kuweka mifumo ya uwazi katika utekelezaji wa miradi ya maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa TZS 5.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Mach 2026, jumla ya TZS 3.30 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Mach 2026, mradi huu umeingiziwa TZS 9.55 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 289 na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa Mpango Mpya wa Maendeleo wa muda wa kati (2026-2031) baada ya ZADEP kufikia mwisho wa utekelezaji wake Juni 2026. | Asilimia ya kazi iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Rasimu ya awali ya mpango mpya wa Maendelo umeandaliwa na sasa upo katika maboresho na kupata maoni ya wadau. |
| Kuratibu zoezi la uthamini na uhakiki wa mali za wananchi wanaopisha utekelezaji wa miradi ya maendeleo. | Idadi ya Miradi iliyofanyiwa Uthamini | 150 | 195 | 130 | Ripoti za uthamini wa malipo ya fidia kwa mali na vipando vya wananchi wanaopisha utekelezaji wa Miradi ya Maendeleo zimeandaliwa na kuwasilishwa Sekta husika kwa hatua za Malipo. |

### c. Mradi wa Kuendeleza Tafiti za Kimkakati

Mradi unalenga kukuza uwezo wa kitaasisi na kitaalamu katika kufanya tafiti zenye mwelekeo wa kimkakati, ambazo zitasaidia kutoa mapendekezo ya kisera, kubaini maeneo ya vipaumbele vya maendeleo na kusaidia katika uundaji wa mipango inayozingatia ushahidi. Mradi huu utaimarisha uratibu wa shughuli za utafiti na kuhakikisha matokeo yanatumika kwa tija katika kupanga na kutekeleza mipango ya maendeleo na unatarajiwa kuchochea ubunifu,

kuimarisha matumizi ya teknolojia ya kisasa katika ukusanyaji na uchambuzi wa takwimu, na kuongeza ushiriki wa vijana na wanawake katika shughuli za utafiti. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi machi 2026, jumla ya TZS 600 milioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia machi 2026, jumla ya TZS 481.36 milioni zimeingizwa kutoka Serikalini sawa na asilimia 80 na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa na kuchapisha Agenda ya Tafiti Zanzibar 2026-2031 | Asilimia ya maandalizi iliyofikiwa | 100 | 80 | 80 | Agenda mpya ya utafiti Kwa kwa sasa ipo katika hatua za mwisho kukamilika kwa kupata maoni ya wadau juu ya maeneo ya vipaumbele yaliyoibuliwa |
| Kuratibu na kufanya tafiti na ubunifu Zanzibar; | Asilimia ya kazi iliyofikia | 100 | 90 | 90 | Programu ya Maendeleo ya Karafuu ipo katika hatua za mwisho za kupokea maoni ya wadau, kuwasilishwa kwenye vikao kwa ajili ya maamuzi. Aidha, Muongozo wa kuratibu fedha za tafiti umekamilika na unatarajiwa kuzinduliwa hivi karibuni ili kuimarisha upatikanaji na usimamizi wa rasilimali za utafiti.<br>Vilevile, Muongozo wa kuimarisha mfumo wa shughuli za ubunifu nchini umeandaliwa na kwa sasa upo katika hatua ya kukusanya maoni ya wadau, ripoti ya tathmini ya kuimarisha zao la chumvi nchini imekamilika na ipo katika hatua ya kupokea maoni ya wadau kabla ya kukamilishwa rasmi. |
| Kujenga uwezo juu ya kuandaa maandiko ya Utafiti, kuandika ripoti na kutumika “software” kwa ajili ya kufanya uchambuzi wa taarifa za tafiti. | Idadi ya wadau waliopatiwa mafunzo | 500 | 320 | 64 | Watendaji 320 wa Serikali na Mashirika, Wanafunzi wa vyuo vikuu, watafiti na wadau mbalimbali wamepatiwa juu ya mbinu za utafiti, uandishi wa tafiti zinazoelekeza sera, pamoja na matumizi ya teknolojia za kisasa kama vile SPSS na KoboCollect. Aiahda, Mafunzo yamefanyika kwa awamu mbili na matarajio ni kuendelea na mafunzo hayo. |

#### 11.2.3.2 Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali

Ofisi ina jukumu la kutoa, kukusanya, kuchambua, kuchapisha, kuhifadhi na kusambaza taarifa na takwimu zilizo rasmi, kutoa takwimu na taarifa zenye ubora na kuhamasisha matumizi ya takwimu katika mipango ya maendeleo, kufanya maamuzi katika masuala ya utawala na uendeshaji pamoja na ufuatiliaji na tathmini kwa shughuli za kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza Programu moja na mradi mmoja wa maendeleo. Kwa

mwaka 2025/2026, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali imepangiwa jumla ya TZS 6.92 bilioni (TZS 2.0 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.91 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa kutekeleza programu moja na mradi mmoja wa maendeleo Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Ofisi imepanga kutumia jumla ya TZS 4.15 bilioni na imetekeleza Programu na miradi kama ifuatavyo: -

**i) Programu ya Uimarishaji Takwimu Tanzania –Awamu ya Pili (TSMP II)**

Programu ina lengo la kuimarisha shughuli za kitakwimu Zanzibar kwa kuwezesha ukusanyaji, upatikanaji na utoaji wa takwimu za kawaida (routine data) kwa wakati, kuweka mazingira mazuri ya kuratibu upatikanaji wa takwimu za Kiuchumi na Kijamii kupitia takwimu za kawaida, sensa na tafiti. Programu inalenga kuwezesha uzalishaji na usimamizi wa takwimu, uimarishaji wa mifumo ya kitakwimu na miundombinu, maendeleo ya rasilimali watu kwa Taasisi za Serikali kupitia Mfumo wa Takwimu Zanzibar ili kusaidia uimarishaji na upatikanaji wa takwimu rasmi. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.60 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 2.75 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, programu hii imepatiwa jumla TZS 3.69 sawa na asilimia134 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na Utafiti wa Kilimo wa mwaka 2025/2026; | Asilimia ya utafiti iliofikiwa | 100 | 75 | 75 | Ofisi imekamilisha zoezi la ukusanyaji wa Taarifa za Utafiti uwandani na kazi inayoendelea ni kutengeneza majadueli na uhakiki wa Taarifa kabla ya kuanza kwa kazi ya uandishi wa ripoti. |
| Kukusanya, kutayarisha na kutoa uchambuzi wa kizio cha Mfumko wa bei (Consumer Price Index); | Asilimia ya utayarishaji Kizio cha Mfumko wa Bei iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Taarifa za bei za bidhaa kutoka masoko ya vijijini zimekusanywa kwa mwezi wa Julai, Agosti na Septemba 2025. Taarifa zimefanyiwa uchambuzi na ripoti imetayarishwa. Takwimu hizi kwa sasa zinatumika kwa ajili ya matumizi ya ndani. |
| Kufanya Utafiti wa mwaka na robo mwaka wa uzalishaji viwandani; | Asilimia ya Utafiti uliofikiwa | 100 | 60 | 60 | Katika Utafiti wa Uzalishaji Viwandani (QSIP) zoezi la ukusanyaji wa taarifa za utafiti zimekusanywa. Aidha, baadhi ya taarifa Ofisi inaendelea kuzifuatilia |
| Kufanya Utafiti wa Watu Wenye Uwezo wa Kufanya Kazi wa mwaka 2023/2024; | Asilimia ya utafiti wa watu iliofikiwa | 100 | 60 | 60 | Zoezi la ukusanyaji taarifa Julai hadi Septemba limekamilika na sasa wanaendelea na ukusanyaji wa robo ya mwisho ya mwkaa 2025(Oktoba hadi disemba) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya (HBS); | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Zoezi la ukusanyaji wa taarifa za Utafiti wa Mapato na Matumizi ya Kaya IHBS- Tanzania 2025 limekamilika na kazi inayoendelea ni ucchambuzi wa taarifa |
| Uwasilishwaji wa ripoti ya utafiti wa uwajiri na mapato; | Asilimia ya ripoti iliofikiwa | 100 | 90 | 90 | Ofisi imekamilisha Rasimu ya viashiria muhimu vya utafiti wa nguvu kazi ya mwaka 2024 ipo tayari na imewasilishwa kwa uongozi. |
| Kufanya utafiti wa sekta zisizo rasmi. | Asilimia ya utafiti wa sekta iliofikiwa | 100 | 50 | 50 | Ofisi imekamilisha zoezi la ukusanyaji taarifa za utafiti ambalo lilianza mwanzoni mwa mwezi wa Aprili 2026 na kazi inayotarajiwa kuendelea ni uchambuzi wa taarifa. |
| Ujenzi wa Jengo la Ofisi ya Mtakwimu Mkuu wa Serikali Pemba | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa | 100 | 73 | 73 | Kazi ya ujenzi inaendelea hatua ya kupiga plasta na kuweka *scheming* |

### a. Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia

Mradi una lengo la kuimarisha uzalishaji na matumizi ya takwimu za jinsia ambazo husaidia katika kubuni sera na mipango ya kijamii, kiuchumi, na kisiasa ambayo inazingatia mahitaji na haki za jinsia hasa katika masuala ya elimu, afya, ajira na haki za kijamii. Vile vile, kutoa elimu ya dhana ya udhalilishaji wa kijinsia na aina zake, kutambua makundi au maeneo ambayo yako katika hatari zaidi ya udhalilishaji wa kijinsia. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.32 bilioni (TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 320.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.39 bilioni (TZS 1.20 bilioni kutoka Serikalini na TZS 192 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) bilioni zilipangwa kutumika, hadi kufikia Machi 2026 jumla ya TZS 178.93 million sawa na asilimia13 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa warsha ya uhamasishaji kwa wazalishaji na watumiaji wa takwimu za jinsia; | Asilimia ya utekelezaji iliofikiwa | 100 | 75 | 75 | Kumefanyika vikao viwili; kimoja Unguja na kimoja Pemba kwa wadau watumiaji na wazalishaji wa takwimu za jinsia. |
| Kufanya utafiti katika Kaya kuhusu maswala ya udhalilishaji wa kijinsia Zanzibar; | Asilimia ya utafiti wa kaya iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Nyezo za utafiti na sampili zimekamilika na matayarisho kwa ajili ya majaribio ya nyenzo yanaendelea |
| Kutoa toleo la kila mwezi la takwimu za jinsia. | Asilimia ya toleo la takwim wa jinsia iliofikiam | 100 | 100 | 100 | Matoleo ya udhalilishaji yametolewa kwa wandishi wa habari na wadau kama yalivyopangwa |

### 11.2.3.3 Ofisi ya Muhasibu Mkuu Wa Serikali

Ofisi ya Mhasibu Mkuu wa Serikali ni taasisi ya msingi katika kuhakikisha uwajibikaji, uwazi na matumizi mazuri ya rasilimali za umma kwa mujibu wa Sheria, Kanuni na Taratibu za fedha za umma. Katika kutekeleza jukumu lake, Ofisi inashirikiana kwa karibu na taasisi nyingine za kifedha, Mamlaka za Serikali za mitaa, Wakaguzi wa nje na wa ndani, pamoja na Wadau wa maendeleo ili kuimarisha mnyororo wa usimamizi wa fedha za Serikali, Washirika wa Maendeleo na wadau wengine wa maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza mradi mmoja utakaogharimu kiasi cha TZS 1.02 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Ofisi imepanga kutumia jumla ya TZS 614.33 milioni na imetekeleza Miradi kama ifuatavyo: -

**a. Mradi wa Uandaaji wa Hesabu (IPSAS ACCRUAL) Kwa Viwango Vya Kimataifa**

Mradi huu una lengo la kuimarisha uwazi, uwajibikaji na matumizi sahihi ya rasilimali za umma kwa kuhakikisha kuwa taarifa za kifedha zinawasilisha hali halisi ya kifedha Serikalini. Kwa mwaka 2025/2026 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 1.02 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 614.33 milioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 564.51 milioni sawa na asilimia 92 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya mapitio ya Miongozo ya Kihasibu; | Idadi ya miongozo ya kihasibu iliyofanyiwa mapitio | 2 | 2 | 100 | Miongozo miwili imefanyiwa mapitio ambayo ni "Accounting Procedures Manual" na "Accounting Policies Manual" kwa lengo la kuimarisha utendaji. |
| Kukijengea uwezo kikosi kazi cha usimamizi wa mradi na kufanya warsha ya wadau kuhusiana na *Accrual* | Idadi ya Maafisa wa kikosi kazi waliojegewa uwezo | 25 | 20 | 80 | Wafanyakazi 20 wa kikosi kazi cha usimamizi wa mradi wameshiriki katika mafunzo ya "Accrual Accounting" yaliyotolewa na taasisi mbalimbali kwa lengo la kujifunza mbinu za kutayarisha taarifa za kifedha kwa kutumia mfumo wa BAMAS. |
| | Idadi warsha zilizofanyika | 2 | 2 | 100 | Mafunzo ya kuwajengea uwezo wahasibu 54 na maafisa ununuzi 54 kuhusiana na matumizi katika utaratibu wa "Accrual" kwa taasisi za umma Unguja na Pemba yamefanyika kwa lengo la kupata uelewa wa utaratibu wa "Accrual" na mabadiliko yake. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya mapitio ya mfumo wa Bajeti na Matumizi (BAMAS) na kuboresha moduli zilizomo ili ziendane na mfumo wa Accrual | Asilimia ya mapitio yatakayofanyika | 100 | 73 | 73 | "Purchase Module" na Advance Payment Module" zimeboreshwa ili kuweza kukidhi mahitaji ya "Accrual Basis Accounting". Pamoja na kuandaa "templete" ya taarifa za fedha kwa mujibu wa viwango vya IPSAS Accrual imefanyika. Aidha, Kikao na maafisa kutoka TRA na ZRA kujadili viwango sahihi vya kodi na utaratibu wa malipo ndani ya mfumo wa BAMAS kimefanyika kwa lengo la kuweka uelewa wa pamoja kuhusu usahihi wa makato ya kodi na uwasilishaji na Mapitio ya voti za serikali zinazotumia BAMAS yamefanyika |
| Ununuzi wa Vifaa vya Tehama na Miundombinu pamoja na ununuzi wa samani na vitendea kazi vya ofisi | Idadi ya Vifaa vya Tehama vilivyonunuliwa | 100 | 70 | 70 | Hatua za Ununuzi zinaendelea kama ifuatavyo .Mzabuni ameshapatikana hatua iliyofikiwa ni kufunga mkataba na vifaa vinatarajiwa kuwasilishwa ndani ya mwezi mmoja baada ya kufunga mkataba |

### 11.2.4 Ofisi ya Rais Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora

Ofisi ina lengo la kuwa na Utumishi wa Umma wenye ujuzi utakaotoa huduma nzuri kwa jamii zenye kuzingatia misingi ya haki, Sheria na demokrasia, ili kuhakikisha wananchi wanapata huduma zinazofuata misingi ya haki za kibinadamu. Aidha, Ofisi inasimamia utekelezaji wa Sera, Sheria na miongozo ya masuala ya misingi yanayotokana na utawala bora kwa jamii ya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026 Ofisi imepanga kutekeleza Programu mbili na miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 7.22 bilioni (TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.72 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Ofisi imepanga kutumia jumla ya TZS 4.3 bilioni TZS 900 milioni Serikalini na TZS 3.4 bilioni Washirika wa Maendeleo  na imetekeleza Programu na miradi kama ifuatavyo: -

**i. Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma Awamu ya II**

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha utendaji wa watumishi wa umma Zanzibar katika utoaji wa huduma stahiki kwa jamii. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), programu ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 600 milioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 428.37 sawa na asilimia 71 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Utayarishaji wa Mfumo wa Kieletroniki wa Usimamizi wa Watumishi Serikalini (Civil Servant Management System - CSMS) | Asilimia ya utayarishaji wa mfumo iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Tume ya Utumishi Serikalini imekamilisha matayarisho ya Mfumo wa Kielektroniki wa Usimamizi wa Watumishi Serikalini (Civil Servants Management System). Hatua za uandaaji wa Mafunzo zinaendelea ambapo wadau mabali mbali wa mfumo ndani na nje ya ofisi ya Tume wanatarajiwa kupata mafunzo hayo. |
| Kutayarisha Mfumo wa Malipo na Mishahara (HRPAYMIS) | Asilimia ya utayarishaji wa mfumo iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Maboresho ya baadhi ya Moduli za taarifa za Watumishi katika Mfumo yanaendelea. Aidha, hatua inayofuata ni kuendeleza zoezi la kuunganisha mfumo na mashirika ya umma, ikiwemo ZSSF, Bodi ya Mikopo ya Elimu ya Juu na mashirika mengine ili kuboresha ufanisi na upatikanaji wa huduma. |
| Kuimarisha Mfumo wa Kielektroniki wa Usajili wa Taarifa za Mali na Madeni ya Viongozi wa Umma | Asilimia ya uimarishaji wa mfumo iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Mfumo upo katika hatua ya kufanywa majaribio ya awali kwa watumishi wa Tume. |

### ii. Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria

Programu imeanza mwaka 2022/2023 na kukamilika mwaka 2027/2028 Programu ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa haki pamoja na kuimarisha uwezeshaji wa wananchi katika masuala ya sheria. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.73 bilioni (TZS 500 milioni kutoka Serikalini na 1.23 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026), programu ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 1.04 bilioni (TZS 300 Milioni kutoka Serikalini na TZS 737.9 milioni kutoka Washirika wa maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha mifumo na uwezo wa Taasisi za Sheria na rasilimali watu | Asilimia ya Mfumo wa Usimamizi wa Utoaji Huduma za Kisheria (LAPMIS) uliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Mfumo umeimarishwa, kazii inayoendelea ni kufanyiwa kazi Maoni yaliopendekezwa na Wadau ili kuwasilishwa katika Ngazi ya Uongozi wa Wizara kwa hatua. |
| | Asilimia ya Mfumo wa Kufundishia (E-learning platform iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Mfumo wa Kufundishia Maafisa Sheria (E – learning) kwa hatua ya kwanza umekamilika na umezinduliwa rasmi tarehe 23/01/2026. |
| | Idadi ya wanasheria waliopatiwa mafunzo | 201 | 201 | 100 | Mafunzo yaliyotolewa ni Uandishi wa Hukumu, Mashtaka, Mbinu za Uchunguzi na Matunzo. |
| Kuziwezesha Asasi za Kiraia kutoa msaada wa kisheria na kuhamasisha jamii juu ya haki za kisheria na za kibinadamu kwa makundi hatarishi. | Idadi ya wanajamii (wanufaika) waliopatiwa msaada wa kisheria | 300 | 300 | 100 | Mafunzo yametolewa kwa jamii yanayohusiana na msaada wa Kisheria, AI na programu zinazolenga masuala ya kusaidia jamii. |
| | Idadi ya wanajamii waliopatiwa msaada wa kisheria | 4,000 | 4,000 | 100 | Wasaidizi wa Sheria wametoa msaada wa kisheria kwa wananchi wa makundi mbali mbali ikiwemo kutatua migogoro ya ardhi, ndoa pamoja na mirathi. |
| | Idadi ya asasi za kiraia zilizowezeshwa kutoa msaada wa kisheria kwa makundi hatarishi | 7 | 7 | 100 | Asasi za kiraia zilizowezeshwa kutoa msaada wa kisheria ni ZAFELA, WEPO, NAPAC, SOPAU, MDIPAO, PACSO pamoja na ZLSC. |
| Kuanzisha utaratibu wa kuelimisha jamii juu ya huduma ya haki katika kesi za unyayasaji wa kijinsia. | Idadi ya wanajamii waliopatiwa uwelewa | 20 | 20 | 100 | Wasaidizi wa Sheria kwa kushirikiana na Idara ya msaada wa kisheria wametoa elimu ya kisheria kuhusu masuala ya udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia (SGBV) |
| | Idadi ya wanafunzi wa Vyuo waliopatiwa uwelewa | 300 | 300 | 100 | Wasaidizi wa Sheria kwa kushirikiana na Idara ya msaada wa kisheria wametoa elimu ya kisheria kwa wanafunzi wa vyuo hususani masuala ya udhalilishaji na unyanyasaji wa kijinsia (SGBV) |
| | Idadi ya wasaidizi wa Sheria walioajiriwa kutoa msaada wa kisheria kwa makundi hatarishi. | 40 | 40 | 100 | Mara tu baada ya Wasaidizi wa Sheria kuajiriwa huunganishwa katika Taasisi za Wasaidizi wa Sheria kulingana na Wilaya anayotoka. |
| Kuandaa mfumo wa kielektroniki wa kupitia mikataba kwa Afisi ya Mwanasheria Mkuu | Asilimia ya uandaaji wa mfumo iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Vifaa vitakavyotumika katika mfumo vimenunuliwa na kufungwa, vifaa ambavyo tayari vimeanza kutumika na Mshauri elekezi ameshapatikana kwa ajili ya kutayarisha mfumo ikiwa ni hatua ya Pili ya Uandaaji wa mfumo. |

### b. Mradi wa Utoaji wa Huduma ya Haki kwa Kuzingatia Jinsia

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/2024 na kumalizika 2025/2026. Mradi una lengo la kupunguza vitendo vya udhalilishaji kwa vijana, wanawake na watoto Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 143.31 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo (UN-WOMEN). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 85.98 milioni. Hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha TZS 49.94 milioni sawa na asilimia 58 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya mikutano ya kuratibu usimamizi wa kesi kwa kila robo mwaka. | Idadi ya Mikutano ya uratibu iliyofanyika | 2 | 1 | 50 | Mkutano wa kuratibu usimamizi wa kesi umefanyika na unaendelea kufanyika kwa kila robo mwaka. |
| Kuzindua Mwongozo wa Uanzishaji na Uratibu wa Jukwaa la Kitaifa la Haki la Wanawake na Wasichana Unguja. | Idadi ya Muongozo uliozinduliwa | 1 | 1 | 100 | Mwongozo wa Jukwaa la Kitaifa la Haki ya Wanawake Zanzibar umezinduliwa rasmi kwa kushirikisha taasisi muhimu za serikali, asasi za kiraia na watoa msaada wa kisheria kutoka Unguja na Pemba. |
| Kuandaa Muongozo wa Kurahisisha Hukumu | Asilimia ya uandaaji ya muongozo iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Muongozo umekamilika kwa vitabu vinne na kutafsiriwa kwa lugha ya Kiswahili ili iwe rahisi kwa wadau mbalimbali kuusoma na kuufahamu. |
| Kuandaa rasimu ya ushirikishwaji wa vyombo vya sheria vinavyohusiana na masuala ya Ukatili wa Kijinsia (GBV) ambavyo vitazalisha matokeo ya kuwa na muhtasari wa Mswada wa GBV. | Asilimia ya uandaaji wa rasimu iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Rasimu imeandaliwa na jumla ya vyombo 9 vya sheria kuhusu Ukatili wa Kijinsia (GBV) vimeshirikishwa. |
| Kutafsiri Muongozo wa Kiuchunguzi, Uendeshaji wa Kesi, na Utoaji wa Hukumu kwa Kesi za Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake, Wasichana na Watoto Zanzibar kwa lugha ya kiswahili. | Asilimia ya muongozo uliotafsiriwa | 100 | 90 | 90 | Rasimu ya Muongozo wa Kiuchunguzi, Uendeshaji wa Kesi, na Utoaji wa Hukumu kwa Kesi za Ukatili na Udhalilishaji dhidi ya Wanawake, Wasichana na Watoto Zanzibar umetafsiriwa na hatua iliobaki ni kuthibitishwa (validation) na kuchapishwa. |
| Kuwajengea uwezo watendaji wa Ofisi ya DPP kitengo cha dawati juu ya kushughulikia mashahidi na waathirika wa kesi za ukatili na udhalilishaji SGBV. | Idadi ya watendaji waliopatiwa mafunzo. | 43 | 43 | 100 | Mafunzo ya siku mbili kwa wafanyakazi wa Dawati la Msaada la Mashahidi wa DPP katika kusaidia mashahidi na waathiriwa wa udhalilishaji na ukatili wa kijinsia (SGBV). |
| Kutoa mafunzo ya muda mfupi kwa Wasaidizi wa Sheria kuhusu masuala ya Kuwalinda waathirika pamoja na Ukusanyaji wa Takwimu kwa Unguja na Pemba). | Idadi ya wasaidizi wa Sheria waliopatiwa mafunzo | 50 | 60 | 120 | Jumla ya Wasaidizi wa Sheria 60 waliopatiwa mafunzo Unguja na Pemba (Wanaume 28 na Wanawake 32) |

### 11.2.4.1 Mahakama Kuu

Ofisi ina jukumu la kupokea, kusikiliza na kuyatolea maamuzi madai ya wananchi yanayowasilishwa mahakamani kwa lengo la upatikanaji wa haki kwa jamii ndani ya muda uliowekwa. Kwa mwaka 2025/2026 Ofisi imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 48.60 bilioni (TZS 13.60 bilioni kutoka Serikalini na TZS 35.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Ofisi imepanga kutumia jumla ya TZS 29.16 bilioni (TZS 8.16 bilioni kutoka Serikalini na TZS 21.0 bilioni Washirika wa Maendeleo) na imetekeleza miradi kama ifuatavyo: -

**a. Mradi wa Ujenzi wa Mahakama za Wilaya na Mikoa**

Mradi huu umeanza mwaka 2023/2024 na ulitarajiwa kukamilika mwaka 2024/2025. Mradi una lengo la kujenga majengo mapya ya Mahakama ambayo yatakuwa na mazingira bora na yatakayoongeza ufanisi katika utoaji wa huduma za kisheria na upatikanaji wa haki. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia jumla ya Shilingi 13.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 7.8 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha TZS 7.66 bilioni sawa na asilimia 98 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kaskazini Pemba katika eneo la Kinyasini | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 84 | 84 | Kwa sasa ujenzi unaendelea, ukiwa katika hatua ya ufungaji wa suspended ceiling pamoja na utekelezaji wa shughuli nyingine ndogo ndogo. |
| Kujenga Mahakama ya Mkoa wa Kusini Pemba katika eneo la Changaweni. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 88 | 88 | Ujenzi unaendelea hatua ya umaliziaji kwa kuweka milango, kuunganisha umeme na kuweka sawa aridhi (Land scaping) |
| Kujenga Mahakama ya Wilaya ya Micheweni Pemba katika eneo la Konde | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 82 | 82 | Ujenzi umefikia hatua za umaliziaji. Kazi zinazoendelea ni uwekaji wa miundombinu ya maji taka (drainage system) katika eneo la nje ya jengo. |
| Kuendeleza ujenzi wa Mahakama ya Mfikiwa Chake chake Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 83 | 83 | Ujenzi umefikia hatua ya kumalizia na kazi zinazoendelea ni kuweka *tiles* na madirisha |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kujenga Mahkama ya Wilaya ya Magharibi B katika eneo la Kisakasaka | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Kujenga Mahkama ya Wilaya ya Mjini katika eneo la Mazizini | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |

### b. Mradi wa Uimarishaji wa Mahakama

Mradi una lengo la kuimarisha Mahakama katika kuwezesha upatikanaji wa haki pamoja na kuongeza ufanisi kwa watendaji wa Mahakama. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 35.60 bilioni (TZS 600 milioni kutoka Serikalini na TZS 35.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 21.36 bilioni (TZS 360 milioni kutoka Serikalini na TZS 21.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 8.52 bilioni sawa na asilimia 40 (TZS 510 milioni sawa na asilimia 142 kutoka Serikalini na TZS 8.01 bilioni sawa na asilimia 38 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa kompyuta na vifaa vyake | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Vifaa vimepokelewa na tayari vishaanza kutumika |
| Ununuzi wa huduma za kimtandao | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Taratibu za manunuzi zinaendelea |
| Ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya- Kigunda | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Tayari mshauri elekezi amepatikana na michoro tayari imewasilishwa kwa Uongozi wa Mahakama na taratibu nyengine zinaendelea. |
| Ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya - Kinduni | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | |
| Ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya - Jendele | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | |
| Ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya- Kijichi | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa jengo la Mahakama ya Wilaya -Makunduchi | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | |
| Ukarabati wa majengo ya Mahakama ya Mahonda | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Tayari mshauri elekezi amepatikana na michoro tayari imewasilishwa kwa Uongozi wa Mahakama na taratibu nyengine zinaendelea. |
| Ukarabati wa majengo ya Mahakama ya Wete | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | |
| Kufanya mafunzo ya utekelezaji na usimamiaji wa mradi kwa watumishi wa mahkama | Idadi ya watumishi waliopatiwa mafunzo | 479 | 350 | 73 | Mafunzo yanaendelea kutekelezwa na tayari ***Training Needs Assessment*** inaendelea kufanyiwa kazi ambapo andiko la awali tayari limewasilishwa. |
| Ununuzi wa gari, gharama za Bima na Leseni za njia. | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Magari yameshapokelewa na kufanyiwa usajili ambapo muda mfupi yataanza kutumika. |
| Kuandaa mfumo wa kielektroniki wa usikilizaji wa mashauri | Asilimia ya hatua iliyofikiwa. | 100 | 95 | 95 | Mfumo umeandaliwa na kuzinduliwa rasmi tarehe 9 Febuari, 2026 katika wiki ya sheria. Aidha, Mafunzo ya yameshaanza kutolewa kwa watumishi na wadau wa Mahakama kwa Unguja na Pemba. |
| Ununuzi wa samani kwa majengo ya Mahakama | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ununuzi wa samani kwa majengo yote ya Unguja na Pemba umefanyika |

### 11.2.5 Ofisi ya Rais-Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ

Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa, Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ ina jukumu la kutoa mwongozo na ushauri kwa Tawala za Mikoa katika kuratibu, kujenga mazingira mazuri na kufuatilia utekelezaji wa shughuli za Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ katika utoaji wa huduma na kuimarisha Utawala Bora. Kwa mwaka wa fedha 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza programu moja na miradi sita ya maendeleo kwa gharama ya TZS 92.12 bilioni (TZS 81.75 bilioni kutoka Serikalini na TZS 10.73 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Ofisi imepanga kutumia jumla ya TZS 55.27 bilioni (TZS 49.05 bilioni kutoka

Serikalini na TZS 6.22 bilioni Washirika wa Maendeleo) na imetekeleza miradi kama ifuatavyo: -

### a. Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama Zanzibar.

Mradi una lengo la kuimarisha usalama wa jamii kwa kuhakikisha kuwa kuna miundombinu ya kisasa ya ulinzi na usalama ikiwemo uwekaji wa mifumo na vifaa vya kisasa vya ulinzi ili kulinda wananchi na mali zao dhidi ya uhalifu na viashiria hatarishi. Kwa kuhakikisha utekelezaji mzuri wa mikakati ya ulinzi na usalama mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali, kwa mwaka 2025/2026 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 25.75 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Mchi 2026, jumla ya TZS 15.45 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 4.83 bilioni sawa na asilimia 31 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vituo vya ufuatiliaji wa matukio ya "CCTV" eneo la Maisara-Unguja, kwa upande wa Pemba - Chake Chake, Wete na Mkoani; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Vipimo vya Udongo (Geotchnical Servey) kwa maeneo manne yanayotaraijwa kujengwa Unguja na Pemba vimefanyika na Mkandarasi ameshakabidhiwa maeneo kuanza ujenzi. |
| Kufanya matengenezo ya kamera za ulinzi na usalama (mfumo mzima wa CCTV); | Asilimia ya matengenezo iliyofikiwa. | 100 | 10 | 10 | Kazi ya urejeshaji wa mfumo wa CCTV kamera zinaendelea kwa baadhi ya maeneo kama vile Michenzani, Kariakao, Mlandege na Bizredi tayari kamera zimeanza kazi. |
| Ununuzi wa zana na vifaa kwa matumizi ya Idara Maalum za SMZ; | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa. | 25 | 5 | 5 | Mkataba wa manunuzi ya vifaa vya Idara Maalum umekamilika na umewasilishwa kwa Mwanasheria Mkuu. |
| Kuimarisha miundombinu ya mawasiliano ya kiulinzi katika Idara Maalum za SMZ; | Asilimia ya uimashaji wa miundombinu iliyofikiwa. | 25 | 10 | 10 | Maombi ya fedha yamepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuingiziwa fedha na kuanza kukarabati. |
| Kukarabati jengo la Ofisi ya mradi eneo la Maisara | Asilimia ya ukarabati iliofikiwa. | 25 | 5 | 5 | Taratibu za maanunuzi zinaendelea za kumpata mzabuni kwa ajili ya ukarabati huo. |
| Kuimarisha mafunzo na vifaa vya kiutendaji kwa Wakala wa Ulinzi, askari na vijana wa JKU; | Idadi ya askari na vijana waliopatiwa mafunzo. | 3,000 | 2 | 2 | Taratibu za maandalizi ya mafunzo yameanza kwa hatua za awali |
| | Asilimia ya vifaa vilivyonunuliwa | 25 | 10 | 10 | Mkataba wa ununuzi wa vifaa vya kiutendaji kwa wakala wa ulinzi umekamilika na mkataba upo kwa Mwanasheria Mkuu kwa kupata idhini ya kusainiwa. |
| Kuimarisha miundombinu na mazingira ya wanafunzi wa Chuo cha Mafunzo. | Asilimia ya miundombinu iliyoimarishwa. | 25 | 5 | 5 | Mkataba umekamilika na mkataba upo kwa Mwanasheria Mkuu kupata idhini ya kusainiwa. |

### b. Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha Zanzibar

Mradi una lengo la kuratibu shughuli mbali mbali za Serikali na kijamii kama vile usajili wa vizazi na vifo, uidhinishaji wa nyaraka na utoaji wa taarifa muhimu kwa wananchi. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, umepangiwa kiasi cha TZS 8.00 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 4.8 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 955.30 milioni sawa na asilimia 20 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa Ofisi za Masheha kwa Shehia 130 Unguja na Pemba; | Asilimia ya ujenzi iliofikiwa. | 100 | 60 | 60 | Ujenzi kwa ofisi 48 Unguja na Pemba na umekamilika kwa hatua ya kujenga matufali (structure). |

### c. Mradi wa Kuimarisha Haki Jinai – Chuo cha Marekebisho ya Tabia

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuwajengea uwezo waendesha mashtaka na wapelelezi katika masuala ya haki jinai. Mradi umedhamiria kuimarisha ushirikiano kati ya wadau wa haki jinai, kuongeza ufanisi na kasi ya upelelezi na uendeshaji wa mashtaka kwa utoaji haki kwa wananchi. Aidha, mradi unahusisha mafunzo kwa wanawake kuhusu kufahamu haki zao katika kesi za jinai na madai. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 18.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 10.80 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha TZS 5.86 bilioni sawa na asilimia 54 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa majengo ya kisasa ya Chuo cha Kurekebisha Tabia cha Hanyegwa mchana | Asilimia ya majengo iliyofikia. | 100 | 30 | 30 | Ujenzi unaendelea kwa majengo sita na ujenzi upo katika hatua mbali mbali:<br>1.Jengo la Utawala na Hospitali yapo katika hatua ya umwagaji wa zege la ghorofa ya kwanza.<br>2. Bweni namba moja na Bweni namba mbili lipo katika hatua ya umwagaji jamvi la chini.<br>3. Bweni namba tatu lipo katika hatua ya maandlizi ya umwagaji wa zege ya ghorofa ya chini.<br>4.Jiko lipo hatua ya kuezeka. |

#### d. Mradi wa Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo Vya Usafiri katika Soko la Mwanakwerekwe

Mradi una lengo la kuimarisha huduma za usafiri na usafirishaji katika eneo la Mwanakwerekwe, kuhakikisha kuwa kuna mazingira bora na salama kwa ajili ya maegesho ya magari kwa usafiri wa umma na binafsi, pamoja na kuongeza ufanisi wa shughuli za kibiashara katika soko hilo. Pia, kuweka mazingira mazuri kwa watumiaji wa soko na utoaji wa huduma za kijamii. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 20.00 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 12.00 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026,shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa kituo cha dalalada na maegesho ya vyombo vya usafiri katika eneo la Mwanakwerekwe. | Asilimia ya ujenzi iliyofikia. | 25 | 5 | 5 | Mkandarasi ameshapatikana na hatua inayoendelea ni utayarishaji wa michoro |

#### e. Mradi wa Kijani -Pemba

Mradi una lengo la kuimarisha huduma za kijamii na kiuchumi kwa kuimarisha miundombinu ya barabara, mifumo ya maji safi na taka, kuwa na maeneo ya kijani ya bustani na viwanja vya michezo. Kuiweka miji katika mazingira safi, salama na yenye kuvutia kwa wakaazi na wageni pamoja na kuwezesha miji kukabiliana na athari za mabadiliko ya tabianchi kwa kutumia teknolojia endelevu na mbinu rafiki kwa mazingira. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 8.27 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 4.96 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa: -

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ukarabati wa masoko mawili Chake Chake na Mkoani Pemba; | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 25 | 5 | 20 | Ukarabati umefaanyika kwa kuongeza miundombinu ya mfumo wa uvunaji wa maji ya mvua katika soko la Kipitacho Mkoani na Michakaini chake chake. |
| Ujenzi wa miundombinu ya usafishaji katika vituo vya huduma za afya Chake Chake na Mkoani Pemba; | Asilimia ya miundombinu ya usafishaji iliyokia | 100 | 40 | 40 | Ujenzi wa vyoo katika kituo cha afya cha RCH Mkoani pamoja ujenzi wa miundombinu ya kunawiya mikona katika kituo cha afya ChakeChake na Uboreshaji wa Usimamizi wa Taka katika Shule za Msingi na Sekondar Michwenii unaendelea. |
| Ukarabati wa viwanja vya michezo eneo la Jadida, Mitiulaya, Micheweni na kuimarisha uhifadhi wa mazingira eneo la bustani ya Jamhuri – Wete; | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 50 | 5 | 5 | Taratibu za manunuzi zinaendelea kwa ukarabati wa viwanja kumi ambavyo Mkoa wa Kaskazini Pemba vinane na kusimi Pemba viwili. |
| Kuongeza uwezo wa utoaji huduma za kijani eneo la msitu wa Ngezi-Vumawimbi; | Asilimia ya utoaji huduma iliyofikiwa | 50 | 15 | 30 | Uandaji wa ramani ya digital inayoonesha mazingira ya msitu na kuweka becon maalum katika msitu pamoja na kuwapatia elimu wafanyakazi unaendelea. |
| Ujenzi wa vituo vya kuchomea taka za Hospitali katika vituo vitano vya afya; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 25 | 17.5 | 70 | Jumla ya vituo Vitatu vya kuchomea taka vimejengwa katika Hospitali ya Mkoani, Hospitali ya Chakechake na Kituo cha afya Mzambarauni. |
| Ununuzi wa vifaa na kuimarisha vikundi vya ukusanyaji taka Mkoa wa Kusini na Kaskazini Pemba; | Asimia ya manunuzi iliyofikiwa | 50 | 30 | 60 | Vifaa vya usafi vimenunulia na ugawaji kwa vikundi mbali mbali Mkoa wa Kaskazini Pemba umefanyika. |
| Kuanzisha Mifumo ya kukusanya maji ya mvua, kufanya matengenezo ya visima na kuimarisha huduma ya maji safi na salama eneo la Wete na Mkoani; | Asilimia ya mfumo iliyofikiwa. | 50 | 50 | 100 | Uchimbaji wa Kisima na ujenzi wa miundombinu ya kuvuna maji ya Mvua katika soko la kipitacho umefanyika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ukarabati na matengenezo ya miundombinu ya maji na usafi wa mazingira kwa Skuli za msingi za Madungu, Shamiani, Ng'ombeni 'A' na 'B'; | Asimia ya ya ukarabati wa miundombinu maji na usafi wa mazingira uliofikiwa | 50 | 50 | 100 | Ukarabati wa vyoo katika skuli ya Miti Ulaya na Micheweni katika Mkoa wa Kaskazini Pemba na Kusini Pemba katika Skuli ya Madungu na Shamiani umefanyika, Aidha, Ujenzi wa vyoo na ukarabati wa bustan - green area katika eneo la Michaikani umekamilika. |
| Ukarabati wa visima viwili eneo la Weni na Kizimbani Pemba; | Idadai ya visima vilivyofanyiwa ukarabati | 2 | 2 | 100 | Ufungwaji wa solar katika visima viwili cha Weni na Kisima namba 7 Wete umekamilka |
| Kutoa huduma na elimu juu ya athari zinazohusiana na usimamizi na uteketezaji wa taka katika skuli ya Jadida na Micheweni; | Idadi ya Shehia zilizopatiwa elimu. | 122 | 30 | 25 | Elimu imetolewa kwa Shehia za Wete na Micheweni pamoja na kusambazwa vifaa vya kukusanyia taka (madastibin) |
| Kuimarisha vikundi vya wanawake na vijana kwa maendeleo ya biashara ndogo ndogo kwa kuanzisha biashara mpya na kuzikuza zilizopo. | Idadi ya vikundi vilivyoimarishwa | 4 | 4 | 100 | Jumla ya vikundi vinne vya Wilaya ya Wete vilipatia ruzuku kwa ajili ya kuendesha biashara zao. |

### 11.2.5.1 Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar

Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii Zanzibar ina jukumu la kusajili na kutoa vyeti kwa matukio muhimu ya kijamii ikiwemo: kuzaliwa, vifo, ndoa na talaka pamoja na utoaji wa vitambulisho vya Mzanzibari Mkaazi. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu kiasi cha TZS 3.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 2.1 bilioni zimepangwa na kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

#### a. Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii

Mradi huu una lengo la kuimarisha mifumo ya usajili ili takwimu za matukio ya kijamii ziwe sahihi na zinapatikana kwa wakati. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, umepangiwa kiasi cha TZS 1.50 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 900 milioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia machi 2026, jumla ya TZS. 741.27 milioni sawa na asilimia 82 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuingiza kumbukumbu za vizazi hai ndani ya mfumo wa usajili wa matukio ya kijamii na takwimu zake; | Asilimia ya uingizaji iliyofikia | 100 | 5 | 5 | Maombi ya fedha kwa ajili ya kutekeleza shughuli hiyo yameshapelekwa Wizara ya Fedha na Mipango |
| Kuimarisha mfumo wa vitambulisho vya Mzanzibari mkaazi; | Asilimia ya uimarishaji iliyofikia | 100 | 100 | 100 | Ofisi imekamilisha kufanya matengenezo kinga ya mfumo na printa ya zamani ya vitambulisho |
| Ujenzi wa kituo cha urejeshaji wa huduma baada ya majanga (Disater Recovery Center). | Asilimia ya ujenzi iliyofikia. | 100 | 50 | 50 | Vifaa tayari vimefika kwa ajili ya utengenezaji wa kituo cha urejeshaji wa huduma baada ya majanga ambapo kituo hicho kinafungwa Kijitomyama Dar es Salaam |

### b. Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijamii.

Mradi huu una lengo la kuweka miundombinu ili kuimarisha utoaji wa huduma. Vituo vya utoaji wa huduma za jamii katika maeneo ya mijini na vijijini vitaimarishwa ili kuhakikisha huduma zinapatikana kwa urahisi kwa wananchi wote. Vile vile, kuimarisha mtandao kwa Ofisi zote za usajili ili kuwezesha mawasiliano na ushirikiano bora kati ya Ofisi zao na Makao Makuu. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, umepangiwa kiasi cha TZS 2.00 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.20 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 605.98 milioni sawa na asilimia 50 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa Ofisi ya Usajili Wilaya ya Kaskazini B - Mahonda; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 60 | 51 | 85 | Ujenzi upo katika hatua ya ujenzi wa ghorofa ya pili na kazi ya umaliziaji wa sehemu ya chini ya jengo na ghorofa ya kwanza zinaendelea |
| Kuimarisha shughuli za mifumo na ununuzi wa gari mbili za Ofisi. | Asilimia ya uimarishaji iliyofikia. | 100 | 100 | 100 | |
| | Idadi ya gari zilizonunuliwa | 2 | 2 | 100 | |

#### 11.2.5.2 Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo (KMKM)

Kikosi Maalum cha Kuzuia Magendo kina lengo la kudhibiti na kuzuia magendo ya bahari, kulinda usalama wa nchi, kupambana na magendo na kuimarisha uchumi wa bahari kupitia uvuvi wa kisasa. Aidha, kikosi kinatekeleza juhudi za Serikali katika kuinua uchumi wa buluu kupitia uvuvi wa bahari. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 5.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 3.0 bilioni zimepangwa na kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

**a. Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM**

Mradi huu una lengo la kuimarisha utendaji kazi na makaazi ya maafisa na wapiganaji wa Idara Maalum za SMZ ili wawe na mazingira mazuri ya kazi. Mradi unatekelezwa kwa fedha za Serikali na kwa mwaka 2025/2026, mradi umetengewa kiasi cha TZS 2.50 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.5 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia machi 2026, Shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa Makao Makuu - Kibweni; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Kikosi kimekamilisha hatua za manunuzi na tayari maombi ya fedha yamepelekwa Wizara ya Fedha na Mipango kwa ajili ya kuanza ujenzi. |
| Ujenzi wa mahanga katika Kambi ya Bwefum. | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 5 | 5 | |

**b. Mradi wa Uzamiaji na Uokozi**

Mradi una lengo la kuimarisha ulinzi na uokozi baharini kwa kutoa huduma za uzamiaji na uokozi pale yanapotokezea maafa ya baharini yanayosababishwa na majanga ikiwemo kuzama kwa vyombo vya baharini, vyombo vya abiria na mizigo kwa Unguja na Pemba. Mradi unatekelezwa kupitia fedha za Serikali. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.50 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2026 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.5 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.49 bilioni sawa na asilimia 100 zimepatikana  na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa Kituo cha Uzamiaji na Uokozi Wete - Pemba na Kizimkazi – Unguja; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Mkataba umekamilika kutayarishwa na upo kwa mwanasheria Mkuu wa Serikali kwa ajili ya kupitiwa na kupata idhini ya kuendelea na ujenzi |
| Ununuzi wa vifaa vya uzamiaji na uokozi. | Idadi ya vifaa vilivyonunuliwa | 33 | 33 | 100 | Kikosi kimeshapokea vifaa vyote vilivyopangwa kununuliwa na tayari vimeshaanza kutumika |

### 11.2.5.3 Kikosi cha Valantia (KVZ)

Kikosi kina lengo la kutoa huduma ya ulinzi na usalama kwa kushirikiana na Taasisi nyengine za ulinzi na usalama za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania. Vile vile, Kikosi kina kazi ya kudumisha amani na mshikamano wa Taifa kwa kutekeleza sera na mipango ya kuleta maendeleo ya jamii na Taifa kwa ujumla. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi kimepangiwa kiasi cha TZS 5.52 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 3.31 bilioni zimepangwa na kutekeleza mradi kama ifuatavyo:-

**a. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari**

Mradi unatekeleza azma ya Serikali ya kuwa na Idara Maalum za SMZ zenye majengo mazuri yatakayoimarisha utendaji kazi kwa wafanyakazi wake. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 5.52 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi machi 2026, jumla ya TZS 3.31 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha TZS 1.19 bilioni sawa na asilimia 36 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa bohari mbili za kuhifadhia vifaa Makao Makuu Mtoni-Unguja na Ndugukitu - Pemba; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 25 | 0 | 0 | |
| Kuendelea na majengo ya utoaji huduma katika kambi ya Makao Makuu- Mtoni; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 75 | 47 | 62 | Jengo ya Hospital ya KVZ Mtoni lipo katika hatua ujenzi wa nguzo za ghorofa ya kwanza na Hospital ya Ndugukitu (Pemba) ujenzi upo katika hatua ya kupiga plasta |
| Kuanza ujenzi wa uwanja wa mpira katika kambi ya Mtoni | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 25 | 5 | 5 | Kikosi kimeshakamilisha taratibu zote za manunuzi na tayari kimeshaomba fedha za Mradi serikalini kwaajili ya kuanza utekelezaji. |

### 11.2.5.4 Chuo cha Mafunzo

Chuo Cha Mafunzo kina lengo la kukuza maadili mema, nidhamu na uwajibikaji kwa wanafunzi ili kuwa raia wema na viongozi bora wa baadae, kutoa elimu ya kivitendo na ujuzi kwa wanafunzi ili kuwawezesha kuwa na uwezo wa kutekeleza majukumu mbali mbali katika taaluma zao, pia chuo cha mafunzo kinajukumu la kuwaandaa vijana na soko la ajira na kuwawezesha kujiajiri. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi kimepangiwa kiasi cha TZS 3.58 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza mradi mmoja wa maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 2.5 bilioni zimepangwa na kutekeleza mradi kama ifuatavyo:-

**a. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga**

Mradi unatekeleza azma ya Serikali ya kuhakikisha watendaji wa Idara Maalum za SMZ wanafanya kazi zao katika makaazi mazuri. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.58 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 2.15 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, kiasi cha TZS 1.62 bilioni sawa na asilimia 75 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa nyumba za ghorofa mbili (G+2) kambi ya Langoni na Hanyegwa Mchana - Unguja; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 25 | 2 | 5 | Mzabuni kwa ajili ya usambazaji wa vifaa vya ujenzi wa nyumba ya ghorofa mbili H/mchana tayari ameshapatikana na hatua inayoendelea ni ufungaji wa mkataba. |
| Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa Makao Makuu Unguja | Asilimia ya ununuzi ilifikia | 100 | 85 | 85 | Vifaa vya Tehema tayari vimeshawasili na kutumika hatua inayofuata kufanya malipo kwa mzabuni wa vifaa hiyo. |
| Kumaliza Ujenzi wa Nyumba tisa katika Kambi ya Hanywega Mchana | Asilimia ya ujenzi ilofikiwa | 100 | 65 | 65 | Ujenzi wa nyumba tisa unaendelea ambapo nyumba tatu zimeshaezekwa, nyumba tatu zipo katika hatua ya kuezeka, nyumba mbili zipo hatua ya linta, nyumba moja ipo hatua ya kufunga mkanda wa chini. |
| Kumalizia ujenzi wa Hanga kambi ya Bumbwini | Asilimia ya ujenzi ilofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi umekamilika kwa hatua zote |

#### 11.2.5.5 Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU)

Jeshi lina lengo la kutoa mafunzo ya kiufundi, elimu ya sekondari na programu za uzalishaji kwa vijana. Vile vile, jeshi linalenga kuimarisha uwezo wa vijana na kuwaandaa kushiriki katika maendeleo ya kiuchumi na kijamii. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi cha JKU kimepangiwa kiasi cha TZS 14.53 bilioni kutoka Serikalini kwa kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 8.72 bilioni zimepangwa na kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

**a. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU**

Mradi una lengo la kuweka mazingira mazuri ya utendaji kazi kwa watumishi wa Idara Maalum za SMZ kwa kuwapatia majengo yenye viwango stahiki. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 5.99 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS. 3.59 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi, 2026 TZS 2.11 bilioni sawa na asilimia  59 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa jengo la ghorofa tano (G+5) la Makao Makuu ya JKU - Saateni; | Asilimia ya ujenzi iliyofikia. | 100 | 15 | 15 | Ujenzi wa jengo la ghorofa tano (G+5) la Makao Makuu ya JKU- Saateni upo katika hatua ya kumalizia ujenzi wa msingi |
| Kuendelea na ujenzi wa nyumba za makaazi ya watumishi wa JKU Ng'ambwa Pemba; | Asilimia ya ujenzi iliyofikia. | 100 | 70 | 70 | Ujenzi unaendelea kwa ghorofa ya pili kwa maandalizi ya kuezeka |

**b. Mradi wa Ujenzi wa Dakhalia**

Mradi una lengo la kutoa huduma ya malazi kwa wanafunzi wanaoishi mbali na maeneo yao ya makaazi. Dakhalia itasaidia kuinua kiwango cha ufaulu na kulinda usalama wa wanafunzi dhidi ya unyanyasaji. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.13 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.88 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 2.06 bilioni sawa na asilimia 110 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi wa skuli ya JKU Mtoni. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 30 | 30 | Ujenzi upo katika hatua ya uwekaji wa jamvi la ghorofa ya pili na kunyanyua nguzo. |

### c. Mradi wa Uimarishaji wa Utoaji wa Huduma za Wakala wa Ulinzi JKU

Mradi una lengo la kuimarisha uwezo wa kulinda raia na mali zao katika maeneo tofauti ikiwemo taasisi za Serikali, biashara na makaazi binafsi. Aidha, mradi una lengo la kuongeza idadi na ufanisi wa walinzi. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 5.42 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 3.25 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 3.2 bilioni sawa na asilimia. 98 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza ujenzi wa ghorofa mbili Makao Makuu ya Wakala wa Ulinzi JKU Mtoni. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 60 | 60 | Ujenzi huu umegawika sehemu tano ambazo ni ujenzi jengo la ghorofa mbili la Afisi, hanga lenye vyumba 48, maegesho, maduka 16 na fensi pamoja na jiko la kisasa. Kwa sasa kazi zilizofanyika ni matayarisho ya uwekaji wa jamvi la ghorofa ya pili, pamoja na ujenzi wa tofali kwa maeneo ya kuta za chini na ghorofa ya kwanza. Pia, ujenzi wa Hanga unaendelea kwa hatua ya kumwaga jamvi na kusimamisha nguzo sambamba na ujenzi wa maduka na fensi unaendelea . |

## 11.2.5.6 Kikosi cha Zimamoto na Uokozi (KZU)

Kikosi kina jukumu la kutoa huduma za haraka na za kitaalamu katika kuhakikisha usalama wa wananchi na mali zao. Vile vile, kutoa elimu na kuhamasisha jamii kuhusu njia bora za kuzuia matukio ya ajali za moto na jinsi ya kukabiliana na majanga. Kwa mwaka 2025/2026, Kikosi kimepanga kutekeleza miradi miwili ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 25.76 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 15.46 bilioni zimepangwa na kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

### a. Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari

Mradi huu una lengo la kuimarisha makaazi mazuri kwa askari wake ambapo mazingira hayo yatawawezesha kutekeleza majukumu yao kwa ufanisi zaidi, mradi pia utapunguza changamoto za makaazi kwa maaskari na kuongeza hamasa katika kazi zao. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.80 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 4.27 bilioni sawa na asilimia. 237 zimepatikana kutoka serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukamilisha ujenzi wa Ofisi Kuu Chanjaani - Pemba; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 5 | 5 | Tenda imekamilika na mkataba umeshasainiwa kwa ajili ya kuanza ujenzi. |
| Ujenzi wa Kituo cha zimamoto na uokozi Finya - Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 5 | 5 | Tenda imekamilika na mkataba umeshasainiwa kwa ajili ya kuanza ujenzi. |

### b. Mradi wa Ununuzi wa Magari na Vifaa vya Kuzimia Moto

Mradi una lengo la kuimarisha uwezo wa Jeshi la Zimamoto na Uokoaji, kuhakikisha kuwa kuna vifaa vya kisasa na vya kutosha ili kuokoa maisha na mali za wananchi pindi inapotokezea ajali ya moto na majanga mengine. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 22.76 bilioni (TZS 2.55 bilioni kutoka Serikalini na TZS 20.21 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 13.66 bilioni (TZS 1.53 bilioni kutoka Serikalini na TZS 12.13 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 14.23 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo sawa na asilimia 104 zimepatikana kutoka kwa  Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa gari mbili na vifaa vya kutolea huduma za uokozi na uzimaji moto. | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Vile vile mkataba wa ununuzi wa gari mbili ushasainiwa na tayari utekelezaji wake umeanza. |
| Ununuzi wa vifaa na magari ya utoaji huduma za uokozi na uzimaji moto; | Idadi ya gari zilizonunuliwa | 20 | 19 | 95 | Kikosi kimepokea gari 19. Gari 8 za kuzimia moto (Municipal), gari 6 Raped Vehicle (RV), Gari 2 za Ngazi (ladder), gari 3 za kubebea maji (Water Buzer), |
| Ununuzi wa boti za uokozi kwa maeneo ya visiwa vidogo vidogo; | Asilimia ya ununuzi uliofikiwa | 1 | 1 | 100 | Boti ya kuzimia moto 1 (Fire Boat) imenunuliwa. |
| Kutoa mafunzo kwa wapiganaji. | Idadi ya wapiganajai waliopewa mafunzo | 1000 | 24 | 2.4 | kwa upande wa mafunzo jumla ya wapiganaji wanne walipatiwa mafunzo nchini Austria na wapiganaji 20 walipatiwa mafunzo ndani ya Zanzibar juu ya ufundi wa magari pamoja na usimamamizi wake. |

### 11.2.6 Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais

Ofisi ina jukumu la kusimamia utekelezaji wa maeneo mtambuka ikiwemo mazingira, watu wenye ulemavu, Ukimwi na udhibiti wa madawa ya kulevya. Ofisi hii imepewa dhamana ya kuhakikisha mshikamano wa kitaifa, ushirikiano wa kisera na kushirikiana na Taasisi nyingine za Serikali. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepangiwa kutekeleza programu moja na miradi miwili ya maendeleo kwa gharama ya TZS 5.91 bilioni (TZS 4.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 1.41 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 3.55 bilioni zimepangwa na kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

**i. Programu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi**

Programu hii ina lengo la kuziwezesha Serikali za Mitaa kuweza kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi. Kwa mwaka 2025/2026, program hii imepangiwa kutumia TZS 598.22 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 358.93 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026 jumla ya TZS 280.46 milioni sawa na asilimia 78 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatzo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa miongozo na vitini vya kutoa elimu ya mabadiliko ya tabianchi kwa Serikali za Mitaa; | Asilimia ya muongozo iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Jumla ya tripu 169 za kokoto zimewekwa kwenye mabwawa. |
| Kuzijengea uwezo Serikali za Mitaa na jamii juu ya uhimili wa athari za mabadiliko ya tabianchi katika maeneo yao | Idadi ya Mamlaka za Serikali za Mitaa zilizojengewa uwezo | 11 | 11 | 100 | Mafunzo ya uhimili wa athari za mabadiliko ya tabianchi yametolewa kwa baraza ya miji yote Unguja na Pemba |
| Kuandaa mfumo wa kuripoti taarifa za athari za mabadiliko ya tabianchi kwa Unguja na Pemba. | Asilimia ya uandaaji wa mfumo iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Hatua za awali za maatarisho ya mfumo zimeanza kufanyika ambapo jumla ya kompyuta 4 zimenunuliwa kwa ajili ya mfumo. |

#### a. Mradi wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani

Mradi umeanza mwaka 2022 hadi mwaka 2027. Mradi huu una lengo la kuhamasisha na kuwawezesha wananchi kuelewa umuhimu wa kuhifadhi miti na misitu iliyopo, kupanda na kuikuza miti ili kuimarisha mazingira kwa ajili ya kizazi cha sasa na cha baadae. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 600 milioni kutoka serikalini zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa vipindi vya TV, redio, mitandao ya | Idadi ya vipindi vya TV vulivyorushwa hewani | 2 | 1 | 50 | Shughuli zilizofanyika zimetumia fedha za bajeti ya mwaka 2024/2025 |

### 11.2.7 Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais- Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi

Ofisi ina dhamana ya kusimamia, kuratibu na kufuatilia shughuli za Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar, sambamba na kuratibu masuala ya Muungano (Zanzibar na Tanzania bara) kwa kufuata misingi ya Katiba na Sheria pamoja na kulinda haki za binadamu na ushirikishwaji wao. Kwa mwaka 2025/2026, Ofisi imepanga

kutekeleza programu moja na miradi miwili itakayogharimu jumla ya TZS 37.65 bilioni (TZS 2.65 bilioni kutoka Serikali TZS 35.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 22.59 bilioni zilipangwa (TZS 1.59 bilioni kutoka Serikalini na TZS 21.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na kutekeleza programu na miradi ya maendeleo ifuatayo:-

**a. Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu (TASAF III)**

Programu inatekelezwa kwa lengo la kuziwezesha Kaya zenye kipato cha chini sana kuongeza vipato vyao, fursa na uwezo wa kugharamia mahitaji muhimu ya kibinadamu hasa chakula, afya na elimu. Programu inakusudia kutekeleza miradi iliyoibuliwa na wananchi katika elimu, afya na ajira za muda mfupi. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kiasi cha TZS 35.10 bilioni (TZS 100.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 35.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 21.06 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 60.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 21.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2025, jumla ya TZS 676.94 milioni sawa na asilimia 3 zimepatikana (TZS 75 milioni kutoka Serikalini na TZS 601.94 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuratibu shughuli za TASAF Unguja, Pemba na Tanzania bara | Idadi vikao vya kuratibu shughuli za Mpango. | 4 | 4 | 100 | Watendaji walihudhuria vikao vya kuratibu shughuli za Mpango na uwasilishaji wa nyaraka za Mpango. |
| Kufanya ufuatiliaji na tathmini ya mradi wa TASAF | Idadi ya shughuli (vipengele vya mradi) zilizofuatiliwa | 3 | 3 | 100 | Shughuli zilizopangwa kufuatiliwa na kufanyiwa tathmini,Uhaulishaji wa fedhaa kwa walengwa, utekelezaji wa miradi ya ujenzi na Mpango wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya. |

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa mikutano ya Kamati ya Uongozi na Kamati ya Wataalamu | Idadi ya mikutano iliyotekelezwa | 2 | 2 | 100 | |
| Ujenzi wa dakhalia ya wavulana na uzio wa kuzunguka dakhalia la wasichana katika Skuli ya Kizimkazi Dimbani | Asilimia ya ujenzi wa uzio iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi wa Uzio na sehemu ya kula umekamilika. |
| Ujenzi wa uzio katika kituo cha afya Donge Vijibweni na Uzi Ng'ambwa | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa Donge vijibweni | 100 | 100 | 100 | |
| | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa uzi Ng'ambwa | 100 | 100 | 100 | |
| Ujenzi wa Madarasa 6, matundu ya vyoo 10 na ofisi ya walimu shehia ya Kendwa. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | |
| Ujenzi wa Madarasa 5, maabara, ofisi ya walimu katika Shehia ya Chwaka Mtangani. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | |
| Ujenzi wa madarasa 3 na maabara Shehia ya Mtangani. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | |
| Ujenzi wa madarasa 7, ofisi ya Mwalimu Mkuu na ofisi ya walimu wengine (staff room) Shehia ya Dodo. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | |
| Ukarabati wa Barabara (ujenzi wa Daraja, uwekaji wa calvet 2 na uwekaji wa kifusi) shehia ya Kilindi. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 100 | 100 | |
| Kuhaulisha fedha kwa Kaya za walengwa wa TASAF | Idadi ya kaya zilizolipwa | 27886 | 27838 | 99.8 | Kaya 48 hazikujitokeza kipindi cha malipo kwa Unguja na Pemba |
| Utekelezaji wa mpango wa kuweka akiba na kukuza uchumi wa kaya | Idadi ya kaya zilizolipwa | 224 | 224 | 100 | Jumla ya kaya 224 zimepatiwa ruzuku ya uzalishaji na kujiendeleza katika shughuli na miradi yao ya uzalishaji |
| Malipo ya walengwa katika utekelezaji wa miradi ya kutoa ajira za muda | Idadi ya kaya zilizolipwa | 1661 | 1661 | 100 | Dirisha mmoja la malipo limefanyika kwa walengwa waliotekeleza miradi ya kutoa ajira za muda kwa shehia 10 za Pemba |

## b. Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha na kuweka mazingira mazuri ya makaazi ya Mheshimiwa Makamu wa Pili wa Rais na wafanyakazi ili kuwa na makaazi yanayoendana na nyadhifa zao. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.2 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 756.41milioni sawa na asilimia 63 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais katika eneo la Tibirinzi Chake Chake - Pemba. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 49 | 49 | Kazi zilizo fanyika ni kumalizia jengo kuu,kuweka miundombinu ya maji,umeme na mifumo ya Tehama |

## 11.2.8 Wizara ya Afya

Wizara ya Afya ina jukumu la kusimamia afya za wananchi kwa kuhakikisha huduma za kinga na tiba zinapatikana pamoja na kutoa maelekezo ya kitaalamu juu ya afya ili kuwa na jamii yenye afya bora. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza programu kumi na miradi mitatu ya maendeleo yenye thamani ya jumla ya TZS 188.24 bilioni (TZS 83.45 bilioni kutoka Serikalini na TZS 104.79 bilioni kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 114.14 bilioni(TZS 51.27 bilioni kutoka Serikalini na TZS 62.87 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepangwa na kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

### i. Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar

Programu hii ina lengo la kumaliza maradhi ya malaria hapa Zanzibar kwa mambukizi ya ndani. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 7.27 bilioni (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 6.27 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 4.36 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 600 milioni kutoka Serikalini na TZS 3.76 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 8.72 bilioni sawa na asilimia 200 (TZS

535.11 milioni kutoka Serikalini na TZS 8.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo ) zimepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| **Shughuli iliyopangwa** | **Kiashiria** | **Shabaha** | **Utekelezaji Halisi** | **Asilimia ya Utekelezaji** | **Maelezo** |
|---|---|---|---|---|---|
| Utumiaji wa taarifa na ufuatiliaji wa wagonjwa hospitalini, vituoni na majumbani | Asilimia ya matumizi iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Jumla ya wagonjwa wa malaria 7,381 (Unguja – 6,916 na Pemba - 521) walioripotiwa kuwa na vimalea vya Malaria, kati ya washukiwa wa malaria 492,513 (394,014 Unguja na 98,499 Pemba) waliochunguzwa malaria pia kati ya waliogundulika wagonjwa 5 wamefariki dunia.<br><br>Jumla ya wagonjwa 5,728 (Unguja – 5,207 na Pemba - 521) wamefuatiliwa kutoka ngazi ya familia (majumbani). |
| Uratibu na usimamizi wa uendeshaji wa shughuli za malaria | Asilimia ya shughuli za uendeshaji na uratibu zilizofikiwa | 100 | 93 | 93 | Maeneo (foci) 110 (74 Unguja na 36 Pemba) yenye maambukizi ya malaria, yalifuatiliwa kwa kina ili kubaini vihatarishi katika ngazi za shehia. Upulizaji wa dawa za majumbani (IRS) ulitekelezwa katika Wilaya 8 kwa Shehia 63, jumla ya nyumba 1,737 (1,476 Unguja na 261 Pemba) zilipuliziwa dawa. |
| Ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa wa malaria | Asilimia ya ufuatiliaji wa mwenendo wa ugonjwa iliyofikiwa | 100 | 89 | 89 | Jumla ya visa 4,100 kati ya 4,608 viliweza kuripotiwa ndani ya masaa 24 kutoka vituo 372 vya serikali na binafsi. Jumla ya mbu 3,359 (3,330 Unguja na 229 Pemba) jamii ya Anopheles walikamatwa kati yao 777 walikamatwa ndani ya majumba (752 Unguja na 25 Pemba) pia mbu 1,711 walikamatwa nje (1,551 Unguja na 160 Pemba)<br><br>Wataalamu wa maabara 60 (40 Unguja na 20 Pemba) wamepatiwa mafunzo elekezi juu ya uchunguzi thabiti wa vimelea wa njia ya hadubini na mafunzo ya kipimo cha haraka walipatiwa Maafisa 500 (300 Unguja na 200 Pemba) katika Hospitali na Vituo vya Afya vya Binafsi na Serikali 346 (210 Unguja na 136 Pemba) pia ufuatiliaji wa MRDT ulifanyika katika vituo vya Serikali 322 kwa njia ya Hadubini na matokeo yanaonesha maambukizi yamebaki chini kwa asilimia 0.9 kwa vituo vya Serikali na 0.7 Binafsi huku maambukizi ya jumla yakiwa ni asilimia 1.62 |
| Udhibiti wa mbu wanaoeneza ugonjwa wa malaria. | Asilimia ya udhibiti iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Jumla ya nyumba 1,765 (981 Unguja na 784 Pemba) kati ya 1,862 (1,032 Unguja na 830 Pemba) zilizopigwa dawa ya kuuwa mbu wa malaria sawa na asilimia 95.<br><br>Zoezi la kuuwa viluilui linaendela kati ya mazalia 798 yaliyogunduliwa. Na kati ya mazalia hayo, mazalia 110 yalikuwa na vilului vya malaria na yametibiwa.<br><br>Jumla ya wanafunzi wa bweni wa Skuli ya Mwambeni 524 (323 wanawake na 201 wanaume), kutoka Wilaya ya Mjini 505 na Wilaya ya Kusini 70 walipimwa na kutibiwa (Track, test and Treat), ambapo watu 7 walibainika kuwa na vimalea vya malaria na kupatiwa matibabu |

### ii. Programu ya Kudhibiti Maradhi ya UKIMWI, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma

Programu hii ina lengo la kupunguza kasi ya maambukizi ya virusi vya Ukimwi, kupunguza vifo vitokanavyo na maradhi ya kifua kikuu, Homa ya Ini na kupunguza Maambukizi ya Ukoma. Kwa mwaka 2025/2026, jumla ya TZS 5.85 bilioni zimetengwa kutekeleza programu hii (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.85 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 3.50 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 600 milioni kutoka Serikalini na TZS 2.90 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 2.33 bilioni (TZS 379 milioni kutoka Serikalini na TZS 1.95 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo), sawa na asilimia 67 ya lengo la TZS 3.50 bilioni zimepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha huduma za matibabu kwa watu na makundi maalum wanaoishi na VVU | Idadi ya wanawake wanaofanya biashara ya ngono waliopimwa virusi vya UKIMWI iliofikia | 4,845 | 4,094 | 84.5 | Lengo limefikiwa kutokana na ushirikiano na Asasi zisizo za kiserikali kwa kutumia njia mbali mbali za kuwapima ikiwemo jipime mwenyewe, kupima kwa kawaida katika vituo vya Afya. |
| | Idadi ya watu wanaojidunga dawa za kulevya kupitia sindano waliopimwa virusi vya UKIWI na kujua hali zao | 1,692 | 1,935 | 100 | |
| | Idadi ya wanaume wanaojamiiana na wanaume wenzao waliopimwa virusi vya UKIMWI na kujua hali zao | 3,069 | 2,812 | 91.6 | |
| | Idadi ya wanawake wanaofanya biashara ya ngono waliofikiwa na kupatiwa huduma za kujikinga na maradhi | 5,002 | 4,132 | 82.6 | Kwa kushirikiana na taasisi zisizo za kiserikali tumeweza kuwafikia kwenye maeneo maalum ikiwemo Baa na vijiwe maalum na kuwapatia huduma |
| | Idadi ya wanaojidunga waliofikiwa na kupatiwa huduma za kujikinga na maradhi | 1,735 | 1,942 | 100 | |
| | Idadi ya wanaume wanaojamiiana na wanaume wenzao waliofikiwa na kupatiwa huduma za kujikinga na maradhi | 3,102 | 2,821 | 91.3 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha utoaji wa huduma za kinga na tiba ya homa ya ini katika jamii | Idadi ya mikutano ya kuelimisha jamii njia za maambukizi, dalili na kinga za Homa ya Ini B na C | 1,500 | 1,057 | 70.5 | Changamoto ya kifedha imepelekea kutoweza kufanikisha vyema kufanya mikutano ya kuelimisha jamii na kutoa mafunzo kwa watoa huduma za afya, chanjo kwa ajili ya kuwakinga watu waliomo hatarini zaidi kupata maambukizi ya homa ya ini B zimenunuliwa. Chagamoto ya jumla iliyopo ni kukosekana kwa chanjo ya kumkinga mtoto aliyezaliwa na mama mwenye maaambukizi ya virusi vya homa ya ini B (Monovalent vaccine) na dawa za kufubaza virusi vya homa ya ini B (Tenofovir 300mg) |
| | Idadi ya watoa huduma za Afya walopatiwa mafunzo ya upimaji na utambuzi wa mapema wa homa ya ini B na C | 50 | 0 | 0 | |
| | Idadi ya vitendashi na chanjo ya homa ya ini B vilivyonunuliwa | 1,250 | 625 | 50 | |
| Uhamasishaji na kuongeza uelewa kwa jamii juu ya kinga dhidi ya maambukizi ya Ukimwi, magonjwa ya kujamiana, homa ya ini, kifua kikuu na ukoma | Idadi ya vipindi vya redio na televisheni vilivyoruka | 26 | 20 | 77 | Vipindi vilirushwa kupitia ZBC TV na Radio, Asaalam Radio, Zenji FM, Radio Adhana, na Al-noor FM Radio. |
| | Idadi ya kaguzi katika klabu za afya za Skuli zilizofanyika | 36 | 14 | 38.9 | Jumla ya klabu za Afya za Skuli 14 zilitembelewa na kukaguliwa. Klabu zote zinahitaji kuboreshwa nyenzo za kufanyia kazi kwa ajili ya kutolea elimu ya afya. |
| | Idadi ya kaguzi elekezi katika Asasi za Vijana zinazotoa huduma za Virusi vya Ukimwi na Kifua Kikuu | 5 | 4 | 80 | Katika kota ya pili hazikufanyika ipasavyo kutokana na changamoto ya kifedha |
| | Idadi ya mikutano katika jamii na vituo vya afya iliyofanyika | 16 | 13 | 81.2 | Jumla ya watu 816 walipewa elimu ya afya, na 496 walichunguzwa Kifua Kikuu ambapo watu 39 walihisiwa kuwa na dalili za Kifua kikuu. Pia, kwenye mikutano hiyo, jumla ya vijana 260 walipewa elimu ya afya, na kufanyiwa upimaji wa Homa ya Ini na virusi vya UKIMWI katika vituo vya Rahaleo, Magirisi, Mahonda na Bwejuu . |
| Uratibu na usimamizi wa kazi za programu ya | Idadi ya mikutano ya timu ya kitaaluma iliyofanyika | 1 | 1 | 100 | Mkutano wa utekelezaji umefanyika ambapo hufanyika kwa mwaka mara moja |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| huduma shirikishi ya homa ya ini, ukimwi, kifua kikuu na ukoma | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 0 | 0 | Vitendea kazi havijanunuliwa kwa sababu ya ukosefu wa fedha kutoka serikalini |
| Kufanya uhamasishaji kwa wanaume juu ya upimaji wa Virusi vya Ukimwi wakati wa mahudhurio ya Kliniki | Asilimia ya kazi iliyofikiwa | 100 | 26 | 26 | Jumla ya wanaume 66 walihamasishwa kupitia Mkutano mmoja wa kuhamasisha upimaji wa VVU katika kliniki ya mama na mtoto kwa Unguja na Pemba. |
| Kuimarisha huduma za kupunguza maambukizi ya VVU kutoka kwa mama kwenda kwa mtoto. | Idadi ya mikutano iliyofanyika | 1 | 1 | 100 | Jumla ya watoa huduma 54 katika kliniki ya mama na mtoto juu ya kumkinga mtoto na maambukizi ya VVU |
| | Idadi ya mikutano ya ukaguzi elekezi kwenye vituo vya afya vinavyoripoti wateja wengi wa maambukizi ya VVU na katika jamii iliyofanyika | 2 | 2 | 100 | Mikutano ilifanyika katika vituo 18 vinavyoibua wateja wengi wa VVU, ambapo mama wote wajawazito wanapata huduma za upimaji VVU, kaswende na homa ya ini B katika hudhurio la kwanza ambavyo ni Mwembeladu, Rahaleo, Ziwani, Police, Selem, Chuini, KMKM, Kianga, Chukwani, Magogoni, Magirisi, Fuoni Kibondeni, Kivunge, Kendwa, Nungwi, B/Misufini, Mahonda, Mwera na Uzini |
| | Idadi ya Mafunzo yaliyofanyika kwa vipimo vya pamoja vya VVU, Kaswendwe na Homa ya Ini B | 1 | 1 | 100 | Mafunzo elekezi yamefanyika kupitia vituo vinavyotoa huduma za mama na mtoto. Jumla ya watoa huduma 57 walifikiwa (36 Unguja, 21 Pemba) kuhusu umuhimu wa upimaji (VVU, Kaswende na Homa ya Ini B) |

### iii. Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi Mama na Mtoto

Programu hii ina lengo la kupunguza vifo vitokanavyo na uzazi pamoja na vifo vya watoto walio chini ya umri wa miaka mitano. Kwa mwaka 2025/2026, jumla ya TZS 6.28 bilioni zimetengwa (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.28 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 3.76 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 600 milioni kutoka Serikalini na TZS 3.16 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 287 milioni sawa na asilimia 8 zimepatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha matibabu jumuishi ya watoto chini ya miaka mitano pamoja na kuimarisha miongozo ya matibabu ya watoto; | Asilimia ya kazi ya uimarishaji iliyofikiwa | 100 | 0 | 0 | Mafunzo hayakufanyika kutokana na ukosefu wa fedha. |
| | Idadi ya miongozo iliyoimarishwa | 1 | 1 | 100 | Muongozo wa lishe wa mama, watoto wachanga, wadogo na vijana baleghe umefanyiwa mapitio |
| | Idadi ya watoto waliopewa huduma ya matone ya vitamin A | 260,917 | 236,672 | 91 | Zoezi la utaoji wa huduma ya matone ya vitamin A limefanyika na watoto 236,672 wenye umri wa miezi 6-59 wamefikiwa |
| | Idadi ya watoto waliopewa huduma ya matibabu ya utapimalo wa kadiri kupitia jiko (PD Hearth) darasa kwenye jamii | 170 | 170 | 100 | Jumla ya watoto 170 walipatiwa huduma ya matibabu ya utapiamlo na 110 hadi sasa wapo vizuri kadiri wanapofanyiwa ufuatiliaji na kupewa elimu ya upikaji wa vyakula vya lishe. |
| Kuimarisha huduma za mama na watoto chini ya umri wa miaka mitano na wachanga; | Asilimia ya kazi ya uimarishaji iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Shughuli za ukarabati wa hospitali 2, (Mwera Pongwe kwa Unguja na Vitongoji kwa Pemba) zilifanyika kwa ajili ya uimarishaji wa huduma ya watoto wachanga wenye mahitaji maalum (NICU). Pia vifaa mbali mbali vilisambazwa kwa ajili ya kuimarisha huduma za mama na mtoto kama vile CPAP mashine, phototherapy, warmer, doppler, ambu bag, drums, penguine, speculum na baby cort |
| Kutoa elimu kwa vijana juu ya athari za mimba za utotoni | Idadi ya vijana waliopatiwa elimu | 16,734 | 14,852 | 89 | Vijana wenye umri wa miaka kati ya 10 hadi 24 wamepatiwa elimu husika katika maeneo ya vituo 15 vya huduma rafiki kwa vijana (Unguja 10,443 na Pemba 4,410) |
| | Idadi ya kina mama wajawazito waliohudhuria kliniki ya kina mama kwa mara ya kwanza | 65,390 | 52,901 | 80 | Kinamama wapatao 52,901 wamehudhuria kliniki kwa mara ya kwanza na kufanyiwa vipimo mbali mbali kama Damu, presha, VVU na hepatatis. |
| Ukarabati wa vituo vya afya kwa vijana, ununuzi wa chanjo, dawa na vifaa tiba; | Idadi ya vituo vya huduma rafiki kwa vijana vilivyokarabatiwa | 2 | 2 | 100 | Vituo vya kutoa huduma kwa vijana rafiki vya Kianga na Matemwe vimekarabatiwa |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha utoaji wa huduma za chanjo ya mama na mtoto; | Idadi ya watoto waliopatiwa chanjo | 55,176 | 49,154 | 89 | Watoto chini ya umri wa miaka 5 wamepatiwa chanjo dozi ya tatu ya Penta kwa Unguja na Pemba |
| Kuimarisha utoaji wa huduma za afya ya uzazi na kupunguza matatizo yatokanayo na vifo vya mama na mtoto; | Asilimia ya vifo vya akina mama vitokanavyo na uzazi vilivyofanyiwa uhakiki | 100 | 38 | 38 | Vifo vya mama 25 vimehakikiwa na kugundua sababu ni kifafa cha mimba, kutokwa na damu nyingi baada ya kujifungua, kuchanika kwa fuko la uzazi, kumwagika kwa damu kabla ya kujifungua, matatizo ya dawa ya usingizi na mshituko wa moyo |
| | Idadi ya vifo vya watoto wachanga vilivyofanyiwa uhakiki | 626 | 593 | 95 | Vifo vya watoto wachanga 593 vimehakikiwa na kugundua sababu ni kupata shida ya kupumua, kupata maambukizi kwa watoto wachanga, kuzaliwa na ulemavu, kumeza uchafu wakati wa kuzaliwa na kupata rangi ya njano |
| | Idadi ya kina mama wajawazito watakaohudhuria kliniki ya kina mama kwa mara ya kwanza | 65,390 | 52,901 | 80 | Kina mama waliohudhuria kliniki kwa mara ya kwanza na kufanyiwa vipimo mbali mbali kama wingi wa damu, kundi la damu, presha, VVU hali ya mkojo na hepatatis. |
| Kufanya majadiliano kwa jamii juu ya wajibu wao katika huduma za uzazi wa mpango; | Idadi ya wateja waliopatiwa huduma za uzazi wa mpango | 28,837 | 22,864 | 79 | Takribani jumla ya wateja wapya 22,864 (Pemba 5,205 na Unguja 17,656) wamejiunga na huduma za uzazi wa mpango. |
| Ukarabati na uwekaji wa vifaa vituo vya mkono kwa mkono vitakavyosaidia kujikinga na ukatili wa kijinsia na ukatili dhidi ya watoto katika Mikoa mitatu; | Idadi ya vituo vya Afya vilivyokarabatiwa | 5 | 5 | 100 | Ukarabati umefanyika katika vituo vya mkono kwa mkono katika mikoa mitatu ya Unguja. Mkoa wa kusini Kitogani na Mwera Pongwe, Mkoa wa Kaskazini Kivunge na Mkoa wa Mjini Magharibi Ijitimai na Mbuzini |

### iv. Programu ya Kuimarisha Huduma za Mama na Mtoto

Programu ina lengo la kuimarisha huduma za afya ya Msingi kwa mama na mtoto. Programu inatekelezwa na Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa jumla ya TZS 25.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 15.0 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha miundombinu ya afya ya mama na mtoto | Asilimia ya uimarishaji miundo mbinu iliofanyika | 100 | 25 | 25 | Katika shughuli hii programu ilipanga kujenga nyumba za wafanyakazi katika hospitali za wilaya Kivunge na Micheweni. Hata hivyo ujenzi wa Nyumba haujaanza isipokua upo katika hatua za awali, ambapo hatua za uthamini zilishafanywa, na ripoti za tathmini hizo zipo kwenye ofisi kuu za WORLD BANK kwa hatua ya kusubiria no Objection. |
| Ununuzi wa dawa na vifaa tiba vya huduma ya afya ya mama na mtoto; | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Wizara imeshapokea madawa na vifaa tiba vya huduma za mama na mtoto kupitia (Wakala wa Bohari Kuu ya Dawa) kutoka UNICEF.<br><br>Aidha, asilimia iliyobakia ya dawa na vifaa tiba vya huduma ya afya ya mama na mtoto vimezuiiliwa baada ya bohari kujaa na pia kutokua na matumizi makubwa kwa wakati huu. |
| Kuimarisha uratibu na usimamizi wa programu | Asilimia ya shughuli za uratibu na usimamizi zilizofanyika | 100 | 90 | 90 | *Social impact* uanzishaji wa kamati za GRM, kuandaa mfumo wa eGRM na uhamasishaji kwa jamii kwa maeneo ya ujenzi wa vituo vya afya ya msingi kama vile Jang'ombe na Fuoni; na maeneo ya ujenzi wa nyumba za wafanyakazi kama vile Micheweni na Kivunge. |
| Ujenzi wa vituo vya afya ya msingi; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa kituo cha Afya Fuoni | 100 | 25 | 25 | Ujenzi wa kituo cha afya Fuoni haujaanza isipokua upo katika hatua za awali, ambapo hatua za uthamini zilishafanywa, na ripoti za tathmini hizo zipo kwenye ofisi kuu za WORLD BANK kwa hatua ya kusubiria (no Objection). |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa kituo cha Afya Jang'ombe | 100 | 25 | 25 | Ujenzi wa kituo cha afya Fuoni haujaanza isipokua upo katika hatua za awali, ambapo hatua za uthamini zilishafanywa, na ripoti za tathmini hizo zipo kwenye ofisi kuu za WORLD BANK kwa hatua ya kusubiria (no Objection). |
| Kusomesha Madaktari wa fani maalum | Idadi ya wafanyakazi watakao kwenda masomoni | 30 | 26 | 87 | Kwa sasa jumla ya wafanyakazi 26 wanaendelea na masomo kwenye vyuo mbali mbali kwa kada za huduma za mama na mtoto (gynecology, paediatriction, nursing, critical care, nutrition and anesthesia. Kwa mwaka huu Wizara imepanga 4 ambao bado hawajakwenda, lengo la mradi kutimiza watu 30. |

### v. Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya

Programu hii ina lengo la kuimarisha miundombinu itakayosaidia utoaji wa huduma za afya zenye ubora na viwango vinavyokubalika Kitaifa na Kimataifa. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 72.35 bilioni (TZS 35.35 bilioni kutoka Serikalini TZS 37.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 43.41 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 21.21 bilioni kutoka Serikalini na TZS 22.20 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 26.41 bilioni (TZS 9.43 bilioni kutoka Serikalini na TZS 16.98 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 61 zimepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzisha Taasisi ya Afya ya Jamii - Binguni | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Hatua ya manunuzi ilofikiwa ni kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya kuandaa michoro, na usimamzi wa ujenzi unaendelea. |
| Kuendelea na ujenzi wa hospital ya wagonjwa wa afya ya akili eneo la Pandani - Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi umekamilika na hospitali imeshaanza kutoa huduma. |
| Ujenzi wa Hospitali ya Mkoa katika eneo la Kitogani na Mahonda | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Mradi haujaanza |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Mkandarsi ameshapatikana na ujenzi umeshaanza kwa hatua za awali |
| Ujenzi wa Hospitali ya Saratani – Binguni | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Mchakato wa kumpata mshauri elekezi umefikia hatua za kusaini mkataba |
| Ujenzi wa kituo cha kudhibiti sumu - Tunguu | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Kwa sasa Mradi upo kwenye hatua ya uandaaji wa michoro. |
| Ujenzi wa Maabara ya Mkemia Mkuu Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Kwa sasa Mradi upo kwenye hatua ya uandaaji wa michoro. |
| Ujenzi wa Maabara katika Mamlaka ya Dawa, Chakula na Vipodozi Chamanangwe Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Mchakato wa kumpata Mkandarasi umefikia hatua za kusaini mkataba |
| Kutekeleza Mradi wa 'Electronic Health Network' | Asilimia ya kazi iliyofanyika | 100 | 0 | 0 | Mradi Umesita kutokana na wafadhili kuondoka. |
| Ujenzi wa Ofisi ya Wizara ya Afya Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Michoro na BOQ zimekamilika |
| Kuimarisha mifumo ya kidigitali kwa afya katika ngazi zote. | Asilimia ya uimarishaji wa mifumo iliyofikiwa | 100 | 35 | 35 | Kuandaa mahitaji ya ununuzi wa vifaa vya TEHAMA zikiwemo komputa 250 kwa vituo 14 vya mradi wa Ukarabati na ujenzi wa vituo vya Afya. Aidha mradi upo katika michakato ya manunuzi ya vifaa hivyo. Baada ya ununuzi Mradi umelenga kutoa mafunzo kwa watumiaji |

## vi. Programu ya Ukarabati ya Vituo vya Afya ya Msingi

Programu hii ina lengo la kuimarisha afya ya msingi kwa kuimarisha miundombinu ya vituo vya afya ya msingi ili viweze kutoa huduma zenye kiwango na kuimarisha afya ya jamii. Programu hii inatekelezwa na Serikali na kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa jumla ya TZS 20.00 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 12 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 15.50 bilioni sawa na asilimia 129 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa vituo 18 vya afya ya Msingi. | Idadi ya vituo vilivyojengwa | 18 | 15 | 83 | |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Nungwi iliyofikiwa | 100 | 75 | 75 | Ujenzi umefikia uwekaji wa tarazo, uvutaji wa waya. |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Tunguu iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Wanamalizia kazi za nje na marekebisho madogo madogo ya mwisho. |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Sebleni iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Mpendae iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Konde i iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Ujenzi umefikia uwekaji wa tarazo, uvutaji wa waya. |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Jadida iliyofikiwa | 100 | 97 | 97 | Ujenzi umefikia hatua za umaliziaji wa kazi za nje |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Chonga iliyofikiwa | 100 | 75 | 75 | Ujenzi umefikia uwekaji wa tarazo na uvutaji wa waya za umeme. |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Mahonda iliyofikiwa | 100 | 99 | 99 | Ujenzi umefikia hatua za umaliziaji wa matengenezo madogo madogo (final tourch) |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Mtambile iliyofikiwa | 100 | 35 | 35 | Ujenzi wa matofali na uwekaji wa jamvi la zege la ghorofa ya kwanza umekamalika. |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Kiuyu Minungwini iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Kazi zilizofanyika ni uwekaji wa umeme, milango na madirisha. Hatua zinazoendelea ni ujenzi wa uzio, na kupaka rangi mkono wa pili |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Mtoni Basra iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Ujenzi umefikia hatua ya plasta, fremu za milango, uwekaji umeme ndani ya jengo |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Welezo iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Ujenzi upo katika hatua ya kujaza kifusi ndani ya msingi (foundation) |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya maziwa ng'ombe iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Ujenzi umefikia hatua ya uwekaji wa plasta, fremu za milango, uvutaji wa waya za mifumo ya ndani ya jengo |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Kojani iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Ujenzi umefikia hatua ya ujenzi wa kuta za tofali katika ghorofa ya kwanza |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Tumbatu iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Ujenzi umefikia hatua ufungaji wa taa na vifaa vya umeme na umaliziaji wa kazi za nje. |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Mombasa iliyofikiwa | 100 | 0 | 0 | Ujenzi upo katika hatua za mchakato wa zabuni |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya kiungoni iliyofikiwa | 100 | 40 | 50 | Ujenzi umefikia hatua ya kumwaga zege katika jamvi la gorofa ya kwanza. |
| Ujenzi wa Vituo vya Afya 35 vya Dispensary-MEHECO. | Idadi ya vituo vilivyojengwa | 35 | 8 | 22.6 | |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Dispensary Kizimbani iliyofikiwa | 100 | 55 | 55 | Ujenzi wa nguzo na beam umemalizika. kazi zinazoendelea ni ujenzi wa paa |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Dispensary Tomondo iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Ujenzi upo katika hatua ya kazi za kumalizia (finishing work) |
| | Asilimi iliyofikiwa a ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Dispensary Bwefum iliyofikiwa | 100 | 60 | 60 | Ujenzi umekamilika katika harua ya msingi, nguzo, beam na paa na sasa upo katika hatua za finishing |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Dispensary uzini iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Ujenzi wa tofali na paa umemalizika hatua zilizofikiwa ni *finishing.* |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Dispensary Ukutini iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Ujenzi wa msingi unaendela (foundation work) |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Dispensary Ukunjwi iliyofikiwa | 100 | 80 | 80 | Hatua ya ujenzi iliyofikiwa ni kukamilisha ujenzi wa paa |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Dispensary Pandani iliyofikiwa | 100 | 32 | 32 | Hatua ya ujenzi wa msingi, kusimamisha nguzo na kujenga beams umekamilika hatua za sasa ni ujenzi wa tofali |
| | Asilimia ya ujenzi wa Kituo Cha Afya Dispensary Finya iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Ujenzi wa foundation unaendelea |

### vii. Programu ya Jamii ni Afya

Programu hii ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma za afya karibu na wananchi kwa kuwapelekea wahudumu wa afya katika ngazi ya Shehia ili jamii waweze kusaidia wananchi huduma za awali wanapopata matatizo ya kiafya. Programu inatekelezwa na Serikali na kwa mwaka 2025/2026, programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.20 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.31 bilioni sawa na asilimia 109 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuongeza idadi na kuwajengea uwezo wahudumu wa afya ya jamii; | Idadi ya wahudumu wa afya waliojengewa uwezo | 1,405 | 1,054 | 75 | Jumla ya wahudumu 1054 wamepatiwa mafunzo ya Muda mrefu katika vyuo mbali mbali vya Unguja na Pemba juu ya majuhkumu wanayopaswa kuyafanya katika kazi zao za kwenye jamii, ambao hawa walishatawanywa kwenye jamii.<br>Na pia katika mwezi wa Novemba jumla ya wahudumu wengine wa afya ya jamii 446 wamepelekwa masomoni kwa ajili ya kupata mafunzo, kwa lengo la kuongeza idadi ya wahudumu hao katika jamii baada ya kumaliza mafunzo hayo. |
| Uratibu wa shughuli za wahudumu wa afya ya jamii; | Asilimia ya kazi iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Ulipaji wa posho kwa wahudumu wa afya ya jamii 1,185 walioanza kazi umefanyika. Kuwajengea uwezo wahudumu wa afya wa ngazi ya jamii na ununuzi wa vifaa vya kutolea huduma ikiwemo simu za kukusanyia taarifa. Jumla ya wastani wa TZS 939,826,940 zimeombwa Tume ya Mipango, ila Mpaka sasa hazijapatikana. |
| Kuimarisha ufuatiliaji na tathmini wa kazi za wahudumu wa afya wa jamii. | Asilimia ya kazi ya ufuatiliaji na tathmini iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Jumla ya wasimamizi wa Wahudumu wa Afya ngazi ya jamii 343 walipaswa kupokea posho zao za usimamizi, hata hivyo maposho hayo hawajapokea kutokana na kutopatikana kwa fedha zilizoombwa kutoka Serikalini. Lakini baadhi ya shughuli zilizolengwa wanaendelea kuzifanya. |

### vii. Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya-Zanzibar

Programu hii ina lengo la kuwasaidia wananchi wasiojiweza na makundi maalumu ikiwemo wazee kuanzia miaka 65, wajawazito, watoto chini ya umri wa miaka mitano na wenye hali ya kipato cha chini (Masikini) kwa lengo la kupata huduma za afya kupitia mfuko wa huduma za afya ya Zanzibar ili kuhakikisha hakuna mwananchi aneachwa nyuma katika kupata kuduma za afya. Kwa mwaka 2025/2026, Programu hii imepangiwa jumla ya TZS 1.53 bilioni (TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 528.80 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 600 milioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha huduma za afya kwa watu wasiojiweza na makundi maalumu katika jamii. | Idadi ya kaya wasiojiweza waliosajiliwa | 70,000 | 28,000 | 40 | Mradi huu umetekelezwa kupitia fedha za wafadhili ambapo kwa sasa mama wajawazito amesajiliwa na mfuko wa huduma za Afya kupitia mradi wa ZHSF. Mradi huu upo kwenye Wilaya 2 (Kaskazini B kwa Unguja na Micheweni kwa Pemba) |

### viii. Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mikoa

Programu hii ina lengo la kuimarisha makaazi kwa wafanyakazi ili wawe na utulivu wa kufanya kazi na kuongeza ufanisi na kuwawezesha watoa huduma kupatikana muda wote itakapotokea dharura. Kwa mwaka 2025/2026, jumla ya TZS 3.00 bilioni zimetengwa kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.80 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 7.11 bilioni sawa na asilimia 395 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa nyumba za wafanyakazi katika Hospitali ya Wilaya Mbuzini | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Ujenzi upo katika hatua za awali za kumpata Mshauri elekezi, na kuandaa ramani ya ujenzi |

### ix. Programu ya Kuimarisha Nguvu Kazi

Programu hii ina lengo la kuimarisha upatikanaji wa madaktari bingwa na bobezi ili kuimarisha huduma za matibabu katika ngazi ya Wilaya, Mkoa na Rufaa. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 2.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.20 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.84 bilioni sawa na asilimia 153 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kusomesha Madaktari bingwa. | Idadi ya madaktari waliopelekwa masomoni | 150 | 140 | 93 | Madaktari bingwa waliojiunga na vyuo vikuu kwa mwaka wa masomo 2025/2026, zikiwemo fani za madaktari bingwa wa akina mama, watoto, mifupa, na fani nyengine tofauti katika vyuo mbali mbali. |

### x. Programu ya Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazimmoja

Programu hii ina lengo la kuimarisha huduma katika Hospitali ya Mnazi Mmoja kwa kuimarisha miundombinu ya utoaji wa huduma za afya na ununuzi wa vifaa tiba vya kisasa. Kupitia mradi huu Serikali imepanga kufanya ukarabati mkubwa katika hospitali ya Mnazi Mmoja ili kuiwezesha kutoa huduma zenye kukidhi mahitaji. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 24.40 bilioni (TZS 14.40 kutoka Serikalini na TZS 10.00 kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 14.64 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 8.64 bilioni kutoka Serikalini na TZS 6.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 2.31 bilioni sawa na asilimia 16 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya Ukarabati na utanuzi wa hospitali ya Mnazi Mmmoja | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Mradi huu umefanikiwa kukamilisha mchakato wa kumpata mkandarasi ambae ni China Jiaxi International Economic and Technical Co-Operational Engineering Company Limited. Kazi zinazoendelea kwa sasa ni kuanza maandalizi ya uchimbaji wa mashimo baada ya kukamilisha kuweka site plan ya eneo ili kutengeneza base ya chini. |

### a) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia Binguni

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za afya katika ngazi ya rufaa na kuimarisha miundombinu ya kufundishia taaluma za Afya. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 17.56 bilioni (TZS 1.700 bilioni kutoka Serikalini na TZS 15.86 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 10.53 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 1.02 bilioni kutoka Serikalini na TZS 9.51 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.56 bilioni sawa na asilimia 15 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa majengo ya hospitali ya Binguni | Asilimia ya ujenzi iliyofikwa | 100 | 10 | 10 | Jumla ya kampuni nne zimefanyiwa tathmini ya kupata mshauri elekezi. Wizara imeshatuma ripoti ya tathmini kwa Mfadhili na inasubiri uthibitisho ili kuendelea na hatua zinazofuata. |
| Ufuatiliaji na usimamizi wa ujenzi katika hospitali ya Binguni | Asilimia ya shughuli za usimamizi wa mradi zilizofanyika | 100 | 25 | 25 | Jumla ya vikao 2 vimefanyika juu ya ujenzi wa hospitali ya Binguni |

### b) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Kidigitali

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa taarifa za afya na kuhakikisha taarifa zote za afya zinapatikana kwenye mfumo mama wa taarifa ili ziweze kutumika katika utungaji wa sera, uandaaji wa miongozo na ufanyaji wa maamuzi katika ufuatiliaji wa mienendo ya maradhi kwa lengo la kupunguza vifo na kukabiliana na maradhi ya miripuko. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 600 milioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha miundombinu ya TEHAMA kwenye vituo vya afya | Idadi ya Vituo vya Afya vilivyoimarishwa | 142 | 95 | 67 | Vituo 23 kati ya hivyo (13) Unguja na (10) Pemba. vimeunganishwa na huduma ya Internet kwa kutumia mkonga na vituo 72 vimewekewa *Routers*. Ili kuwezesha vituo hivyo kutumia mfumo wa ZanEMR. |
| Kutoa mafunzo kwa wasimamizi na watumiaji wa mifumo | Idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo | 1,150 | 537 | 47 | Washirki kutoka katika Vituo 95 vya Afya wamepatiwa mafunzo ya matumizi ya mifumo. Idadi hiyo ilitokana na uchache wa vitendea kazi kwa watumiaji wa mifumo ya TEHAMA na ZanEMR jambo linalopelekea kutotumika mfumo wa ZanEMR katika vituo vyote vya Unguja |
| Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA | Idadi ya vifaa vya TEHAMA vilivyonunuliwa | 1,421 | 866 | 60 | Vituo 47 vya Afya ya Msingi (Health Centers) vimepatiwa Laptops 4 na Tablet 1 kila kimoja, na Health Center 5 mpya zimewekewa Laptop 10 na Tablet 1 kila kimoja. Vile vile Zahanati (Dispensaries) 90 zimepatiwa Laptop 2 na Tablets 1 kila kimoja, na vituo 65 viliongezewa tablets 2 kila kimoja. Wasimamizi wa mifumo ngazi ya Wilaya Unguja na Pemba walipatiwa Laptop kila mmoja. Ongezeko hilo na vifaa vya TEHAMA kumeweza kuimarisha matumizi ya mifumo ya Digitali kwenye Vituo vya Afya ya Msingi ikiwa ni pamoja na mtumizi ya Mfuko wa Huduma za Afya. |

### 11.2.9 Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi

Wizara ya Ardhi na Maendeleo ya Makaazi ina jukumu la kuhakikisha kuwa ardhi inatumiwa kwa njia endelevu, kuepuka migogoro na matumizi mabaya ya yanayoweza kuathiri mazingira na maendeleo ya kijamii sambamba na utoaji na uendelezaji wa nyumba na makazi kwa wananchi. Wizara inaratibu sekta ya makaazi ambayo inahusisha ujenzi wa miji na makazi yanayokidhi viwango vya kisasa vya miundombinu na kuweka mazingira mazuri ya kuishi, ikiwa ni pamoja na huduma za jamii, usalama, na mazingira ya afya. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara hii imepanga kutumia kiasi cha TZS 335.69 bilioni kutoka Serikalini kwa utekelezaji wa programu mbili za maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 201.41 bilioni zilipangwa kutumika.

### i. Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo.

Programu hii ina lengo la kujenga nyumba za kisasa na bora ili kukidhi mahitaji ya makazi, hasa katika maeneo yenye ongezeko la idadi ya watu na mahitaji ya nyumba. Programu pia ina lengo la kujenga nyumba za bei nafuu kwa wananchi wa kipato cha chini na cha kati, ili kupunguza changamoto ya uhaba wa makazi. Programu inatekelezwa kwa fedha za Serikali. Kwa mwaka 2025/2026, imepangiwa jumla ya TZS 300.12 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, program imepangiwa jumla ya TZS 180.07 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa nyumba za bei nafuu Chumbuni na maeneo mengine; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 48 | 48 | Ujenzi wa Nyumba 1,095 awamu ya kwanza Chumbuni unaendelea ambapo kazi zinazoendelea ni ujenzi wa majengo 8 ikiwa majengo 6 yameshasimama na yanaendelea kujengwa kuta za matofali na majengo mawili (2) yapo katika hatua za kumalizia (finishing).<br>Kwa upande wa block 'A 09' ujenzi upo katika hatua ya kufunga vifaa vya umeme na maji. Aidha, kwa bloki A11 na bloki A19 ujenzi upo katika hatua ya kujenga msingi. |
| Ujenzi wa nyumba za makaazi na biashara Mkungu Malofa - Chake Chake, Wete - Pemba na Nyamanzi - Unguja; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 27 | 27 | Ujenzi wa jengo la Mkungu Malofa (Mabatini) Phase II unaendelea na upo katika kupiga plasta sehemu ya chini na ujenzi unaendelea ghorofa ya kwanza |
| Ujenzi wa nyumba 209 za makaazi Saateni; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 2 | 2 | Ujenzi wa Nyumba za Makaazi Saateni umeanza kwa hatua za awali ambapo kazi zilizofanyika ni maandalizi ya kumpata Mkandarasi na Mshauri Elekezi. |
| Ujenzi wa jengo moja la Nyumba za Makaazi 22 Mombasa – kwa Mchina (Phase II) | Asilimia ya ujenzi iliyofikia | 100 | 70 | 70 | Mradi unaendelea katika hatua za kumalizia na kufikia asilimia 70 ya utekelezaji wake ambapo kazi zinazoendelea ni kuweka slab ya mwisho pamoja na kujenga kuta za tofali, kupiga plasta na kufanya skimming. |
| Ujenzi wa mji mpya wa Kisakasaka 'B', 'C' na 'D' Unguja | Asilimia ya ujenzi iliyofikia Kisakasaka 'B'. | 100 | 20 | 20 | Ujenzi wa nyumba 548 za Makaazi na Biashara Kisakasaka "B" (phase I) utakuwa na majengo 30 unaendelea, hatua iliyofikia ni Ujenzi wa Ofisi za Wakandarasi, Kuanza kujenga misingi ya majengo na kuanza kusimamisha nguzo. |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikia Kisakasaka 'C' | 100 | 10 | 10 | Ujenzi wa nyumba 288 za Makaazi na Biashara Kisakasaka"C upo katika hatua ya manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi na Mshauri Elekezi wa ujenzi wa Mradi huo. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Asilimia ya ujenzi ilyofikiwa kisaksasa 'D' | 100 | 13 | 13 | Ujenzi wa nyumba 312 za Makaazi na Biashara Kisakasaka"D" unaendelea na hatua iliyopo Ofisi za Mkandarasi na Mshauri Elekezi zimekamilika kujengwa. Hatua inayoendelea sasa ni kazi za kujenga misingi ya majengo hayo na kujaza fusi (back feeling). |

### 11.2.10 Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda

Wizara ina lengo la kukuza viwanda vidogo vidogo na vya kati sambamba na kuimarisha mazingira ya kufanya biashara, ili kuleta maendeleo ya kijamii na kiuchumi nchini. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza programu moja na mradi mmoja kwa gharama ya TZS 46.36 bilioni kutoka Serikalini.

**i. Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonesho Zanzibar**

Programu hii ina lengo la kutoa huduma za kuimarisha sekta ya biashara na viwanda kwa kutoa msaada kwa wafanyabiashara wadogo wadogo na wa kati katika maeneo ya Dimani na Chamanangwe. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa jumla ya TZS 10.80 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 6.48 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 2.95 bilioni sawa na asilimia 45 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa ghala la kuhifadhia vifaa, jengo la kuuzia chakula, eneo la kufurahishia watoto pamoja na ukumbi wa mikutano wa kisasa katika kituo cha Dimani. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Ujenzi wa ghala za kuhifadhia vifaa na chakula upo katika hatua ya jamvi na kusimamisha nondo kwa ajili ya ujenzi wa nguzo. |

**a) Mradi wa Kuanzisha na Kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Industrial Pack)**

Mradi huu una lengo la kukuza uchumi kupitia uimarishaji wa sekta ya viwanda na mazingira mazuri ya biashara katika maeneo makuu matatu Dunga, Pangatupu

na Chamanangwe. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 35.56 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 21.33 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.56 bilioni sawa na asilimia 7 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa miundombinu ya maji na barabara katika eneo la Chamanangwe na Pangatupu | Asilimia ya ujenzi wa miundombinu uliofikiwa | 100 | 40 | 40 | Ujenzi wa tangi la maji upo katika hatua ya kujenga zege kwa ajili ya kitako cha kuwekea tenki ya maji |

### 11.2.11 Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali

Sekta ya elimu ni msingi wa mafanikio ya kiuchumi na kijamii. Uwekezaji katika Sekta ya elimu ni muhimu katika mustakabali wa maendeleo ya Taifa, kwani huandaa kizazi chenye uwezo wa kutatua changamoto za sasa na zijazo kwa ufanisi. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara ya Elimu imepanga kutekeleza Programu moja na Miradi miwili ya Maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 522.47 bilioni (TZS 321.86 bilioni kutoka Serikalini na TZS 200.62 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), jumla ya TZS 313.48 bilioni (TZS 193.11bilioni kutoka Serikalini na TZS 120.37 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepangwa kutumika

#### i. Programu ya Uimarishaji wa Mindombinu ya Elimu

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha Miundombinu ya Sekta ya Elimu kiujumla ili kuwawezesha wanafunzi kupata elimu bora yenye viwango na ufanisi. Programu hii inatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa jumla ya TZS 439.32 bilioni (TZS 247.65 bilioni kutoka Serikalini na TZS 191.68 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), jumla ya TZS 263.59 bilioni zimepangwa kutumika. (TZS 148.58 bilioni kutoka Serikalini na TZS 115.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 199.15 bilioni (TZS 95.09 bilioni kutoka Serikalini na TZS 104.06 bilioni kutoka kwa

Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 76 ya lengo la TZS 263.59 bilioni zimepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa skuli 20 za maandalizi, 17 za msingi (tisa za chini na nane za ghorofa) na 12 za ghorofa za sekondari | Asilimia ya ujenzi wa skuli iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Michoro ya awali kwa skuli zote imekamilika na imefanyiwa maboresho kwa kuongeza idadi ya madarasa. Skuli za msingi kutoka madarasa 15 hadi 21 na skuli za sekondari kutoka madarasa 8 hadi 16. Hatua za kumtafuta mkandarasi zinaendelea. |
| Ukarabati wa skuli 108 | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Tathmini ya awali imekamilika kwa ajili ya kubaini skuli zenye uhitaji wa haraka zaidi na hatua za kumtafuta mkandarasi zinaendelea. |
| Ukamilishaji wa madarasa 103 yaliyoanzishwa kwa nguvu za wananchi | Asilimia ya ukamilishaji iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Tathmini ya awali imekamilika na hatua za kumtafuta mkandarasi zinaendelea. |
| Ujenzi wa skuli tatu za Elimu Mjumuisho | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 0 | 0 | Utaratibu wa kutafuta maeneo ya ujenzi wa skuli unaendelea na kwa sasa eneo moja limepatikana Langoni (Mkoa wa Mjini Magharibi) |
| Ujenzi wa vyoo 300 kwa skuli za maandalizi, msingi na sekondari | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Jumla ya vyoo 300 vinakadiriwa kujengwa. Aidha, tathmini ya awali imeanza kwa ajili ya kubaini skuli zenye uhitaji wa haraka zaidi. Kwa sasa Wizara inakamilisha taratibu za kumpata mkandarasi wa ujenzi wa vyoo |
| Kuziwekea miundombinu ya umeme wa jua skuli 19 za ghorofa za msingi | Idadi ya skuli zilizowekewa miundombinu ya umeme wa jua | 19 | 0 | 0 | Tathmini ya awali kuhusu skuli hizo imekamilika na skuli zenyewe ni kama ifuatavyo : - Michakaeni, Michenzani, Jobwe – Mwambe, Kipitacho, Kojani, Chumbuni, Kijichi, Abeid Amani Karume (Mwera), Vuga Mkadini, Fuoni Rocky, Donge Msingi, Tumbe A, Mambosasa msingi, Wingwi Kije, Mwera Mtofaani, Shakani, Ziwani, Ndagoni Wambaa, Potoa. |
| Ujenzi wa Karakana 25 kwa skuli za sekondari | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Maeneo ya ujenzi wa karakana za ufundi tayari yamepatikana (Bububu, Mtoni Kigomeni, Abeid Amani Karume, Kwarara, Mwanakwerekwe A, Chumbuni, Forodhani, Hurumzi, Mikunguni technical secondary school, Nyerere, Kwamtipura, Mahonda, Machui, Bambi, Vitongoji, Ole , Gando, Wete Sekondari, Kengeja technical secondary school, Uweleni, Micheweni, Konde, Hassan Kh. Hafidh (Munduli), |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | | | | | Langoni, Fuoni) na hatua ya kuandaa michoro (design) inaendelea. |
| Ujenzi wa dakhalia 9 na nyumba 10 za walimu | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Utambuzi wa maeneo ya ujenzi wa dakhalia umefanyika kwa baadhi ya skuli kama vile maeneo ya Bambi, Koani, Finya, Mohammed Juma Pindua, Donge na Mikindani |
| | Asilimia ya ujenzi wa nyumba za walimu iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Michoro ya ujenzi imekamilika na Mkandarasi ameshapatikana na tayari washafunga mkataba kwa ajili ya kuanza ujenzi huo |
| Kuendelea na ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi 500 ya wanawake na kuanza ujenzi wa dakhalia ya wanafunzi 500 wanaume katika chuo cha SUZA | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Ujenzi wa Dakhalia umeshaanza na upo katika hatua ya kuchimba msingi. |
| Ujenzi wa Chuo cha Ubaharia | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Ujenzi wa chuo umeshaanza na upo katika hatua ya kujenga misingi kwa majengo yote matatu (Utawala, bwawa la kuogelea na Karakana ya zimamoto) |
| Ujenzi wa karakana za Uhandisi Mitambo, Uhandisi ujenzi, magari katika Taasisi ya Sayansi na Teknolojia ya Karume na kuzipatia vifaa | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 60 | 60 | Ujenzi unaendelea kwa hatua ya kupaka rangi na ufungaji wa milango na madirisha. |
| Kujenga ukumbi wa Taasisi ya Karume ya Sayansi na Tekonolojia; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Michoro ya ujenzi imekamilika .Hatua za kumtafuta mkandarasi zinaendelea. |
| Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha IIT Madras; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Ujenzi wa dakhalia umekamilika, hatua inayoendelea ni ufungaji wa vifaa vya TEHAMA (simu na kamera za CCTV), sambamba na kuweka maandalizi ya mandhari sawa (landscape) pamoja na ujenzi wa uwanja wa mpira. |
| Kuvifanyia ukarabati vituo vya Ualimu (TCs), vituo vya Elimu Mbadala na Watu Wazima Rahaleo na Forodhani; | Asilimia ya ukarabati uliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Michoro kwa ajili ya ukarabati imekamilika na Mkandarasi ameshapatikana na hatua inayoendelea ni kumuonesha maeneo na kusaini mkataba kwa ajili ya kuanza kazi hiyo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa vyuo vitano vya Amali | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Ripoti za tathmini za zabuni (evaluation report) za kumtafuta mkandarasi zimewasilishwa benki kwa ajili ya kupata ridhaa (no objection). |
| Ujenzi wa Ofisi ya Mamlaka ya Mafunzo ya Amali | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Uandaaji wa mchoro wa jengo la ofisi umekamilika. Hatua za kumtafuta Mkandarasi zinaedelea |
| Kuanzisha Kituo cha kuchapisha mitihani na Ujenzi wa jengo la Ofisi ya Baraza la Mitihani | Asilimia ya ujenzi wa kituo iliyofikiwa. | 100 | 0 | 0 | Ombi la eneo kwa ajili ya ujenzi wa Kituo cha Kuchapisha Mitihani limewasilishwa Wizara ya Ardhi. |
| | Asilimia ya ujenzi wa Ofisi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Michoro kwa ajili ya ujenzi imekamilika hatua inayoendelea ni kumpata mkandarasi ambae atajenga |
| Ukarabati na utanuzi wa Kituo cha Habari za Elimu Kwarara - Unguja na Mkoroshoni - Pemba | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa (Unguja) | 100 | 2 | 2 | Tathmini ya awali imefanyika na kuwasilishwa katika ngazi za maamuzi |
| | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa (Pemba) | 100 | 100 | 100 | |
| Ukarabati wa Maabara za Kompyuta | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 1 | 1 | Tathmini ya awali imeanza kwa ajili ya kubaini skuli zenye uhitaji wa haraka zaidi |
| Kujenga Maktaba Kuu ya kisasa | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Rasimu ya awali ya michoro imekamilika na uchunguzi wa udongo unaendelea |
| Kujenga viwanja viwili vya kisasa katika skuli zenye michepuo ya michezo na Ujenzi wa "Sports Academy". | Idadi ya viwanja vilivyojengwa | 2 | 0 | 0 | Michoro (BoQ) imekamilika na Mkataba umeshasainiwa. Ujenzi utaanza baada ya kupatikana kibali cha ujenzi kutoka mamlaka husika. Viwanja hivyo vitajengwa skuli ya Hailesellassie kwa Unguja na Mohammed Juma Pindua kwa Pemba. |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (Sports Academy) | 100 | 1 | 1 | Tathmini ya awali tayari imekamilika |
| Kuendelea na ujenzi wa skuli 2 zenye dakhalia. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 0 | 0 | Utaratibu wa kutambua maeneo unaendelea |
| Ujenzi wa jengo la utawala, skuli ya elimu, nyumba za wafanyakazi, kituo cha wanafunzi na kiwanja cha michezo (SUZA). | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (jengo la utawala) | 100 | 5 | 5 | Mkataba umeshasainiwa kwa ajili ya kuanza ujenzi |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (nyumba za wafanyakazi) | 100 | 5 | 5 | |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa (kituo cha wanafunzi na kiwanja cha michezo) | 100 | 5 | 5 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuunganisha mkonga wa Taifa na skuli, vituo vya ubunifu wa kisayansi (HUBs) na vituo vya ualimu (TCs); | Idadi ya taasisi zilizounganishwa na mkonga wa Taifa | 100 | 100 | 100 | Skuli zote na vituo vya ualimu pamoja na maabara 100 tayari yamefikiwa na Mkonga wa Taifa na zinapata huduma ya mtandao kwa ajili ya kujifunzia na kufundishia. |
| Ujenzi wa jengo la skuli ya kilimo na maabara ya sayansi ya kisasa na utoaji wa taaluma ya mahitaji maalum katika Kampasi ya Tunguu; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 70.77 | 70.77 | Ujenzi unaendelea kwa utiaji wa tarazo, fitting ya umeme na maji, upigaji wa plasta na rangi, ufungaji madirisha ya *grill* pamoja na fremu za madirisha ya alluminum na fremu za milango |
| Kuendelea na ujenzi wa Chuo cha Amali | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Zabuni ya kumpata mshauri elekezi kwa ajili ya ujenzi wa Chuo cha Mkoa (Politechnic College) imefanyika. |
| Kuendelea na ujenzi wa jengo la Wizara Chake Chake- Pemba. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 75 | 75 | Hatua iliyofikiwa ni kufungwa kwa lift, kuezekwa na kazi ya *skimming* ndani inaendelea |

### a) Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha utoaji wa elimu katika ngazi zote kwa kuwapatia walimu na wanafunzi vifaa vya kujifunzia na kufundishia, mafunzo ya walimu na matumizi ya TEHAMA. Mradi huu unatekelezwa kwa kutumia fedha kutoka Serikalini na Washirika wa Maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 48.15 bilioni (TZS 39.21 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.94 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 28.89 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 23.52 bilioni kutoka Serikalini na TZS 5.36 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 14.37 bilioni (TZS 13.49 bilioni kutoka Serikalini na TZS 881.0 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 50 ya lengo la TZS 28.89 bilioni zimepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa vifaa vya usafi, maabara na maktaba kwa ajili ya skuli mpya. | Idadi ya skuli zilizopatiwa vifaa | 52 | 36 | 69.2 | Jumla ya skuli 36 zimepatiwa vifaa, zikiwemo skuli za sekondari 15 skuli za msingi 5 na skuli za maandalizi 16. Skuli za sekondari ni Tunguu, Regeza Mwendo, Maungani, Chukwani, Mbuzini, Chuini, Koani, Mwenge, Furaha, Kije, Sizini, Vuga Mkadini, Gamba, Kifundi na Makunduchi. Skuli za Msingi ni Mkadini, Potoa, Mwera Mtofaani, Maziwango'mbe na Muungano. Skuli za Maandalizi ni Kibuyuni, Kitogani, kinyasini, Donge , Kitope , Kizimkazi , Jumbi, Koani, Dole, Fuoni Kipungani, Kivugo, Mbuzini, Maziwang'ombe, Karume, Mwera Mtofaani na Bumbwisudi. |
| Kuimarisha miundombinu ya skuli/dakhalia kwa kuziwekea mifumo ya gesi asilia. | Idadi ya skuli/dakhalia zilizowekewa mifumo ya gesi asilia | 13 | 0 | 0 | Mfumo wa gesi upo katika mchakato wa manunuzi. |
| Kuziwekea miundombinu ya umeme wa jua skuli 19 za ghorofa za sekondari. | Idadi ya skuli zilizowekewa miundombinu ya umeme wa jua | 19 | 0 | 0 | Upembuzi yakinifu umefanyika katika skuli zifuatazo : - Tumekuja, Dr Shein, Donge, Mkokotoni, Ali Hassan Mwinyi, Kiembe Samaki Sekondari, Tumbatu, Makoba, Balozi Seif Ali Iddi ( Misufini), Dr. Samia, Maziwang'ombe, Dr Amani, Kiwani, Hemed Abdulla Suleiman, Idrisa Abdulwakil, Utaani, Konde, Ole na Regeza Mwendo. |
| Ununuzi wa magodoro 10,000 kwa ajili ya dakhalia mpya. | Idadi ya magodoro yaliyonunuliwa | 10,000 | 3,224 | 32.24 | Jumla ya magodoro 3,224 yamenunuliwa kwa ajili ya wanafunzi wanaotarajiwa kuishi katika dakhalia ya Chuo cha Ualimu Nkrumah |
| Kuzipatia Karakana vifaa vya kufanyia mazoezi. | Asilimia ya karakana zilizopatiwa vifaa | 100 | 30 | 30 | Baadhi ya makontena yamewasili na vifaa vitaanza kugawiwa baada ya ujenzi kukamilika. |
| Kuwapatia walimu mafunzo ya fani ya Amali na Ufundi. | Idadi ya walimu waliopatiwa mafunzo | 506 | 171 | 34 | Mafunzo yametolewa kwa walimu 171 na taratibu za kuwapatia walimu waliosalia zinaendelea |
| Kuandaa, kuchapisha na kusambaza vitabu kwa ajili ya Mtaala mpya. | Idadi ya vitabu vilivyochapishwa | 1,108,270 | 1,108,270 | 100 | Skuli 227 za sekondari zimepatiwa vitabu vya kidato cha kwanza na cha pili kwa ajili ya mtaala mpya Unguja na Pemba |
| Kuzipatia skuli vifaa vya michezo na vifaa vya TEHAMA zikiwemo *"Smart Screen", "Desktop", "Laptop"* na *"Printer"*. | Asilimia ya skuli zilizopatiwa vifaa vya TEHAMA | 100 | 50 | 50 | Smart screen 25,desktop 2000,na laptop 3000 zimenunuliwa. Hatua inayofuata ni kusubiri kuwasili na kusaambazwa katika maeneo husika. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa samani kwa ajili ya skuli za maandalizi, msingi na sekondari. | Idadi ya skuli za maandalizi zilizopokea samani | 20 | 16 | 80 | Idadi ya skuli 16 ambazo zimepatiwa samani ni :- Kibuyuni, Kitogani, kinyasini, Donge , Kitope , Kizimk azi , Jumbi , Koani, Dole, Fuoni Kipungani, Kivugo, Mbuzini, Maziwang'ombe, Karume, Mwera Mtofaani na Bumbwisudi. |
| | Idadi ya skuli za msingi zilizopokea samani | 21 | 5 | 23.8 | Skuli za Msingi ni Mkadini, Potoa, Mwera Mtofaani, Maziwango'mbe na Muungano. |
| | Idadi ya skuli za sekondari zilizopokea samani | 12 | 15 | 125 | Idadi ya skuli 15 ambazo zimepatiwa samani ni :- Tunguu, Regeza Mwendo, Maungani, Chukwani, Mbuzini, Chuini, Koani, Mwenge, Furaha, Kije, Sizini, Vuga Mkadini, Gamba, Kifundi na Makunduchi. |
| Ununuzi wa vifaa vya TEHAMA kwa ajili ya Maktaba Mtandao katika skuli 33 za Unguja na Pemba | Idadi ya skuli zilizopatiwa vifaa | 33 | 33 | 100 | Skuli 33 zimeshawekewa vifaa vya Maktaba mtandao Unguja na Pemba. |

### b) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu

Lengo la mradi huu ni kuongeza idadi ya wataalamu wazalendo katika visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 35.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 21.0 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 20.50 bilioni sawa na asilimia 98 ya lengo la TZS 21.0 bilioni zimeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwapatia mikopo wanafunzi wa Elimu ya juu Zanzibar | Idadi ya wanafunzi wapya waliopatiwa mikopo | 4,877 | 8,975 | 184 | Jumla ya Wanafunzi 18,593 wamepatiwa mikopo kutoka katika vyuo vya ndani na Nje ya Tanzania |
| | Idadi ya wanafunzi wanaoendelea waliopatiwa mikopo | 9,618 | 9,618 | 100 | |

## 11.2.12 Wizara ya Habari, Vijana, Utamaduni na Michezo

Wizara hii inatekeleza majukumu yake ya utoaji wa habari kwa wasikilizaji na watazamaji kupitia magazeti, TV na Redio, kuwawezesha vijana kwa kuwatafutia fursa za ajira, kudumisha utamaduni na kuimarisha michezo. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza Programu moja na miradi miwili ya Maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 433.58 bilioni (TZS 432.95 bilioni kutoka Serikalini na TZS 633.98 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 260.15 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 259.77 bilioni kutoka Serikalini na TZS 380 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS

219.44 bilioni sawa na asilimia 84 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza programu na miradi ya maendeleo ifuatayo:-

i. **Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo**

Programu ina lengo la kuiwezesha sekta ya michezo kwa kujenga na kuimarisha miundombinu ya michezo Zanzibar itakayokidhi viwango vya Kitaifa na Kimataifa. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kiasi cha TZS 414.08 bilioni (TZS 413.45 bilioni kutoka Serikalini na TZS 633.98 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 248.45 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 248.07 bilioni kutoka Serikalini na TZS 380 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 47.36 bilioni sawa na asilimia 192 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa kiwanja kipya cha mpira pamoja na viwanja viwili vya mazoezi; | Asilimia ya ujenzi wa kiwanja kipya iliyofikiwa | 100 | 40 | 40 | Ujenzi wa kiwanja kipya umeanza kwa kuweka msingi wa majukwaa pamoja na nguzo za majukwaa hayo pamoja na kuanza matayarisho ya kuandaa “Formwork” ya level ya pili kwa ajili ya kumwaga Zege. |
| | Asilimia ya ujenzi wa viwanja vya mazoezi iliyofikiwa | 100 | 32 | 32 | Usafishaji wa eneo la (Stadium, Ferry pier), Viwanja vya kufanyia mazoezi pamoja na eneo litakalojengwa Uwanja wa kuogelea (Swimmingpool) unaendelea. |
| Ujenzi wa Hospitali na hoteli ya kisasa (4 star); | Asilimia ya ujenzi wa hoteli iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Shughuli iliyofanyika ni kusafisha eneo tu la hoteli kwa ajili ya kuanza ujenzi. |
| Ujenzi wa viwanja 17 vya michezo vya Wilaya na Mkoa. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 58 | 58 | Ujenzi wa viwanja 17 vya Wilaya na Mikoa unaendelea na ujenzi ni kama ifuatavyo:- Matemwe(20%), Unguja Ukuu (85%), Micheweni (98%), Kinyikani (52%) na Kangani (96%), Ukutini (82%), Pangatupu (85%), Pandani (83%) na Maruhubi (0%). |
| | Idadi ya viwanja vilivyojengwa | 17 | 8 | 47 | Viwanja vilivyokamilika ni Chake chake (Gombani) 100%, Maisara 100%, Prizi 100%, kitope 100%, Kitogani (100%), Mombasa (100%), Mwehe (100%) na Mao |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa viwanja sita vyenye miundombinu ya michezo ya aina nne katika kiwanja kimoja (four in one) Unguja na Pemba. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi wa viwanja vya 4 in 1 umekamilika na maeneo yaliyobahatika kujengwa kwa viwanja hivyo ni Skuli ya Sekondari Tumbatu, Chuo cha Ufundi wa amali Mkokotoni na skuli ya Sekondari Regeza Mwendo kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba ni Skuli ya Sekondari Mchanga Mdongo, Skuli ya Sekondari kangani na Chake Chake. Mradi unahusisha ujenzi wa viwanja vitatu kwenye eneo moja (4 in1) navyo ni kiwanja cha Basketball, Kiwanja cha nettball, kiwanja cha Tennis na Volleyball. |
| | Idadi ya viwanja vilivyojengwa | 6 | 6 | 100 | Skuli ya Sekondari Tumbatu, Chuo cha Ufundi wa amali Mkokotoni na skuli ya Sekondari Regeza Mwendo kwa upande wa Unguja na kwa upande wa Pemba ni Skuli ya Sekondari Mchanga Mdongo, Skuli ya Sekondari kangani na Chake Chake. |

### a. Mradi wa Vituo vya Mafunzo kwa Vijana Awamu ya Pili

Mradi una lengo la kuwajengea uwezo vijana kwa kuwapatia mafunzo ya stadi za maisha na ufundi. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 16.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 9.90 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 2.23 bilioni sawa na asilimia 22 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa vifaa na samani vya kituo cha mafunzo kwa vijana Bweleo Unguja na Weni - Pemba; | Asilimia ya manunuzi iliyofikia | 100 | 80 | 80 | Hatua na ukamilishaji wa manunuzi wa upatikanaji wa vifaa zimeshakamilika hatua iliyobaki ni kufanya malipo ili vifaa viweze kukabidhiwa. |

### b. Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni

Lengo la mradi ni kuweka miundombinu kwa ajili ya mafunzo na utaalamu wa sanaa katika tasnia ya sanaa ikiwemo kuibua, kukuza na kuhuisha vipaji kwa vijana ili kukuza ajira na vipato vyao. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 3.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.80 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.86 bilioni sawa na asilimia 104 ya lengo la TZS 1.80 bilioni zimepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa nyumba ya Sanaa Mwanakwerekwe; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 98 | 98 | Ujenzi umekamilika na asilimia mbili zimewekwa katika hatua ya uangalizi |
| Ununuzi wa samani na vifaa vya Ofisi. | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Maandalizi ya vifaa na samani za ofisi yamekamilika ambapo vifaa viligawanywa katika magroup saba vikiwemo vifaa vya ICT na studio, vifaa vya uchongaji, ufumaji, ushoni, uchoraji, uchoraji wa hina, pamoja na vifaa vya batik. |

### 11.2.13 Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo

Wizara imehusisha sekta muhimu katika ukuzaji uchumi kwa kutoa mchango wa moja kwa moja kwa wananchi katika kupambana na umasikini, kuongeza uzalishaji, kuwa na uhakika wa chakula, utoaji wa ajira pamoja na kuimarisha huduma. Wizara pia inasaidia upatikanaji wa pembejeo na utoaji wa mafunzo kwa wakulima na wafugaji. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza programu tatu na miradi minne itakayogharimu jumla ya TZS 58.18 bilioni (TZS 24.70 bilioni kutoka Serikalini na 33.48 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 34.91 bilioni(TZS 14.82 bilioni kutoka Serikalini na TZS 20.09 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo) zimepangwa kutumika na kutekeleza program na miradi kama ifuatavyo:-

### i. Programu ya Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji

Programu imeanzishwa kwa lengo la kuendeleza miundombinu ya umwagiliaji ili kuongeza uzalishaji wa zao la mpunga, kuwawezesha wakulima kwa kuwajengea uwezo wa uzalishaji kwa kutumia pembejeo za kilimo. Kwa mwaka 2025/2026, program imepangiwa kutumia TZS 5.81 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 3.4 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 4.03 bilioni kutoka washirika wa maendeleo sawa na asilimia 116 zimepatikana na kukamilisha malipo kwa kazi za ujenzi wa miundombinu ya umwagiliaji katika bonde la Cheju ‘B’

### ii. Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo.

Programu ina lengo la kuimarisha na kuinua sekta ya kilimo na mifugo kwa wakulima na wafugaji wadogo wadogo Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, programu inatarajia kutekeleza miradi minne (4) kama ifutavyo:-

#### a) Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuendeleza miundombinu ya mifugo kwa kutoa huduma bora kwa jamii za wafugaji na wakulima, kuimarisha miundombinu ya utafiti wa mifugo na kudhibiti ndege waharibifu wa mazao ya kilimo na mifugo (kunguru) pamoja na kuimarisha maudhui ya kilimo TV. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.50 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.5 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 791.89 milioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 53 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa mtambo wa kuzalisha gesi ya nitrojeni ili kuhifadhia mbegu za madume kwa ajili ya kupandishia ng'ombe kwa njia ya sindano; | Idadi ya mitambo iliyonunuliwa | 1 | 0 | 0 | Msambazaji yuko katika hatua za uzalishaji wa mtambo na tayari ameshalipwa fedha kiasi cha asilimia 20 ya fedha zilizopangwa. Fedha hizi zilitiwa mwaka wa fedha 2024/2025 |
| | Asilimia ya manunuzi iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | |
| Ujenzi wa miundombinu ya karantini ya Kisakasaka – Unguja na Gando Nziwengi – Pemba; | Asilimia ya ujenzi wa Kisakasaka – Unguja iliyofikiwa | 100 | 75 | 75 | Mazizi (paddock) 6 tayari yameshawekwa nguzo za zege na fitting ya umeme kwa ajili ya kuweka taa katika nguzo, kilichobaki ni kuweka wire wa uzio, sehemu ya kushukia na kupakia wanyama na ujenzi wa josho upo katika hatua za ukamilishaji na kazi zinazoendelea ni uwekaji wa miundombinu ya maji. |
| | Asilimia ya ujenzi Nziwengi–Pemba; iliyofikiwa | 100 | 45 | 45 | Ujenzi wa Nguzo za mazizi (paddock) 6 tayari, josho, sehemu za kushushia na kupakia wanyama, miundombinu ya maji pamoja na umeme unaendelea |
| Ujenzi wa miundombinu ya utafiti wa mifugo ikiwemo maabara ya utafiti wa magonjwa ya wanyama, mabanda ya mbuzi, kuku, kondoo na Ofisi Unguja na Pemba | Asilimia ya ujenzi wa maabara ya utafiti wa magonjwa ya wanyama kwa Unguja | 100 | 60 | 60 | Ujenzi umemalizika, upo kwenye kufunga vifaa |
| | Asilimia ya ujenzi wa mabanda ya mbuzi na kondoo kwa Unguja | 100 | 70 | 70 | Mabanda yashaezekwa, yapo kwenye hatua za mwisho za ujenzi |
| | Asilimia ya ujenzi wa ofisi kwa Unguja | 100 | 90 | 90 | Ujenzi umekaribia kumaliza, upo kwenye hatua za kumalizia uwekaji wa madirisha na milango |
| Kudhibiti wanyama waharibifu wa mazao ya kilimo na mifugo (kunguru); | Idadi ya kunguru waliotokomezwa | 37,500 | 9,600 | 26 | Fedha kwa ajili ya kutekeleza hazijaidhinishwa kufuatia kutokamilika kwa Mpango wa Manunuzi |

### b) Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki.

Mradi huu una lengo la kuimarisha sekta ya ufugaji nyuki isaidie katika ukuaji wa uchumi shirikishi pamoja na kuiwezesha asali inayozalishwa kuwa na viwango vya ubora na kukubalika katika masoko ya ndani na nje. Mradi huu unatekelezwa kisiwani Pemba na kwa mwaka 2025/2026, umepangiwa jumla ya TZS 100.0 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 60 milioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzisha na kuendeleza hifadhi za nyuki katika misitu ya jamii; | Idadi ya hifadhi zilizoanzishwa | 2 | 2 | 100 | Hifadhi za Nyuki katika Misitu ya Jamii Kiungoni na Mwambe Chaleni zipo tayari. Ingawa taratibu za kufanikisha mikataba ya kuwa Misitu ya Jamii (COFMA) Kiungoni na Mwambe Chaleni zinaendelea. |
| | Idadi ya hifadhi zilizoendelezwa | 5 | 5 | 100 | Hifadhi za Nyuki katika misitu 5 ya jamii zipo tayari. Taratibu za kufanya mapitio ya mikataba ya Misitu ya Jamii zimekamilika na sasa mikataba hiyo ipo Wizarani kwa kusainiwa na Mheshimiwa Waziri. Hifadhi hizo zipo katika misitu ya jamii Mjini Wingwi, Shanake, Mtambwe Kusini, Pujini na Wambaa. |
| Kuendeleza upatikanaji wa pembejeo za ufugaji nyuki kwa kutoa mizinga kwa wafugaji | Idadi ya mizinga iliyotolewa kwa wafugaji nyuki | 200 | 200 | 100 | Mizinga ya kufugia nyuki 100 imetolewa kwa vijana 20 kutoka Pemba waliopatiwa mafunzo ya ufugaji bora wa nyuki katika Chuo cha Mafunzo ya Nyuki (BTI) Tabora. Vijana hawa pia wamepatiwa vifaa vya kujikinga na nyuki kwa ajili ya ufanisi mzuri katika shughuli zao.<br>Aidha, mizinga 100 imetolewa kwa hifadhi za nyuki 5 za Pemba ili kuongeza nguvu shughuli za ufugaji katika hifadhi hizo. Hifadhi hizo ni Kiungoni, Mtambwe Kusini, Shanake, Pujini na Mwambe Chaleni. |
| Kutoa mafunzo ya ufugaji wa nyuki. | Idadi ya wafugaji wa nyuki waliopatiwa mafunzo | 600 | 559 | 93 | Wafugaji nyuki 559 (wanaume 323 na wanawake 236) wamepatiwa mafunzo ya ufugaji nyuki bora kutoka kwa maafisa misitu wa wilaya 4 za Pemba. Hii ni muendelezo wa kufundisha wafugaji nyuki 1,000 kwa mwaka kisiwani Pemba |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| | Idadi ya wafugaji wa nyuki Viongozi waliopatiwa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji asali | 20 | 20 | 100 | Jumla ya wafugaji wa nyuki Viongozi 20 (wanaume 15 na wanawake 5) walipatiwa mafunzo bora ya ufugaji nyuki ili waweze kusambaza utaalamu kwa wafugaji wa karibu yao. Hawa ni wawakilishi wa wafugaji wa Wilaya zote 4 za Pemba. |
| | Idadi ya wafugaji wa nyuki vijana waliopatiwa mbinu bora za uzalishaji asali | 20 | 20 | 100 | Jumla ya vijana 20 (15 Me, 5 Ke) walipatiwa mafunzo ya ufugaji wa nyuki bora katika Chuo cha Mafunzo ya Nyuki Tabora ili waweze kusambaza utaalamu kwa wafugaji hususan vijana wa karibu yao. Hawa ni wawakilishi wa vijana wa wilaya zote 4 za Pemba |
| Kuanzisha Vituo cha Mauzo ya Mazao ya Nyuki Pemba | Idadi ya vituo vya Mauzo ya Mazao ya Nyuki Pemba | 1 | 1 | 100 | Kituo cha Mauzo ya Mazao ya Nyuki (Marketing Centre) kimejengwa eneo la Maonesho ya Kilimo Chamanangwe Pemba. Kituo hiki kitaendeshwa na Jumuiya ya Wafugaji Nyuki Pemba (PEBA) chini ya usimamizi wa Idara ya Misitu. |
| Kuimarisha Skuli ya Kilimo (SoA) ili kuweza kutoa mafunzo ya vitendo ya uzalishaji wa asali na upatikanaji wa masoko. | Asilimia ya uimarishaji iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Jumla ya wageni 809 (wanaume 537 na wanawake 272) walipita na kujifunza katika banda la nyuki la Skuli ya Kilimo (SoA). Wageni hao wanajumuisha wafugaji wa nyuki wa Wilaya za Unguja, wakulima, wafugaji ambao wameshajiika na ufugaji nyuki, wanafunzi wa Skuli, Vyuo vya Kati na Vyuo Vikuu ambao wamejenga mwamko wa taaluma ya ufugaji nyuki, watumishi wa umma, wajasiriamali na Viongozi wa Serikali wakiwemo Makatibu Wakuu na Wakurugenzi wa Taasisi mbalimbali. |

### c) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa Kuongeza Tija na Uzalishaji kupitia Huduma za Kisasa za Kilimo katika Umwagiliaji

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuchangia uimarishaji na uhakika wa chakula na kuongeza kiwango cha kipato kwa wakulima wa mpunga Zanzibar pamoja na kuongeza tija ya mpunga katika mashamba ya umwagiliaji. Mradi unatekelezwa kwa mashirikiano baina ya Serikali na Washirika wa Maendeleo.

Kwa mwaka2025/2026, mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 3.95 bilioni (TZS 200.00 milioni kutoka Serikalini na TZS 3.75 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 2.37 bilioni zilipangwa kutumika (TZS 120 milioni kutoka Serikalini na TZS 2.25 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 17.32 bilioni sawa na asilimia 731ya lengo la TZS 2.37 bilioni zimepatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza Shuguli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa Mafunzo ya udereva wa zana za kilimo kwa madereva wa Wakala wa matrekta na zana za kilimo na wakulima | Idadi ya madereva wa zana za kilimo waliopatiwa mafunzo | 60 | 45 | 75 | |
| Ununuzi wa matrekta ya kilimo katika mabonde ya umwagiliaji, ununuzi wa mashine ya kuvunia mpunga na kutoa mafunzo kwa Jumuiya za wakulima wa mpunga; | Idadi ya Trekta-45HP zilizonunuliwa | 6 | 5 | 83.33 | Trekta 1 inatarajiwa kufika Juni, 2026. |
| | Idadi ya Trekta-65HP zilizonunuliwa | 4 | 3 | 75 | Trekta 1 limefelishwa kutokana na kuwa tayari limetumika. |
| | Idadi ya majembe ya kuchimba/kuburuga yaliyonunuliwa | 8 | 3 | 37.5 | Majembe yaliobakia yanatarajia kuletwa Juni 2026. |
| | Idadi ya mashine ya kukorogea (Rotavetor) zilizonunuliwa. | 8 | 2 | 25 | Mashine za kukorogea zilizobakia zinatarajiwa kuja Juni 2026. |
| | Idadi ya mashine za kuvuna mpunga "Combine Harvester" zilizonunuliwa. | 9 | 9 | 100 | |
| | Idadi ya majembe ya kuweka konde sawa (Land levelers) yaliyonunuliwa. | 4 | 1 | 25 | Majembe ya kuweka konde sawa yaliobakia yanatarajia kuja Juni 2026. |
| | Idadi ya wakulima na mabibi/bwana shamba wailopatiwa mafunzo. | 330 | 322 | 97.57 | |
| Ujenzi wa barabara za kuingilia mashambani katika mabonde ya Kibokwa1.02km, Kinyasini(0.27km, Kilombero 2.14km na Mlemele 0.84km. | Urefu wa barabara za kuingilia shambani zilizojengwa (km) . | 4.27 | 3.65 | 85 | |

### ii) Programu ya Usimamizi na Uhifadhi wa Chakula

Programu ina lengo la kusimamia sekta za kilimo kwa kuongeza upatikanaji wa mazao ya kilimo yaliyosalama, upatikanaji wa chakula katika ngazi ya Kitaifa pamoja na kuwajengea uwezo wakulima juu ya mifumo ya chakula. Kwa mwaka 2025/2026, programu inatarajia kutekeleza miradi mitano ya Maaendeleo kama ifuatavyo:-

#### a) Mradi wa Ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula

Mradi umeanzishwa kwa lengo la kuwa na upatikanaji wa chakula katika ngazi ya Kaya na Taifa kwa ukarabati wa maghala ya chakula na ujenzi wa vihenge. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 20.0 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 12.0 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.76 bilioni sawa na asilimia 15 zimeingizwa kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukarabati wa maghala tisa (Unguja matatu na Pemba sita) pamoja na ununuzi wa chakula; | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa unguja | 100 | 5 | 5 | Mkandarasi hakuendelea na ujenzi kwa sababu ya kutolipwa malipo yake ya awali (Advance payment) |
| | Asilimia ya ukarabati iliyokiwa Pemba | 100 | 70 | 70 | Ukarabati unaedelea kwa hatua mbali mbali, kizimbati, Mkoani na Ole Dodeani tayari majengo yashawekwa mageti na kazi zinazoendelea kusugua tarazo pamoja na kuweka miundombinu ya umeme na kwa upande wa ghala la weni lipo hatua ya kuezeka |
| | Idadi ya tani za mchele zilizonunuliwa | 556 | 0 | 0 | Mchakato wa kufanya makubaliano (MoU) ya ununuaji wa mpunga kutoka Tanzania Bara ulishakamilika. Mchakato wa manunuzi ya mchele kutoka NFRA bado haujaanza |
| Ujenzi wa Kituo cha Uhifadhi wa Chakula – Unguja | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Taratibu za manunuzi kwa kumpata Mshauri Elekezi wa ujenzi umeshaanza. Kituo cha hifadhi kitakuwa na ukubwa wa G+2 na maabara. |

### b) Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania

Mradi huu una lengo la kusaidia uhimilivu wa mfumo wa chakula kwa kuimarisha utoaji wa huduma za kilimo, kupitisha teknolojia za kilimo zinazohimili mabadiliko ya tabianchi pamoja na kujenga uwezo wa uhimilivu katika mifumo ya chakula. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka wa fedha 2025/26, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 12.5 bilioni chini ya udhamini wa Mkopo wa Benki ya Dunia. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 7.5 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 15.79 bilioni sawa asilimia 211 zimepatikana kutoka Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanza hatua za ukarabati wa majengo ya maabara, miundombinu ya mbegu na vituo vya huduma kwa wakulima; | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Mkataba wa kuanza shughuli za ukarabati umesainiwa. |
| Kutoa mafunzo kwa maofisa ugani juu ya namna bora ya kutoa huduma kwa kutumia teknolojia ya habari na mafunzo kwa wakulima juu ya mbinu bora za uzalishaji na teknolojia ya kilimo shadidi na kuwafundisha vijana kutoa huduma mashambani kwa kutumia trekta ndogo ndogo za kilimo; | Idadi ya Maofisa ugani waliopatiwa mafunzo | 170 | 170 | 100 | Maofisa ugani wamefundishwa namna ya kutumia mfumo wa KilimoApp na usajili wa wakulima. Usajili wa wakulima unaendelea |
| | Idadi ya wakulima waliofundishwa njia bora za kilimo kwa kutumia teknolojia, kilimo biashara na udhibiti wa upotevu wa mazao baada ya mavuno. | 400 | 400 | 100 | Shughuli hii imetekelezwa kwa mafunzo ya mbinu bora za uzalishaji, na teknolojia ya kilimo shadidi. Shughuli inaendelea hadi wakati wa mavuno. |
| | Idadi ya vifaa vilivyonunuliwa | 24 | 24 | 100 | Vifaa vyote vimeshawasilishwa na mafunzo kwa vijana yameanza. |
| Kuendeleza tafiti ili kupata mbegu bora zinazoweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi; | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Shughuli hii ni endelevu. Tafiti tatu za kupata mbegu bora zinazoweza kuhimili athari za mabadiliko ya tabianchi (Mpunga, Muhogo na viazi) zimefikia hatua ya uthibitishaji |
| | Asilimia ya utafiti wa afya ya udongo iliyofkiwa | 100 | 40 | 40 | Shughuli hii ni endelevu na utafiti unaendelea. Jumla ya kanda sita za aina za udongo zimetambuliwa kwa kila kisiwa Unguja na Pemba. |
| Kukamilisha usarifu wa michoro kwa mabonde 16, kutafuta wajenzi na kuanza ukarabati wa miundombinu ya umwagiliaji katika mabonde 10 ya Bumbwisudi, Mtwango, Kianga, Kibokwa, Mwera, Makombeni, Tibirinzi, Weni, Saninga na Kinyakuzi. | Idadi ya hekari za miundombinu zilizofanyiwa ukarabati | 434 | 0 | 0 | Mkataba wa kuanza shughuli za ukarabati umesainiwa |

### c) Mradi wa Kuendeleza Mfumo wa Chakula, Matumizi na Urejeshaji wa Ardhi

Mradi una lengo la kuhifadhi misitu katika maeneo ya Kaskazini ‘A’ na ‘B’, kushirikisha sekta za kilimo, mazingira, ardhi na sekta nyengine zenye mnasaba pamoja na uhifadhi wa misitu na kusimamia rasilimali hiyo. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.2 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 720 milioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Uanzishwaji wa mfumo wa Taarifa na Mawasiliano | Asilimia ya utayarishaji wa mfumo iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Mfumo tayari upo katika server ya ndani kabla kuweka mtandaoni |
| Kuajiri Bwana na Bibi Shamba (Extension Officers) | Idadi ya bwana/bibi shamba waliojiriwa | 2 | 2 | 100 | Tayari bwana shamba mmoja na bibi shamba mmoja ameshaajiriwa |
| Mafunzo ya Jinsia na Usalama (Gender and Safe Guard) | Idadi ya maafisa waliopatiwa mafunzo | 1 | 1 | 100 | Mfanyakazi mmoja wa Mradi amepatiwa mafuzo hayo Tanzania Bara |
| Kuandaa Jukwaa jumuishi la Wadau (MSP) | Idadi ya Jukwaa Jumuishi lililoandaliwa | 1 | 1 | 100 | Kazi hii inahusishwa kuanzisha Jukwaa Jumuishi ambalo litapokea masuala ya kiutekelezaji wa Mradi ikiujumuisha Taasisi za Kiserikali, Jumuiya na sekta binafsi, hadi sasa iko ngazi ya Mkoa kwa ajili ya kukubalika kwa Jukwaa na kuzinduliwa |
| Mpango wa Usimamizi wa Mandhari Unganishi kwa maeneo ya Kinyasini Kisongoni Chaani na Kiashange Mkokotoni. | Mpango wa Usimamizi wa Mandhari Unganishi | 1 | 1 | 100 | Kazi hii inahusu Kuwepo kwa Mpango maalum wa Usimamizi juu ya maeneo ya kukusanya maji ikiwa kwa sasa mpango huo ushakabidhiwa kwa ngazi ya Mradi |
| Tathmini ya changamoto na fursa za kuboresha mifumo ya umiliki wa ardhi na usimamizi wa maji. | Asilimia ya tathmini ya maboresho iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Kazi hii inahusu mapendekezo ya sera na sheria kwa umiliki wa Ardhi na usimamizi wa Maji kwa Kaskazini Unguja ikiwa tathmini hiyo ishafanyika na kukabidhiwa katika ngazi ya Mradi |
| Tathmini ya kazi za mezani na uwanja wa mnyororo wa thamani wa mpunga (rice value chain) uliopo kwa lengo la kuangazia maeneo yanayoweza kuboreshwa katika uendelevu. | Asilimia ya tathmini iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Kazi hii inahusu tathmini ya wakulima wa mpunga kwa eneo la Kaskazini Unguja kwa sasa tathmini hiyo ishamalizika na kutoa maeneo stahiki yanayopaswa kufanyiwa kazi |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa Mikutano ya timu ya mradi wa mandhari na Wadau wa Ufuatiliaji Tanzania Bara na Unguja | Idadi ya Mikutano iliyofanyika | 3 | 100 | 100 | Kumefanyika mikutano ya timu ya mradi wa mandhari na Wadau wa Ufuatiliaji Tanzania Bara na Unguja (miwili Unguja na mmoja Tanzania Bara). |

## d) Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi

Mradi una lengo la kubadili mifumo ya chakula ili kuchochea uchumi jumuishi, kuongeza usalama wa chakula na lishe nchini pamoja na kuimarisha minyororo ya thamani ya mazao ya chakula ikiwemo: migomba, mihogo na mwani kwa kutumia mbinu jumuishi zinazokabiliana na mabadiliko ya tabianchi, kuongeza ujuzi na uwezo wa vijana na wanawake waweze kujiajiri na kupata fursa za kilimo katika miradi ya kijamii. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 1.44 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 865.05 milioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa vifaa vya umwagiliaji na uzalishaji wa mazao ya baharini; | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Wakulima 550 (wanawake 300 na wanaume 250) watapatiwa vifaa.<br>*Specifications* za vifaa zimeshaandaliwa na zipo katika hatua ya manunuzi |
| Kuanzisha mashamba yenye ukubwa wa ekari 1 au zaidi ya mfano ya uzalishaji kibiashara kwa kutumia dhana ya shamba darasa; | Idadi ya mashamba yaliyoanzishwa. | 30 | 5 | 17 | Jumla ya mashamba 30 (Kaskazini Unguja 15 na Kaskazini Pemba 15) yamepangwa kuanzishwa kati ya hayo 5 (Kaskazini Unguja 3 na Kaskazini Pemba 2) yameanza kufanyiwa kazi. Na tayari Mkataba umesainiwa baina ya FAO na Taasisi isiyo ya Kiserikali (RECODA) kwa ajili ya kuandaa mashamba mengine 26 na kuwajengea uwezo wakulima husika |
| Kuanzisha mashamba ya kibiashara ya uzalishaji na usambazaji wa mbegu bora za mihogo; | Idadi ya mashamba yaliyoanzishwa. | 8 | 0 | 0 | Mashamba yanatemegemewa kuanzishwa (Kaskazini Unguja 4 na Kaskazini Pemba 4). Aidha, Mkataba umeandaliwa baina ya FAO na Taasisi ya Utafiti wa Mazao ya Kilimo na Mifugo Zanzibar (ZALIRI) kwa ajili ya kusaidia wakulima kuzalisha na kusambaza mbegu. |
| Kutoa taaluma ya uhifadhi wa mazao, uongezaji wa thamani, ubora wa bidhaa na utafutaji wa masoko | Asilimia ya taaluma iliyotolewa | 100 | 2 | 2 | Hatua za awali zimeanza hususan katika zao la mwani |
| Kutengeneza Mpango Mkakati wa zao la mwani na kushauri muundo wa kitaasisi. | Asilimia ya mpango mkakati iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | ToR kwa ajili ya kumtafuta Mshauri Elekezi kuifanya kazi hiyo imeandaliwa na taratibu za manunuzi zinaendelea |

### e) Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na Kuhakikisha Usalama wa Chakula

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mfumo wa Kitaifa wa udhibiti wa uingizaji na usafirishaji wa mazao ya kilimo, kuongeza upatikanaji mazao ya kilimo na kukuza masoko ya Kitaifa na Kimataifa. Vile vile, kuimarisha afya ya mimea na mifumo ya ulinzi wa mimea. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.37 bilioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.42.96 bilioni zilipangwa kutumika Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuwajengea uwezo watumishi wa Kitengo cha Utibabu wa Mimea na Ukaguzi wa Mazao; | Idadi ya watumishi waliopatiwa mafunzo | 25 | 25 | 100 | Watendaji 25 wa Divisheni kutoka Unguja na Pemba walipatiwa mafunzo ya usimamizi wa viuwatilifu ikiwemo ukaguzi wa maghala ya kuhifadhi viuwatilifu na maduka ya viuwatilifu. Aidha, Watendaji walipatiwa mafunzo ya kutumia mfumo wa kidigitali wa *Kobotoolbox* kwa malengo ya kufanya tathminiina ufuatiliaji katika sekta ya Afya ya Mimea |

### f) Mradi wa Kuimarisha usimamizi wa Hifadhi ya Akiba ya Ufufuma -Pongwe

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuwaunganisha na kuwalinda wanyama adimu ambao wanapatikana katika hifadhi, kuongeza mapato yatokanayo na rasilimali za Misitu kwa Shehia zitakazonufaika na mradi. Kupitia Mradi huu zimetangazwa rasmi hekta 1,988 za msitu kuunganisha hifadhi za Jozani na Kiwengwa pamoja na kuimarisha usimamizi na kuongeza alama za vipimo vya ufuatiliaji na usimamizi wa maeneo yaliyohifadhiwa. Mradi huu unatekelezwa kwa fedha za Washirika wa Maendeleo na kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS120.00 milioni. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 72 milioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa ramani za êneo lililopendekezwa na kuutambulisha mradi kwa wadau; | Asilimia ya Uandaaji wa ramani iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ramani ya eneo imeandaliwa ambapo wapimaji pamoja na wanajamii wa Shehia husika walipita kwenye maeneo yote. Aidha, eneo la Chwaka limetolewa kutokana na kuwa wananchi wake hawakutoa ridhaa. |
| | Idadi ya Shehia zilizofikiwa | 8 | 8 | 100 | Wadau wote walifikiwa kwa lengo la kuutambulisha Mradi |
| Kufanya Mapitio ya Mkataba wa Usimamizi wa Misitu ya Jamii na kuzitangaza katika gazeti rasmi la Serikali; | Asilimia ya mapitio iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Mkataba umeanza kufanyiwa mapitio kwa Shehia 7 kwa kufanya mapitio kwenye Kamati za Usimamizi wa Misitu ya Jamii. |
| Kutoa elimu kwa shehia juu ya uhifadhi na usimamizi shirikishi kwa jamii ikiwemo wanafunzi; | Idadi ya Shehia zilizopatiwa elimu. | 8 | 8 | 100 | Elimu imetolewa kwa wanajamii na wanafunzi katika Skuli za karibu na eneo la misitu kwenye Shehia 8 (Bambi, Pagali, Umbuji, Jendele, Chwaka, Marumbi, Uroa na Pongwe) |
| Kufanya mapitio ya azma na kuitangaza hifadhi (Final order); | Asilimia ya mapitio iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Azma (notice of intent) ya kuitangaza hifadhi hiyo imeandaliwa na ipo kwa Mchapaji wa Serikali kwa lengo la kuitangaza katika Gazeti rasmi la Serikali. |
| Kuandaa mfumo wa kuweka kumbukumbu ya malalamiko na kero za wanajamii | Asilimia ya uandaaji wa Mfumo iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Mafunzo ya Mfumo ambao utaweza kutekelezeka na kuweza kutatua kero yametolewa kwa watekelezaji wa Mradi kutoka Ofisi mbali mbali za SMZ pamoja na Viongozi wa Shehia na Kamati za Uhifadhi ndani ya Shehia. |

### 11.2.14 Wizara ya Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto

Wizara hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha ustawi wa jamii kwa upatikanaji wa huduma bora za jamii, wazee na watoto sambamba na kushajihisha maendeleo ya kijamii na kuleta usawa wa kijinsia. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza miradi mitatu ya maendeleo itakayogharimu jumla ya TZS 6.49 bilioni (TZS 1.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 4.99 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 3.89 bilioni (TZS 900 milioni kutoka Serikalini na TZS 2.99 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa kutekeleza miradi kama ifuatavyo:-

### a. Mradi wa Hifadhi ya Wazee.

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2026 Mradi una lengo la kukuza ustawi wa wazee kwa kuimarisha usalama wao, kuhakikisha wanaishi katika makaazi mazuri na wanapata huduma zao za msingi. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1.5 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai hadi Machi 2026 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 900 milioni Hadi kufikia Machi, 2026. Jumla ya TZS 1.39 bilioni sawa na asilimia 155 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ukarabati katika makaazi ya wazee Sebleni – Unguja; Limbani – Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa Sebleni | 100 | 70 | 70 | |
| | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa Limbani | 100 | 90 | 90 | |

### b. Mradi wa Mapambano Dhidi ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Wasichana.

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2023/2024 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2028/2029 Mradi una lengo la kumaliza vitendo vya udhalilishaji kwa wanawake na wasichana. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 636.32 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 381.79 milioni. Hadi kufikia Machi, 2026 shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa Sera ya Maendeleo ya Jamii | Asilimia ya uandaaji iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Rasimu ya awali ya Sera maendeleo ya Jamii imeshatayarishwa hatua iliyobakia ni kupelekwa kwa wadau kwa kuipitia na kuiboresha. |
| Kuandaa Mpango Mkakati wa kupambana na ukatili na udhalilishaji; | Asilimia ya uandaaji iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Mkakati wa Mpango wa Kitaifa wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji umekamilika. |

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya uhamasishaji wa Vikundi vya Wanajamii vinavyojishughulisha na mapambano dhidi ya Vitendo vya Udhalilishaji | Idadi ya Vikundi vitakavyofikiwa | 65 | 50 | 77 | Vikundi hivyo vipo katika Wilaya ya Kusini Unguja na Mkoani Pemba wilaya ambazo zinanufaika na mradi huo. |
| Kufanya Mapitio ya sera ya Jinsia ya mwaka 2016 | Asilimia ya mapitio iliyofikiwa | 100 | 60 | 60 | Rasimu ya mapitio ya sera imekamilika na kupelekwa kwa wadau Pemba, hatua iliyobakia ni kuwasilishwa kwa wadau Unguja na Kamati ya uongozi ili iendelee na hatua nyengine ya uandaaji wa sera mpya. |

### c. Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2024/25 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2028/29 Mradi una lengo la kukuza fursa za kiuchumi kwa wanawake pamoja na kukabiliana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji Tanzania. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 4.35 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha miezi tisa kuanzia Julai 2025 hadi Machi 2026, mradi ulipangiwa kutumia Jumla ya TZS 2.61 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026 jumla ya TZS 4.25 bilioni sawa na asilimia 163 zimepatikana kutoka Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa muongozo wa jamii wa uendeshaji na utoaji wa mikopo | Asilimia ya uandaaji wa muongozo iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Muongozo umekamilika. Kwa sasa, umewasilishwa Benki ya Dunia kwa ajili ya maoni ya mwisho. |
| Kufanya kikao cha robo mwaka cha uratibu wa usimamizi wa mikopo na Timu ya Utekelezaji ya Wilaya | Idadi ya vikao vya vilivyofanyika | 3 | 1 | 33 | Kikao kimoja kimefanyika kwa lengo la kuandaa Timu ili iweze kufanya uhamasishaji wa mradi katika ngazi ya Shehia, hususan vikundi vya kiuchumi vya wanawake. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa muongozo wa uendeshaji wa mikopo, fomu na mikataba. | Asilimia ya muongozo iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Mradi umeandaa Mwongozo wa Uendeshaji wa Mikopo unaoweka taratibu za utoaji na usimamizi wa mikopo. Fomu ya maombi ya mkopo inayojazwaa na muombaji wa mkopo na Mkataba wa makubaliano baina ya muombaji wa mkopo na Mamlaka ya Uwezeshaji wananchi kiuchumi |
| Kufanya utafiti wa awali kuhusu mila, desturi na mienendo hasi ya kijamii inayokwamisha usawa wa kijinsia na kuchochea ukatili wa kijinsia | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 2 | 2 | Hadidu rejea imetayarishwa na ipo katika hatua ya kutafuta mshauri elekezi kwa ajili ya kufanya utafiti huo |
| Kufanya utambuzi wa watoa huduma za udhalilishaji wa kijinsia katika Wilaya (Unguja na Pemba). | Idadi ya Wilaya zilizofanyiwa utambuzi | 8 | 8 | 100 | |
| Kuwezesha timu ya kitaalamu kuandaa miongozo (Mwongozo wa Uendeshaji kwa Wasimamizi wa vituo vya kijamii vya malezi ya watoto, Miongozo ya Malezi na Makuzi ya Watoto (ECD), na muongozo wa kujifunzia kwa vituo vya kijamii vya malezi ya watoto . | Idadi ya miongozo iliyoandaliwa | 3 | 0 | 0 | Hadidu rejea zimeshatayarishwa kwa ajili ya kutafuta mtaalamu wa kufanya kazi hii. |

### d. Mradi wa Kuimarisha mfumo wa Hifadhi ya Mtoto

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2010 yenye lengo la kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa watoto. Kwa mwaka 2025/2026, mradi huu umepangiwa kutumia jumla ya TZS 150 milioni kutoka kwa washirika wa maendeleo (UNICEF). Katika kipindi cha Julai 2025 hadi Machi, 2026. Jumla ya TZS 90 milioni zimepangwa. Hadi Machi 2026 mradi huu umetekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya ziara za usimamizi na ushauri elekezi wa vitendo kwa maafisa wa ustawi wa Jamii wa wilaya katika kusimamia mashauri ya watoto wanaoikinzana na sheria. | Idadi ya Ziara zilizofanyika | 13 | 13 | 100 | Ziara zilifanyika katika ngazi za Wilaya kwa ajili ya kufanya mashauriano ya pamoja katika kushughulikia mashauri yanayohsu watoto ambapo baadhi ya Wilaya zilitembelewa zaidi ya mara moja hasa za Mkoa wa Mjini Magharibi |
| Kuchapisha muongozo wa malezi ya malezi | Idadi ya nakala za muongozo iliyochapishwa | 200 | 0 | 0 | Nakala zipo katika hatua ya kuchapishwa. |
| Kuchapisha vitabu vya kuelimisha Watoto na wazazi kuhusu ukatili wa Watoto kwa njia ya mtandao. | Idadi ya vitabu vilivyochapishwa | 500 | 0 | 0 | Vitabu vipo katika hatua ya kuchapishwa. |
| kufanya ziara za ufuatiliaji kwa familia kwa watoto wanaohudhuria mpango wa marekebisho ya tabia na waliomaliza programu | Idadi ya ziara zilizofanyika | 70 | 90 | 128.5 | Watoto waliofanyiwa ziara na kufikiwa walikuwa 90 ambapo 6 watoto wa kike na 84 wa kiume |
| Kuandaa Muongozo wa Programu ya Marekebisho ya tabia wa Zanzibar. | Asilimia ya uandaaji wa muongozo iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | |
| Kufanya kikao cha kupitia tafsiri ya Muongozo wa Programu ya marekebisho ya tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria | Idadi ya vikao vilivyofanyika | 1 | 1 | 100 | |
| Kuandaa kikao cha wadau cha kurasimisha Muongozo wa Programu ya Marekebisho ya Tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria | Idadi ya vikao vilivyofanyika | 1 | 1 | 100 | |
| Kufanya kikao na Kamati ya Uongozi wa Wizara kwa ajili ya kupitia Muongozo wa Programu ya Marekebisho ya Tabia kwa watoto wanaokinzana na sheria | Idadi ya vikao vilivyofanyika | 1 | 1 | 100 | |
| Kuandaa kikao na maafisa Ustawi wa jamii wa Wilaya wa kujadili maendeleo na changamoto za Mfumo wa kuhifadhia taarifa za hifadhi ya mtoto CPIMS (PRIMERO) | Idadi ya vikao vilivyofanyika | 4 | 1 | 25 | Kikao cha robo ya kwanza kimefanyika kinachowakutanisha maafisa Ustawi wa Jamii wa Wilaya na wa ngazi ya Taifa pamoja na wasimamizi wa mfumo |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kufanya tathmini ya mahitaji ya utekelezaji wa mmfumo wa kuhifadhia taarifa ya hifadhi ya mtoto (PRIMERO) katika ngazi ya Wilaya Unguja na Pemba | Asilimia ya tathmini iliyofanyika | 100 | 100 | 100 | Tathmini imefanyika na ilijikita kujua mahitaji, hali halisi na changamoto za utumiaji wa mfumo katika ofisi za Wilaya na watendaji kwa ajili ya kupata mapendekezo na kuuboresha. |
| Kuandaa kikao cha kikosi kazi jumuishi cha kusimamia utafiti wa Ukatili dhidi ya watoto na vijana 2024 | Idadi ya vikao vilivyoandaliwa | 2 | 2 | 100 | Vikao viwili vya kikosi kazi jumuishi vilifanyika kwa miezi miwili ambavyo ni vikao vya mwisho baada kukamilika utafiti. |
| Kufanya kikao cha wataalamu na wadau cha kutengeneza mpango wa matumizi ya taarifa na ripoti ya utafiti wa Ukatili dhidi ya Watoto 2024 | Idadi ya vikao vilivyoandaliwa | 2 | 2 | 100 | Kikao cha kwanza kilifanyika Dar Es Salaam na kikao cha pili cha kumalizia mpango wa matumizi kimefanyika Zanzibar. |
| Kuandaa kikao cha kamati elekezi cha viongozi wa Serikali na Taasisi kutoka Tanzania Bara na Zanzibar (steering Committee) kwa ajili ya kupokea ripoti ya utafiti na kujadili matumizi ya taarifa za utafiti. | Idadi ya vikao vilivyoandaliwa | 1 | 1 | 100 | Kikao cha Kamati elekezi ya viongozi kilikuwa ni kikao cha pili na cha mwisho baada kukamilika utafiti ambacho cha kwanza kilifanyika wakati wa kuanza utafiti. |
| Kununua vifaa vya ofisi kwa ajili ya kuimarisha ofisi | Asilimia ya ununuzi iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Printa 1ya rangi na makabati 2 yalinunuliwa kwa ajili ya matumizi ya ofisi. |

### e. Mradi wa Kusimamia Sheria ya Jinsia na Sera

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2002 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2025. Mradi una lengo la kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji kwa wanawake na watoto. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 862.57 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya TZS 517.54 milioni zilipangwa. Hadi kufikia Machi 2026 shughuli zifuatazo zilitekelezwa kwa fedha za bajeti ya mwaka 2024/2025:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa Mpango Mkakati wa kupambana na vitendo vya ukatili na udhalilishaji; | Asilimia ya uandaaji wa Mipango iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Mpango Mkakati wa Mikoa wa kupambana na vitendo vya Ukatili na udhalilishaji kwa upande wa Mkoa wa Mjini magharibi umeshaandaliwa na umeshakamilika. |
| Kuwajengea uwezo watendaji hasa watu wenye ulemavu | Idadi ya Mikutano iliyofanywa. | 5 | 4 | 80 | Mikutano ya namna ya kuwajengea uwezo watendaji juu ua Mpango Mkakati wa Mkoa Mjini Magharibi imefanyika |
| Kuandaa mikutano ya kuratibu na kuripoti kesi za vitendo vya ukatili na udhalilishaji Unguja na Pemba; | Idadi ya Mikutano iliyofanyika | 4 | 2 | 50 | Mikutano 2 imefanyika Unguja na Pemba |
| Kufanya mikutano na viongozi wa Dini katika Mkoa wa Kaskazini Unguja na Pemba | Idadi ya Mikutano iliyopangwa | 4 | 2 | 50 | Mikutano miwili (2) imefanyika Unguja na Pemba. |
| Kufanya Mkutano wa Chaguo langu haki yangu | Idadi ya Mikutano iliyofanyika | 4 | 2 | 50 | Mikutano imefanyika, washiriki waliweza kuwasilisha ripoti za utekelezaji kwa kipindi cha robo ya kwanza Julai hadi Septemba 2025/26 |
| Kutoa Mafunzo ya uhamasishaji wa rasilimali kwa majukwaa ya Usimamizi wa Kesi za Ukatili wa Kijinsia | Idadi ya washiriki waliohudhuria | 60 | 60 | 100 | Mafunzo yamefanyika kwa majukwaa ya usimamizi wa kesi za ukatili wa kijinsia |
| Kutoa mafunzo juu ya kuripoti taarifa zinazohusiana na Vitendo vya Ukatili wa kijinsia (GBV/VAWC) kwa waandishi wa habari | Idadi ya waandishi wa Habari waliopatiwa mafunzo | 28 | 28 | 100 | Vyombo vya habari vilivyohusika katika mafunzo ni ZBC redio na TV, Zanzibar leo, Daily News, Mwananchi, TBC na Redio Jamii Tumbatu**.** |
| Mafunzo ya amali kwa wanawake na wasichana walio katika mazingira hatarishi | Idadi ya wanawake waliopatiwa mafunzo | 20 | 23 | 115 | Mafunzo yamefanyika kwa kipindi cha miezi 6 ambapo wanawake 12 wamekamilisha mafunzo ya ushonaji, 10 mafunzo ya ushoni na mmoja mafunzo ya huduma za uembo na saluni. |
| Warsha ya usambazaji wa Mpango Mkakati wa Utekelezaji wa Kupinga Vitendo vya Ukatili dhidi ya Wanawake na Watoto kwa Ngazi ya Mkoa wa Mjini Magharib na Mkoa wa Kusini Pemba | Idadi ya washiriki waliohudhuria | 70 | 70 | 100 | |
| Kuendesha Mafunzo juu ya utumiaji salama na makini wa teknolojia ya mtandao (intaneti) kwa wanafunzi wa vyuo vikuu | Idadi ya wanafunzi waliopatiwa mafunzo | 100 | 45 | 45 | Vyuo vikuu mbali mbali viliweza kushiriki vikiwemo Zanzibar University (ZU) SUMAIT, Chuo cha Maendeleo ya Jamii TENGERU na SUZA |

### 11.2.15 Wizara ya Maji, Nishati na Madini

Wizara hii inasimamia sekta kuu tatu ambazo ni maji, nishati na madini ambazo ni nguzo muhimu katika kuchochea maendeleo ya nchi pamoja na ustawi wa wananchi wa Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutumia jumla ya TZS 205.36 bilioni (TZS 65.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 139.97 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) kwa ajili ya kutekeleza Programu mbili. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 123.21 bilioni (TZS 39.23 bilioni kutoka Serikalini na TZS 83.98 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zimepangwa kugharamia program za maendeleo kama ifuatavyo:-

#### i. Programu ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuhakikisha upatikanaji endelevu wa maji safi na salama katika maeneo ya mijini na vijijini kwa Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutekeleza miradi tisa ya maendeleo:-

#### a) Mradi wa Uhuishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar

Mradi wa Uhuishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar (Miji 25 - INDIA) ni sehemu ya juhudi upatikanaji wa huduma ya maji safi na usafi wa mazingira Zanzibar. Kazi kuu za mradi ni uimarishaji wa huduma za Maji Endelevu Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 16.17 bilioni (TZS 2.52 bilioni kutoka Serikalini na TZS 13.65 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 9.70 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS1.51 bilioni kutoka Serikalini na TZS 8.19 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 14.27 bilioni sawa na asilimia 147 zimepatikana  kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Malipo ya awali ya Mkandarasi kwa ajili ya utekelezaji wa shughuli za mradi | Asilimia ya malipo iliyofanyika | 100 | 2 | 2 | Taratibu za manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi zinaendelea |

### b) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar

Mradi huu una lengo la kuimarisha miundombinu ya maji kwa kufanya usambazaji na uzalishaji wa maji safi na salama katika maeneo ya visiwa vya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026 mradi huu umepangiwa jumla ya TZS 15.78 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS9.47bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia machi 2026, jumla ya TZS16.95 bilioni sawa na asilimia 179 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa pampu maalumu, vifaa na bomba za kusafirishia maji | Idadi ya pampu zilizonunuliwa | 50 | 40 | 80 | Pampu za maji zinaendelea kunuliwa |
| Ujenzi wa hifadhi za "hydrant" pamoja na ununuzi wa vifaa vya maji na bomba za kusafirishia maji. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 50 | 50 | Hatua za ujenzi wa "hydrant", na ununuzi wa vifaa vya maji na bomba za kusafirishia maji zinaendelea. |
| Ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji. | Idadi ya Matangi yaliyojengwa | 12 | 12 | 100 | Malipo ya fedha ya ununuzi wa Matangi kwa Kampuni "SBS Solution East Africa ltd" ya Kenya yanaendelea kufanyiwa kazi. Tayari ujenzi wa foundation kwa ajili ya kufunga Matangi manne ya maji ya Zink Aluminium inaendelea katika maeneo ya Kengeja 1, Mtambwe Kusini 1, Mtambwe Kaskazini 1 na Raha 1.<br>Aidha, ukarabati wa tangi la lita 250,000 la Kengeja umekamilika. |
| Ulipaji wa fidia za vipando na majengo katika maeneo ya uimarishaji wa miundombinu ya maji (Maeneo yenye visima vya Ras el Khaimah). | Asilimia ya malipo yaliyofanyika. | 100 | 50 | 50 | Ulipaji wa fidia unaendelea |

### c) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji Maji Mkoa wa Mjini Magharibi

Mradi huu una lengo la kuongeza uzalishaji na usambazaji wa maji katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi na Wilaya zake ili kupunguza changamoto za

upatikanaji wa huduma hiyo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 41.49 bilioni (TZS 1.54 bilioni kutoka Serikalini na TZS 39.95 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS24.89 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS.924 milioni kutoka Serikalini na TZS 23.97 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 59.69 milioni sawa na asilimia 0.2 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa taarifa ya kina ya kitaalamu (details design) ya mradi. | Asilimia ya taarifa iliyoandaliwa. | 100 | 100 | 100 | Kazi hiyo imekamilika. |
| Kuandaa mpango na utaratibu wa manunuzi kwa ajili ya kupata Mkandarasi. | Asilimia ya mpango na utaratibu wa manunuzi ulioandaliwa | 100 | 70 | 70 | Mpango wa manunuzi kwa ajili ya kumpata Mkandarasi unaendelea. |
| Kuandaa Mikataba kwa ajili ya Mkandarasi. | Asilimia ya mikataba iliyoandaliwa. | 100 | 65 | 65 | Mshauri Elekezi ameshaandaa tender document kwa ajili ya Mkandarasi, ambayo kwa sasa ipo kwa Washirika wa Maendeleo JICA kwa ajili ya kuweka mapendekezo.<br>Ripoti ya EIA imeandaliwa ili kuweza kukamilisha taratibu na masharti ya mradi. |

### d) Mradi wa Uboreshaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Kaskazini Unguja

Mradi huu una lengo la kuimarisha upatikanaji wa huduma ya maji hususan katika Mkoa wa Kaskazini Unguja kwa kufanya ukarabati wa visima na kuweka miundombinu ya umeme na pampu zinazotumia umeme wa jua kwa ajili ya kuendeshea visima hivyo. Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Kampuni ya National Energy Centre (NEC) ya Oman. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.60 bilioni kutoka Serikalini). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS1.56 bilioni zilipangwa kutumika. kutoka Serikalini Hadi kufikia Machi 2026,j umla

ya TZS 7.32 bilioni sawa na asilimia 469 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kukarabati na kuchimba visima vipya pamoja na ujenzi wa matangi ya kuhifadhia maji | Idadi ya visima vilivyochimbwa | 3 | 3 | 100 | Visima vimechimbwa Mahonda (2) na Kiashangi - Matemwe (1) |
| | Idadi ya matangi yaliyojengwa | 3 | 2 | 66 | Matangi mawili ya Kilindi yako katika hatua za juu za ujenzi GLSR civil 100% (mechanical pending), ESR RCC work inaendelea; Mahonda bado kwenye hatua ya kuanza civil works. GLSR design approved lakini civil haijaanza. |
| | Idadi ya vibanda vilivyojengwa | 15 | 15 | 100 | Jumla ya vibanda nane (8) ni vipya na saba (7) Vimefanyiwa marekebisho |
| Kuweka mifumo ya umeme wa jua katika visima na kununua pampu zinazotumia umeme huo | Idadi ya pampu zilizonunuliwa | 51 | 19 | 37 | Pump houses mpya ziko 85% average completion; rehab only 5% complete. Kazi bado inaendelea kwenye stages za roofing, fencing, solar & commissioning |
| | Idadi ya kilomita zilizolazwa mabomba kwa wananchi | 22.835 km | 4.648 km | 20.35 | Kutoka Machui, Kilindi TL na sehemu za Kiwengwa kazi inaendelea lakini bado chini ya 25%.. |
| | Idadi ya kilomita zilizolazwa mabomba | 7 | 7 | 100 | |
| | Asilimia ya ununuzi wa mita uliofanyika | 10,000 | 100 | 100 | Mita zimeagizwa na zinatarajiwa kuwasili katika kota ijayo. |
| Ununuzi wa Vifaa Muhimu (Solar Panels, Tank Materials, Pumps) | Asilimia ya Vifaa Vilivyowasili | 100 | 40 | 40 | Vifaa katili vimewasili (pipes, fittings), lakini solar panels & tank roof materials ziko transit; mechanical works hazijaanza. |
| Kuweka Miundombinu ya Solar Pumping | Asilimia ya Ufungaji wa Solar uliofikiwa | 100 | 35 | 35 | Solar foundations 35% complete; mounting & installation = 0%; panels bado hazijafika site |
| Kuunganisha Kaya na huduma za maji safi na salama | Asilimia ya kaya ziliofikiya | 100 | 20 | 20 | House connection bado kwenye hatua ya "finalization"; survey imeanza lakini installation haijaanza |
| Ufuatiliaji wa Hatari (Risk Management) | Idadi ya Hatari zilizofuatiliwa | 6 | 6 | 100 | Hatari zinazoathiri mradi: (1) kuchelewa kwa SBLC, (2) vifaa kuchelewa, (3) solar installation delay, (4) rehabilitation slow progress, (5) heavy rock breaking delays, (6) delays in compensation. |
| Uzingatiaji wa ESMP (Mazingira + Usalama Kazini) | Asilimia ya Utekelezaji iliyofikiwa | 100 | 75 | 75 | Usalama kazini unazingatiwa; lakini trench excavations, rock breaking & waste disposal zinahitaji usimamizi wa karibu. |
| Uwezo wa Miundombinu Kuanza Kufanya | Asilimia ya Utayari iliofikiwa | 100 | 20 | 20 | Commissioning haijaanza; pumps, PLC, solar systems na mechanical works za tanks bado hazijawekwa. |

**e. Mradi wa Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar**

Mradi huu una lengo la kuimarisha hali ya upatikanaji wa huduma ya maji safi na salama katika maeneo ya kisiwa cha Pemba. Mradi unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW). Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 71.43 bilioni (TZS 2.60 bilioni kutoka Serikalini na TZS 68.83 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 42.85 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 1.56 bilion kutoka Serikalini na TZS 41.29 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 119.39 milioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 0.28 ya lengo la TZS 42.85 bilioni kutoka Serikalini kwa ajili ya uendeshaji na usimamizi wa mradi.

**f. Mradi wa Kuimarisha Usalama wa Maji na Uhimili wa Tabianchi Katika Maeneo ya Mijini**

Mradi huu una lengo la kuijengea uwezo sekta ya maji juu ya usimamizi wa usalama na upatikanaji wa maji nchini. Mradi umelenga kutekeleza maeneo makuu matatu (3) ambayo ni kusaidia Wizara katika usimamizi wa mikakati na miongozo ya mageuzi, kuanzisha mfumo jumuishi wa kukabiliana na mabadiliko ya tabinchi na uchafuzi wa kimazingira na kuijengea uwezo Mamlaka ya Maji Zanzibar ili iweze kujiendesha kibiashara. Mradi huu unatekelezwa kwa pamoja baina ya Serikali ya Mapinduzi ya Zanzibar na Benki ya Maendeleo ya Ujerumani (KfW) kupitia Shirika la Maendeleo la Ujerumani (GIZ). Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 2.01 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi2026, jumla ya TZS 1.21 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuandaa miongozo mbali mbali ya sekta ya maji na usafi wa mazingira | Asilimia ya uandaaji wa miongozo iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Muongozo na vibali vya utiririshaji wa majitaka, muongozo wa uchimbaji wa visima, muongozo wa utoaji vibali vya uchotaji maji ya chini ya ardhi na muongozo wa usimamizi wa maji na majitaka kwa hoteli unaendelea |
| Kusaidia Wizara ya Maji, Nishati na Madini (MoWEM) katika kuandaa Sheria ya Maji na Usafi wa Mazingira na Sheria ya Usimamizi wa Rasilimali za Maji. | Asilimia ya uandaaji wa Sheria iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Mshauri Elekezi wa kuandaa Sheria ya maji ameshapatikana. Hatua za mazungumzo na mikataba zinaendelea. |
| Kuhuisha (update) Utafiti wa Gharama za Huduma na mwongozo wa upangaji wa viwango vya ada za maji kwa mchakato shirikishi. | Asilimia ya utafiti iliyofikia | 100 | 10 | 10 | Mshauri Elekezi amepatikana kwa ajili kufanya utafiti huo. |
| Kuandaa Mpango wa miji kwa pamoja (Joint Town Planning - JTP) kwa miji iliochaguliwa | Asilimia ya mpango miji iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hatua za manunuzi ya kumpata Mshauri Elekezi kwa ajili ya taratibu za upangaji wa miji kwa pamoja (JTP) katika mji wa Chake Chake zinaendelea |
| Ushirikiano na Tume ya Utalii na Chama cha Wamiliki wa Hoteli Zanzibar (ZATI) katika kusaidia taasisi hizo kukuza usimamizi endelevu wa maji kwa hoteli. GIZ imekuwa ikitoa mafunzo na programu za kujenga uwezo kwa hoteli kuhusu matumizi ya majitaka | Asilimia ya utoaji mafunzo iliyofikiwa | 100 | 10 | 10 | Huduma za ushauri zimepatikana. Ushirikiano na wadau umeshafanyika |
| Kufanya utafiti wa mbinu za ukusanyaji wa maji ya mvua | Asilimia ya ukusanyaji maji ya mvua iliofikiwa | 100 | 100 | 100 | Utafiti unaohusu ukusanyaji wa maji ya mvua (RWH) katika miji umekamilika na matokeo yake yametolewa |
| Kujenga uwezo kwa Vikundi 14 vya Wanawake wa Chama cha Watumiaji wa Maji (Women Water User Association) Unguja kwa kushirikiana na Wizara ya Kilimo, Maliasili na Mifugo (MoAIL). | Idadi ya vikundi vilivyopatiwa mafunzo | 14 | 7 | 50 | Mafunzo yametolewa kuhusu ufanisi wa maji na hatua za kulinda vyanzo vya maji katika mipango ya umwagiliaji ili kulinda vyanzo vya maji. |

### g. Mradi wa Ununuzi wa "Chlorine", Usimamizi na Uangalizi Bora wa Maji

Mradi huu unatekelezwa kwa pamoja baina ya Mamlaka ya Maji Zanzibar na Shirika la Umoja wa Mataifa la kuhudumia Watoto Duniani (UNICEF). Lengo kuu la programu hii ni kutambua idadi ya visima binafsi pamoja na kutoa vifaa na dawa za kutibu maji. Kwa kipindi cha mwaka wa fedha 2025/2026 programu hii ilipangiwa kutumia TZS 40.0 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 24.0 milioni zilipangwa kutumika kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa kwa fedha za bajeti ya mwaka 2024/2025:-

| Shughuli iliopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji halisi | Asilimiaya utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutibu Maji | Asilimia ya Maji yaliopatiwa tiba. | 100 | 100 | 100 | Kiwango cha fedha kilipatikana cha kutosha na Maji yakaweza kupatiwa tiba ili wananchi watumie maji safi na salama. |
| Kuvitambu\a Visima binafsi | Idadi ya Visima vilivyotambuliwa | 25,460 | 22,634 | 88.9 | Zoezi la kuvitambua visima binafsi limekamilika. |

## ii. Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar

Programu ina lengo la kuwa na umeme wa kujitosheleza ikiwa ni nyenzo muhimu ya kuimarisha shughuli za kiuchumi, usafiri na huduma za jamii. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepanga kutekeleza miradi minne ya maendeleo.

### a) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme

Mradi huu una lengo la kuimarisha huduma za umeme pamoja na miundombinu ya umeme katika vijiji 305 (180 Unguja na 125 Pemba) ili kupata huduma ya umeme yenye uhakika. Kukamilika kwa mradi huu kutapunguza changamoto ya upungufu wa umeme katika maeneo tofauti ya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 7.00 bilioni kutoka Serikalini). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 4.20 bilioni zilipangwa kutumika kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2026, Shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Usambazi wa umeme katika vijiji vya Unguja na Pemba | Idadi ya Vijiji vilivyosambazwa umeme. | 65 | 61 | 93 | Vijiji 61 vilisambazwa umeme (33 Unguja na 28 Pemba). Kazi ya usambazaji umeme inaendelea katika maeneo mengine |
| Ununuzi wa nguzo na vifaa vya umeme | Idadi ya Nguzo zilizonunuliwa | 510 | 518 | 101 | |
| Ubadilishaji nguzo; | Idadi ya Nguzo zilizobadilishwa | 2500 | 1676 | 67 | Jumla ya nguzo za Umeme 1676 zimebadilishwa (Pemba ni 521 na Unguja ni 1,155) |
| Uunganishaji wa Wateja Wapya; | Idadi ya Wateja Wapya walio unganishwa Umeme Uguja na Pemba. | 43000 | 38,800 | 90 | Jumla ya wateja wapya 38,400 wameunganishwa (Pemba 15,200 na Unguja 23,200). |
| Uvutaji wa njia mpya za umeme | Idadi ya Wateja waliounganishwa | 2,500 | 2,650 | 106 | Jumla ya wateja wapya 2,650 wameunganishwa, kwa Pemba ni 825 na Unguja ni 1,825. |

### b. Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati Zanzibar (ZESTA)

Mradi una lengo la kuimarisha miundombinu ya umeme na kuzijengea uwezo Taasisi zinazoshughulikia masuala ya nishati ili ziweze kuimarisha utoaji wa huduma za usambazaji wa umeme katika maeneo tofauti ya visiwa vya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 6.47 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 3.88 bilioni zilipangwa kutumika kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa kwa fedha za bajeti ya mwaka 2024/2025:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa laini kubwa ya umeme yenye uwezo wa kilovoti 132 pamoja na kufanya malipo kwa Mshauri Elekezi | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Mkandarasi anaendelea na kazi ya kufyeka njia ya umeme na ameanza uchimbaji wa misingi wa nguzo za umeme, Ripoti (Feasibility Study) ya solar pv na BESS zimekamilika. Aidha, tathmini ya kiufundi (technical evaluation) kwa ajili ya kumpata Mkandarasi atakayesambaza na kufunga mitambo ya kuhifadhia umeme (BESS) imekamilika, Ujenzi wa ukuta kwa ajili ya solar PV umekamilika na Ripoti ya SCADA imekamilika inayomuezesha mkandarasi kuanza ujenzi. |
| | Asilimia ya malipo yaliyofanyika | 100 | 25 | 25 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Uwekaji wa mfumo wa kidigitali wa usimamizi na uendelezaji wa miundombinu ya umeme | Asilimia ya uwekaji wa mfumo iliyofikiwa | 30 | 28 | 93 | Mkandarasi anaendelea na ujenzi wa vituo vya umeme kwa ajili ya ufungaji wa mitambo |
| Kuanza ujenzi wa miundombinu ya umeme wa jua pamoja vituo vya kupozea umeme katika maeneo ya Makunduchi, Ubago na Matemwe | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 20 | 0 | 0 | Tathimini ya kiufundi imepelekwa benki ya Dunia kwa ajili ya kupata idhini (No objecton) ili kuendelea na mapendekezo ya kifedha (Financial Proposal). |
| Kusimamia masuala ya jinsia katika sekta ya nishati | Asilimia ya usimamizi iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | |
| Kuwajengea uwezo watendaji katika sekta ya nishati | Idadi ya watendaji waliopatiwa mafunzo | 30 | 28 | 93 | Mafunzo yalifanyika katika maeneo ya utaalam wa kada na umeme wa jua nchini India |
| | Asilimia ya uzalishaji wa umeme wa jua iliofikia | 100 | 10 | 10 | Kazi ya kumpata mkandarasi kwa ajili ya ujenzi wa kihifadhio cha nishati ya umeme (BESS) katika eneo la Mtoni kwenye robo ya nne kwa Mwaka wa Fedha 2025/26 inaendelea. |
| Automatic Meter Reading (AMR) Integration of billing software | Asilimia ya Kukamilisha mifumo ya utoaji bili | 100 | 100 | 100 | Mafunzo kwa wataalamu wa ZECO kwa ajili ya ujengaji uwezo maswala ya bili yalishafanyika kwa mujibu wa Mkataba. Aidha, ZECO itaingia mkataba mfupi na Kampuni ya HEXING ya China ambayo itasaidia katika kukamilisha mfumo wa taarifa za wateja. |
| Ulipaji wa fidia katika maeneo yatakayoathirika na mradi | Idadi ya watu waliolipwa fidia | 1510 | 1,450 | 96 | Ulipaji wa fidia katika maeneo yatakayoathirika na mradi unaendelea.<br>Waathirika ambao hawajalipwa bado hawajawasilisha taarifa zao kwa ajili ya amalipo. |
| Utoaji wa mafunzo ya shughuli za uhamishaji wa wananchi katika maeneo ya mradi; | Asilimia ya mafunzo yaliyotolewa | 100 | 100 | 100 | Mafunzo yametolewa kwa wananchi katika maeneo ya mradi; |
| Mshauri Elekezi kwa ajili ya kuandaa Mpango Mkuu wa Umeme wa Miaka ishirini | Asilimia ya Ripoti ya Mpango Mkuu | 100 | 100 | 100 | Ripoti ya Mpango Mkuu wa Umeme imekamilika. |
| Kuandaa Mpango wa Bei ya Umeme kwa ZURA | Asilimia ya Mpango iliyofanyika | 100 | 100 | 100 | Ripoti ya Mpango wa bei ya umeme imekamilika |

### c. Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar

Mradi huu unalengo la kuboresha Mfumo wa Umeme Zanzibar na kuondoa changamoto ya umeme mdogo pamoja na kukatika kwa umeme mara kwa mara. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 33.36 bilioni kutoka Serikalini. ). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 20.01 bilioni zilipangwa kutumika kutoka Serikalini. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 54.23 bilioni sawa na asilimia 271 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa miundombinu ya umeme na kuweka vifaa maalumu vya kudhibiti na kuongeza nguvu za umeme | Asilimia ya uwekaji wa vifaa iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Uwekaji Voltage regulators kwa maeneo 8, Capacitor Bank kwa maene 26 na Usanikishaji wa kifaa maalumu STATCOM umekamilika. |

## 11.2.16 Wizara ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi

Wizara hii ina lengo la kuigeuza Zanzibar kuwa kitovu cha maendeleo ya Uchumi wa Buluu sambamba na kuimarisha usimamizi na matumizi endelevu ya rasilimali za baharí, kupitia fursa za uwekezaji katika uchumi wa buluu ikiwemo uvuvi wa bahari kuu, kilimo cha bahari, ufugaji wa mazao baharini, utalii wa baharini na fukwe, utafutaji na uchimbaji wa mafuta na gesi asilia na uratibu wa utawala na mazingira ya baharini. Wizara imedhamiria kuwawezesha wajasiriamali katika kukuza ubunifu, uwezo wa kupata zana, mitaji na masoko, pamoja na kuchangia katika sekta ya biashara na viwanda ambazo zitasaidia upatikanaji wa ajira na masoko kwa vijana. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza Programu nne na mradi mmoja wa maendeleo ambayo imepangiwa jumla ya TZS 157.08 bilioni (TZS 131.24 bilioni kutoka Serikalini na TZS 25.84 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) Kwa kipindi cha miezi tisa Julai 2025 hadi Machi 2026 jumla ya TZS 94.24 (78.74 bilioni kutoka Serikalini na TZS 15.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) zilipangwa kutekeleza Programu na Miradi kama ifuatavyo :-

### a) Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi

Programu hii ina lengo la kuongeza faida katika biashara ya mbegu za mazao, uvuvi na ufugaji wa samaki, kwa kutilia mkazo uwezeshaji wa wanawake na

na ushiriki wa vijana. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kiasi cha TZ 13.14 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, TZS 7.88 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ununuzi wa meli ya uvuvi wa bahari kuu; | Idadi ya meli zenye mita 25 zilizonunuliwa. | 1 | 0 | 0 | Uandaaji wa sifa za meli (specifications) umekamilika na umepata ridhaa kutoka IFAD. Hatua iliyofikiwa ni kufanyika kwa zabuni na kuchaguliwa mshindi atakaeweza kuiuzia wizara meli hizo. |
| | Idadi ya meli zenye mita 18 zilizonunuliwa | 5 | 0 | 0 | |
| | Asilimia ya ununuzi wa meli uliofikiwa | 100 | 30 | 30 | |
| Ununuzi wa gari aina ya lori na jokofu la tani 10 kwa ajili ya kampuni ya ZAFICO | Idadi ya malori ya jokofu yaliyonunuliwa | 3 | 1 | 33 | Utafiti wa majongoo bahari umekamilika. Aidha, utafiti wa kaa na samaki unaendelea kutekelezwa kwa kuzingatia malengo (research objectives) yaliyowekwa, ambapo baadhi ya malengo tayari yameshakamilika. Kwa sasa, hatua inayoendelea ni ununuzi wa vifaa vya kusaidia utafiti wa kaa na samaki. Mzabuni wa vifaa hivyo tayari amepatikana na mkataba umesainiwa, na vifaa vinatarajiwa kuwasilishwa ifikapo tarehe 17 Juni 2026. |
| | Asilimia ya ununuzi wa lori uliyofikiwa | 100 | 65 | 65 | |
| Kuanzisha mashamba darasa mawili ya ufugaji wa samaki kwa kutumia mabwawa na matangi na kuanzisha Karakana kwa ajili ya matengenezo ya vifaa na mitambo Unguja na Pemba; | Idadi ya mashamba darasa yaliyoanzishwa | 2 | 0 | 0 | Hadidu rejea (TOR) za kumtafuta mshauri elekezi zimekamilika. Hatua ya sasa ni kutafuta mshauri elekezi kupitia ZBA kubuni michoro na gharama za vifaa (BOQ) kwa kuanza ujenzi. |
| | Asilimia ya ujenzi uliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hadudi rejea (TOR) zimekamilika na kuwasilishwa Wakala wa Majengo (ZBA) kwa ajili ya kuendelea na taratibu za kuandaa michoro na BOQ |
| Ujenzi wa vituo viwili vya mafunzo ya Uvuvi na Ufugaji wa viumbe bahari (Mariculture Trainning Center) Unguja na Pemba | Asilimia ya ujenzi uliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea kufanya utafiti wa uzalishaji na ukuzaji wa aina tatu za mazao ya baharini (majongoo bahari, kaa na mwatiko); | Asilimia ya utafiti iliyofikiwa | 100 | 65 | 65 | Utafiti wa aina tatu za samaki na ununuzi wa vifaa vya utafiti huo unaendelea. |
| Kuandaa mpango wa ushirikiano kati ya sekta ya Umma na Binafsi (PPP) kwa kuendesha kiwanda na meli; | Asilimia ya kazi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hadidu Rejea (ToR) imekamilika na tangazo la zabuni lilishatolewa, kutokana na kupatikana kwa mwombaji mmoja (mshauri elekezi) imeshauriwa zabuni hiyo itangazwe tena ambapo hadi sasa mzabuni wa kazi hii hajapatikana. TAFICO na ZAFICO wanaendelea kushauriana na Kituo cha Ubia kati ya Sekta ya Umma na Binafsi (PPP Centre) ili kupata mwongozo sahihi wa namna bora ya kutekeleza kazi hio. |
| Ujenzi wa vituo vya kusarifu mwani | Asilimia ya ujenzi uliofikiwa | 100 | 5 | 5 | Hadudi rejea (TOR) zimekamilika na kuwasilishwa Wakala wa Majengo (ZBA) kwa ajili ya kuendelea na taratibu za kuandaa michoro na BOQ. |
| Ununuzi wa mashine tano za kuchakata mwani na vifaa vya kuongeza thamani zao la mwani; | Idadi ya mashine zilizonunuliwa | 5 | 5 | 100 | Ununuzi wa mashine umeshakamilika na mzabuni tayari ameshawasilisha wizarani. Hatua ya sasa ni kuzigawa kwa wanufaika wa programu Unguja na Pemba. |
| Kuendelea kutoa mafunzo kwa wakulima wa mwani kwa kutumia njia ya za kisasa (double loop method); | Idadi ya wakulima (jamii) wa mwani waliopatiwa mafunzo | 2,000 | 3,543 | 177 | Kazi imekamilika, ambapo jumla ya wakulima wa mwani 3,543 (wanawake 2,900 na wanaume 643) kutoka Unguja na Pemba wamepatiwa mafunzo kuhusu ukulima wa mwani katika kina kirefu. Aidha, jumla ya wakulima 9,999 (wanawake 7,690 na wanaume 2,309) wamepatiwa mafunzo ya mbinu bora za ukulima wa mwani katika kina kirefu kwa kutumia njia ya kamatia chini (double loop), kwa lengo la kuongeza tija na uzalishaji.. |
| Kuwapatia mafunzo na vifaa vijana wanaojitolea wa kituo cha *Building Better Tomorrow* kwa lengo la kuwasaidia kuongeza kipato chao | Idadi ya vijana waliopatiwa mafunzo | 1,000 | 536 | 54 | Jumla ya wanufaika 536 (356 mmke, 177 mme) wakiwemo wakulima wa mwani, wafungaji na Wavuvi wamepatikwa mafunzo juu ya fursa na taratibu za kupata mikopo kupitia wakala wa uwezeshaji wananchi kiuchumi (ZEA) pamoja na mafunzo ya viwango vya uzalishaji wa bidhaa za mazao ya Baharini kutoka ZBS |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzisha vitalu vya mwani kwa Unguja na Pemba | Idadi ya vitalu vilivyoanzishwa | 125 | 40 | 32 | Jumla ya vitalu vya mwani 40 vimeanzishwa kwa upande wa Unguja. Aidha kazi hii inaendelea kwa upande wa Pemba |

### b) Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini

Mradi una lengo la kuwawezesha wakulima wa mwani na wasindikaji wa mazao ya baharini kufikia maendeleo endelevu kwa kuongeza mnyororo wa thamani. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 2.69 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 1.61 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 2.68 bilioni sawa na asilimia 167 zimepatikana kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuanzisha mashamba manane ya majaribio ya mwani na majongoo bahari; | Asilimia ya uanzishaji wa mashamba ya mwani iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Uthibitishaji wa maeneo yaliyolengwa kwa ajili ya utekelezaji wa mradi umekamilika, ambapo maeneo ni Bweleo, Muungoni, Wambaa na Chokocho. Aidha, alama za mipaka zimewekwa katika maeneo husika kwa ajili ya ujenzi wa mashamba darasa ili kuhakikisha utambuzi sahihi wa maeneo na matumizi bora ya ardhi.Vilevile, muundo wa mashamba darasa umekamilika, ukihusisha matumizi ya mifumo ya ufugaji ya floating na Piling Systems. Sambamba na hilo, mchakato wa zabuni kwa ajili ya kuchagua kampuni ya kusambaza vifaa vya ujenzi wa mashamba hayo umekamilika. |
| Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu mwani Chokocho- Pemba | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 15 | 15 | Ujenzi wa kiwanda cha Chokocho Pemba, Kampuni ya Lupton, ni Mmshauri Elekezi na msimamizi wa mchakato wa ujenzi, tayari amekamilisha michoro ya kina ya kiwanda husika. Aidha, tathmini ya athari za kimazingira (EIA) kwa eneo la mradi imekamilika na ripoti yake imewasilishwa kwa mamlaka husika. Shughuli za usafishaji na ujenzi wa ukuta katika eneo hilo tayari zimeanza. |
| Kutoa mafunzo kwa wanawake 2000 wakulima wa mwani na majongoo bahari; | Idadi ya wanawake wakulima wa mwani waliopatiwa mafunzo | 2,000 | 716 | 36 | Jumla ya wakulima 238 wanaojishughulisha na kilimo cha mwani na majongoo bahari walipatiwa mafunzo ya ushirika. Mafunzo hayo yalikuwa shirikishi na yalijumuisha vipengele mbalimbali, yakilenga kubainisha changamoto zinazowakabili wanachama na kuwajengea uwezo wa kuzitatua kwa njia endelevu na za kiutendaji. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa mafunzo ya teknolojia ya kisasa ya kilimo cha mwani, kaa na majongoo bahari. | Idadi ya washiriki waliopatiwa mafunzo | 50 | 50 | 100 | Jumla ya wafanyakazi 50 walishiriki katika mafunzo yaliyogawanyika katika awamu tatu. Kati ya awamu hizo, awamu mbili zilifanyika nchini Korea, huku awamu moja ikifanyika Zanzibar ambapo wataalamu kutoka Korea walifika na kutoa mafunzo hayo. |

### c) Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki

Mradi una lengo la kuwawezesha wavuvi kupata huduma za msingi za bandari na masoko kwa kuwajengea miundombinu ya kisasa ya kuhifadhia na kuuzia samaki katika maeneo mbalimbali ya Unguja na Pemba. Kwa mwaka 2025/2026 mradi umepangiwa kiasi cha TZS 27.68 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 16.60 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 8.61 bilioni sawa na asilimia 52 bilioni zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa madiko na masoko katika maeneo ya Kama, Bumbwini, Nungwi na Kizimkazi kwa Unguja na kwa Pemba Kiwani, Kengeja na Msuka. | Asilimia ya ujenzi wa diko na soko la Fungurefu iliyofikiwa | 100 | 90 | 90 | Ujenzi wa majengo ya Biashara, Maduka ya bidhaa na Ghala la kuhifadhia samaki katika diko la kisasa na soko la samaki (Fungurefu - mkokotoni) Unguja, lipo katika hatua za ukamilishaji ikiwemo upigaji wa plasta ndani ya Soko, na uwekaji wa milango ya katika maduka na vyumba vya kuhifadhia samaki. |
| Ujenzi wa diko la kisasa na soko la samaki Mkoani Pemba. | Asilimia ya ujenzi wa diko na soko la Mkoani iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Ujenzi umekamilika na soko limefunguliwa na kuanza kutumika rasmi |

### d) Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya Kusarifu na Kuchakata Samaki

Mradi huu una lengo la kuimarisha mnyororo wa sekta ya uvuvi na uongezaji wa thamani wa bidhaa ya dagaa kupitia usindikaji wa kisasa pamoja na kujenga viwanda vitakavyoshughulikia ukusanyaji, uchakataji, uhifadhi na usambazaji wa dagaa kwa masoko ya ndani na nje ya nchi. Kwa mwaka wa 2025/2026, mradi umepangiwa kiasi cha TZS 51.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha

Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 30.60 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zifuatazo zimetekelezwa:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa kiwanda cha kusarifu dagaa Fungurefu, Ndagoni na Kama. | Asilimia ya ujenzi wa kiwanda cha Fungurefu iliyofikiwa | 100 | 16 | 16 | Ujenzi upo katika hatua za awali (*foundation)* |
| | Asilimia ya ujenzi wa kiwanda cha Kama iliyofikiwa | 100 | 62 | 62 | Majengo kama vile maduka, Ujenzi wa Barabara kwa kiwango cha zege, majengo ya kubeba kushusha na kuchemsha dagaa, majengo ya kubadilishia nguo, maeneo ya kuanika dagaa, jengo la kuhifadhi takataka na ujenzi wa kuhifadhia kemikali upo katika hatua za ukamilishaji, Ujenzi wa kiwanda cha kukausha dagaa upo katika hatau ya kuweka zege |
| | Asilimia ya ujenzi wa kiwanda cha Ndagoni iliyofikiwa | 100 | 43 | 43 | Baadhi ya majengo yamefikia hatua ya umaliziaji, jengo la kiwanda husika lipo katika hatua ya msingi hatua zinazoendelea na ujenzi wa Kiwanda na kukamilisha majengo mengine. |

### e) Mradi wa Utafiti wa Uchumi, Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii

Mradi una lengo la kupendekeza mikakati ya kukuza uchumi wa jamii, kuimarisha usalama wa chakula na maisha mazuri kwa jamii kwa kutumia mbinu shirikishi na endelevu za utafiti na maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 13.00 milioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 7.80 milioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 19.79 milioni sawa na asilimia 254 zimepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kutoa udhamini wa masomo kwa elimu ya juu ili kudumisha uchumi, usalama wa chakula na maendeleo endelevu kwa jamii. | Idadi ya wafanyakazi waliopatiwa udhamini wa masomo | 1 | 1 | 100 | Mwanafunzi huyo anaendelea na masomo |

### 11.2.17 Wizara ya Ujenzi, Mawasiliano na Uchukuzi

Wizara ina lengo la kuimarisha miundombinu wezeshi itakayochochea ukuaji wa Uchumi. Wizara inatekeleza miradi kupitia sekta kuu tatu (3) ambazo ni sekta ya Ujenzi,Mawasiliano na Uchukuzi.Wizara imepanga kutekeleza programu tano (5) na miradi miwili (2) ya maendeleo. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 1,549.46 bilioni (TZS 923.95 bilioni kutoka Serikalini na TZS 625.51 bilioni kutoka katika Washirika wa maendeleo).Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026 kiasi cha TZS 929.68 bilioni zilipangwa kutekeleza programu na miradi ya maendeleo kama ifuatavyo:-

**i. Programu ya Ujenzi na Matengenezo ya Miundombinu ya Barabara**

Programu inalengo la kuendeleza sekta ya miundombinu na kuimarisha maendeleo ya kiuchumi nchini, kwa kuweka miundombinu itakayounganisha miji na maeneo mengine ya kiuchumi. Programu itaendeleza ujenzi na matengenezo ya barabara kuu pamoja na barabara za kuunganisha maeneo yenye kutoa huduma za kijamii na kiuchumi. Kwa mwaka 2025/2026, programu hii inatekeleza miradi minne kama ifuatavyo:

**a. Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu**

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuunganisha miji mikubwa ya Zanzibar kwa lengo la kuhuisha uchumi na uwekezaji. Barabara hizi ni kiunganishi cha miji na maeneo mengine ya kiuchumi ikiwemo viwanja vya ndege na bandari. Kwa mwaka 2025/2026, Programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 329.03 bilioni (TZS 133.39 bilioni kutoka Serikalini na TZS 195.64 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 197.42 bilioni (TZS 80.03 bilioni kutoka Serikalini na TZS 117.38 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 289.01 bilioni (TZS 274.71 bilioni kutoka Serikalini na TZS 14.29 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 146 ya fedha imepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendeleza ujenzi wa misingi ya maji ya mvua, uwekaji wa michoro, alama na taa za barabarani; | Idadi ya km za mitaro iliyojengwa | 22.2 km | 7.0 km | 31 | Kazi ya ujenzi wa mitaro imefanyika kwa barabara ya Wete - Chake-Chake. Kuchelewa kukabidhiwa Mkandarasi eneo lote la ujenzi kutokana na changamoto za fidia kumeathiri utekelezaji wa kazi hii. |
| | Idadi ya km za barabara zilizowekwa taa | 6.0 km | 0.4 km | 7 | Taa zimewekwa katika eneo la barabara ya juu ya Mwanakwereke. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa kilomita 277 za barabara kuu Unguja na Pemba; | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 17.0 km | 10.6km | 62.3 | Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa barabara ya Kitogani – Paje (10.6km) kwa kiwango cha lami, Mkwajuni- Kijini (0.6km) kwa tabaka la pili la kifusi. Barabara ya Unguja Ukuu –Uzi ng'ambwa (6.5km) utekelezaji ulisita kutokana na changamoto za fidia. Kwa upande wa Pemba kazi ya uwekaji wa kifusi tabaka la kwanza 3km kwa barabara ya Chanjamjawiri -Tundaua yenye urefu wa 10.73km imefanyika. |
| Ujenzi wa daraja la Uzi-Ng'ambwa 2.2km | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 56 | 56 | Kazi zilizofanyika ni uwekaji wa kalvati 98, tabaka la kifusi (2.75km), hatua inayoendelea ni uwekaji wa kifusi tabaka la mwisho, uwekaji wa *slab*, ujenzi wa ukuta kwa ajili ya kuzuia mmomonyoko (retaining wall). Utekelezaji umedhorota kutokana na kuchelewa kupata idhini ya eneo la ujenzi wa daraja ambalo lilikuwa na mikoko mingi pamoja na ujazaji wa malihafi kwa kiwango kinachohitajika. |
| Ujenzi wa barabara ya Mkoani – Chake Chake ( 43.5km) kwa kiwango cha lami | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 7.0 km | 0 | 0 | Kazi za awali za ujenzi (Pre-construction works) zimefanyika ambapo upimaji na uchunguzi wa udongo (Topographical and Geotechnical Surveys), ujenzi wa kambi ya Mkandarasi, manunuzi ya vifaa pamoja na kuajiri wataalamu mbalimbali zimetekelezwa. Aidha, Mkandarasi anaendelea na kuandaa usanifu wa michoro ya ujenzi ya barabara husika. |
| Ujenzi wa barabara ya Tunguu – Makunduchi (48km) na Fumba – Kisauni (12km) kwa kiwango cha lami | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 10 km | 0 | 0 | Kazi za *Topographical and Geotechnical Surveys* zimekamilika, Manunuzi ya vifaa pamoja na kuajiri wataalamu mbalimbali yanaendelea. Mkandarasi amekamilisha ujenzi wa Kambi maeneo ya Muyuni na Kibele. Aidha, amekamilisha 70 ya *mobalization* ya vifaa. Kwa upande wa *Design,* hatua ya sasa Mkandarasi amewasilisha *Draft Preliminary Design* na Mshauri Elekezi anaendelea na mapitio. |
| Ujenzi wa barabara ya Tazari - Kilimani (3km). | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 3.0 km | 3.0 km | 100 | Ujenzi wa barabara hii umekamilika |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa barabara ya Bumbwini - Pangatupu-Mahonda (11.3km) na daraja la Pangatupu (mita 100). | Idadi ya km za barabara | 11.3 km | 11.3 km | 100 | Daraja la Pangatupu linaendelea kwa ujenzi wa sehemu za kuingilia (Inlet) na kutokea maji (Outlet) na limefikia asilimia 98 ya ujenzi. |
| Ujenzi wa barabara ya Mangapwani-Zingwezingwe - Mahonda (8.4 km). | Idadi ya km za barabara | 8.4 km | 8.4 km | 100 | Ujenzi wa barabara hii unaendelea na hatua ya uchimbaji wa mitaro na jumla ya 6.72km zimekamilika. |
| Ujenzi wa barabara ya Mfenesini-Mangapwani (7.2km). | Idadi ya km za barabara zilizowekwa kifusi | 7.2 km | 7.2 km | 100 | Ujenzi wa barabara hii umeanza kwa hatua ya usafishaji kwa baadhi ya maeneo (by section) yasikuwa na changamoto za fidia. |
| Kukamilisha ujenzi wa barabara ya Wete - Chake Chake (2.5 km). | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 2.5 km | 2.5 km | 100 | Kazi iliyobakia ni uwekaji wa *walkways* na mitaro. |
| Ujenzi wa barabara kilomita 210. | | 57 km | 41km | 72 | Ujenzi kwa kiwango cha lami umefanyika kwa barabara ya Bwereu-Nungwi (4km), ujenzi wa barabara ya Kigunda -Nungwi (4km), Malindi Gapco - round about ZPC (0.3km), Malindi Bwawani – Msikiti Mabuluu (0.9km), Old Dispensary – Golden Tulip – PADDC0 (0.3km), Kichwele – Mwachalale (4km), Malindi Police station Car Park (0.3km) na Selem – Mfenesini – Spur (2.5km), Chunga – Mwera (6.2km), Hanyegwa mchana - Chuchumile - Cheju na Chuo cha Mafunzo (9km), Mbuzini – Kitundu msikiti wa waarabu (6km), Mbuzini district hospital – Osterbay – Mwembe Wanga – Kitundu (2.5km), Kibondeni kilangi (1km) na Mwera Usalama – Mji Mwema (1.3km). Aidha barabara za Mahonda Mkataleni (4km), Chunga – Mewera (6.2km), Mwera- Dole – Mfenesini (14.3km), Dunga – Kilombero-Kinyasini (19km), Kinazini junction-Mkokotoni –Nungwi (18km), Tunguu-Dunga (7km) ujenzi utaendelea mara baada ya kukamilika malipo ya fidia kwa wanachi watakaothirika na ujenzzi huo. |

### b. Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Ndani

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kujenga barabara za ndani zenye urefu wa kilomita 275.9 katika maeneo ya mijini na vijijini Unguja na Pemba. Mradi utaunganisha mitaa na maeneo mengine ikiwemo barabara kuu. Aidha, kukamilika kwa mradi huu utasaidia kupunguza msongamano katika barabara

kuu pamoja na kuongeza haiba ya kupendezesha miji na mitaa katika maeneo ya Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 78.03 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), Mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 46.82 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 143.49 Bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 306 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imepatikana na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa barabara za vijijini kilomita 275.9 | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 70km | 68.88 km | 98.4 | Jumla ya km 33.58 zimejengwa kwa kiwango cha lami kwa barabara ya Kajengwa-Koba-Kinandi-Mnarani 4.98km, Kajengwa-Uwandani-Kibwegele, 6.75km, Kigaeni-Blue Moon 4.2km, Mtandao-Chiyabonde 1.36km, Mtegani-Miwaleni 1.21km, Kuungoni-Kae Kuu-Madete 0.92km, Wawi Mesi-Mzambaraumboko 6.4km, Penjewani-Mjini Kiuyu 2.27km, Mgagadu-Kwautao 5.49km, Pembeni-Pandani 3.38km, Mzambarautakao-Mchangamdogo 6.3km, Kiungoni-Tovuni 2.96km, Gando-Chokaani 2.1km, Gando-Chaoni 1.0km, Bwagamoyo-Kele 5.25Km, Uondwe-Nyali 1.96km, Barawa-Mleteni 1.5km pamoja na Jambang'ome Jct – Jambangome 2.42km kwa upande wa Pemba. Kadhalika, Jumla ya kilomita 34.4 zimejengwa kwa hatua mbali mbali za kifusi. |
| Ujenzi wa barabara kilomita163.22 | | 36.39 km | 14.16 km | 38.9 | Jumla ya 14.16km zimejengwa kwa kiwango cha lami Unguja na Pemba ambapo Unguja ni 8.85km na Pemba ni 5.31km. Barabara hizo ni pamoja na barabara ya Istiqama-Zanzibar University 0.395km, Nganani - Kumbini - Chuini - Bungi - Mtegani Spur 1.91km, Barabara ziendazo kwenye viwanja vya Michezo vya Wilaya 0.7km, Tasani - Mnarani – Pwani 1.63km, Mnarani – Kigaeni 2.19km, Madete skuli - Skuli ya Kusini 0.35km pamoja na Mwembesanda – Mavua 1.68km kwa upande wa Unguja na barabara ya Minazini-Mabaoni (Gando) 0.34km pamoja na Chanjaani-Mitamani-Pujini 4.97km kwa upande wa Pemba. |
| Ujenzi wa barabara kilomita 65.5 | | 57.6 km | 18.10 km | 31.42 | Barabara ya Wete-Konde - Gando imejengwa kwa kiwango cha lami na kilomita 50.48 zimejengwa kwa hatua mbali mbali za kifusi. |
| Ujenzi wa barabara (34 km) ikiwemo Kitope – Ndagaa– Kidimni (19km), na Ndagaa – Bumbwisudi-Kitundu (7km) | Idadi ya km za barabara zilizojengwa kwa kiwango cha lami | 26 km | 26 km | 100 | Barabara ya Kitope – Ndagaa – Kidimni (19km), Ndagaa – Bumbwisudi-Kitundu (7km) zimekamilika kwa kiwango cha lami. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa barabara ya Kianga – Jitimai (3 km), Langoni-Kisauni kwa Bi Asha (4.5km), Ubago-Jumbi (6.5 km), Mbuzini-Kijichi (km 6), Gando- Wete-Konde (26.5 km), Mtambile-Kengeja (10km), Goli la Mpira- Kwapopo (4.2 km), Mihogoni –Uhanga-Amani (2.2 km), Skuli ya Pujini-Chuo cha Mwalimu Nyerere (2.6 km); | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 21 km | 12.7 km | 60.5 | Barabara ya Mtambile-Kengeja imesafishwa (Clearance) 10km na hatua inayoendelea ni usanifu (Design) wa barabara kwa ajili ya ujeB Asha (4.5km), Ubago - Jumbi (6.5 km), Mbuzini-Kijichi (km 6) zinaendelea na ujenzi kwa hatua mbali mbali za kifusi. |
| Ujenzi wa barabara ya Kitope – Ndagaa– Kidimni (19 km), na Ndagaa – Bumbwisudi-Kitundu (7 km) | Idadi ya km za barabara zilizojengwa kiwango cha lami | 26 km | 26 km | 100 | Kazi ya ujenzi imekamilika. |
| Ujenzi wa barabara za Tumbatu 15.2 km | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 15.2 km | 0.35 km | 2.3 | Barabara hii ilikuwa inajengwa kwa *block stone* na sasa itajengwa kwa zege. Mabadiliko ya mpango wa ujenzi ni miongoni mwa sababu ya asilimia ya utekelezaji iliyofikiwa. Mkandarasi ameongeza vifaa vya ujenzi vya zianda ili kuendana na mabadiliko hayo. |
| Ujenzi wa barabara ya Kazole-Matetema-Zingwezingwe(5.3 km) | Idadi ya km za barabara zilizowekwa kifusi | 5.3 km | 5.3 km | 100 | Barabara hii inaendelea na hatua ya ujezi wa mitaro. |
| Ujenzi wa barabara ya Fuoni-Kipungani (9.2 km), | Idadi ya km za barabara zilizowekwa lami | 9.2 km | 9.2 km | 100 | Kazi ya ujenzi mekamilika. |
| Ujenzi wa barabara ya Skuli ya Fuoni na Hospitali ya Tawakal (1km); | Idadi ya km za barabara zilizowekwa lami | 1 km | 1 km | 100 | Kazi ya ujenzi imekamilika. |

### c. Mradi wa Matengenezo ya Barabara za Mjini

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha haiba ya mji wa Zanzibar kwa ujenzi wa barabara katika maeneo ya mjini. Mradi unahusu ujenzi wa kilomita 100.9 za barabara za mjini na uimarishaji wa barabara katika maeneo ya Mkoa wa Mjini Magharibi. Kukamilika kwa programu hii kutaongeza haiba na kupendezesha Mji wa Zanzibar na kusaidia kuimarika kwa baadhi ya sekta ikiwemo sekta ya usafirishaji, utalii na biashara. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 35.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi

cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi huu ulipangiwa kutumia jumla ya TZS 21.00 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 32.26 kutoka Serikalini bilioni sawa na asilimia 154 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Usafishaji wa maeneo na kuanza uwekaji wa fusi na tabaka la lami kwa baadhi ya barabara | Idadi ya km za barabara zilizowekwa kifusi | 10 km | 9.23 km | 92.3 | Kazi hiyo imefanyika kwa barabara ya Kinazini-Mtoni (2 km- Kinazini-Sateni na Maruhubi-Verde kwa upande mmoja wa barabara), Mombasa Soko la Mboga – Azania (1.3 km), Mchina mwisho – Kwa Shein (0.93 km) |
| | Idadi ya km za barabara zilizowekwa lami | 10 km | 9.45 km | 94.5 | Barabara ya Mombasa Soko la Mboga – Azania (1.3 km), Kwa kira-Kituo kipya cha Uwanja wa Ndege (1.03 km), Kinazini-Mtoni (0.86 km RHS) na Mkapa road 5 km zimekamilika kwa kiwango cha lami. Barabara ya Amani roundabout–Mikunguni-Biziredi (2.55 km) na Kariakoo – Mwanakwerekwe (3.71 km), hazijaanza kutoka na changamoto za fidia. |
| Kuendelea na ujenzi wa mitaro kwa baadhi ya barabara; | Idadi ya km za mitaro zilizojengwa | 30 km | 24.58 km | 82 | Ujenzi umefanyika katika baadhi ya barabara ikiwemo barabara ya Uwanja wa Ndege (0.9 km), Mombasa planned area (5.61km), Mazizini Polisi-Chukwani Jeshini (9.3 km) na barabara ya Kiembesamaki junction-Amani – Mtoni junction (0.8 km), Nyumba za Magereza – Ziwa maboga (2.64 km), kwa Kira-Uwanja wa Ndege (2.06 km), Msikishurba – Mshelishelini- Matarumbeta (0.61 km), Mombasa soko la mboga –Azania (2.66 km). Taratibu za fidia kwa waathirika wa ujenzi wa barabara hizzo zinaendelea. |
| Ujenzi wa mtaro wa soko la Chuini pamoja na barabara | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 92 km | 92 | Kazi za uchimbaji (excavation and levelling) uwekaji wa zege Pamoja na kalvati zimefanyika. Kwa upande wa barabara kazi zilizofanyika ni uchimbaji, uwekaji wa kifusi (CRR), uwekaji wa zege na *finishing.* Kuchelewa malipo ya fidia na mvua za vuli zimedhorotesha utekelezaji wa mradi. |
| | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 0.5 km | 0.5 km | 100 | |
| Uwekaji wa taa na njia za waenda kwa miguu; na | Idadi ya taa zilizowekwa | 75 km | 75 km | 100 | Taa hizo zimewekwa katika barabara ya Uwanja wa Ndege na baadhi ya maeneo ya barabara ya Chukwani na K/samaki. |
| | Idadi ya km za njia za watembea kwa miguu zilizojengwa | 35 km | 31 km | 88 | Miongoni mwa barabara (walkways) hizo ni Mazizini polisi - Chukwani, barabara za ndani za Chukwani, Uwanja wa Ndege - Kinuua miguu, Kituo kipya cha Uwanja wa Ndege - Kwakira, Mbweni afya – Madina - Matrekta na barabara zilizozunguka mtaa huo (Associated street roads), Mombasa planed area road, Chukwani mwisho – Buyu, K/samaki junction – Mtoni junction |
| Kukamilisha ujenzi wa barabara za Mjini kilomita 20.9. (Masingini single Carriage way) | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 16.29 km | 16.29 km | 100 | Barabara hizo ni pamoja na barabara ya Buyu-Fumba 4.88 km, Masingini 1 km, Mombasa soko la mboga 1.3 km, Chukwani ndani 1.97 km |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa barabara za juu (flyover) katika mzunguko (Roundabout) ya Mwanakwerekwe | Asilimia ya ujenzi wa barabara iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Imekamilika. |
| Ujenzi wa barabara za juu (flyover) katika mzunguko (Roundabout) ya Amani. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 70 | 70 | Ujenzi wa nguzo tatu za kubeba deki ya flyover zimekamilika. Aidha, ujenzi wa chelezo kwa pande zote mbili unaendelea Kusini na Kaskazini. |

### ii. Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege

Programu hii imeanzishwa kwa lengo la kuimarisha miundombinu ya usafirishaji wa abiria na mizigo kwa njia ya anga ili iweze kuwa katika viwango vya Kimataifa. Programu itahusisha ujenzi wa uwanja wa ndege wa Pemba ikiwemo maegesho ya ndege, njia za kupitia ndege pamoja na sehemu za kukaa abiria. Kwa mwaka 2025/2026, Programu hii imepangiwa kutumia jumla ya TZS 284.00 bilioni (TZS 124.50 bilioni kutoka Serikalini na TZS 159.50 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), programu ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 170.40 bilioni (TZS 74.70 bilioni kutoka Serikalini na TZS 95.70 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 114.51 bilioni (TZS 18.46 bilioni kutoka Serikalini na TZS 96.40 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo) sawa na asilimia 67 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendelea na ujenzi wa jengo la abiria Terminal II AAKIA; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 85 | 83 | Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa paa na upakaji rangi, ufungaji wa *conveyer belt*, ujenzi wa *immigration counter*, uwekaji wa nguzo za kuunganisha *TB II* mpya na *TB III* pamoja na kazi za umaliziaji kwa kupaka poda, dari na kuweka marumaru. |
| Ujenzi wa mnara wa kuongozea ndege katika uwanja wa AAKIA | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 50 | 50 | Usanifu wa michoro ya ujenzi wa *terminal II* awamu ya pili pamoja ujenzi wa mnara wa kuongezea ndege unaendelea. |
| Ujenzi wa Apron katika Uwanja wa Ndege wa AAKIA; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 40 | 40 | Usanifu wa michoro ya ujenzi wa *Apron* pamoja na utanuzi wa *taxway* umekamilika. Kazi inayoendelea ni uchimbaji na usafishaji wa eneo la mradi |
| Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 25 | 25 | Kazi za awali zimekamilika ikiwemo Ujenzi wa Kambi ya Mkandarasi, Michoro ya awali, kuwasili kwa Vifaa vya awali, pamoja na kuajiri wataalamu. Ujenzi umeshaanza ambapo kwa sasa kazi zinazoendelea ni kazi za uwekaji wa kifusi katika eneo la *Terminal Building*.<br><br>Aidha, Mkandarasi ameanza kazi ya uchimbaji na uwekaji wa kifusi katika eneo la ndani ya Uwanja (Airside) kwa ajili ya kuanza kujenga njia ya kuruka na kutua ndege (Runway). |

### iii. Programu ya Kuimarisha Bandari

Programu hii ina lengo la kujenga bandari jumuishi ya kisasa Mangapwani (Multipurpose Port) ambayo itajumuisha ujenzi wa gati ya mizigo, eneo la ushushaji na upakiaji wa mafuta. Vile vile ujenzi wa chelezo cha kukarabati meli pamoja na bandari ya abiria na mizigo Maruhubi. Programu hii inatarajia kutekelezwa kwa kushirikiana na sekta binafsi. Kwa mwaka 2025/2026, Programu hii imepangiwa jumla ya TZS 335.10 bilioni (TZS 205.10 bilioni kutoka Serikalini na TZS 130.00 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), programu hii ilipangiwa kutumia jumla ya TZS 123.06 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 186.04 bilioni kutoka Serikalini sawa na asilimia 151 ya fedha iliyopangwa imeingizwa na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa bandari ya makontena na mizigo mchanganyiko Mangapwani | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 20 | 20 | Kazi zilizofanyika ni uchunguzi wa udongo, upimaji wa kina cha maji, usafishaji wa eneo pamoja na uandaaji wa michoro kwa ajili ya ujenzi. Kazi zinazoendelea ni uchimbaji wa eneo la juu ili kufukia usawa wa eneo la bahari. |
| Ujenzi wa bandari ya mafuta na gesi pamoja na chelezo Mangapwani; | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 8.8 | 8.8 | Kazi zilizofanyika ni kufungwa kwa vifaa vya ujenzi vikiwemo Flowmeter, manifold, buoys na pipe line na Platform. Kazi za kuweka miundombinu ya bandari inaendelea. |
| Kukamilisha ujenzi wa nyumba 370 za fidia; | Idadi ya nyumba zilizojengwa | 35 | 35 | 100 | Ujenzi wa nyumba za fidia 170 unaendelea kwa uwekaji wa miondombinu ya maji na umeme pamoja na hatua za mwisho za ujenzi (finishing works) wa baadhi ya nyumba hizo kama milango na madirisha. Aidha nyumba 200 zimekamilika katika mwaka wa fedha 2025/2026. Utekelezaji wa kazi yote ya ujenzi kwa ujumla imefikia asilimia 80. |
| Kukamilisha ujenzi wa barabara za ndani (Dual Carrige way) (km 12) katika eneo la Mangapwani | Idadi ya km za barabara zilizojengwa | 12 km | 5.6 km | 47 | Ujenzi wa barabara za ndani (12 km) zinazounganisha bandari ya Mangapwani kwasasa umesita kutokana na kusubiria kulipwa fidia kwa waathirika wa ujenzi huo. |
| | Idadi ya km za barabara zilizowekwa taa | 6.4 km | 0 | 0 | Kazi ya uwekaji wa taa za barabarani itafanyika baada ya kukamilika ujenzi wa km 6.4 za barabara za ring roads ambao umesita kutokana na kusubiri kulipwa fidia kwa waathirika wa ujenzi wa barabara. |
| Ujenzi wa Bandari ya Mpigaduri | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 87 | 87 | Kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa ghala na maduka, ujenzi wa causeway, mizani ya kupimia mizigo, ujenzi na ufungaji wa Tishali lenye uwezo wa kuhudumia meli nne (RoRo) kwa wakati mmoja. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuendeleza ufukiaji bahari (sea reclamation) katika eneo la Maruhubi; | Asilimia ya ufukiaji iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Kazi ya ufukiaji (Phase 1A) imekamilika. |
| Ujenzi wa boti mbili za abiria | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 35 | 35 | Mkandarasi anaendelea na utengenezaji wa Plate na injini zinaendelea kutengenezwa nchini Ujerumani na zinatarajiwa kukamilika mwezi Machi, 2026. |

### iv. Programu ya Mageuzi ya Kidigitali

Mradi huu umeanzishwa kwa lengo la kuimarisha mifumo ya mawasiliano ambayo itarahisisha utoaji wa huduma za kimtandao na utoaji wa huduma Serikalini. Mradi huu utahusisha mifumo mbali mbali ya Serikalini inayotumika katika utoaji wa huduma zenye ufanisi zaidi za mawasiliano na kuongeza ukusanyaji wa mapato ya Serikali. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia TZS 76.05 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha miezi tisa (Julai 2025 hadi Machi 2026), mradi ulipangiwa kutumia TZS 46.97 bilioni. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 1.09 bilioni sawa na asilimia 2.3 ya fedha iliyopangwa kwa kipindi hicho imeingizwa kutoka kwa Washirika wa Maendeleo na kutekeleza shughuli zifuatazo: -

| Shughuli Iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Utoaji wa huduma ya mtandao katika maeneo ya umma (Public Wi-Fi ); | Idadi ya maeneo yanayopata huduma ya mtandao (Public Wi-Fi) | 1 | 1 | 100 | ZICTIA imeanza kwa hatua ya awali (dharura ya michuano ya CHAN) kuweka huduma hii katika eneo la Uwanja wa Amani Complex (VIP). Taratibu za manunuzi zinaendelea ili kumpanta Mkandarasi akamilishe kazi kwa uwanja wa Amani Complex na kuendelea katika maeneo mengine yenye mkusanyiko mkubwa ikiwemo uwanja mpya wa Fumba, masoko, forodhani na vituo vya mabasi. |
| Ujenzi wa kituo cha kuhifadhia taarifa (Data Center); | Asilimia ya Ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | ZICTIA imekamilisha uandaaji wa hadidu rejea (TOR) na inaendelea na taratibu za manunuzi ili kumpata Mzabuni mwenye sifa zinazohitajika. |
| Kufanya matengenezo na uwekaji wa mkonga; | Idadi ya kilomita za Mkonga zilizofanyiwa matengenezo | 200 km | 72 km | 36 | Kazi ya kuhamisha Mkonga kutokana na matengenezo ya barabara imeendelea katika maeneo (route) mbalimbali ikiwemo Mkwajuni, Mizingani, Bango la Mkoa, Kwa Mchina, Bumbwini, Bwejuu, K/Majongoo, Jang'ombe, Mbuyu mnene, Kidimni, Kiungoni, Mtuhaliwa, Pujini, Konde, Mchanga mlima, Micheweni, Vikutani, Mali nne na Kiwani. |
| Uimarishaji wa mfumo wa Mawasiliano | Asilimia ya uimarishaji wa vifaa iliyofikiwa | 100 | 60 | 60 | ZICTIA imeendelea na kazi ya uimarishaji wa vifaa kwa kuweka Rack pamoja na Rectifier kwa vituo (SITE) vyote Unguja na Pemba. |

### 11.2.18 Wizara ya Utalii na Mambo ya Kale

Wizara ina jukumu la kusimamia utalii na mambo ya kale kwa kuibua na kuongeza vivutio vipya vya utalii na kuendelea kuitangaza Zanzibar. Kwa mwaka 2025/2026, Wizara imepanga kutekeleza programu mbili na miradi miwili ya maendeleo inayotarajiwa kugharimu jumla ya TZS 37.03 bilioni (TZS 22.00 bilioni kutoka Serikalini na TZS 15.03 kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 22.22 bilioni zilipangwa kutumika. (TZS 13.2 bilioni kutoka Serikalini na TZS 9.01 bilioni kutoka kwa Washirika wa Maendeleo). Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 406.01 milioni sawa na asilimia 2 zimepatikana na kutekeleza programu na miradi ya maendeleo ifuatayo:-

#### i) Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria

Programu ina lengo la kuendeleza Sekta ya Utalii kwa kulinda, kuhifadhi na kutunza maeneo ya kihistoria yaliopo nchini kwa faida ya kizazi cha sasa na cha baadae. Vile vile, Programu inasimamia kukuza shughuli za utalii kwa kuongeza fursa za ajira, vivutio vya utalii na kuongeza Pato la Taifa. Kwa mwaka 2025/2026, programu imepangiwa kutumia jumla ya TZS 6.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 3.6 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, jumla ya TZS 406.01 milioni sawa na asilimia 11 zimepatikana kutoka Serikalini na kutekeleza shughuli zifuatazo:-

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ujenzi wa uzio katika maeneo ya kihistoria | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa | 100 | 5 | 5 | Kazi ya kuweka uzio kwa baadhi ya maeneo ya kihistoria ipo katika hatua za kumpata Mkandarasi atakae jenga uzio katika maeneo hayo. |
| Kuimarisha eneo la kihistoria la Mangapwani | Asilimia ya Uimarishaji iliyofikia | 100 | 95 | 95 | Kazi katika maeneo yote matatu imeshakamilika kwa asilimia 95. Hatua iliyobaki ni usafi wa eneo, pamoja na kurekebisha kisima kimoja ambacho maji yake hayaridhishi. |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Kuimarisha eneo la kihistoria la Ras Mkumbuu. | Asilimia ya ujenzi iliyofikiwa. | 100 | 90 | 90 | Ujenzi wa Duka (shop building), Mgahawa (Restaurant), Sehemu ya mapumziko (lounge) na Ofisi umekamilika.<br><br>Kisima na hodhi la maji vimekamilika na usambazaji wa maji umekamilika<br>Ukarabati wa majengo ya kihistoria yaliyopo katika eneo la mradi umekamilika<br>Utengenezaji wa njia za kupita na sehemu ya maegesho, upandaji wa bustani, ujenzi wa vyoo pamoja na huduma ya kufikisha umeme katika majengo zimekamilika<br>Ujenzi wa ukuta wa kuzuiya maji ya bahari umekamilika. Kazi iliyobakia ni kujaza udongo nyuma ya ukuta wa kuzuia maji ya bahari kwa kiwango kinachotakiwa, kulipa fidia na kujenga nguzo za zege kuzunguka mipaka ya eneo. |

### a. Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Mji Mkongwe

Mradi huu umeanzishwa mwaka 2024/2025 ni mradi endelevu. Mradi una lengo la kuimarisha majengo yaliyo katika hali mbaya ya uchakavu katika maeneo ya Mji Mkongwe ili kubaki kuwa ni ukumbusho wa Hisotia ya Zanzibar kwa kuyahifadhi na kuyalinda. Kwa mwaka 2025/2026, Mradi umepangiwa kutumia jumla ya TZS 10.00 bilioni kutoka Serikalini. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 6.0 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zilizotekelezwa zimetumia bajeti ya mwaka 2024/2025.

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukarabati wa Jengo namba 2312 -Vuga | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Mradi huu umetekelezwa na Kampuni ya K'S Builders Ltd na umegharimu Shilingi **480,470,075.60/=.** kazi zilizofanyika ni pamoja na kurekebisha paa, dari, vyoo, kuweka plasta, kupaka rangi, kufanya "fitting" ya umeme na maji. Utekelezaji wake umeanza Novemba 2024 na ulikamilika Julai 2025 na tayari jengo limekabidhiwa kwa wamiliki wake ambao ni "Culture Music Club" . |

| | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|
| Ukarabati wa Jengo namba 1196/97 - Malindi | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 95 | 95 | Mradi huu umetekelezwa na Kampuni ya M/s Yassin & Sons Company Ltd Kazi zilizofanyika ni ujenzi wa paa jipya, ujenzi wa dari mpya ya boriti, ukarabati wa milango na madirisha, kupiga plasta, kuweka mifumo mipya ya umeme, maji safi na maji taka pamoja na upakaji rangi. Aidha, kwa sasa Mkandarasi anamalizia sehemu ambazo alitakiwa kufanya marekebisho ili aweze kukabidhi mradi. Utekelezaji wake umeanza Disemba 2024 na unatarajiwa kukamilika Aprili, 2026. |
| Ukarabati wa Jengo namba 1065- Malindi Funguni | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 100 | 100 | Mradi huu umetekelezwa na Kampuni ya Kin Investment Company Ltd na umegharimu **Shilingi 742,862,222.5/=** kazi zilizofanyika ni pamoja na ujenzi wa paa jipya, ujenzi wa dari mpya ya boriti, ukarabati wa milango na madirisha, kupiga plasta, kuweka mifumo mipya ya umeme, maji safi na maji taka pamoja na upakaji rangi. Utekelezaji wake umeanza Novemba 2024 na umekamilika Novemba, 2025. |
| Ukarabati wa Jengo namba F06A-Forodhani | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 75 | 75 | Mradi huu unatekelezwa na Kampuni ya Faster (fst) Company Limited. Mradi huu unagharimu Shilingi 713,680,512.50/= Kazi zilizofanyika ni ukarabati wa paa, kukamilika kwa ujenzi wa ghorofa ya pili na ghorofa ya kwanza, ukarabati wa milango na madirisha, kupiga plasta, kuweka mifumo mipya umeme, maji safi na maji taka kwa ghorofa ya kwanza na ya pili. Utekelezaji wake umeanza kutekelezwa Januari 2025 na unatarajiwa kukamilika Aprili 2026. |

### b. Mradi wa Kulifanyia Ukarabati Jengo la Beit Al-Jaib

Mradi huu una lengo la kulinda na kurudisha jengo hilo ikiwa ni alama inayoitambulisha Zanzibar Kimataifa. Kwa mwaka 2025/2026, mradi umepangiwa jumla ya TZS 15.03 bilioni kutoka Washirika wa Maendeleo. Kwa kipindi cha Julai 2025 hadi Machi 2026, jumla ya TZS 9.01 bilioni zilipangwa kutumika. Hadi kufikia Machi 2026, shughuli zilizotekelezwa zimetumia bajeti ya mwaka 2024/2025.

| Shughuli iliyopangwa | Kiashiria | Shabaha | Utekelezaji Halisi | Asilimia ya Utekelezaji | Maelezo |
|---|---|---|---|---|---|
| Uendelezaji wa shughuli za kulifanyia matengenezo jengo la Beit Al Jaib. | Asilimia ya ukarabati iliyofikiwa | 100 | 69 | 69 | Mamlaka inaendelea na kutoa ushauri wa kitaalamu katika kazi za Ukarabati wa mradi wa ukarabati wa Jengo la Beit-el -Ajaib ambapo Mkandarasi amemaliza kazi ya kuweka dari ya zege sehemu ya juu iliyovunjika na pia anaendelea na kazi za ukarabati wa milango na madirisha, ukarabati wa Mlango mkubwa wa mbele na kupiga plasta. Mkandarasi wa mradi huu ni “Nandhra Engineering & Construction Company” na Mshauri elekezi wa mradi huu ni “Distruct Solution” ya Lebanon. |

| PROGRAMU/MIRADI INAYOTARAJIWA KUTEKELEZWA NA SERIKALI NA WASHIRIKA WA MAENDELEO KWA KIPINDI CHA JULAI 2025-MACHI 2026 MWAKA | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| WIZARA/TAASISI | KILICHOPANGWA | | | KILICHOTOKA | | | ASILIMIA | | |
| PROGRAMU/MIRADI | SMZ | WM | JUMLA | SMZ | WM | JUMLA | SMZ | WM | JUMLA |
| **OFISI YA RAIS - IKULU** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuimarisha Majengo ya Ikulu | 3,600,000 | **0** | **3,600,000** | 500,000 | | **500,000** | **14** | **0** | **14** |
| ii) Mradi wa Uimarishaji Mfumo wa Ulinzi na Usalama katika Majengo ya Ikulu na Makaazi ya Mheshimiwa Rais | 1,200,000 | **0** | **1,200,000** | 727,331 | **0** | **727,331** | **61** | **0** | **61** |
| iii) Mradi wa Kuimarisha Mawasiliano ya Mfumo wa Sema na Rais (SNR) | 420,000 | **0** | **420,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **5,220,000** | | **5,220,000** | **1,227,331** | **0** | **1,227,331** | **24** | **0** | **24** |
| **TAASISI YA AFISI YA RAIS UFUATILIAJI NA USIMAMIZI WA UTENDAJI SERIKALINI** | | | | | | | | | |
| Programu Shirikishi ya Maendeleo kwa Makuzi ya Awali ya Mtoto Zanzibar | **0** | 793,800 | 793,800 | **0** | 305,125 | **305,125** | **0** | 38 | **38** |
| **JUMLA YA FUNGU** | | **793,800** | **793,800** | **0** | **305,125** | **305,125** | **0** | **38** | **38** |
| **OFISI YA RAIS- KAZI, UCHUMI NA UWEKEZAJI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uimarishaji wa Maeneo Huru ya Uwekezaji** | 9,000,000 | **0** | **9,000,000** | 3,293,674 | **0** | **3,293,674** | **37** | **0** | **37** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **9,000,000** | **0** | **9,000,000** | **3,293,674** | **0** | **3,293,674** | **37** | **0** | **37** |
| **WAKALA WA UWEZESHAJI WANANCHI KIUCHUMI** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuwasaidia Wajasiriamali Wadogo Wadogo, Wakati na Wakubwa | 2,700,000 | 3,060,000 | 5,760,000 | 5,227,500 | 0 | 5,227,500 | 194 | 0 | 91 |
| Mradi Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja) | 0 | 600,000 | 600,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,700,000** | **3,660,000** | **6,360,000** | **5,227,500** | **0** | **5,227,500** | **194** | **0** | **82** |
| **OFISI YA RAIS- FEDHA NA MIPANGO** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ujenzi wa Ofisi za Serikali Zanzibar** | | | | | | | | | |
| i) Ukamilishaji wa Ofisi za Serikali | 35,745,846 | **0** | 35,745,846 | 28,176,211 | **0** | 28,176,211 | 79 | **0** | 79 |
| ii) Ujenzi wa Mji wa Serikali | 40,033,296 | **0** | 40,033,296 | 44,767,465 | **0** | 44,767,465 | 112 | **0** | 112 |
| **Programu ya Ulipaji wa Fidia za Miradi ya Maendeleo** | 126,239,850 | **0** | 126,239,850 | 108,751,571 | **0** | 108,751,571 | 86 | **0** | 86 |
| **Programu ya Mageuzi Katika Usimamizi wa Fedha (PFMRP)** | 210,000 | 2,640,000 | 2,850,000 | 350,000 | **0** | 350,000 | 167 | **0** | 12 |
| **Programu ya Ukuzaji Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG-Z)** | **0** | 19,500,000 | 19,500,000 | 0 | 53,999,078 | 53,999,078 | | 277 | 277 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| i) Mradi wa Uimarishaji wa Rasilimali za ndani na Usimamizi wa Maliasili (ISP-DRMNRG) | 30,000 | 0 | 30,000 | 50,000 | **0** | 50,000 | 167 | **0** | 100 |
| ii) Ulipaji wa Madeni kwa miradi ya Maendeleo | 187,200,000 | **0** | 187,200,000 | 38,367,327 | 0 | 38367327 | 20.495367 | **0** | **20** |
| iii) Mradi wa Kukuza Uwezo wa Uhamasishaji Utafutaji Rasilimali Fedha | 0 | 165,690 | 165,690 | 0 | 1,134,443 | 1,134,443 | 0 | 0 | **685** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **389,458,992** | **22,305,690** | **411,764,682** | **220,462,574** | **55,133,521** | **275,596,095** | **57** | **247** | **67** |
| **TUME YA MIPANGO** | | | | | | | | | |
| **Uratibu wa Programu ya Urasimishaji Ardhi na Biashara** | 2,700,000 | **0** | **2,700,000** | 1,920,000 | **0** | 1,920,000 | 71 | **0** | **71** |
| **Miradi** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuratibu, Kupanga na Usimamizi wa Mipango ya Maendeleo | 3,300,000 | **0** | **3,300,000** | 9,551,484 | **0** | 9,551,484 | 289 | **0** | **289** |
| ii) Mradi wa Kuimarisha Ufanisi katika Utekelezaji wa Mipango ya Maendeleo ya Taifa | 1,080,000 | **0** | **1,080,000** | 1,009,805 | **0** | 1,009,805 | 94 | **0** | **94** |
| iii) Mradi wa Kuendeleza Tafiti za Kimkakati | 600,000 | **0** | **600,000** | 481,355 | **0** | 481,355 | 80 | **0** | **80** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **7,680,000** | **0** | **7,680,000** | **12,962,644** | **0** | **12,962,644** | **169** | **0** | **169** |
| **OFISI YA MTAKWIMU MKUU WA SERIKALI** | | | | | | | | | |
| i) Mpango Mkuu wa Uimarishaji Takwimu Tanzania Awamu ya Pili (TSMP II) | **0** | 2,759,262 | **2,759,262** | **0** | 3,697,255 | 3,697,255 | **0** | 134 | **134** |
| ii) Mradi wa Uimarishaji wa Takwimu za Jinsia | 1,200,000 | 192,000 | **1,392,000** | 178,930 | 0 | 178,930 | 15 | 0 | **13** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,200,000** | **2,951,262** | **4,151,262** | **178,930** | **3,697,255** | **3,876,185** | **323** | | **93** |
| **OFISI YA MHASIBU MKUU WA SERIKALI** | | | | | | | | | |
| Mradi wa Uandaaji wa Hesabu (IPSAS ACCRUAL) kwa Viwango vya Kimataifa | 614,325 | - | **614,325** | 564,510 | 0 | 564,510 | 92 | 0 | **92** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **614,325** | | **614325** | **564,510** | **0** | **564,510** | **92** | **0** | **92** |
| **OFISI YA RAIS - KATIBA, SHERIA, UTUMISHI NA UTAWALA BORA** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Mageuzi ya Utumishi wa Umma (Phase II)** | 600,000 | 0 | **600,000** | 428,366 | 0 | 428,366 | 71 | 0 | **71** |
| **Programu ya Mageuzi ya Sekta ya Sheria** | 300,000 | 737,926 | **1,037,926** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |
| Mradi wa Utoaji wa Huduma ya Haki kwa Kuzingatia Jinsia | 0 | 85,985 | **85,985** | 0 | 49,943 | 49,943 | 0 | 58 | **58** |
| Mradi wa Kujenga Msingi Imara wa Mapambano Dhidi ya Rushwa Tanzania | 0 | 2,606,093 | **2,606,093** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | **0** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JUMLA YA FUNGU** | **900,000** | **3,430,004** | **4,330,004** | **428,366** | **49,943** | **478,309** | **53** | **1** | **11** |
| **MAHKAMA KUU** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Mahkama za Wilaya na Mikoa | 7,800,000 | 0 | 7,800,000 | 7,660,829 | 0 | 7,660,829 | 98 | 0 | 98 |
| ii) Mradi wa Uimarishaji wa Mahkama | 360,000 | 21,000,000 | 21,360,000 | 510,169 | 8,010,197 | 8,520,366 | 142 | 38 | 40 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **8,160,000** | **21,000,000** | **29,160,000** | **8,170,998** | **8,010,197** | **16,181,195** | **100** | **38** | **55** |
| **AFISI YA RAIS TAWALA ZA MIKOA, SERIKALI ZA MITAA NA IDARA MAALUM ZA SMZ** | | | | | | | | | |
| Programu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi | **0** | 1,260,000 | 1,260,000 | | 578,137 | 578,137 | | 46 | 45.88 |
| i) Mradi wa Kuimarisha Ulinzi na Usalama | 15,450,000 | 0 | 15,450,000 | 4,833,471 | 0 | 4,833,471 | 31.28 | 0 | 31.28 |
| ii) Mradi wa Ujenzi wa Ofisi za Masheha Zanzibar | 4,800,000 | 0 | 4,800,000 | 955,305 | 0 | 955,305 | 19.90 | 0 | 19.90 |
| iii) Mradi wa Kuimarisha Haki Jinai | 10,800,000 | 0 | 10,800,000 | 5,859,926 | 0 | 5,859,926 | 54.26 | 0 | 54.26 |
| iv) Mradi wa Ujenzi wa Kituo na Maegesho ya Vyombo vya Usafiri katika Soko la Mwanakwerekwe | 12,000,000 | 0 | 12,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| v) Mradi wa Mji bila Taka | 6,000,000 | 0 | 6,000,000 | | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vi) Mradi wa Kijani - Pemba | 0 | 4,963,182 | 4,963,182 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **49,050,000** | **6,223,182** | **55,273,182** | **11,648,701** | **578,137** | **12,226,838** | **23.75** | **0** | **22.12** |
| **WAKALA WA USAJILI WA MATUKIO YA KIJAMII ZANZIBAR** | | | | | | | | | |
| Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usajili wa Matukio ya Kijamii | 900,000 | 0 | 900,000 | 741,269 | 0 | 741,269 | 82 | 0 | 82 |
| Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Ofisi za Wakala wa Usajili wa Matukio ya Kijami | 1,200,000 | 0 | 1,200,000 | 605,982 | 0 | 605,982 | 50 | 0 | 50 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,100,000** | **0** | **2,100,000** | **1,347,251** | **0** | **1,347,251** | **64** | **0** | **64** |
| **KIKOSI MAALUM CHA KUZUIA MAGENDO** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi na Ukarabati wa Kambi na Nyumba za KMKM | 1,500,000 | 0 | 1,500,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Kuimarisha Shughuli za Uzamiaji na Uokozi | 1,500,000 | 0 | 1,500,000 | 1,496,156 | 0 | 1,496,156 | 100 | 0 | 100 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **3,000,000** | **0** | **3,000,000** | **1,496,156** | **0** | **1,496,156** | **50** | **0** | **50** |
| **KIKOSI CHA VALANTIA** | | | | | | | | | |
| Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Maaskari | 3,314,400 | 0 | 3,314,400 | 1,186,016 | 0 | 1,186,016 | 36 | 0 | 36 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **3,314,400** | **0** | **3,314,400** | **1,186,016** | **0** | **1,186,016** | **36** | **0** | **36** |
| **CHUO CHA MAFUNZO** | | | | | | | | | |
| Mradi wa Ujenzi wa Nyumba za Makaazi na Mahanga | 2,146,800 | 0 | 2,146,800 | 1,615,000 | 0 | 1,615,000 | 75 | 0 | 75 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,146,800** | **0** | **2,146,800** | **1,615,000** | **0** | **1,615,000** | **75** | **0** | **75** |
| **JESHI LA KUJENGA UCHUMI** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba na Mahanga ya Kambi za JKU | 3,591,600 | 0 | 3,591,600 | 2,113,051 | 0 | 2,113,051 | 59 | 0 | 59 |
| ii) Mradi wa Ujenzi wa Dakhalia | 1,875,060 | 0 | 1,875,060 | 2,062,473 | 0 | 2,062,473 | 110 | 0 | 110 |
| iii) Mradi wa Uimarishaji wa Utoaji wa Huduma za Wakala wa Ulinzi JKU | 3,253,800 | 0 | 3,253,800 | 3,200,368 | 0 | 3,200,368 | 98 | 0 | 98 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **8,720,460** | **0** | **8,720,460** | **7,375,892** | **0** | **7,375,892** | **85** | **0** | **85** |
| **KIKOSI CHA ZIMAMOTO NA UOKOZI** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Mahanga na Nyumba za Maaskari | 1,800,000 | 0 | 1,800,000 | 4,270,161 | | 4,270,161 | 237 | | 237 |
| ii) Mradi wa Ununuzi wa Magari na Vifaa vya Kuzimia Moto | 1,530,000 | 12,126,034 | 13,656,034 | | 14,230,121 | 14,230,121 | 0 | 117 | 104 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **3,330,000** | **12,126,034** | **15,456,034** | **4,270,161** | **14,230,121** | **18,500,282** | **128** | **117** | **120** |
| **OFISI YA MAKAMO WA KWANZA WA RAIS** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi** | **0** | 358,930 | 358,930 | **0** | 280,455 | 280,455 | **0** | 78 | 78 |
| i) Mradi wa Kuimarisha Uhimili wa Mabadiliko ya Tabianchi kwa Jamii za Pwani | **0** | 489,132 | 489,132 | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| ii) Mradi wa Kukabiliana na Mabadiliko ya Tabianchi na Usimamizi wa Mazingira | 2,700,000 | 0 | 2,700,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,700,000** | **848,062** | **3,548,062** | **0** | **280,455** | **280,455** | **0** | **0** | **8** |
| **MAMLAKA YA USIMAMIZI WA MAZINGIRA** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuwezesha Mamlaka za Serikali za Mitaa Kukabiliana na Athari za Mabadiliko ya Tabianchi** | **0** | 91,260 | 91,260 | **0** | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| Mradi wa Kuirithisha Zanzibar ya Kijani | 600,000 | 0 | 600,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **600,000** | **91,260** | **691,260** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **MAMLAKA YA KUDHIBITI NA KUPAMBANA NA MADAWA YA KULEVYA** | | | | | | | | | |
| Mradi wa Kuimarisha Mamlaka ya Kupambana na Dawa za Kulevya | 2,700,000 | 0 | 2,700,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **2,700,000** | **0** | **2,700,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **OFISI YA MAKAMU WA PILI WA RAIS, SERA, URATIBU NA BARAZA LA WAWAKILISHI** | | | | | | | | | |
| **Mpango wa Kunusuru Kaya Masikini Awamu ya Tatu (TASAF III)** | 60,000 | 21,000,000 | 21,060,000 | 75,000 | 601,941 | 676,941 | 125 | 3 | 3 |
| **Miradi** | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| i) Mradi wa Ujenzi wa Nyumba ya Makamu wa Pili wa Rais | 1,200,000 | **0** | 1,200,000 | 756,409 | **0** | 756,409 | 63 | **0** | 63 |
| ii) Mradi wa Ukarabati wa Ofisi ya Uratibu Dar-es-salaam | 330,000 | **0** | 330,000 | **0** | **0** | 0 | 0 | **0** | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **1,590,000** | **21,000,000** | **22,590,000** | **831,409** | **601,941** | **1,433,350** | **52** | **3** | **6** |
| **WIZARA YA AFYA** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kumaliza Malaria Zanzibar** | 600,000 | 3,762,191 | 4,362,191 | 535,105 | 8,187,988 | 8,723,093 | 89 | 218 | 200 |
| **Programu Shirikishi ya Afya ya Uzazi wa Mama na Mtoto** | 600,000 | 3,168,639 | 3,768,639 | 0 | 287,962 | 287,962 | 0 | 9 | 8 |
| **Programu ya Kudhibiti Maradhi ya Ukimwi, Homa ya Ini, Kifua Kikuu na Ukoma** | 600,000 | 2,908,211 | 3,508,211 | 379,100 | 1,957,166 | 2,336,266 | 63 | 0 | 67 |
| **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Afya** | 21,210,000 | 22,200,000 | 43,410,000 | 9,428,444 | 16,982,560 | 26,411,004 | 44 | 76 | 61 |
| **Programu ya Ukarabati na Ujenzi wa Vituo vya Afya ya Msingi** | 12,000,000 | 0 | 12,000,000 | 15,502,948 | 0 | 15,502,948 | 129 | 0 | 129 |
| **Programu ya Kuimarisha huduma za Mama na Mtoto** | 0 | 15,000,000 | 15,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Wafanyakazi Katika Hospitali za Wilaya na Mkoa** | 1,800,000 | 0 | 1,800,000 | 7,117,014 | 0 | 7,117,014 | 395 | 0 | 395 |
| **Programu ya Jamii ni Afya** | 1,200,000 | 0 | 1,200,000 | 1,311,200 | 0 | 1,311,200 | 109 | 0 | 109 |
| **Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar** | 600,000 | 0 | 600,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Programu ya Kuimarisha Nguvu Kazi** | 1,200,000 | 0 | 1,200,000 | 1,836,050 | 0 | 1,836,050 | 153 | 0 | 153 |
| **Programu ya Kusaidia Watu Wasiojiweza Kujiunga na Mfuko wa Huduma za Afya Zanzibar** | 600,000 | 317,280 | 917,280 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Miradi** | | | | | | | | | |
| ii) Mradi wa Ukarabati na Utanuzi wa Hospitali ya Mnazi Mmoja | 8,640,000 | 6,000,000 | 14,640,000 | 2,310,068 | 0 | 2,310,068 | 27 | 0 | 16 |
| ii) Mradi wa Ujenzi wa Hospitali ya Rufaa na Kufundishia Binguni | 1,020,000 | 9,518,456 | 10,538,456 | 1,560,803 | 0 | 1,560,803 | 153 | 0 | 15 |
| Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Kidigitali | 1,200,000 | 0 | 1,200,000 | 300,000 | 0 | 300,000 | 25 | 0 | 25 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **51,270,000** | **62,874,777** | **114,144,777** | **40,280,732** | **27,415,676** | **67,696,408** | **79** | **44** | **59** |
| **WIZARA YA ARDHI NA MAENDELEO YA MAKAAZI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ujenzi wa Nyumba za Maendeleo** | 180,072,000 | 0 | 180,072,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Upangaji wa Miji na Usimamizi wa Ardhi** | 21,339,000 | 0 | 21,339,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **201,411,000** | **0** | **201,411,000** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **WIZARA YA BIASHARA NA MAENDELEO YA VIWANDA** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuendeleza Viwanda** | | | | | | | | | |
| Kuanzisha na kuendeleza Maeneo Maalum ya Viwanda (Indurstrial Parks) | 21,336,000 | 0 | 21,336,000 | 1,557,164 | 0 | 1,557,164 | 7 | 0 | 7 |
| **Programu ya Kuendeleza Vituo vya Biashara na Maonyesho Zanzibar** | 6,482,322 | 0 | 6,482,322 | 2,945,958 | 0 | 2,945,958 | 45 | 0 | 45 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **27,818,322** | **0** | **27,818,322** | **4,503,122** | **0** | **4,503,122** | **16** | **0** | **16** |
| **WIZARA YA ELIMU NA MAFUNZO YA AMALI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Elimu** | 148,588,740 | 115,005,412 | 263,594,152 | 95,089,607 | 104,060,753 | 199,150,360 | 64 | 90 | 76 |
| **Miradi** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuimarisha Upatikanaji wa Vifaa vya Kujifunzia na Kufundishia | 23,524,860 | 5,365,172 | 28,890,032 | 13,492,202 | 881,000 | 14,373,202 | 57 | 16 | 50 |
| i) Mradi wa Uimarishaji wa Elimu ya Juu | 21,000,000 | 0 | 21,000,000 | 20,500,000 | | 20,500,000 | 98 | | 98 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **193,113,600** | **120,370,584** | **313,484,184** | **129,081,809** | **104,941,753** | **234,023,562** | **67** | **87** | **75** |
| **WIZARA YA HABARI, VIJANA, UTAMADUNI NA MICHEZO** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuendeleza Viwanja vya Michezo** | | | | | | | | | |
| i) Ujenzi wa Viwanja vya Michezo vya Wilaya | 24,330,000 | 380,389 | 24,710,389 | 47,364,128 | 0 | 47,364,128 | 195 | 192 | 192 |
| ii) Ujenzi wa Kiwanja Kipya cha Michezo | 223,740,000 | | 223,740,000 | 174,312,364 | 0 | 174,312,364 | 78 | 78 | 78 |
| iii) Mradi wa Ujenzi wa Chuo cha Sanaa na Utamaduni | 1,800,000 | | 1,800,000 | 1,864,432 | 0 | 1,864,432 | 104 | 104 | 104 |
| iv) Mradi wa Vituo vya Mafunzo kwa Vijana Awamu ya Pili | 9,900,000 | 0 | 9,900,000 | 2,227,334 | 0 | 2,227,334 | 22 | 22 | 22 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **259,770,000** | **380,389** | **260,150,389** | **225,768,258** | **0** | **225,768,258** | **87** | 87 | **87** |
| **WIZARA YA KILIMO, UMWAGILIAJI, MALIASILI NA MIFUGO** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ujenzi wa Miundombinu ya Umwagiliaji** | **0** | 3,483,731 | 3,483,731 | 0 | 4,034,841 | 4,034,841 | 0 | 116 | 116 |
| **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Mifugo** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuendeleza Miundombinu ya Mifugo na Misitu | 1,500,000 | **0** | 1,500,000 | 791,896 | 0 | 791,896 | 53 | **0** | 53 |
| ii) Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Bidhaa za Nyuki | 0 | 60,000 | 60,000 | 0 | **0** | 0 | **0** | **0** | **0** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| iii) Mradi wa Mageuzi ya Uzalishaji wa Maziwa kwa Wafugaji Wadogo Unazingatia Mabadiliko ya Tabianchi. | 0 | 3,150,000 | 3,150,000 | 0 | 2,372,767 | 2,372,767 | **0** | 75 | 75 |
| **Programu ya Usimamizi na Uhifadhi wa Chakula** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa ukarabati wa Maghala na Uhifadhi wa Chakula | 12,000,000 | 0 | 12,000,000 | 1,756,335 | 0 | 1,756,335 | 15 | 0 | 15 |
| ii) Mradi wa Uhimilivu wa Mifumo ya Chakula Tanzania (TFSRP) | 0 | 7,500,000 | 7,500,000 | 0 | 15,796,532 | 15,796,532 | 0 | 211 | 211 |
| iii) Mradi wa Kuimarisha Mifumo ya Chakula kwa Kuongeza Tija na Uzalishaji Kupitia Huduma za Kisasa za Kilimo katika Umwagiliaji | 120,000 | 2,250,000 | 2,370,000 | 0 | 17,316,324 | 17,316,324 | 0 | 770 | 731 |
| iv)Mradi wa Kuendeleza Mifumo ya Chakula, Matumizi na Urejeshaji wa Ardhi (FOLUR) | 0 | 720,000 | 720,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| v) Mradi wa Mabadiliko ya Mfumo wa Chakula kwa Kukuza Uchumi Jumuishi | 0 | 865,050 | 865,050 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vi) Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea na Kuhakikisha Usalama wa Chakula (STREPHIT) | 0 | 1,419,354 | 1,419,354 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vii) Mradi wa Kuanzisha Bustani ya Mimea (Botanic Garden) | 1,200,000 | | 1,200,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| viii)Mradi wa Kujenga Mazingira Wezeshi kwa Huduma Endelevu za Ugani wa Kilimo (ENSURE) | 0 | 240,000 | 240,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ix) Mradi wa Kuimarisha Usimamizi wa Hifadhi ya Akiba ya Ufufuma -Pongwe | 0 | 72,000 | 72,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| x) Mradi wa Ujasiriamali wa Vijana kwa Mustakabali wa Sekta ya Kilimo | 0 | 329,427 | 329,427 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **14,820,000** | **20,089,562** | **34,909,562** | **2,548,231** | **39,520,464** | **42,068,695** | **17** | **197** | **121** |
| **WIZARA YA MAENDELEO YA JAMII, JINSIA,WAZEE NA WATOTO** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Hifadhi ya Wazee | 900,000 | **0** | 900,000 | 1,396,869 | **0** | 1,396,869 | **155** | **-** | **155** |
| ii) Mradi wa Mapambano Dhidi ya Vitendo vya Ukatili na Udhalilishaji kwa Wanawake na Wasichana | 0 | 381,793 | 381,793 | 0 | **0** | 0 | **0** | **0** | **0** |
| v) Mradi wa Kukuza Usawa wa Kijinsia Tanzania (Pamoja) | 0 | 2,612,520 | 2,612,520 | 0 | 4,251,856 | 4,251,856 | **0** | **163** | **163** |
| **JUMLA YA FUNGU** | **900,000** | **2,994,313** | **3,894,313** | **1,396,869** | **4,251,856** | **5,648,725** | **155** | **142** | **145** |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **WIZARA YA MAJI, NISHATI NA MADINI** | | | | | | | | | |
| **Program ya Kuimarisha Huduma za Usambazaji Maji Safi na Salama Zanzibar** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Uhuishaji wa Huduma za Usambazaji Maji na Usafi wa Mazingira Zanzibar | 1,510,002 | 8,190,000 | 9,700,002 | 0 | 14,267,859 | 14,267,859 | 0 | 174 | 147.1 |
| ii) Mradi wa Kuimarisha Usalama wa Maji na Uhimili wa Tabianchi Katika Maeneo ya Mijini | 0 | 1,205,274 | 1,205,274 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iii) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Usambazaji Maji Mkoa wa Mjini Magharibi (ZUWDFIP) | 924,600 | 23,969,847 | 24,894,447 | 59,693 | 0 | 59,693 | 6 | 0 | 0.2 |
| iv) Mradi wa Ununuzi wa "Chlorine", Usimamizi na Uangalizi Bora wa Maji | 0 | 24,000 | 24,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| v) Mradi wa Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Zanzibar | 9,466,134 | 0 | 9,466,134 | 16,950,024 | 0 | 16,950,024 | 179 | | 179 |
| vi) Mradi wa Uboreshaji na Uimarishaji wa Miundombinu ya Maji Kaskazini Unguja | 1,560,000 | 0 | 1,560,000 | 7,319,109 | 0 | 7,319,109 | 469 | 0 | 469 |
| vii) Mradi wa Uimarishaji Huduma Endelevu za Maji Safi Zanzibar | 1,560,000 | 41,297,331 | 42,857,331 | 119,385 | 0 | 119,385 | 8 | 0 | 0.28 |
| viii) Mradi wa Kuandaa Mpango Mkuu wa Maji Safi na Usafi wa Mazingira Zanzibar | 0 | 2,017,772 | 2,017,772 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ix) Mradi wa Usimamizi wa Rasilimali Maji Chini ya Ardhi | 0 | 1,009,714 | 1,009,714 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Programu ya Kuimarisha Miundombinu ya Umeme Zanzibar** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuimarisha Miundombinu ya Umeme | 4,200,000 | 0 | 4,200,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Kuifanyia Mabadiliko Sekta ya Nishati Zanzibar (ZESTA) | 0 | 3,884,574 | 3,884,574 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iii) Mradi wa Uboreshaji wa Mfumo wa Umeme Zanzibar | 20,013,411 | 0 | 20,013,411 | 54,232,158 | 0 | 54,232,158 | 271 | 0 | 271 |
| iii) Mradi wa Ulazaji wa Waya wa umeme Bahari (Zanzibar Submarine Cable Project) (New) AfDB | 0 | 2,381,400 | 2,381,400 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **39,234,147** | **83,979,911** | **123,214,058** | **78,680,369** | **14,267,859** | **92,948,228** | **201** | **17** | **75** |
| **WIZARA YA UCHUMI WA BULUU NA UVUVI** | | | | | | | | | |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Kuendeleza Sekta ya Kilimo na Uvuvi** | **0** | 7,883,095 | 7,883,095 | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** | **0** |
| **Programu ya Kutengeneza Miundombinu ya Mafuta na Gesi Asilia** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhi Taarifa za Mafuta na Gesi Asilia (NDR) | 4,200,000 | **0** | 4,200,000 | 9,511,746 | **0** | 9,511,746 | 0 | **0** | **0** |
| ii) Mradi wa Usambazaji wa Gesi | 5,400,000 | **0** | 5,400,000 | **0** | **0** | 0 | 0 | **0** | **0** |
| **Programu ya Kuimarisha na Kuendeleza Miundombinu ya Sekta ya Uvuvi** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Madiko na Masoko ya Kisasa ya Samaki | 16,605,336 | 0 | 16,605,336 | 8,614,474 | 0 | 8,614,474 | 52 | 0 | 52 |
| Mradi wa Ujenzi wa Bandari ya Uvuvi | 17,996,886 | 0 | 17,996,886 | 6,941,902 | 0 | 6,941,902 | 39 | 0 | 39 |
| Mradi wa Ujenzi wa Viwanda vya Kusarifu na Kuchakata Samaki | 30,600,000 | 0 | 30,600,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Programu ya Usimamizi na Uimarishaji wa Mazao ya Baharini** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Kuendeleza Mnyororo wa Thamani wa Mwani (SESEP) | 3,945,000 | 0 | 3,945,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi Jumuishi wa Uwezeshaji wa Wanawake katika Ufugaji wa Mazao ya Baharini | 0 | 1,611,000 | 1,611,000 | 0 | 2,685,000 | 2,685,000 | 0 | 167 | 167 |
| iii) Mradi wa Kukuza Usimamizi Endelevu wa Uvuvi na Ukuzaji wa Viumbe Maji wa Bahari Tanzania - TASFAM | 0 | 6,000,000 | 6,000,000 | 0 | 16,248,104 | 16,248,104 | 0 | 271 | 271 |
| iv) Mradi wa Utafiti wa Uchumi, Usalama wa Chakula na Maisha Endelevu kwa Jamii - SAMAKI | 0 | 7,800 | 7,800 | 0 | 19,790 | 19,790 | 0 | 254 | 254 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **78,747,222** | **15,501,895** | **94,249,117** | **25,068,122** | **18,952,894** | **44,021,016** | **90** | **122** | **90** |
| **WIZARA YA UJENZI NA UCHUKUZI** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Ujenzi na Matengenezo ya Miundombinu ya Barabara** | | | | | | | | | |
| i) Mradi wa Ujenzi wa Barabara Kuu | 80,035,774 | 117,383,347 | 197,419,120 | 274,718,759 | 14,292,000 | 289,010,759 | 343 | 12 | 146 |
| ii) Mradi wa Ujenzi wa Barabara za Ndani | 46,820,400 | 0 | 46,820,400 | 143,493,480 | 0 | 143,493,480 | 306 | 0 | 306 |
| iii) Mradi wa Matengenezo ya Barabara za Mjini | 21,000,000 | 0 | 21,000,000 | 32,261,657 | 0 | 32,261,657 | 154 | 0 | 154 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| iv) Mradi wa Ujenzi wa Misingi ya Maji, Barabara pamoja na Matengenezo ya Maziwa Katika Maeneo ya Mji. | 162,000,000 | 0 | 162,000,000 | 6,560,131 | 0 | 6,560,131 | 4 | 0 | 4 |
| Programu ya Ukuzaji wa Uchumi Jumuishi Zanzibar (BIG - Z) | 0 | 84,000,000 | 84,000,000 | 0 | 83,833,848 | 83,833,848 | 0 | 100 | 100 |
| **Programu ya Kuimarisha Viwanja vya Ndege** | | | | | | | | | |
| i) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Pemba | 1,200,000 | 95,700,000 | 96,900,000 | 92,570 | 96,047,214 | 96,139,784 | 8 | 100 | 99 |
| ii) Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II AAKIA | 18,000,000 | 0 | 18,000,000 | 18,374,041 | 0 | 18,374,041 | 102 | 0 | 102 |
| iii) Mradi wa Ujenzi wa Jengo la Abiria Terminal II AAKIA (Phase II) | 18,000,000 | 0 | 18,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iv) Ujenzi wa Uwanja wa Ndege wa Nungwi | 13,500,000 | 0 | 13,500,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| v) Ujenzi wa Apron katika kiwanja cha Ndege cha AAKIA | 24,000,000 | 0 | 24,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Programu ya Kuimarisha Bandari** | | | | | | | | | |
| i) Ujenzi wa Bandari Jumuishi - Mangapwani | 123,060,218 | 0 | 123,060,218 | 186,036,471 | 0 | 186,036,471 | 151 | | 151 |
| ii) Ujenzi wa Bandari ya Abiria Maruhubi | 0 | 78,000,000 | 78,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **Programu ya Mageuzi ya Kidigitali** | | | | | | | | | |
| i) Kulaza Mkonga wa Kimataifa wa Baharini Zanzibar (International Gateway) | 18,000,540 | 0 | 18,000,540 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Utoaji wa Huduma ya Mtandao katika Maeneo ya Umma (Public Wi-Fi ) | 6,030,000 | 0 | 6,030,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iii) Ujenzi wa Kituo cha Kuhifadhia Data | 18,000,000 | 0 | 18,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| iv)Uimarishaji Mfumo wa Mawasiliano | 3,600,000 | 0 | 3,600,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| v) Mradi wa Uwekaji wa Kamera za Kusimamia Vyombo vya Usafiri Barabarani | 1,123,800 | 0 | 1,123,800 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| vi) Mradi wa Kuimarisha Mfumo wa Usafiri wa Umma Zanzibar | 0 | 224,603 | 224,603 | 0 | 1,090,743 | 1,090,743 | 0 | 486 | 486 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **554,370,732** | **375,307,949** | **929,678,681** | **661,537,109** | **195,263,805** | **856,800,914** | **119** | **52** | **92** |
| **WIZARA YA UTALII NA MAMBO YA KALE** | | | | | | | | | |
| **Programu ya Kuimarisha Maeneo ya Kihistoria** | 3,600,000 | 0 | 3,600,000 | 406,014 | 0 | 406,014 | 11 | 0 | 11 |

| | | | | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| **Programu ya Uimarishaji wa Miundombinu ya Utalii** | 3,600,000 | 0 | 3,600,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| i) Mradi wa Ukarabati wa Majengo ya Mji Mkongwe | 6,000,000 | 0 | 6,000,000 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| ii) Mradi wa Kulifanyia Ukarabati Jengo la Beit Al Jaib | 0 | 9,015,493 | 9,015,493 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA FUNGU** | **13,200,000** | **9,015,493** | **22,215,493** | **406,014** | **0** | **406,014** | **3** | **0** | **2** |
| **Fedha za kazi za kawaida (Recurrent activities)** | **0** | **0** | **0** | 0 | 4,251,079 | 4,251,079 | 0 | 0 | 0 |
| **JUMLA YA KUBWA** | **1,938,840,000** | **784,944,167** | **2,723,784,167** | **1,451,557,748** | **491,752,081** | **1,943,309,829** | **75** | **63** | **71** |